**15 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 15 Mei, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. GRACE V. TENDEGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Grace Tendega.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nimwite Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba, sasa aulize swali lake.

Na. 339

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Muleba**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Muleba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Muleba imetengewa shilingi 1,825,662,000 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali hiyo. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya hospitali hiyo mpaka itakapokamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oscar Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yenye kutia matumaini. Sitakuwa na swali la nyongeza ila naipongeza Serikali kwa kuliona hilo na niwaombe sasa wakajenge hiyo hospitali kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Muleba. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametoa pongezi kwa Serikali kwa kuendeleza ujenzi wa miundombinu hii muhimu na sisi kama Serikali tunapokea pongezi hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya inayojengwa kule Mabogini katika Jimbo la Moshi Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hospitali yake hii ya halmashauri itajengwa kwa sababu katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi bilioni 43.84 kwa ajili ya

kukamilisha miradi viporo ya hospitali za halmashauri. Kwa hiyo nimhakikishie Serikali inakuja kujenga hospitali hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Iringa Vijijini ina majimbo mawili, hospitali ya wilaya ilijengwa katika Jimbo la Ismani ambayo wananchi wa Kalenga hawaitumii kwa sababu ipo mbali sana. Je, ni lini Serikali itajenga hospitali katika Jimbo la Kalenga? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakusudia kusogeza huduma za afya msingi karibu na wananchi na ndiyo maana kila mwaka inatenga fedha kwa ajili ya kuendelea kukamilisha miradi ya hospitali hizi za halmashauri. Kwa hiyo nimhakikishie Serikali ipo kazini na itahakikisha inasogeza huduma ya afya msingi kwa wananchi kwa kuendelea kuleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hizi za halmashauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021/2022, Serikali ilitupatia shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya ya Makete, baada ya hapo hatujapata fedha nyingine yoyote. Je, ni ipi *commitment* ya Serikali kutuongezea fedha ili Hospitali ya Wilaya ya Makete irudi kwenye hadhi yake ambayo wananchi wa Makete wanaitegemea na ni ahadi ya Serikali? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu hapo awali katika Mwaka wa Fedha

2024/2025, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 43.84 kwa ajili ya kuhakikisha inaendelea kuboresha miundombinu katika hospitali zetu hizi, kwa sababu tayari Serikali imekuwa ikitenga fedha kuhakikisha ujenzi wa hospitali hizi unaendelea. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali italeta fedha kwa ajili ya kuboresha na kukamilisha miundombinu katika hospitali yako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya Rais Samia mwaka juzi Wilayani Bunda aliagiza hospitali ya halmashauri ijengwe katika Jimbo la Mwibara. Je, ni lini hospitali hiyo itajengwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Viongozi Wakuu wa Nchi ikiwemo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kipaumbele kikubwa sana katika utekelezaji wa miradi hii ya Serikali. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itakuja kuhakikisha kwamba inatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetwaa eneo la *KIA* kwa ajili ya Uwanja wa Ndege na Zahanati ya Tindigani imechukuliwa kwenye eneo hilo. Je, ni lini sasa Serikali itajenga zahanati nyingine kufidia hii ya Tindigani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa afya msingi na kadri ya upatikanaji wa

fedha itaangalia vipaumbele muhimu kama alichokitaja Mheshimiwa Mbunge ili kuhakikisha kwamba inaboresha na kujenga miundombinu hii muhimu kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya msingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, swali kwa kifupi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa shilingi bilioni tatu laki tano mia sita hamsini elfu kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, lakini mpaka leo ni miaka minne hospitali hiyo haijamalizika. Je, ni lini Serikali itamalizia hospitali hiyo ili iweze kufanya kazi kwa Halmashauri ya Bunda? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali imetenga shilingi bilioni 43.84 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo ya hospitali za halmashauri. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba, Serikali italeta fedha ili kuhakikisha inakamilisha mradi wa hospitali hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, nimwite sasa Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Tadayo.

Na. 340

**Ujenzi wa Soko la Kisasa Kata ya Kiwira- Rungwe**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO K.n.y. MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Kisasa katika Kata ya Kiwira-Rungwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Soko la Kisasa la Kiwira kwa wananchi wa Wilaya ya Rungwe. Kwa kutambua hilo hatua mbalimbali zimechukuliwa na Serikali kuwezesha ujenzi wa soko hilo ambapo upembuzi yakinifu na michoro ya kihandisi imekamilika, upimaji wa udongo wa eneo la ujenzi umefanyika na andiko la mradi huo limeandaliwa. Aidha, andiko la mradi huo limeshapita katika hatua za awali za uchambuzi na hatua inayoendelea ni tathmini ya athari za mazingira na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo ukikidhi vigezo utatengewa fedha kupitia utaratibu wa miradi ya kimkakati. Aidha, mradi huo utakapokamilika utakuwa na eneo la soko, mgahawa, maduka ya kibiashara, kiwanda kidogo cha kuchakata zao la ndizi, jengo la taasisi za kifedha na ghala baridi *(cold room)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa mradi huu uliombewa toka Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mpaka sasa haujaanza kwa sababu hizo nzuri ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mwantona mara baada ya Bunge hili kwenda kuwahakikishia wananchi wa Kata ya Kiwira ambao wana imani sana na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan juu ya ujenzi wa soko hili kama alivyoeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni Jimbo langu la Mwanga, je, ni lini Serikali itajenga Soko la Kisasa katika Halmashauri ya Mwanga? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge, nikipata nafasi kwa sababu Mheshimiwa Mbunge hayupo leo, lakini tutazungumza naye ili tuweze kukubaliana ratiba ya kwenda kwenye jimbo lake; kwenda kukagua eneo la mradi huu na kukutana na wananchi wake kama alivyoleta maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kwenye halmashauri kupitia mapato ya ndani zinaweza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa masoko. Pia, kuna njia nyingine ambayo ni ya kuomba mradi wa kimkakati. Kwa hiyo nichukue nafasi hii kuendelea kumkumbusha mkurugenzi aweze kuona katika nafasi hizo mbili; ya kwanza kutenga mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa soko, lakini kuna njia nyingine ya kuandika andiko maalum kwa ajili ya kuomba mradi wa kimkakati wa ujenzi wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa njia hizo mbili Mheshimiwa Mbunge anaweza kuleta maombi, lakini kutenga fedha kwenye mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa soko au kuleta maombi kwa ajili ya kupatiwa fedha ya kujenga mradi wa kimkakati wa soko katika jimbo la Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami, swali la nyongeza. Naomba mliotaka kuuliza swali msimame tena. Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, je, ni lini Serikali itajenga mapaa kwenye Masoko kongwe ya Mwika, Marangu, Kisambo, Lyamombi na Himo kwenye Jimbo la Vunjo ambapo wanawake hususan wanaofanya biashara huku wananyeshewa na mvua na kupigwa na jua kali mwaka mzima? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa umuhimu wa miundombinu hii ya maghala, Serikali kwa kadri ya upatikanaji wa fedha itaona jinsi gani inaweza kukamilisha ujenzi wa majengo haya muhimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Lamadi la kimkakati ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2022?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, ahadi za viongozi wakuu wa nchi ni kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge bila shaka tayari andiko hili lilishafika na limepita katika ngazi zote, kwa hiyo Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuja kutekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kwa muda mrefu sana wananchi wa Mto wa Mbu Wilayani Monduli Mkoa wa Arusha waliahidiwa soko la kisasa lakini hadi leo ahadi hiyo haijatekelezwa. Lini Serikali itatekeleza ahadi hii kwa wananchi wa Mto wa Mbu?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri kupitia

mapato ya ndani waweze kutenga fedha kwa ajili ya kujenga soko hili. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali kupitia mapato ya ndani itahakikisha kwamba inafanya tathmini na kuweka katika mipango ya kibajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa soko hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa Wilaya ambazo zina uzalishaji mkubwa sana wa mahindi, lakini hatuna soko la kisasa ambalo lingeweza kusaidia mapato kwa ajili ya Wilaya ya Kilindi. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kututengea fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo? Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuendelea kumkumbusha mkurugenzi anaweza akafanya tathmini, wakaandika andiko la kuonesha uhitaji, lakini kuonesha kwamba soko hili linaweza likawa lina tija kwa wananchi kama Mheshimiwa Mbunge alivyozungumza, apitishe katika michakato yote na ikikidhi vigezo kwa kweli Serikali italeta fedha kwa ajili ya kuhakikisha soko hili muhimu linajengwa kwa maslahi mapana ya wananchi. Sifa mojawapo muhimu sana katika mchakato huu ni kwamba ni lazima halmashauri iwe ilipata hati safi kwa miaka mitatu mfululizo.

Kwa hiyo andiko hili likikidhi vigezo hivi vyote, basi namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali italeta fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko hili.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, nimwite sasa Mheshimiwa Shabani Omar Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, aulize swali lake.

Na. 341

**Ujenzi wa Barabara kwa Kutumia Zege**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, *TARURA* ina mpango gani wa kujenga barabara kwenye kona kali na milimani kwa kutumia zege katika Jimbo la Lushoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya uwepo wa kona na miinuko mikali katika baadhi ya barabara za Jimbo la Lushoto. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hizo, Serikali imekuwa ikitenga fedha na kujenga vipande vya matabaka ya zege katika maeneo yenye milima mikali na kona ili kuondoa changamoto ya upitaji kwa vyombo vya usafiri kwa kuzingatia vipaumbele na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, *TARURA* inajenga tabaka la zege lenye urefu wa meta 900 katika Barabara ya Halmashauri ya zamani – Kwembago - Irente kwa gharama ya shilingi milioni 512.74. Aidha, katika mwaka 2024/2025, shilingi milioni 181.75 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa maeneo yenye kona kali na miinuko katika Barabara ya Dochi - Gare kwa kujenga kwa tabaka la zege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti zijazo ili kuondoa changamoto hizi kwenye maeneo yenye milima na kona kali kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shelukindo, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shekilindi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, majina ya kilugha yana shida sana, Shekilindi siyo Shelukindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na mvua nyingi zilizonyesha na kuharibika kwa miundombinu ya barabara hasa maeneo ya Malibwi, Kwekanga hadi Makole na Mbelei, Baga hadi Mgwashi pamoja na Migambo hadi Kifungilo. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kutengeneza barabara hizo ili kuwaondolea adha wanaoendelea kuipata wananchi wangu hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa kuona ni kuamini, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kuongozana na mimi ili akaone mazao ya wananchi yanavyoharibika mashambani kwa sababu ya ubovu wa barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi za Wilaya na ndiyo maana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameongeza bajeti ya barabara za Wilaya, kwa maana bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni mia mbili sabini na tano mpaka sasa shilingi bilioni mia saba na kumi, yote hii ni kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara hizi za Wilaya inakuwa mizuri kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaweza kuifikia huduma lakini pia inawajenga kiuchumi kwa kufanya shughuli zao za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, barabara yake aliyoitaja ya Mbelei – Baga – Mgwashi ya kilometa 42, katika mwaka wa fedha 2023/2024 tayari imepokea shilingi 30,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa kalvati mistari nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mwaka wa fedha 2024/2025, imetengwa shilingi milioni 207.5 kwa ajili ya kuendelea kuboresha barabara hiyo. Kwa mfano, barabara yake ya Mabwi – Kwekwanga – Ngwelo ya kilometa 16.8 na yenyewe katika mwaka wa fedha 2024/2025, imetengewa jumla ya shilingi milioni 295. Kwa hiyo namuhakikishia Mheshimiwa Mbunge Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa hizi barabara za Wilaya ikiwemo barabara ambazo zipo katika Jimbo lako na itaendelea kuhakikisha inaleta fedha kwa ajili ya kuziboresha na kuzijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili ambalo ameuliza kama nipo tayari kuambatana na yeye kwende Jimboni kwake kujionea mazingira haya, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu, tutakutana pembeni tutakubaliana ratiba ili niweze kufika katika Jimbo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara ya kutoka Ihemi ambayo ni Jimbo la Kalenga kwenda mpaka Ihimbo ambayo itapita Mgama imekuwa ni mbovu na inasumbua wananchi kwa sababu wanalima mazao mengi na imeharibika wakati wa mvua.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanatengeneza barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, Serikali inaweka kipaumbele

kikubwa sana kuhakikisha kwamba barabara zetu hizi za Wilaya zinapitika ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za uzalishaji lakini kuweza kufikia huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kuleta fedha kuhakikisha kwamba inaifikia barabara hii uliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ili wananchi waweze kupata huduma nzuri ya barabara nzuri na waweze kuendelea na shughuli zao za kilimo na za uzalishaji mali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mvua kubwa zilizonyesha Tanzania nzima pamoja na Chemba, zimeharibu kabisa miundombinu ya barabara. Baadhi ya barabara hizo ambazo kwa sasa hazipitiki ni Barabara ya Kwa Mtoro – Sanzawa – Mpendo, Soya – Chandama, Soya – Magasa na maeneo mengine mengi. Tumeomba fedha za dharura lakini mpaka leo hatujapewa fedha kabisa. Naomba kujua ni ipi *commitment* ya Serikali kuhakikisha miundombinu inarudi ili watu waendelee na kazi zao kama kawaida? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi za Wilaya. Kwa wakati huu Serikali pia inatambua kwamba barabara zetu hizi nyingi zimeharibika kutokana na mvua kubwa ambayo imekuwa ikinyesha na ndiyo maana fedha ya dharura Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan ameongeza bajeti kutoka bajeti ya shilingi bilioni 21 mpaka shilingi bilioni 13, kwa ajili ya kuhudumia Barabara ambazo zinapata uharibifu mkubwa kama huu ili ziweze kutengenezwa kwa udharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua changamoto ya miundombinu

katika Jimbo la Mbunge na itahakikisha kwamba inaleta fedha kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu inaimarika katika Jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kutokana na mabadiliko ya tabianchi, barabara nyingi zimekuwa zikiharibika na kuifanya Serikali iwe na matengenezo ya mara kwa mara. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kutumia rasilimali ya mawe tuliyonayo hasa katika maeneo ya miji ili kuwa na barabara imara ambazo hazitasumbua wakati wa mvua? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni hoja ya msingi sana, kwa kutambua hilo, Serikali tayari imeshaanza kutumia teknolojia mbadala katika ujenzi wa barabara zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeanza kutumia teknolojia ya barabara ambazo tunaziita *eco roads* ambazo zenyewe zina gharama nafuu katika ujenzi lakini pia zina *life span* kubwa zaidi, zinakaa kwa muda mrefu haziharibiki kama hizi barabara zetu zingine za kawaida. Pia teknolojia aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ya kutumia mawe, kwa hiyo Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kutumia teknolojia hizi mbadala na tayari imeshaanza majaribio kwenye baadhi ya maeneo ili kuona ufanisi na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuthibitika, baada ya hicho kipindi cha majaribio, Serikali inaona umuhimu mkubwa sana wa kujenga barabara hizi ambazo zitakuwa na gharama nafuu lakini zitaweza kuishi kwa muda mrefu zaidi na kupunguza adha ya wananchi kuharibikiwa na barabara na kupata changamoto

kutokana na barabara zetu hizi kuharibika na hasa kipindi cha mvua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Namuita Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 342

**Wafanyakazi Kupandishiwa Mishahara**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapandishia mishahara wafanyakazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kikwete.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Serikali kupandisha mishahara ya watumishi wake. Hivyo, Serikali inaendelea na itaendelea kupandisha mishahara ya watumishi. Mathalani, Julai, 2022 Serikali iliongeza mshahara kiwango cha kima cha chini kwa Watumishi wa Umma kwa asilimia 23.3, kutoka shilingi 300,000 hadi shilingi 370,000/= kwa mwezi. Nyongeza hiyo ya mishahara ilitolewa pia kwa watumishi wote wa umma kwa viwango tofauti tofauti kulingana na viwango vya mishahara vya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetumia kiasi cha shilingi bilioni 153.9 kwa ajili ya nyongeza ya mwaka ya mishahara *(annual salary increment)* kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, katika sherehe za Mei Mosi mwaka huu, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Philip Isdor Mpango wakati wa kujibu risala ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini *(TUCTA)*, kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, alieleza kuwa suala la nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma ni jambo linaangaliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali hasa kwa kuzingatia kwamba wafanyakazi wamepata ahadi ya kupata neno la kuhusiana na mishahara yao wakati wowote Mheshimiwa Rais atakapoamua kuongea na umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechanganyikiwa kidogo, ukiangalia wakati Serikali inaongeza mishahara ya watumishi wa umma kutoka shilingi 300,000 mpaka shilingi 370,000, kwenye sekta ya binafsi bado hali yao ni duni sana. Utaangalia kwa mfano tunaambiwa kwenye zile sekta 13, kwenye hoteli kubwa za kitalii, mishahara kima cha chini shilingi 300,000. Mheshimiwa Rais kafanya jitihada kubwa, *Royal Tour* imekuja, watalii wameongezeka lakini bado mishahara ipo chini.

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kujua je, Serikali kwa kupitia Wizara ya Utumishi na Utawala Bora, ina mpango gani wa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuhakikisha kwamba mishahara ya kima cha chini inakuwa angalau shilingi 370,000 pia na kwa sekta binafsi?

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi, kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa kwenye swali lililoulizwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kupitia Bunge lako hili Tukufu kwamba, tayari Serikali Novemba, mwaka 2022 ilitoa mwongozo wa kima cha chini cha mshahara cha sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mwongozo ule kutoka, Shirikisho la Vyama vya Waajiri *(ATE)*, walitoa *secular* ya Disemba ambayo ilianza kutekelezwa Januari mwaka 2023, lakini mawazo yake tunayachukua na mchango wake tunauchukua na hivi sasa tayari kuna timu ambayo imeshaundwa na imeanza kazi mwezi Aprili kwa ajili ya kufanya mapitio tena ya kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya timu hiyo kukamilisha mapitio hayo, basi tutaleta hapa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge wote waweze kufahamu. Timu hiyo inahusisha utatu kwa maana ya wataalam kutoka Serikalini, kutoka *TUCTA* vilevile kutoka *ATE* ambapo ikikamilisha kazi tutaleta majibu hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi. Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Watumishi zaidi ya 850 wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya hawakulipwa mshahara wao wa mwezi wa tatu. Jambo hili limepelekea pia huduma ya Bima ya Afya kwa watumishi hao kufungwa, nataka kupata kauli ya Serikali juu ya watumishi hawa, nini tatizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hiyo changamoto iliyotokea katika Halmashauri ya Rorya, ilitokana na ukweli kwamba Serikali katika kupitia mfumo mpya wa upimaji wa utendaji ndani ya watumishi wa umma, wako baadhi ya watu ambao walionekana kwamba taarifa zao za mwenendo wa utendaji kila siku hazikuletwa katika ofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yako ilitoa maagizo kwa Halmashauri ya Rorya ili waweze kutupatia taarifa za watumishi wote hao. Nakiri mbele ya Bunge lako kwamba taarifa zilizotoka katika Ofisi ya Mkurugenzi Rorya, zilileta taarifa ya kwamba wako wafanyakazi zaidi ya 700 ambao walikuwa hawajajiorodhesha katika jedwali lile la utendaji *(PEPMIS)* kama ambavyo imeelekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Serikali ulieleza kwamba watumishi wote ambao hawakujiorodhesha wanatakiwa wafungiwe mishahara yao. Taratibu zilifanyika lakini baada ya kufanyia utaratibu tena kuangalia, tumegundua kwamba yako baadhi ya maeneo kulikuwa na changamoto ikiwemo taarifa ambazo zimeletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi yako ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, imekwishalifanyia kazi jambo hilo na imeshapeleka ombi jipya kwa ajili ya utatuzi wa hiyo kero iliyoingia ya mishahara ambayo kupitia Wizara ya Fedha, tunategemea kwamba tutapata fedha hizo na ili jambo litakwisha ndani ya wiki hii. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba asiwe na wasiwasi, watumishi wake watarudishiwa *payroll* zao na mambo yataendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo langu kwa Halmashauri zote, watumishi wote walio chini ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, wajiorodheshe na wajiunge na mfumo huu ili tuendelee kupimana katika utekelezaji wa majukumu kama ambavyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kwa majibu yako.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, namwita sasa Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 343

**Mkopo kwa Kutumia Mali Zilizorasimishwa**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO K.n.y. MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, mikopo kiasi gani imetolewa na Taasisi za Fedha kwa dhamana ya mali zilizorasimishwa na wanawake wangapi wamenufaika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki na taasisi za fedha hutoa mikopo yenye dhamana inayotosheleza *(fully secured)*, yenye dhamana inayotosheleza sehemu tu ya mkopo *(partially secured)* na isiyo na dhamana *(unsecured)*. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2023, zilikuwa zimetoa mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 33,194.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haina takwimu zinazotenganisha mikopo iliyotolewa kwa wanaume na wanawake. Hata hivyo, Benki kuu ya Tanzania inatengeneza mfumo ambao ukikamilika utaweza kukusanya takwimu zinazotenganisha mikopo

iliyotolewa kwa wanaume na wanawake kutoka kwenye benki na taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea na mchakato wa kuandaa Sheria ya Miamala Salama na Masjala Bayana ya Kielektroniki itakayotumika kusajili dhamana zinazohamishika ili kupanua wigo wa dhamana na hivyo kuwezesha wananchi wengi zaidi kupata mikopo kutoka benki na taasisi za kifedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo kwa niaba ya Mheshimiwa Shally, swali nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani maswali ya nyongeza hayatakuwepo kwa sababu, maeneo aliyokuwa amejikita, na majibu yanakinzana. Alikuwa amekusudia kujua maeneo yanayorasimishwa, yale maeneo ambayo yamejengwa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo huna swali Mheshimiwa Priscus?

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayapo kwa sababu jibu halijaenda moja kwa moja.

**MWENYEKITI:** Basi tunakushukuru. Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza. Mheshimiwa Cecilia Paresso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Benki zetu bado riba ni kubwa sana. Je, Serikali haina mpango wa kufikiria kupunguza riba ili angalau wananchi walio wengi waweze kukopa katika benki zetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko kwenye mpango huo na jambo hilo linalohusisha riba ni jambo mtambuka, lina hatua nyingi mpaka kufikia kwenye hatua hiyo. Moja ya hatua ambayo Serikali imefanya, umeona kwenye masuala ya sensa na makazi, masuala ya vitambulisho vya Taifa, hayo yote ni ya kuwezesha wananchi watambulike ili kupunguza *risk* na *risk* zikipungua, *definitely* tutakuwa tunaenda kwenye uelekeo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea pia kuongea na Benki Kuu pamoja na benki zingine, kuweza kuona utekelezaji wake ili uweze kufanyika bila kuathiri sekta ya fedha.

**MWENYEKITI:** Tunakwenda kwenye swali linalofuata, namwita Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 10 Mei, 2024, nilipata taarifa ya kujibiwa swali, utaratibu wa kupata bidhaa moja kwa moja kutoka Tanzania na Kenya mpakani Sirari. Hili swali, haliendani na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyasoma hapa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Hebu rudia Mheshimiwa Mwikwabe. Mheshimiwa Mwikwabe, si ungeuliza swali lako la msingi? Swali la msingi.

Na. 344

**Utaratibu wa kupata Bidhaa moja moja kutoka Tanzania na Kenya mpakani Sirari**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaweka kituo kidogo cha forodha katika Kata ya Itiryo/Bikonge pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kupata bidhaa kutoka Kenya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha forodha Kata ya Itiryo/Bikonge ni miongoni mwa vituo tarajiwa vya forodha vitakavyofanyiwa tathmini na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika mwaka 2024/2025. Tathmini itafanyika kwa kuzingatia vigezo mahsusi ikiwemo uwiano wa gharama za ukusanyaji wa mapato na kiwango cha kodi kinachotarajiwa kukusanywa katika kituo hicho. Endapo kituo hicho kitakidhi vigezo, mchakato wa uanzishwaji utaanza kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwaelekeza wafanyabiashara wanaotumia mpaka wa Tanzania na Kenya uliopo Kata ya Itiryo/Bikonge, kuendelea kutumia vituo rasmi vya forodha vya karibu ikiwemo Kituo cha Forodha cha Sirari ili kurahisisha zoezi la ulipaji kodi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwikwabe, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alienda Sirari. Ilianza mwanzoni kwamba, nilitaka anieleze utaratibu wa kupata bidhaa moja kwa moja kutoka Kenya na Tanzania. Kwa sababu wale wachuuzi wa kawaida hawaruhusiwi kupitisha bidhaa pale na Jumamosi gari ya *TRA* ilimfukuza kijana akiwa na bidhaa ya plastiki ikampiga ikamwingiza kwenye mtaro na ninavyozungumza ndugu zake wameshazika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anachozungumza hapa ni habari ya mikonge ambayo niliuliza mwaka jana. Bidhaa kutoka Kenya, sasa hivi kule Sirari mbolea ya Tanzania ni ghali kuliko ya Kenya; hakuna utaratibu hata wa kawaida kwa wakulima. Mabati yanatoka Kenya, ya Tanzania ni ghali. Sasa nataka nipate majibu kwamba ni lini Mheshimiwa Waziri ataweka utaratibu wa kawaida? Mtu wa kawaida bati 10 au tano, *cement,* mafuta ya kula, sukari

wanapataje kutoka Kenya kuliko wale ambao wananunua kwa *bulk procurement?* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria bidhaa yeyote inayotoka nje ya nchi hata kama ni kalamu moja inapaswa kufuata utaratibu. Kwa hiyo anachokisema Mheshimiwa Mbunge anasemea kwamba kama mtu wa kawaida akiwa na bati 15 au 20. Kwa mujibu wa utaratibu, bidhaa yoyote inayotoka nje inatakiwa ifuate utaratibu wa kuvuka mpaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachoweza tu kufanya sasa hivi tunaongea na wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuangalia si tu kwa mpaka wa mikonge na maeneo mengine kuangalia utaratibu wa kuwarahisishia wananchi ambao wanatoka maeneo ya mbali zaidi na hicho ndiyo ambacho tunafanyia tathimini. Kwa sababu yako maeneo yale nilishamsikia ndugu yangu wa Ngorongoro, nimemsikia ndugu yangu wa Kakonko na mipaka mingine mingi Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkiongelea. Kwa hiyo tunatafuta jawabu la moja kwa moja kwa wananchi ambao wako mbali sana na mpaka na bidhaa walizobeba siyo nyingi, lakini kwa Sheria ilivyo sasa hivi bidhaa yoyote inatakiwa ipite mpaka ulio rasmi na iweze kuwa *cleared* na *customs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kushauriana na wenzetu Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao *coverage* yao iko kubwa kuliko ofisi zetu za forodha ili tuweze kuona namna ambavyo tunaweza tukawarahisishia wananchi wa mipakani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Waziri mwaka 2021, ulifika Jimboni kwetu Momba ukafanya ziara, ukaangalia pale mahali

tulikuwa tunapendekeza kupata Kituo cha Forodha Chipumpu, Kata ya Kapele. Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba wenzetu wa Zambia pia wametembelea upande ule wameona panafaa. Swali letu; je, mmefikia wapi mpaka sasa ili tuweze kupata hicho Kituo cha Forodha kipya ambacho kina maslahi mapana sana kwa Taifa letu lakini na kwa mapato ndani ya Halmashauri ya Jimbo la Momba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilipita katika eneo lile nilishaliona na tathmini hiyo inaendelea. Kupitia vikao vya pamoja vya ujirani mwema ambavyo ni *high-level* ambavyo vilihusisha viongozi wetu Wakuu wa Nchi ya Tanzania pamoja na Zambia, maelekezo yaliyotolewa ni tufanyie kazi vituo hivyo vyote ili tuweze kupunguza *congestion* ambayo inatokea pale Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hilo ni moja ya jambo ambalo litaendelea kufanyiwa kazi pamoja na kule Kalambo. Kwa hiyo tathimini zitakapokamilika Mheshimiwa Mbunge tutakujulisha na kazi zitaendelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 20 Desemba, 2016, Serikali ilisaini Mkataba na Kampuni ya *Motor Van* kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Forodha cha Nyakanazi kwa thamani ya shilingi bilioni 25. Ujenzi ulianza lakini baadaye ukasimama na Kituo hicho kimetelekezwa na miundombinu ile iliyokuwa imefanyika mwanzo yote inaharibika sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kauli ya Serikali, ni lini umaliziaji wa Kituo kile utafanyika ili pesa walipa kodi ambayo ilikuwa imewekezwa pale iweze kukamilika na hatimaye thamani ile

ambayo tulitarajia kuipata watu wa Biharamulo tuipate kupitia kituo kile? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni la kiutawala na ni utekelezaji wa mradi ambao unafuata mtiririko wa fedha. Nimelipokea tutaongea na wenzetu wa Mamlaka ya Mapato pamoja na Wizara ya Fedha ili kuweza kuhakikisha kwamba fedha zinafuata mtiririko ili kuweza kukamilisha mradi uliotajwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, nimwite Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swali lake.

Na. 345

**Uhitaji wa Vitendea Kazi kwa Wakulima wa Tumbaku**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, upi mpango wa kuwasaidia wakulima wa tumbaku kupata vitendea kazi mapema na kupunguza bei vikiwemo *Jute Twine* na *Cotton Twine?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Hussein Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia 2020/2021 hadi 2023/2024 upatikanaji wa pembejeo za tumbaku umekua kwa kiwango kinachoridhisha.

Aidha, changamoto ya upatikanaji wa *Jute twine* na *Cotton Twine* umejitokeza katika msimu wa 2023/2024 ambapo pembejeo hizo zilichelewa na msingi wa ucheleweshwaji huo ni benki kuchelewa kutoa *letter of credit.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto hii, Serikali inaendelea kuhamasisha makampuni ya ndani yawekeze kwenye uzalishaji wa ndani wa kamba na magunia. Aidha, Serikali imeandaa utaratibu wa kutumia Bodi ya Tumbaku, Kampuni yetu ya Serikali ya *TFC* na Muungano wa Vyama Vikuu vya Ushirika – *TCJE* kuagiza pembejeo za misimu miwili miwili. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo za zao kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wakulima wa tumbaku nao wanapata mbolea ya ruzuku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wako wakulima wa tumbaku ambao waliuza tumbaku yao tangu kipindi cha kilimo mwaka 2021. Wameuza tumbaku yao mpaka leo hawajalipwa na wanawadai walionunua zaidi ya shilingi milioni 72. Je, Serikali inawasaidiaje wakulima wa tumbaku wa Urambo ambao jambo hili linawakwaza sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mama Samwel Sitta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya wakulima wa msimu wa 2019/2020 ambapo ni kama jumla ya dola milioni tano kwa Sekta

nzima. Nataka tu kumhakikishia cha kwanza Serikali imefutia hizi Kampuni zote ununuzi na ushiriki kwenye Sekta ya Tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; Serikali sasa hivi tuko kwenye hatua za mwisho kuwapeleka Mahakamani kwa ajili ya madai haya ya wakulima. Pia, tunawapeleka Mahakamani pamoja na Wakurugenzi *at a personal capacity* kwa sababu walikuwa ni *guarantor* kwenye biashara hii. Kwa hiyo nataka nimhakikishie kwamba Serikali imeendelea kuchukua hatua katika hili na mwaka uliofuata mpaka sasa Kampuni yoyote ambayo imekuwa ikicheleweshа malipo ya wakulima tumekuwa hatuiruhusu kuendelea kuwepo katika Sekta ya Tumbaku kwa hiyo tunaendelea kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie na ni wahakikishe wakulima wa tumbaku kwamba sasa hivi tumeamua kuwapeleka mahakamani hawa wafanyabiashara na tutachukua hatua ili tuweze ku-*recover* fedha za wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ruzuku nataka tu niwahakikishie wakulima wa tumbaku. Katika bajeti yetu mliyotupitishia Waheshimiwa Wabunge mwaka huu, zao la tumbaku tumeliweka kuwa moja ya zao ambalo tunalipatia ruzuku katika uzalishaji kuanzia mwaka ujao wa fedha. Kwa sababu mwaka huu wakulima wa tumbaku wamepata tatizo la mvua nyingi, uzalishaji kwa maana ya *quantity* haijaathirika lakini ubora wa tumbaku kidogo umeshuka kwa sababu ya mvua nyingi. Serikali imeamua kwamba zao la tumbaku litakuwa sehemu ya *subsidy scheme* kwenye *NPK* 10-18-24 yenye thamani ya shilingi bilioni 13 ili kuweza kushusha gharama zao za uzalishaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa bei za zao la tumbaku mwaka huu zinaonekana ziko chini sana baada ya zao la tumbaku kukumbwa na tatizo la mvua nyingi. Serikali ina

mkakati gani wa kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji ambazo zimewalazimu mwaka huu watumie pembejeo mara mbili ya kile kiwango kinachotakiwa, Serikali wanatusaidiaje wakulima wa tumbaku?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani narudia tena jibu nililojibu kwenye swali la Mheshimiwa Margaret Sitta. Ni kwamba baada ya kuona hali ya mvua na gharama za uzalishaji na wakulima wametumia pembejeo zaidi ya mara moja au mara mbili mwaka huu ili kulinda zao la tumbaku. Serikali itatoa ruzuku ya shilingi bilioni 13 kwenye gharama za uzalishaji kwa wakulima wa tumbaku katika mwaka huu wa fedha ambao tunaendelea nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza kukusanya takwimu kupitia Vyama vyao vya Ushirika na Bodi ya Tumbaku ili kuweza kuwapunguzia gharama, kwa sababu tusipofanya hivyo wanaweza wakapata hasara na kuwavunja moyo kwa sababu sasa hivi kwa jitihada walizofanya wakulima Tanzania imekua ni nchi ya pili ya uzalishaji wa tumbaku Afrika kutoka nchi ya tano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali la nyongeza, nilikuona na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia soko la uhakika wakulima wa mazao ya viungo katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ishengoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; mazao ya *spice* yalikuwa hayajawekwa katika utaratibu mzuri na kuya-*categorize* katika eneo

gani la mazao. Serikali ilichukua hatua ya kuyaweka katika mazao mbayo yanatazamwa kama ni mazao ya *horticulture;* kwa hiyo hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Serikali imechukua hatua kwa ajili ya kuhakikisha tunapata ithibati ya Kimataifa ili mazao yetu yaweze kufunguliwa katika masoko mbalimbali. Nataka niwape taarifa kwamba sasa hivi mazao yetu ya viungo yamepata ithibati ya kuwa miongoni mwa mazao ambayo ni *organic* katika Soko la Dunia na yameanza kutoka kwenda maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, kama Serikali ili kuweza kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga wa mazao ya viungo. Serikali imechukua hatua ya kukigeuza Kituo chetu cha Utafiti cha Tanga kuwa *Center of Excellency* kwa ajili ya *spice*. Kwa hiyo na yenyewe nayo tumeyaweka katika ramani kama mazao muhimu ya *export* na tunaendelea kufanya jitihada. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nimwite Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 346

**Kiwanda cha Kuchakata Samaki katika Ukanda wa Bahari ya Hindi**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza: -

Je, nini mkakati wa Serikali kujenga Kiwanda cha Kuchakata Samaki katika Ukanda wa Bahari ya Hindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Alexander Mnyeti.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi *(AFDP)* chini ya mfuko wa *IFAD* inaendelea kuliwezesha Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki katika eneo la Kilwa Masoko. Ambapo, eneo la ujenzi wa kiwanda hicho lina ukubwa wa ekari 8.5. Aidha, mpaka sasa taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu imewasilishwa *TAFICO* kwa ajili ya kufanyiwa mapitio na inategemewa kukamilika mwisho wa mwezi Mei, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Januari, 2022 Kampuni ya *Albacora Group* kutoka nchini Hispania inayomiliki Meli ya *FV Pacific Star* inayopeperusha Bendera ya Tanzania iliingia makubaliano na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu *(DSFA)* ya kujenga kiwanda cha kuchakata samaki katika eneo la Kijiji cha Mwambani kilichopo Halmashauri ya jiji la Tanga. Aidha, hatua inayofuata kwa sasa katika eneo hilo ni kufanya tathimini ya athari za kimazingira itakayowezesha kuanza kwa ujenzi wa kiwanda hicho. Vilevile, Serikali inaendelea kuwekeza, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuboresha miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Ukanda wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa niaba ya Mheshimiwa Ulenge, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Mkoa wa Tanga umezungukwa na bahari, pamoja na mipango mizuri ya Serikali; je, Serikali haioni haja sasa ya kutoa mafunzo kwa wavuvi wa Mkoa wa Tanga kupitia Chuo cha

*VETA* cha Tanga Mjini na Mkinga kama vile walivyofanya wenzao wa Chato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam umezungukwa na Bahari ya Hindi sehemu za kuanzia Jimbo la Kawe mpaka kule Jimbo la Kigamboni limezungukwa na Bahari ya Hindi lakini sioni kama kuna mpango wowote wa kujenga kiwanda cha kuchakata mazao ya samaki. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga Kiwanda cha Kuchakata Samaki katika Mkoa wa Dar es Salaam? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la kwanza kwamba kutoa mafunzo kwa wavuvi katika Mkoa wa Tanga. Kwanza Wizara tayari imeshaanza kutoa mafunzo kwa wavuvi katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa hivyo tuko tayari pia kuendelea kutoa mafunzo katika Mkoa wa Tanga na kama *specific* Mheshimiwa Mbunge anajua kuna wavuvi wanahitaji mafunzo pia tuko tayari kuwapa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshaendelea kutoa mafunzo katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na maeneo mbalimbali na sasa tuko tayari kutoa mafunzo katika Mkoa wa Tanga kwa wavuvi wanaozunguka kwenye Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa kujenga viwanda pembezoni. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba mwambao wa Bahari ya Hindi Serikali tayari ina mpango wa kujenga kiwanda kule Tanga kupitia wawekezaji. Pia, wale maeneo ya Dar es Salaam tuko tayari kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya bahari. Kwa mfano kule *TAFICO* tunafufua hilo Shirika letu la *TAFICO* ambalo litakuwa na uwezo wa kuchakata mazao yetu ya baharini kwa ajili ya kuyaongeza uthamani, kuongeza ubora na kuyafanya kuwa na thamani katika mazao yetu yote ya baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kujipanga kuhakikisha kwamba tunaongeza viwanda lakini pia tunahamasisha wawekezaji mbalimbali kupitia maeneo mbalimbali ambao wako tayari kuwekeza katika eneo hilo pia tunahamasisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Mbunge kama ana nafasi hiyo tunamwomba pia na yeye tushirikiane kwa pamoja kuhamasisha wawekezaji wa mazao hayo ili tuweze kuongeza viwanda vya samaki. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Ziwa Nyasa ni Ziwa kubwa na lina samaki zaidi ya aina 10; je, hamuoni umuhimu sasa Serikali ikajenga kiwanda cha kuchakata samaki katika Ziwa lile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Nyasa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Serikali tunaendelea kuhamasisha wawekezaji mbalimbali. Kimsingi Serikali haiwezi kujenga viwanda kila sehemu ndiyo maana Serikali inazidi kuhamasisha wawekezaji mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali kuja kuwekeza katika maeneo haya. Kwa hiyo nimhakikishie Mbunge kwamba tutalifanyia kazi, tutatafuta wawekezaji kuja kuwekeza katika eneo hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, kwa kifupi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kwa kuwa Serikali imeanzisha programu ya kugawa boti na vizimba ambavyo vitapelekea uzalishaji mkubwa sana wa samaki na kwa kuwa Mkoa wa Mara tulikuwa na viwanda vitano vya kuchakata samaki na kwa sasa

vimekufa. Nataka nijue ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inafufua viwanda vile ili sasa hayo mazao ya samaki ambayo yanavuliwa kutokana na vizimba na boti ambazo mmeanzisha yaweze kupata sehemu ya kuchakatwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba viwanda vilivyokuwa vikizunguka maeneo ya Kanda ya Ziwa vingi vimekufa na vimekufa kwa sababu hakuna mazao yanayoweza kuchakatwa kwenye viwanda hivyo. Kwa hiyo mkakati wa kwanza wa Serikali kama tulivyosema hapo jana kwamba tunahamasisha wavuvi wajikite kwenye ufugaji wa kisasa ambao ni ufugaji wa vizimba. Ufugaji huu wa vizimba *production* yake itakapoanza *automatic* viwanda vitarudi vyenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukweli ni kwamba viwanda vimekufa baada ya kukosa *material,* sasa *raw material* zikishapatikana *automatic* viwanda hivyo vitarudi. Kwa hiyo nimhakikishie Mbunge kwamba tutakapoanza kuzalisha wale samaki kupitia vile vizimba, viwanda lazima vifufuliwe, vifufuke ili kuweza kuchakata mazao hayo ya samaki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Uchukuzi, nimwite sasa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 347

**Kudhibiti Mabasi Kukwepa Kuingia Stendi**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** auliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti mabasi yanayokwepa kuingia stendi na kushusha abiria barabarani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabasi yote ya masafa marefu hupangiwa ratiba na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)* ambazo huonyesha stendi za kupakia na kushushia abiria pamoja na muda wa kusimama kwenye stendi hizo. Aidha, mabasi ya masafa marefu yamepangiwa kusimama katika stendi moja tu kwa kila Mkoa isipokuwa pale ambapo basi hilo lina abiria anayeshuka katika stendi ya wilaya. Utaratibu huo umepangwa ili kuondoa usumbufu na ucheleweshaji wa abiria wa masafa marefu kwa kuwalazimisha kuingia kwenye stendi hata kama hawana abiria wa kupanda au kushuka. Hivyo Basi hailazimiki kuingia katika stendi ya Wilaya iwapo hakuna abiria wanaoshuka au kupanda basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madereva wanaokaidi kuingia stendi za mikoa na kushushia abiria nje ya stendi hususan barabarani, madereva hao wanakiuka maelekezo ya kifungu cha 50(1) cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 kinachomzuia mtu yeyote kuegesha au kusimamisha gari barabarani bila kujali watumiaji wengine wa barabara, hivyo wanavunja sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa bado kuna ukiukwaji wa utaratibu huu na kwamba bado wananchi wanaosafiri kwa kutumia mabasi ya mbali wanaendelea kupata usumbufu mkubwa barabarani, swali la kwanza; je, ni lini Serikali itaweka vifaa mtandao vya kidijitali kwenye stesheni zote ili kuhakikisha kwamba jambo hili linadhibitiwa kijumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, ni lini Serikali itaweka ripoti walau ya mwezi ya kuonesha waliohalifu amri hii na faini au adhabu walizopata ili kuwa fundisho kwa wengine?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi. Magari na mabasi makubwa hayafungwi wala kulazimishwa kushusha abiria au kusimama kwenye stendi za wilaya isipokuwa za mkoa. Kwa maana ya stendi za mkoa yale ambayo hayasimami na kwa maana ya hoja ya Mheshimiwa Mbunge, kwamba tuweke mfumo wa kidijitali, tayari Serikali imeshaanza na hivi ninavyozungumza tumeshaanza majaribio katika stendi mbili. Stendi ya Nanenane Jijini Dodoma pamoja na Stendi ya Magufuli Jijini Dar es Salaam. Tunataka tufike wapi? Tunataka tufike mahali msafiri wa basi awe anaona kwenye *screen* kama inavyokuwa kwenye *airport,* kwamba basi langu lipo wapi, litafika saa ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la pili, kwamba ni lini tutaweka ripoti za wahalifu na faini tulizowapiga hadharani. Kwa sasa Serikali haijaanza mchakato huo au mfumo huo. Tutapokea kama ushauri, tuchakate na kupima kama je, tuko tayari kwa sasa kuanza kuainisha wahalifu wote kwenye nchi yetu, kwamba wamekosa wapi na wamepigwa faini kiasi gani. Tukiona ina tija tutaanza kutekeleza pia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Maji, nimwite sasa Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini ili aulize swali lake.

Na. 348

**Tatizo la Maji – Wilaya ya Nkasi**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza changamoto ya maji Wilaya ya Nkasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi ina jumla ya vijiji 90, ambapo kati ya hivyo vijiji 66 vinapata huduma ya majisafi. Katika kuboresha huduma ya maji wilayani humo Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi minne inayohudumia Vijiji vya Lyazumbi, Kacheche, Masolo pamoja na Itindi. Aidha, utekelezaji wa miradi mitatu itakayohudumia Vijiji vya Korongwe, Isale na Matala inaendelea, ambapo inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kunufaisha wananchi wapatao 52,192 wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepanga kutekeleza miradi ya maji itakayonufaisha Vijiji vya Ninde, Kipili, Kalila, Mkombe, Mpenge, Mandakerenge, Bumanda, Isaba Kazovu, Utinta, Uhuru, Kasanga, Kisambala, Msamba pamoja na Izinga. Pia, mwezi Juni, 2024 washirika wa maendeleo *USAID* watatekeleza miradi itakayonufaisha vijiji saba vya Wampembe, Kizumbi, Katenge, Lyapinda, Ng'anga, Mwinza na Kasapa; wakati vijiji vinne vya Mbwendi, Kalundi, Lyele na Ng'undwe vitachimbiwa visima na kujengewa miundombinu kupitia programu ya visima 900. Kukamilika kwa miradi hiyo, kutawezesha kuboresha huduma ya maji Wilayani Nkasi kutoka wastani wa 50.3% ya sasa na kufikia wastani wa 87.1% ifikapo Juni, 2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimepokea majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika mwaka wa fedha ambao tunaumaliza mwezi ujao, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kujenga

Mradi wa Mji wa Namanyere wenye gharama ya bilioni 6.75. Mpaka sasa hapa ninapozungumza bado mwezi mmoja tu na wamepeleka milioni 950. Je, ni lini watapeleka fedha iliyobaki kwa muda huu uliobakia na mkandarasi aende *site* kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri hapa kwamba upatikanaji wa maji ni 50%, lakini upotevu wa maji ni 47%. Je, Serikali hawaoni kwamba kuna haja sasa ya kupeleka fedha haraka ili tuanze ukarabati, kwa sababu hata kwenye hicho kiasi kidogo kinapotea?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, anafanya kazi kubwa sana kwa wananchi wake wa Nkasi Kaskazini na kwa kweli anaendelea kushirikiana vizuri sana na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba anashiriki katika utekelezaji wa miradi inayopatikana katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba tuna mradi wa bilioni 6.75 na mwisho wa mwezi huu Serikali tunakwenda kusaini mkataba na mkandarasi ili aweze kuingia. Hizo fedha ambazo zilitengwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024 ni fedha ambazo ni kwa ajili ya malipo ya awali. Kwa hiyo, mkandarasi akishasaini mkataba basi fedha hizo atalipwa na ataingia *site* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu upotevu wa maji. Ni kweli kabisa, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, kwamba upotevu ni 47% ilhali upatikanaji wa maji ni 52.9%. Kikubwa ambacho naweza kukisema hapa ni kwamba, upotevu wa maji unaweza ukatokana na miundombinu, usimamizi

na teknolojia tunayoitumia. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa maelekezo. Tunaondoka kwenye *mechanical meters* tunakwenda kwenye *smart prepaid water meters.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni katika kuhakikisha pia kuwa tuna-*reduce* upotevu wa maji na vile vile kuhakikisha kwamba tunapeleka. Mwezi Aprili Mheshimiwa Mbunge tumempelekea shilingi milioni 400 kwa ajili ya ukarabati wa Mji wa Namanyere. Hii ni katika kuhakikisha kwamba ule uharibifu na upotevu ambao ulikuwa unatokea, basi wananchi waweze kurejeshewa huduma na waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Awack kwa kifupi sana. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuwasaidia wananchi wa Mji wa Karatu, ambao wamepata changamoto ya kujaa bwawa pale Mji wa Karatu na pampu mbili kushindwa kufanya kazi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali daima imekuwa na utaratibu wa kuchukua hatua za dharura pale ambapo panatokea matukio ya dharura. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, naomba nilipokee na tuwaagize wataalam wetu wakafanye tathmini ili tuone kwamba tunatakiwa kuchukua hatua gani ili kutatua changamoto hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza, kwa kifupi tafadhali.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dodoma bado linakumbwa na adha kubwa ya upatikanaji wa maji. Pamoja na jitihada kubwa za *DUWASA* kuchimba visima Nzuguni lakini maji bado ni shida kwa wakazi wa Dodoma. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuiongezea fedha *DUWASA* ili iweze kukidhi mahitaji ya upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Jiji la Dodoma? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua na Serikali inatambua changamoto ya maji. Tunatambua umuhimu wa kuwa na maji ya kutosha kwa wakazi wa Jiji la Dodoma kwa sababu ndiyo Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mkakati wa muda mfupi wa kuchimba visima vya Nzuguni pamoja na Nala vile vile tuna mpango wa kati na muda mrefu. Juzi hapa tumetangaza *tender* ya Bwawa la Farkwa ambapo tunaamini kwamba Bwawa hilo likishapata mkandarasi na kuanza kujengwa litatatua. Huo ni mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imejipanga kuhakikisha kwamba *DUWASA* inaongezewa nguvu ili iweze kutatua changamoto ambazo zinajitokeza kila mara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay, kwa kifupi tafadhali.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Bajeti ya mwaka huu tulipangiwa kuchimbwa visima Mbulu Vijijini. Je, ni lini watachimba visima hivi ili wananchi wapate maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasikia vizuri.

**MWENYEKITI:** Anasema hajasikia vizuri.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu ambayo inakwisha mwezi ujao kuna visima vitano tulikuwa tuchimbe Mbulu Vijijini. Je, ni lini tunachimba visima hivi ili wananchi wapate maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpomgeze Mheshimiwa Flatei Massay kwa kazi nzuri anayoifanya. Serikali na Sekta ya Maji tuna maelekezo mahsusi kutoka kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kupitia miradi yote ya 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024 ili kuhakikisha kwamba kule ambako tumeshafanya mkataba na wananchi kwamba tunawapelekea maji basi miradi hiyo tukaikamilishe kwa wakati ili Watanzania wapate maji safi na salama. Ahsante

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nimwite sasa Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, aulize swali lake.

Na. 349

**Mkakati wa Kupanga Matumizi Bora ya Ardhi**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanga matumizi bora ya ardhi kutokana na kasi ya ongezeko la watu nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Pinda.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali hili naomba kwanza niombe radhi, kwamba Mheshimiwa aliyeuliza swali ni

Mbunge wa Mbarali na si Mbunge wa Viti Maalum. Naomba hiyo iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa, jumla ya vijiji 4,024 kati ya vijiji 12,318 vilivyopo nchini vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi. Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa vijiji vyote nchini vinaandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi. Miongoni mwa mikakati inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na kuzihimiza mamlaka za upangaji kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji, kuendelea kutenga bajeti kwa Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, kuandaa, kuwezesha na kusimamia upangaji wa matumizi ya ardhi, kuhamasisha wadau kuchangia upangaji wa matumizi ya ardhi na kubuni miradi ambayo inawezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilibuni na kutekeleza Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki *(LTIP),* ambao umelenga kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi miradi 1,667 katika kipindi cha miaka mitano. Aidha, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya shilingi 5,041,232,000 kwa ajili ya kuiwezesha Tume kuendelea kupanga matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Mbarali na maeneo mengine ya nchi kuwa azma ya Serikali ni kupanga miji na vijiji vyote ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya ardhi linalochangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la watu. Niendelee kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge, kuhakikisha kwamba halmashauri zao zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kupanga miji na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa muda mrefu tumeshuhudia ndani ya Bunge lako Bajeti ya Wizara yetu ya Ardhi ikiendelea kupanga fedha kwa kiasi kidogo kwenye suala la upimaji wa ardhi, kitu ambacho kimesababisha uotaji holela wa miji, lakini vile vile 25% tu ya Taifa letu ndiyo iliyopimwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kibajeti wa kuongeza fedha katika bajeti inayokuja kwa ajili ya kupima ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tumeona kwamba Sekta hii ya Ardhi ni sekta kubwa na yenye changamoto nyingi. Sasa mnaonaje mkaanzisha mamlaka maalum ya kusimamia sekta hii muhimu nchini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali lake la kwanza la nyongeza, kwamba tumekuwa tukiwekewa kiasi kidogo cha fedha katika mpango wa kupima miji yetu. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba Wizara ina mikakati mbalimbali. Kwa sasa imeanzisha mazungumzo na Wizara ya Fedha ili kuona uwezekano wa kupata fedha za ziada kwa ajili ya kukamilisha miradi hii ambayo kimsingi itakapokuwa imekamilika itatupunguzia migogoro mingi ya ardhi ambayo inaendelea hapa nchini kwa sababu ya kugongana kutokana na kutopimwa kwa miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu kuwa na mamlaka maalum inayosimamia ardhi; ni kweli, ni mpango wa Wizara na tayari tumeshaanza mchakato. Tunaanzisha Kamisheni ya Ardhi ambayo itakwenda kufanya kazi kama zilivyo mamlaka nyingine kama vile Idara ya Maji na *TARURA*. Hawa wanafanya kazi *separate* ingawa wanahudumia wananchi kule kule vijijini. Kwa hiyo hata sisi tutakuwa na Kamisheni ya Ardhi ambayo itakuwa na Kamishna Mkuu na mtiririko wake utakwenda mpaka vijijini huko ambako kutakuwa na wawakilishi wa idara yetu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunakwenda Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Namwita sasa Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, aulize swali lake.

Na. 350

**Tatizo la Mtandao wa Simu Tabora Mjini**

**EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la mtandao wa simu kwenye baadhi ya maeneo katika Jimbo la Tabora Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Nape Nnauye.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imejenga minara ya mawasiliano ya simu saba katika Jimbo la Tabora Mjini. Minara hiyo ilijengwa na *Vodacom* na *Halotel* katika Kata za Itetemia, Kabila, Kalunde, Ndevelwa, Tumbi na Uyui kupitia awamu mbalimbali za miradi iliyotekelezwa kati ya 2017 na 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Ifucha na Kiloleni zitajengewa minara na Kampuni ya Honora *(Tigo)*. Kwa upande wa Kata ya Kakola, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umeingia mkataba na *TTCL* kwa ajili ya kujenga mnara katika kata hiyo. Utekelezaji wa mradi huu ni wa miezi 24 kuanzia tarehe 13 Mei, 2023, mkataba uliposainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hii, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itafanya tathmini ya hali ya mawasiliano katika Jimbo la Tabora Mjini ili kubaini mahitaji halisi ya mawasiliano ya simu na kuchukua hatua stahiki kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka, maswali ya nyongeza kama yapo?

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kwa kuipongeza Serikali, hasa kwa kuboresha mitandao ya mawasiliano katika Jimbo langu la Tabora Mjini. Pamoja na hayo nina swali moja tu la nyongeza. Kata ya Malolo, maeneo ya wafugaji, maeneo ya Usenge, pia na Kata ya Ikomwa, pamoja na Kata ya Ntalikwa bado kuna matatizo makubwa ya mawasiliano, sijui Serikali…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Waheshimiwa Wabunge hivyo ndivyo jina linavyoitwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa ya mawasiliano.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mawasiliano katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza, Kata ya Malolo eneo la Usenge, Kata ya Ikomwa na Ntalikwa kuna matatizo ya

mawasiliano. Nawaagiza *TCRA* na *UCSAF* baada ya bajeti yetu kupita kesho waende maeneo hayo, wafanye tathmini, walete ripoti ili tufanye uamuzi wa kupeleka mawasiliano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Maeneo makubwa ya Jimbo langu la Mtambwe, Pemba yana shida ya mtandao wa simu. Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hili?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imejenga minara 48 katika Visiwa vya Pemba na Unguja kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata mawasiliano. Tumepeleka mpaka kwenye visiwa ambako wananchi wanafanya shughuli zao za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea pia ombi la Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama kuna maeneo ambayo bado yana tatizo tutakuja kufanya tathmini baada ya hii miradi ya minara 48. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunayo minara mingine, tutaiongeza kwenye maeneo yale ambayo bado yana changamoto ya mawasiliano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Nadhani unaendelea na majibu.

Nimwite Mheshimiwa Kavejuru Felix, Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 351

**Mikakati ya Kukomesha Wizi Mtandaoni**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukomesha wizi wa mtandaoni?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imechukua hatua kadhaa kwa ajili ya kuweka mazingira salama kwa wananchi hususan kwenye mitandao. Mwaka 2015 Serikali ilitunga Sheria ya Makosa ya Mitandao na Sheria ya Miamala ya Kielektroniki kwa lengo la kutambua miamala inayofanyika kimtandao lakini pia kutambua kisheria makosa yanayofanyika kwenye mitandao ili kuweza kuchukua hatua stahiki yanapobainika makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga mazingira salama ya kisheria, pia Serikali imetunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 ambayo lengo kuu ni kuweka utaratibu wa kuhakikisha wakusanya taarifa wote wanafuata misingi ya kulinda taarifa za mwananchi. Aidha, Serikali ilianzisha Kitengo cha Uhalifu wa Mitandao Nchini chini ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa makosa ya mitandao, ikiwemo wizi wa aina yoyote kwenye mtandao na kuandaa majalada ya kufungulia mashtaka kwa kusaidiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, Serikali kwa kushirikiana na watoa huduma wa simu za mkononi imeanzisha mfumo kupitia namba '15040' ya kupokea na kuzifungia namba ambazo zimeripotiwa na kuthibitika kutuma ujumbe au kupiga simu za utapeli. Baada ya kuthibitisha namba hizo kufanya vitendo hivyo, namba husika hufungiwa, kitambulisho cha *NIDA* kilichotumiwa

kusajili namba husika kufungiwa kusajili na kifaa kilichotumika (simu) pia kufungiwa ili kisifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea kuongeza jitihada za kuelimisha umma namna nzuri ya kutumia TEHAMA ili kuendelea kudhibiti matukio ya utapeli na wizi wa kimtandao kupitia simu za mkononi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felix Kavejuru, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mheshimiwa Waziri, bado wizi mtandaoni unaendelea, ni nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa laini zote zilisajiliwa na *TCRA* na polisi kisheria inaruhusiwa kwenda kuchukua taarifa zozote za laini zilizotumika katika uhalifu kule *TCRA*, ni nini kinachofanya watu hao wasikamatwe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kazi ya kuwakamata wahalifu ni kazi ya Jeshi la Polisi. *TCRA* tunawezesha Jeshi la Polisi kupata ushahidi wa wahalifu, lakini kazi ya kufungia laini zilizofanya utapeli kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi, ni kazi ya *TCRA* tukishirikiana na watoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kwamba uhalifu wa mtandanoni unaendelea kupungua kwa takwimu zifuatazo:-

Mheshimwa Mwenyekiti, Septemba 2023, tulikuwa na laini za uhalifu 23,328. Disemba mwaka huo huo 2023 zikafikia 21,000; Machi mwaka huu 2024 zimefikia 17,318. Tulipoanza kufanya uhakiki tulikuwa na laini 9,045,602, zilikuwa hazijahakikiwa. Tulipozihakiki tukafunga laini 900,746. Maana yake ni nini; maana yake ni

kwamba, zoezi la kufanya mtandao uendelee kuwa salama linaendelea. Wito wetu kama Serikali, tunawaomba wananchi inapotokea tatizo wafuate utaratibu; moja, kwa kutumia namba 14040 kuiripoti laini iliyofanya uhalifu na tunaifungia laini ya simu, tunafungia kitambulisho cha *NIDA* kilichohusika na kusajili hiyo laini na tunakifungia kifaa kilichotumika, tukishirikiana kwa pamoja tutaendelea kupunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, Jeshi la Polisi limeendelea kufanya kazi nzuri ya kuwakamata hawa wahalifu, wanapelekwa Mahakamani na baadhi yao tumeanza kuwatangaza hadharani na tunao mfano pale Dar es Salaam. Walikamatwa wahalifu, mwanzoni kulikuwa na suala la haki za binadamu, kwamba tusubiri mpaka twende mahakamani tufanye hivi. Tukasema nadhani uhalifu unaendelea sana, tukiwakama tuseme tumemkamata ni mtuhumiwa, akienda kushinda mbele ya safari basi ashinde mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, usalama mtandaoni unaendelea kuimarishwa kwa sababu tunakwenda kwenye uchumi wa kidijiti, lazima paendelee kuwa salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Jambo la dharura ...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Naomba watu wanaoomba miongozo wakae chini kwanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali kwa kweli umekwisha na tumeongeza kidogo zaidi ya ule muda wa kawaida. Kwa hiyo, tunaendelea na kuna swali namba 343 ambalo lilikuwa la Mheshimiwa Shally Raymond, liliulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Priscus Tarimo, akasema kwamba hajaridhika na majibu yaliyojibiwa.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni zetu hapa, Mbunge ambaye siyo muuliza swali la msingi akipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na iwapo hataridhika na majibu ya Serikali, anaweza kuleta swali la msingi kwa ajili ya swali hilo. Kwa hiyo, tunamshauri Mheshimiwa Shally Raymond alilete hilo swali tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye orodha ya wageni tuna wageni wengi katika Bunge letu leo; nianze na wageni ambao wamekaa Jukwaa la Spika. Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu Zahor Matelephone, mfanyabiashara wa simu kutoka Kariakoo Jijini Dr es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni kwenye kundi la pili ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Waziri wetu wa Mambo ya Ndani ya Nchi na nitawataja. Naanza na Ndugu Ally Senga Gugu ambaye ni Katibu Mkuu; Dkt. Maduhu Kazi, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Camillus Wambura, *Inspector General* wa Polisi; tuna Mzee R. Nyamka, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza; Ndugu John Masunga, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Dkt. Anna Makakala, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji; ahsanteni sana, tunawakaribisha sana Bungeni. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunao pia Deusdedit Buberwa, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; *CPA*. Moremi A. Marwa, Afisa Mtendaji Mkuu Shirika la Magereza; Ndugu Wanja Mtawazo, Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizarani. *(Makofi)*

Tunao vile vile *Bishop*. Dkt. Alex Malasusa, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (K.K.K.T); Dkt. Prosper Mbowe Kiramuu, huyu ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi; Sheikh Dkt. Abubakar Zuberi Bin Ally, huyu ni Shekh Mkuu na Mufti wa Tanzania; Askofu Dkt. Gervas John Nyaisonga, huyu ni Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania; Ask. Dkt. Barnabas Mtokambali, huyu ni Mwenyekiti wa Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania; Ndugu Mahamoud Mussa Wadi, huyu ni Naibu Mufti Zanzibar. Sheikh Hassan Othman Ngwali, huyu ni Kadhi

Mkuu Zanzibar; Sheikh Dkt. Alhad Mussa, huyu ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania; Ndugu Boniphace Mwamposa, huyu ni Kiongozi Mkuu wa Kanisa la Inuka na Uangaze; na Sheikh Tahir Mahmoud Chaudhry Amir, huyu ni Mwenyekiti wa *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania*. Ahsanteni na Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Masauni ni Ndugu Thania Ali Abdullah, huyu ni mke wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, karibu sana, karibu sana shemeji yetu, wengine wifi yetu. *(Makofi/Vigelegele)*

Wengine ni Ndugu Mohamed Yussuf Masauni, kaka wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani; na Ndugu Sharif Abdulkadir, Mkurugenzi wa Taasisi ya Alkhema. Karibuni sana kwenye Bunge letu, naona Bunge letu lina upako mkubwa sana leo hii. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Makamishna wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, *CP*. Hamad Khamis Hamad, Kamishna wa Polisi Kamisheni ya Polisi Zanzibar; *CP*. Charles Mkumbo, Kamishna wa Polisi Intelijensia ya Jinai; *CP*. Liberat Sabas, Kamishna wa Polisi Fedha na Lojistiki; *CP*. Awadhi Haji, Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo; *CP*. Faustine Shilogile, Kamishna wa Polisi Kamisheni ya Polisi Jamii; na *CP*. Ramadhani Kingai, Kamishna wa Polisi Kurugenzi ya Upelelezi ya Makosa ya Jinai. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao vilevile Jeremiah Katundu, Kaimu Kamishna Utawala na Rasilimali Watu, Jeshi la Magereza; Athmani Kitiku, Kaimu Kamishna wa Urekebu, Jeshi la Magereza; Chacha Jackson, Kaimu Kamishna wa Fedha na Mipango, Jeshi la Magereza; Mbaraka Semwanza, Kamishna wa Fedha na Utawala, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Hassan Ally Hassan, Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar; Jerald Kihinga, Kamishna wa Pasipoti na Uraia; Hamza Hussein Shabani, Kamishna wa Fedha na Utawala, Idara ya Uhamiaji; Novaita Mrosso, Kamishna wa Huduma za Sheria, Idara ya Uhamiaji; na Anjela Shija, Kaimu

Kamishna wa Vibali la *Visa*. Ahsanteni, karibuni sana Makamanda kwenye Ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi/Vigelegele)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni 13 wa Mheshimiwa Spika, hawa ni wanafunzi wa kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania *Campus* ya Mbeya, naona wako pale na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Daniel Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, wapiga kura wake kutoka Babati Vijiji, Mkoa wa Manyara. Wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Muharami Mkenge, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Bagamoyo Mkoa wa Pwani, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, ndugu yake kutoka Jiji la Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine ambao wameletwa na Mheshimiwa Agnes Marwa, hawa ni rafiki zake kutoka Tarime. Huyu ni Mbunge wa kwanza wa wanawake kuleta wageni kwa wingi hapa, karibu sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Juma Usonge, rafiki zake kutoka Mkoa wa Mara. Nimewaona pale. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Kavejuru Felix, huyu ni Mwalimu na Balozi wa Mazingira kutoka Mkoa wa Kigoma, karibu sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 10 wa Mheshimiwa Simon Songe, hawa ni Wachungaji kutoka Busega Mkoa wa Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 13, hawa ni wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, hawa ni viongozi wa CCM na viongozi wa dini kutoka kata za Geita Mjini, karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna wageni ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 60 na walimu nane wa shule ya Sekondari ya *Destiny* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 50 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Kikombo iliyoko Jijini Dodoma. Karibuni sana watoto wetu kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Abubakar Asenga, Inspekta wa Jeshi la Magereza kutoka Mkoa wa Morogoro, karibu sana, nahisi ni Mstaafu. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa, ah, hawa nadhani bado hawajaingia. Bado hawajaingia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa hayo ndiyo majina ya wageni ambao wako ndani ya Bunge letu, tunawakaribisha sana wageni wetu siku yetu ya leo.

Tunaendelea.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jambo la Dharura.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Naomba mliouliza miongozo kwanza tukae, tuanze na mmoja mmoja. Tuanze na Mheshimiwa Festo Sanga. *(Makofi)*

## JAMBO LA DHARURA

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 54 ambayo inazungumzia Jambo la Dharura na lenye umuhimu kwenye manufaa ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa nikiomba mwongozo wako. Jeshi la Polisi lilitangaza ajira tarehe 9 Mei, 2024. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwamba anaendelea kutoa fursa ya vijana wa Kitanzania na Watanzania kuajiriwa, lakini toka wametangaza hili tangazo tarehe 9 Mei, 2024 na kesho tarehe 16 Mei, 2024 ndiyo utakuwa mwisho wa ku-*submit* maombi, kwa maana ukisoma kipengele cha pili wanasema, "Utaratibu wa kutuma maombi ya kujiunga na Jeshi la Polisi, waombaji wote wanatakiwa waandike barua." Hicho ni kipengele namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele namba mbili wanasema waombaji wote wafanye maombi yao kupitia kwenye mfumo wa Ajira ya Polisi *(Tanzania Police Force Recruitment Portal)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye mfumo huu kwa kipindi hiki ambacho Afrika Mashariki na Serikali imepitia changamoto ya *internet,* kwa maana ya mtandao, vijana hawa wako nje wanahangaika jinsi gani ya ku-*access* hii *website,* ili waombe ajira hizo. Pili, ni mtandao huu licha ya kwamba, upo chini, *website* hii, kwa maana ya hii *portal* imezidiwa vijana wengi hawawezi kuwa na *access* kutokana na kwamba, *either* uwezo wa hii *portal* ni mdogo au ni jinsi gani ambavyo mfumo haufanyi kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, vijana wako *stranded* huko nje, wana-*pressure,* kesho ni tarehe 16. Taifa limepitia kwenye mtikisiko wa kukosa *internet* na Serikali hadi dakika hii haijatoa kauli yeyote kuhusu vijana hawa. Naomba Mwongozo wako kwa sababu, jambo hili lina maslahi makubwa kwa vijana wa Kitanzania na ikiwezekana nitatoa hoja, ili wezangu waweze kuniunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Sanga.

Waheshimiwa Wabunge tuelewane, amesimama kwa Kifungu cha 54 ambacho kinataka Bunge lisimamishe shughuli zake na kama hoja ni ya dharura, lakini Kiti ni lazima kijiridhishe udharura wa jambo hilo. Kwa hiyo, kabla sijaamua nadhani ni vizuri tukaipa Serikali nafasi, ili tujue kuna udharura au haupo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri husika, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani kwenye jambo hili, aweze kutoa maelezo kulingana na hoja iliyowekwa hapa mbele. Karibu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Seneta Sanga kwa jinsi ambavyo amekuwa mtetezi wa masuala ya msingi na hii hoja yake ni moja katika mambo ya msingi kwa kweli, lakini namthibitishia kwamba, kwa kuzingatia misingi hiyo hiyo kwa hoja yenyewe hata sisi Serikali tumeshaiona hii. Jana tulikaa na timu ya Wizara pamoja na Jeshi la Polisi tukakubaliana kwamba, tuongeze siku tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Sanga usiwe na wasiwasi, waambie vijana waendelee kuchangamkia fursa hii kwa siku tano zilizobakia. Wananafasi ya kuendelea kuomba, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru. Mheshimiwa Sanga nadhani umepata majibu.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata majibu ya Serikali kwenye jambo moja kwamba, wameongeza siku na ninaipongeza Serikali imefanya maamuzi hayo, lakini kuna changamoto ya *portal* yao. *Portal* yao imezidiwa, haina *access* hata kipindi ambacho *internet* inapatikana watu hawawezi ku-*access,* kuingia ndani. Sasa tunaiomba Serikali, kama inaweza ikaangalia namna nyingine iweze kuwasaidia vijana wawe na

*access* kwa sababu, unaweza ukaongeza siku tano na bado wasipate fursa ya kuingia kwenye huu mtandao kutokana na *portal* kuwa na uwezo mdogo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza uamuzi wa Wizara ya Mambo ya Ndani wa kuongeza siku ni jambo la kiungwana kwa sababu, tulikuwa tunapitia changamoto kubwa ya upatikanaji wa mtandao. Hivi tunavyoongea zaidi ya 80% ya mtandao umerudi katika hali yake na tunategemea leo, kufikia mchana, tutakuwa tupo katika mazingira mazuri. Kwa hiyo, nawaomba vijana waendelee ku-*apply*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Serikali sikivu, itaangalia hali itakavyokuwa. Sisi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani tutafanya tena tathmini tuone mtandao unavyofanya kazi, halafu tutashauriana na kuchukua hatua namna ya kusonga mbele pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nadhani kwa hoja ambazo Serikali imezitoa na maelezo aliyoyatoa, wameongeza siku tano na nadhani wanalifanyia kazi. Basi naomba mwendelee kulifanyia kazi jambo hilo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nina walioomba Mwongozo, siyo mmoja, haupo peke yako Mheshimiwa Waitara. Nakwenda kwa *list* yangu hapa kwa hiyo naomba ukae chini, Mheshimiwa Chiwelesa.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. *ENG*. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na mimi nimekusudia kusimama kwa Kanuni ya 54, naongelea hoja hiyo hiyo ya vijana, lakini kwa sababu, imejibiwa na Serikali ninaomba tu *commitment* ya Serikali kwenye hili. Unaposema siku tano *while* Serikali ina-*confess* kwamba mtandao umefikia 80% tu, siku tano tunazihesabu lini? Tutakapokuwa kwenye 100%, ndiyo tuanze kuhesabu siku tano au siku tano tunahesabu leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungependa kujua majibu ya kina ya Serikali, *if it is five days extension,* ianze pale ambapo Serikali ime-*confirm* kwamba, mtandao umepatikana. Kwa sababu, unaweza ukatoa siku tano leo ikabaki 80% mpaka kesho kutwa na siku tano zikaisha na hatuna muda wa kurudi hapa. Kwa hiyo, naomba tupate *clarification.* Kama *clarification* haitaniridhisha ninaomba nitoe hoja Bunge lako lijadili, ili tuishauri Serikali ni nini cha kufanya. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri, ulishatoa maelezo kwenye jambo hili. Waheshimiwa wabunge turidhike na maelezo kwamba ni siku tano ambazo zinatolewa, sasa swali ni kutoka lini?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siku tano zinaanza baada ya *deadline* ya mwanzo kukamilika na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwamba, sasa hivi mtandao upo 80% kwa hiyo, unafanya kazi. *Commitment* ya Serikali, kama alivyozungumza ni kwamba, kadiri siku zinavyoendelea mbele mtandao utaimarika, lakini hata hivyo tutakaa pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Habari tuone hali itakavyokwenda. Ikiwa hali itakuwa mbaya tunaweza kufikiria namna nyingine ya kufanya, lakini kwa sasa hivi kwa hali ilivyo tunadhani siku tano kuanzia *deadline* zinatosha kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo. Maelekezo ya Kiti ndiyo hayo, kadiri ya mlivyosema wenyewe kwamba, mmeomba siku tano na tunaomba tupate taarifa kadiri hali inavyokwenda.

Tunaendelea. Kulikuwa na Mheshimiwa Getere na yeye aliomba. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilikuwa ninataka kutoa taarifa kama hiyo, lakini kwa sababu Serikali imesema, nataka kuongezea tu. Kwani kuna haraka gani ya kutoongeza mwezi mzima huu, ili wanafunzi waweze kupata…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, nadhani tumeshatoa Mwongozo na Maelekezo ya Kiti kwenye suala hilo. Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea kulijadili.

Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, natumia Kanuni ya 76, naomba tu Mwongozo wa Kiti chako, wakati napata majibu ya Serikali kwa swali namba 344, lilisema utaratibu unaotumika kukusanya kodi kule Sirari, Isebania, umeleta madhara makubwa kwa vijana wetu na kuna mauaji. Nimesema, Jumamosi gari la *TRA* limemfukuza kijana mwenye bidhaa za plastiki na lilim-*push* yule kijana akaingia kwenye mtaro na amefariki dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia katika maeneo haya watu wamekuwa wanapigwa risasi. Sasa kama tunatoa taarifa za mauaji ya watu wetu, na ni vizuri tukisema watu wanauawa Tarime, tupewe uzito wa pekee kwa sababu, inaweza ikafikia mahali watu wakaanza kuchukua Sheria mkononi. Nadhani ingependeza sana Serikali ikatoa Kauli, je ni sahihi kutafuta kodi ya Serikali kwa njia ya damu? Kwamba, unakusanya kodi kwa kuuwa watu? Siyo mara moja, watu wetu wa *TRA* kule Sirari kwenye magari yao wana mipini ya majembe, wanawapiga vijana wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka Serikali itoe Kauli juu ya hili jambo, ili tuone wanachukua hatua. Wachukue kodi kiustaarabu na kama kuna mtu ana magendo akamatwe na achukuliwe hatua za kisheria bila ya kuleta madhara kwa watu wetu na kujenga chuki dhidi ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama pamoja na *TRA*. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mwongozo wako katika jambo hili. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, hapa Kiti hakina *document* wala maelezo yoyote ya kuweza ku-*verify* hilo jambo unalolisema. Kwa hiyo, nalipokea na tutarudi kwenu au kwako kwa wakati, kadri ya kanuni zinavyoturuhusu na ninakushauri, labda ungeleta swali la msingi ili uweze kupata majibu ya Serikali.

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tunaendelea na hatua ya pili. Namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa *Engineer* Masauni. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kujadili na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

Fedha ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha naomba hotuba yangu yote nitakayowasilisha ipokelewe na kutambuliwa kama Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu katika Bunge hili Tukufu. Natumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha nampongeza kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu vyema ikiwa ni pamoja na kusimamia amani, usalama, utulivu na mshikamo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na kuwashukuru viongozi wote wa kitaifa kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake pamoja na miongozo wanayonipa katika kuongoza Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Viongozi hao ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa uteuzi huo uliyofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 30 Agosti, Mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge ya Afrika kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa *IPU,* ni heshima kwa Taifa letu na wanawake wote duniani. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, pamoja na wewe na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusaidia kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu kwa

ushirikiano mnaoendelea kuutoa kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote. Aidha, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya NUU na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo na Wabunge wote Wajumbe wa Kamati hii ya NUU kwa ushirikiano ambao wanaendelea kutupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imechambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na kutoa ushauri uliosaidia kuboresha bajeti kwa Mwaka 2024/2025 na utendaji wa Wizara kwa ujumla. Kwa hakika najiona kuwa mwenye bahati kubwa sana kuwa sehemu ya kamati hii makini kabisa. Kwa mara nyingine namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kufanya uteuzi wa Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tarehe 31 Machi Mwaka 2024 alimteua Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia, tarehe 15 Machi, 2024 Mheshimiwa Rais alimteua ndugu Ally Senga Gugu kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nawapongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi hizo. Katika muda mfupi wakiwa katika dhamana za uongozi wao waliopewa wameonesha ushirikiano na umahiri mkubwa uliowezesha kuharakisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Jumanne Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na ndugu Kaspar Mmuya, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma kwa mchango wao mkubwa walioutoa ambao umesaidia kuweka misingi ya mafanikio ambayo Wizara tunaendelea kujivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza *Inspector General* wa Jeshi la Polisi *(IGP)* Camillus Wambura, Kamishna Jenerali wa

Magereza, Mzee Ramadhani Nyamka na Kamishna Jenerali wa Zima Moto, John William Masunga pamoja na Kamishna wa Uhamiaji Dkt. Anna Peter Makakala kwa kutunukiwa nishani ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 24 Aprili, 2024. Pia, nawapongeza maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama waliotunukiwa nishani hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais, Bunge, wanafamilia na wananchi kwa ujumla kwa misiba mikubwa iliyotokea hapa nchini ikiwemo msiba wa Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Alli Hassan Mwinyi, aliyefariki tarehe 29, Mwezi Februari, 2024. Aidha nchi yetu pia, ilipata msiba wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu Hayati Edward Lowassa, aliyefariki dunia tarehe 10 Februari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha Hayati Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, aliyefariki tarehe 01/07/2023 na kifo cha Hayati Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani, Zanzibar, aliyefariki tarehe 8 Aprili, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile natoa pole kwa ndugu na wananchi wote waliopoteza ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali ikiwemo mafuriko yaliyotokea katika baadhi ya maeneo nchini pamoja na maporomoko ya udongo yaliyotokea katika Wilaya ya Hanang, Mkoani Manyara na eneo la Gombe Wilaya ya Mbeya Mjini, Mkoa wa Mbeya. Vilevile, natoa pole kwa Askari wote waliopoteza maisha na walioumia wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa namana ya kipekee kabisa nawashukuru viongozi wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waheshimiwa Wabunge na wananchi mbalimbali kwa kunifariji katika kipindi cha maombolezo ya msiba wa baba yangu mzazi, Hayati Mzee Masauni Yussuf Masauni, aliyefariki dunia tarehe 23 Februari, Mwaka 2024.

Tunawaombea marehemu wote Mwenyezi Mungu azilaze roho zao pema peponi. Amini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Upandishwaji wa Vyeo. Kuanzia Julai, Mwaka 2023 hadi Aprili Mwaka 2024 Wizara imewapandisha vyeo jumla ya watumishi 9,397 katika ngazi mbalimbali za uongozi. Hali hiyo imeongeza morali ya utendaji kazi wa watumishi hao. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara itawapandisha vyeo jumla ya watumishi 26,876.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi nyingi sana na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa upandishaji huu wa kihistoria kabisa wa vyeo hivi kwa vyombo vya usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, kwa kuzingatia jinsia miongoni mwa aliowapandisha vyeo ni Manaibu Kamishna wa Polisi saba, ambao ni wanawake. Upandishwaji vyeo wa aina hii ni wa kwanza kutokea katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajira na Mafunzo kwa Askari na Watumishi Raia. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuipatia Wizara na vyombo vya usalama ajira, ili kuendelea kuimarisha usalama wa watu na mali zao. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imeajiri jumla ya watumishi 8,542. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 4,887.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Wizara, mafunzo ya kuwajenga uwezo yametolewa kwa Maafisa na Askari Watumishi, raia 11,167. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara imepanga kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi 10,640.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya shilingi trilioni 1.29. Hadi kufikia Mwezi Aprili, mwaka wa fedha 2024 jumla ya shilingi trilioni 1.06 zimepokelewa ambayo ni sawa na 83% ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, jumla ya shilingi milioni 303 zimekusanywa kama maduhuli ya Serikali, sawa na 77% ya lengo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itatekeleza maeneo sita ya kipaumbele, kama ifuatavyo:-

(1) Kuendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai.

(2) Kukamilisha, kuendelea na kuanza ujenzi wa ofisi, vituo na makazi ya askari.

(3) Kuongeza vitendea kazi vya kisasa katika kutoa huduma ikiwemo magari, pikipiki, maboti na *helicopter*.

(4) Kuanza utekelezaji wa miradi ya kimkakati, ikiwemo Mradi wa Miji Salama *(Safer Cities)*, Mradi wa Ukaguzi wa Magari wa Lazima *(Mandatory Vehicle Inspection)*, Mradi wa Udhibiti wa Barabara Kuu *(Highway Road Patrol)*.

(5) Kuimarisha mifumo ya matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

(6) Kutumia nishati safi kwenye magereza, kambi za wakimbizi na vyuo vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ikiwa ni utekelezaji wa mikakati ya Kitaifa ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi. Wajibu wa Jeshi la Polisi ni kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zao unaimarika na amani inatawala nchini, ili kuwezesha wananchi kufanya kazi zao za kiuchumi na kijamii. Katika kutekeleza wajibu huo, Jeshi la Polisi linashirikiana na jamii na wadau wengine, ili kuhakikisha uhalifu wa aina zote unadhibitiwa. Ushirikiano huu umewezesha nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024. Makosa makubwa ya jinai ambayo yamekuwa yakiripotiwa katika vituo vya Polisi yamepungua kutoka makosa 45,485 hadi kufikia 43,146 sawa na asilimia tano, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalifu umepungua kutokana na Jeshi la Polisi kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kufanya doria, misako na operesheni za kubaini, kuzuia, kutanzua na kupambana na uhalifu katika maeneo ya mijini, pamoja na vijijini, barabara kuu na mipakani. Aidha, elimu kwa umma juu ya utekelezaji wa dhana ya Ulinzi Shirikishi katika kudhibiti uhalifu inaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuharakisha upelelezi; katika kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Vikosi wanaendelea kutekeleza agizo la kukamilisha upelelezi kabla ya kumkamata mtuhumiwa. Watuhumiwa hao ni ambao makosa yao yanadhaminika kwa mujibu wa sheria. Kwa wale ambao upelelezi umekamilika wanafikishwa Mahakamani kwa wakati. Aidha, mafunzo na ukaguzi kwa vitendo umefanyika kwa wapelelezi 2,453 katika Mikoa yote. Pia, ukaguzi wa pamoja na Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, TAKUKURU na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali umefanyika katika Mikoa 35 ya Kipolisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama barabarani; hadi Aprili, 2024, jumla ya matukio ya usalama barabarani 1,463 yaliripotiwa ikilinganishwa na matukio 1,283 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Hivyo, matukio 180 yameongezeka ambayo ni sawa na ongezeko la 12%. Miongoni mwa sababu za

ongezeko la ajali za barabarani ni pamoja na mwendokasi, uzembe wa watumiaji wa barabara, ubovu wa miundombinu ya barabara na uchakavu wa vyombo vya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Jeshi la Polisi katika kudhibiti ajali za barabarani ni udhibiti wa madereva wa magari ya abiria na mizigo; kuhakiki leseni zao na vyuo vinavyotoa mafunzo ya udereva; na kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya barabara. Mikakati mingine ni kuongeza doria ya masafa katika barabara kuu. Aidha, Jeshi la Polisi limepokea magari 43 yatakayotumika kufanya doria kwenye barabara kuu na kuyasambaza katika mikoa mbalimbali ya kipolisi ikiwa ni miongoni mwa hatua za utekelezaji wa mikakati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Polisi Jamii, kupitia kauli mbiu ya "Polisi Jamii kwa Ulinzi na Usalama wetu" elimu ya uhamasishaji juu ya masuala ya usalama na uzalendo kwa Taifa imeendelea kutolewa. Elimu hiyo imetolewa katika shule za msingi, sekondari, nyumba za ibada na vituo vya bodaboda kupitia Maafisa wa Polisi Jamii na askari waliopo kwenye kata zote 3,956 na shehia zote 388.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwapongeza askari kata wanaotekeleza majukumu yao kwa moyo wa kujituma na ubunifu wa hali ya juu kote nchi nzima. Kwa niaba yao leo tunaendelea na utaratibu wetu tuliojiwekea wa kuwatambulisha mbele yenu, kuwapongeza Pamoja na kuwazawadia askari kata waliofanya vizuri zaidi kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi; Mwezi Machi, 2024 Jeshi la Polisi lilipokea magari 44 aina ya *GWM* kati ya magari 200 ambayo yanatarajiwa kupokelewa. Magari 156 yaliyobaki yanatarajiwa kuingia nchini wakati wowote. Vilevile, Mheshimiwa Rais ameridhia Jeshi la Polisi kupatiwa shilingi 72,000,000,000 kwa ajili ya kununua magari ya polisi kuanzia ngazi ya Taifa hadi Vituo vya Polisi. Kati ya fedha hizo, shilingi 15,000,000,000 zimeshapokelewa na taratibu za ununuzi zinaendelea

kwa ajili ya kununua magari 147 ya Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wakuu wa Polisi wa Wilaya zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024 shilingi bilioni 11.6 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi wa boti 10 za kufanya doria maeneo ya bahari na maziwa kote nchini, pikipiki 19 za kuongoza misafara ya viongozi na magari 24 ambapo mzabuni ameshapatikana. Katika mwaka 2024/25 jumla ya shilingi bilioni 36 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari 181. Aidha, shilingi bilioni 118.1 zimetengwa ili kununua vifaa mbalimbali vya kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba za makazi, ofisi na vituo vya polisi; hadi kufikia Aprili, 2024 Jeshi la Polisi limekamilisha miradi 15 ya ujenzi. Miradi iliyokamilika inahusisha wa ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Mikoa ujenzi wa vituo vya polisi na nyumba za makazi ya Askari Polisi. Kama ilivyooneshwa katika ukurasa wa 20 na miradi inayoendelewa imeoneshwa katika ukurasa wa 21 hadi 22 kwenye kitabu cha hotuba yangu, ambayo inajumuisha miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kipaumbele ya Jeshi la Polisi katika Mwaka 2024/2025; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekamilisha andiko la mradi wa ujenzi wa Vituo vya Polisi Daraja "C" ngazi ya Kata. Utekelezaji wake utaanza katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, ambapo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa zitajenga vituo vipya vya Polisi Kata 12 na kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata 77 vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa maelekezo haya ambayo yatasaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata katika mikoa yote. Miradi mingine inayotekelezwa katika mwaka 2024/2025 ni kama ilivyooneshwa katika ukurasa wa 25 na 26 wa kitabu cha hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha mifumo ya TEHAMA; kwa kutumia wataalam wa ndani ya nchi, Jeshi la Polisi limetengeneza mfumo wa kielektroniki utakaounganishwa na Taasisi za Haki Jinai *(Case File Management Information System)*. Hadi kufikia Aprili, 2024 Vituo Vikuu vya Polisi *(Central Police Stations)* katika mikoa 25 vilivyounganishwa kwenye Mkongo wa Taifa vinasomana na mfumo wa kielektroniki wa vituo vya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama. Kazi ya kuunganisha mikoa mingine inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi; Serikali inaendelea kuchukua hatua kwa lengo la kuimarisha usalama wa miji na majiji ili kuchochea shughuli za uwekezaji, utalii na ufanyaji wa biashara kwa wananchi na wageni. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza miradi ya kimkakati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kwanza, ni Mradi wa Miji Salama *(Safer Cities),* mradi huu una lengo la kuboresha mifumo ya usalama iliyopo nchini kwa kutumia teknolojia za kisasa. Mradi utaanza kutekelezwa mwaka 2024/2025 katika majiji kwa kuanzia na Majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Ambapo, jumla ya Kamera 6,500 zenye Teknolojia ya Akili Bandia *(Artificial Intelligence Technology)* zinatarajiwa kufungwa katika maeneo mbalimbali. Mkataba wa kibiashara kati ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi na mkandarasi tayari umesainiwa. Utekelezaji wa mradi utaanza baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo wa Dola za Marekani milioni 145 kutoka Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ukaguzi wa Magari wa Lazima, mradi una lengo la kutumia teknolojia za kisasa na kupunguza ajali za barabarani zinazochangiwa na ubovu wa vyombo vya moto, kuongeza ufanisi na kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa na lenye kutoa huduma bora kwa wananchi. Mradi huo utaanza kutekelezwa baada ya taratibu za kumpata mbia kukamilika. Mradi huu ni wa miaka mitano na una thamani ya Dola za Marakeni 112,000,000 sawa na takribani Shilingi za Kitanzania bilioni 286.16. Mradi huu utatekelezwa kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Udhibiti wa Barabara Kuu *(Highway Road Patrol);* kutokana na ongezeko la ajali barabarani, utafiti umefanyika na kubainisha maeneo yenye changamoto kubwa ikiwemo barabara kuu mfano Barabara ya Dodoma - Dar es Salaam. Taarifa ya upembuzi yakinifu za mradi zimewasilishwa na kupitishwa katika Kituo cha *PPP*, Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi pamoja na *(Standing Committee)* ya Wizara ya Fedha inayojumuisha Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, andiko hilo limepitishwa na mradi unatarajia kutekelezwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi kwa njia ya ubia kwa kushirikiana na sekta binafsi, ambapo utawezesha kufungwa vilevile kwa kamera katika maeneo mbalimbali ili kufuatilia mienendo ya madereva kwenye barabara kuu. Kutoa taarifa za hali za usalama wa barabara kwa watumiaji na kuwawezesha kuchukua tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 jumla ya wafungwa na mahabusu 27,461 walikuwepo katika magereza yote nchini. Idadi hii ni sawa na 91.8% ya uwezo wa magereza kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Hii ni hatua kubwa iliyofikiwa na Serikali ikilinganishwa na kipindi cha miaka mitano iliyopita ambapo mwaka 2019/2020 kulikuwa na jumla ya wafungwa na mahubusu 38,501. Kupungua kwa msongamano wa magerezeni kumechangiwa na hatua zifuatazo: -

(i) Matumizi ya adhabu mbadala, jumla ya wafungwa 621 walitolewa magerezani kupitia utaratibu wa Kifungo cha Nje *(EML)* na wafungwa 93 waliachiliwa huru kupitia huduma za *Parole;*

(ii) Msamaha kwa wafungwa, Wizara inamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa msamaha kwa jumla ya wafungwa 3,326 walioachiwa huru katika siku za maadhimisho ya sherehe za Kitaifa;

(iii) Ushirikiano na Taasisi za Haki Jinai, Wizara inaendelea kufanya maboresho ya mfumo wa Haki Jinai ambapo watuhumiwa ambao upelelezi haujakamilika na makosa yao yanadhaminika hukaa nje ya magereza kwa dhamana; na

(iv) Huduma za uangalizi wa wafungwa wa vifungo vya nje, wafungwa 2,675 walihukumiwa kutumikia adhabu zao kwenye jamii. Hatua hii pia imeiwezesha Serikali kuokoa jumla ya shilingi bilioni 3.6 ambazo zingetumika kuwahudumia kwa chakula wafungwa kama wangeendelea kukaa magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 shilingi 1,000,000,000 imetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upekuzi magerezani. Vifaa hivyo vitafungwa katika magereza matano ambayo ni: Gereza la Karanga - Kilimanjaro, Gereza la Maweni - Tanga, Gereza la lilungu - Mtwara, Gereza la Uyui - Tabora na Ruanda - Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za urekebu, maboresho ya programu za urekebu, hususani mitaala ya mafunzo kwa Jeshi la Magereza ni maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi ya kuboresha mitaala ya mafunzo ya vyuo vya magereza imefanyika kwa kushirikiana na *NACTVET,* Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Chuo cha Ustawi wa Jamii. Rasimu ya mitaala hiyo imewasilishwa *NACTVET* kwa ajili ya kupata idhini ya matumizi. Mitaala hiyo itaanza kutumika katika vyuo vya Jeshi la Magereza kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya nishati safi Magerezani, Jeshi la Magereza linatekeleza mkakati wa nishati safi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 jumla ya shilingi milioni 390.1 zimepokelewa kwa ajili ya kujenga mifumo ya *Bio-gas* katika Magereza ya Kimbiji na *Wazo Hill,* Dar es Salaam pamoja na Ngara, Kagera. Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa mifumo hiyo unaendelea na umepangwa kukamilika mwezi Julai, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mkakati huo Jeshi la Magereza linashirikiana na taasisi mbalimbali. Kupitia ushirikiano huo, Kampuni ya Taifa Gesi imefunga mfumo wa gesi ya *LPG* katika Magereza ya Ukonga – Dar es Salaam na Butimba – Mwanza, ambapo ipo katika hatua ya majaribio. Aidha, programu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ya miaka mitatu (2023/2024 – 2025/2026) itakayogharimu shilingi bilioni 35.44 imeandaliwa na itatekelezwa kwa kushirikiana na *REA*. Utekelezaji utafanyika katika vituo 211 vya Magereza vinavyohusisha Magereza 129, kambi za Magereza 47, vituo vinne na ofisi za Magereza 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Magereza (SHIMA), Wizara imefanya maboresho ya kimkakati na kiutendaji ya Shirika la Magereza ili kujiendesha kibiashara. Maboresho hayo yamesaidia Shirika kutoka kwenye faida ya shilingi milioni 162 mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi bilioni 3.7 mwaka 2022/2023. Aidha, Shirika limeongeza eneo la kilimo kutoka ekari 5,385 mwaka 2022/2023 hadi ekari 7,400 katika msimu wa kilimo wa mwaka 2023/2024 ambalo ni ongezeka la 45%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za viwanda na ujenzi, shirika linatekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Ujenzi wa miundombinu ya Kiwanda cha Kuchakata Bidhaa za Ngozi cha *Kilimanjaro International Leather Company Limited* chenye thamani ya shilingi bilioni 3.6 ambao umefikia 94% na umepangwa kukamilika mwezi Julai, 2024;

(ii) Ujenzi wa majengo ya Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa wenye thamani ya shilingi bilioni 1.4 umefikia 75%; na

(iii) Ujenzi wa majengo ya Halmashauri ya Manispaa Singida wenye thamani ya shilingi milioni 354.3 ambao umefikia 85%. Miradi miwili imepangwa kukamilika ifikapo Juni, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kuimarisha usalama wa watu na mali zao ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 limezima moto na kufanya uokoaji katika matukio 2,756 kwa kushirikiana na wadau. Aidha, ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto ulifanyika kwenye maeneo 58,064 na ramani za majengo 2,134 zimeidhinishwa baada ya kukidhi vigezo vya kinga na tahadhari ya moto. Jumla ya shilingi bilioni 9.9 zimekusanywa kutokana na shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile vikundi 14 vya wazimamoto wa kujitolea vimeanzishwa vyenye wanachama 178 katika Mikoa ya Katavi, Morogoro, Mtwara, Mwanza na Tanga. Vikundi hivyo vinasaidia katika utoaji wa elimu na kushiriki kwenye uokoaji pindi majanga yanapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji nchini, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea magari 28. Kati ya hayo, magari 15 ni kwa ajili ya shughuli za utawala na ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto na magari 12 ya kuzima moto na uokoaji yayonunuliwa kupitia mkopo wa masharti nafuu uliotolewa na Serikali ya Austria na gari moja la uokoaji ni msaada kutoka Serikali ya Ujerumani. Aidha, Halmashauri ya Mji wa Tunduma imenunua gari moja la kuzima moto. Naipongeza Halmashauri ya Mji wa Tunduma kwa jitihada hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia shilingi bilioni 1.8, kwa ajili ya ununuzi wa magari 11 ya utawala na ukaguzi. Magari hayo yatapokelewa katika mwaka 2024/2025. Aidha, katika mwaka 2024/2025 shilingi bilioni 1.4 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari tisa ya utawala na ukaguzi na shilingi 500,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuzima moto na uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha taratibu za upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya dola za Marekani milioni 95 uliosainiwa tarehe 15 Februari, 2024 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Falme za Kiarabu. Aidha, Serikali imechangia dola za Marekani milioni tano

sawa na asilimia tano ya gharama za mradi huo. Hivyo, ununuzi wote utagharimu jumla ya dola za Kimarekani milioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mkopo husika vitendea kazi vya kisasa vitapokelewa katika awamu nne kwa miaka miwili kuanzia 2024/2025 hadi 2025/2026. Vitendea kazi hivyo ni pamoja na magari 150 ya kuzima moto na uokoaji, magari 40 ya kubebea wagonjwa, boti 23, *command cars* 30 na *mobile workshops* sita, magari matatu ya kuzima moto wa kemikali, helikopta moja pamoja na vifaa vya mawasiliano ya kuzima moto na uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa makazi ya Maafisa na Askari vituo vya zimamoto na uokoaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekamilisha ujenzi wa majengo sita ya makazi ya kuishi familia 60 ya askari katika eneo la Kikombo Jijini Dodoma. Katika mwaka 2024/2025 shilingi bilioni 2.5 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo mawili yenye uwezo wa kuishi familia 20 za askari katika eneo hilo. Aidha, shilingi bilioni 2.6 zilitumika kukamilisha ujenzi wa vituo saba vya zimamoto na uokoaji katika Mikoa ya Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Njombe, Simiyu na Songwe. Shilingi milioni 236.5 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa viwanja vya ujenzi wa makazi ya askari na vituo vya zimamoto na uokoaji. Shilingi milioni 150 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya *Fire Hydrants* 140. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji, katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya wageni 1,695,350 waliingia nchini ikilinganishwa na wageni 1,143,645 walioingia katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Hili ni ongezeko la wageni 557,705 ambayo ni sawa na 48%. Kuongezeka kwa wageni kumetokana na jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuvutia wawekezaji, utalii, biashara na shughuli nyingine za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2024, jumla ya vibali vya ukaazi 18,813 vilitolewa. Katika kuongeza wigo wa uwekezaji katika miradi mikubwa ya makazi na kurahisisha ukaazi wa wageni katika

makazi hayo, Kanuni za Uhamiaji za mwaka 1997, zimefanyiwa marekebisho kupitia Tangazo la Serikali Na.428 la 2023. Marekebisho hayo yameweka vibali vipya vya ukaazi Daraja *C11* kwa wanaotaka kununua nyumba za miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2023/2024, nilitangaza kuondolewa kwa Nchi ya Ethiopia katika orodha ya nchi zinazohitaji *Visa* Rejea. Kufuatia uamuzi huo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, jumla ya Waethiopia 3,569 waliingia nchini kupitia vituo rasmi na 3,531 walitoka ikilinganishwa na Waethiopia 2,290 walioingia nchini na 2,364 waliotoka katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya hatua hiyo ya Serikali ni pamoja na kukusanya mapato ya Dola za Marekani 178,450 sawa na takribani shilingi bilioni 456. Kutokana na huduma za *Visa* na kuokoa shilingi bilioni 8.5 ambazo zingetumika kwa gharama za chakula cha wafunga Raia wa Ethiopia. Kupungua kwa wahamiaji haramu, kupunguza msongamano magerezani ambapo kwa sasa Raia wa Ethiopia waliopo magerezani ni 577 ikilinganishwa na 1,205 waliokuwepo mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Idara ya Uhamiaji. Hadi kufikia Aprili, 2024 Idara ya Uhamiaji imepokea jumla ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 200.2 ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara ambao umefikia 89%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji itaendelea kuimarisha na kuboresha mfumo wa uthibiti na usimamizi wa uingiaji na utokaji wa watu ili kuhakikisha wanaingia nchini kwa mujibu wa sheria. Aidha, utekelezaji wa miradi ifuatayo utaanza ikiwemo ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Songwe, ujenzi wa nyumba za makazi ya Maafisa katika eneo la Msalato Jijini Dodoma na kuendeleza ujenzi wa makazi ya wakufunzi katika Chuo cha Raphael Kubaga Mkoani

Tanga, ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa NIDA. Kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya vitambulisho 7,698,819 vimezalishwa na hivyo kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 20,578,325 sawa na 99% ya idadi ya Namba za Utambulisho 20,701,956 zilizozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 bilioni 2.9 zimetegwa kwa ajili ya kusajili na kutambua watu 2,389,290 wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa kila mwananchi mwenye namba ya utambulisho Tanzania Bara na Zanzibar anapata kitambulisho cha Taifa. Naomba nitoe rai kwa wananchi ambao hawajapata vitambulisho vya Taifa kufika katika ofisi Serikali za Mtaa walipojiandikisha kwa ajili ya kuvichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2024 *NIDA* imeunganisha taasisi 21 katika mfumo wa usajili na utambuzi, hivyo kufanya taasisi zilizounganishwa kufikia 107. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 jumla ya Taasisi 35 za umma na binafsi zinatarajiwa kuunganishwa katika mfumo huo ili kuwezesha ushirikishanaji wa taarifa na hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwahamasisha watoa huduma kujiunga na mfumo wa *NIDA* ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za wateja. Taarifa hizo, zitasaidia katika utambuzi wa wananchi kabla ya kutoa huduma na hivyo kupunguza udanganyifu ikiwemo ukwepaji wa kodi, utoaji wa mikopo na usajili wa namba za simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwa wakimbizi. Hadi kufikia Aprili, 2024, Tanzania inahifadhi jumla ya wakimbizi na walioomba hifadhi 249,803. Kati ya hao, 160,948 ni wenye asili ya Burundi, 88,257 wana asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC)* na 598 ni

kutoka mataifa mengine. Waomba hifadhi wapya 3,232 walipokelewa kutoka mataifa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama nchini itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika kambi na makazi ya wakimbizi kwa kufanya doria. Wizara itaendelea kusimamia huduma zote muhimu zinazotolewa kwa wakimbizi ambapo jumla ya bilioni 1.7 zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa jumuiya za kidini na zisizo za kidini. Kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya jumuiya 213 zilisajiliwa ikilinganishwa na Jumuiya 371 zilizosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Kati ya hizo, jumuiya za kidini ni 95 na jumuiya zisizo za kidini ni 118. Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia utendaji wa Jumuiya zilizosajiliwa, kufanya ukaguzi pamoja na kufanya uhakiki wa jumuiya hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa watu wote kuhakikisha wanafuata taratibu zote za kisheria katika kusajili jumuiya na kuepuka kuendesha jumuiya zisizosajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 jumla ya shilingi milioni 880.3 zimetengwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Msajili. Wizara itaendelea kuziratibu na kuzisimamia jumuiya za kidini na zisizo za kidini ili ziendelee kushirikiana na Serikali katika kudumisha amani, utulivu na usalama nchini. Aidha, Wizara inaendelea kuwahamasisha viongozi wa jumuiya za kidini kuendelea kuliombea Taifa na Viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati ya moyo wangu viongozi wa dini kwa kuitikia wito wa mwaliko wa kuhudhuria kwenye tukio hili muhimu, hii ni ishara ya utayari wa viongozi wa dini na taasisi zake kuendelea kushirikiana na Serikali katika kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa usafirishaji haramu wa binadamu. Wizara imewaokoa waathirika 184 waliokuwa wakitumikishwa kinyume na sheria. Wahalifu wanne waliokuwa wakijihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu walihukumiwa kifungo gerezani na watuhumiwa 11 kesi zao zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, elimu kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu imetolewa kwa wadau 157 ambao ni Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Polisi, Maafisa Kazi, Maafisa Wahamiaji, Maafisa wa Ustawi wa Jamii na watoa huduma kutoka taasisi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha udhibiti wa usafirishaji haramu wa binadamu katika pande zote za Muungano, Wizara imefungua Ofisi ya Sekretarieti Zanzibar. Tarehe 30 Julai, 2023 Wizara ilizindua mtandao wa kupinga usafirishaji haramu wa lengo ni kusaidia jitihada ya Serikali katika kutoa huduma ya usafirishaji haramu wa binadamu na kutoa elimu kwa umma. Mtandao huo unaundwa na Mashirika 105 Yasiyo ya Kiserikali kutoka katika Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Wizara imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya kazi zifuatazo:-

(i) Kujenga nyumba salama moja kwa ajili ya kutoa hifadhi ya muda na ulinzi kwa waathirika na mashahidi wa usafirishaji haramu wa binadamu;

(ii) Kuokoa, kusaidia na kuwaunganisha waathirika wa wasafifishaji haramu;

(iii) Kuokoa, kusaidia na kuunganisha waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na familia zao;

(iv) Kuandaa mpango kazi wa kitaifa wa kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu; na

(v) Kutoa elimu kwa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Nitumie fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Daniel Sillo - Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Ndugu Ally Senga Gugu - Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Dkt. Maduhu Kazi - Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kunisaidia kusimamia vema utekelezaji wa majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, natoa shukrani zangu kwa Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Camillus M. Wambura, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee R. Nyamka, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John W. Masunga, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala. Pia nawashukuru Wakurugenzi wa Taasisi na Idara zilizopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kazi nzuri ambazo wanafanya katika kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu nchini na kuwezesha wananchi kutekeleza shughuli zao za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, natoa shukrani kwa Mheshilimiwa Balozi Khamis Kagasheki ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Parole na Inspekta Jenerali wa Polisi Mstaafu Saidi Ally Mwema - Mwenyekiti wa Bodi ya SHIMA, pamoja na Wajumbe wote wa Bodi hizo kwa kusimamia vema bodi hizo na kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani nyingine nazitoa kwa watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natoa shukrani za dhati kwa nchi mbalimbali, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Taasisi za Umma, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Taasisi za Dini, Vyombo vya Habari, wananchi kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na kwa umuhimu wa kipekee naishukuru kwa dhati familia yangu, mke wangu Thania Ally Abdula na watoto wetu ambao ni Riziki, Asha na Bareek, ndugu, marafiki na jamaa kwa kunipa nguvu na moyo wa kutekeleza majukumu yangu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha,nawashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa ushirikiano na imani kubwa wanayoendelea kunipa katika majukumu ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla ambapo leo hapa wamewakilishwa vema na Mabalozi wa Chama cha Mapinduzi waliokuja kuniunga mkono. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea kuimarisha usalama wa watu na mali zao kupitia vyombo vya usalama vilivyopo chini yake. Jukumu hili litatekelezwa kwa kushirikiana na wadau muhimu wakiwemo wananchi katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 403,300,000,000 kupitia vyanzo mbalimbali. Ili kuhakikisha kiasi hicho cha fedha kinakusanywa, Wizara itaimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa maduhuli, kuimarisha huduma za mtandao katika Ofisi za Uhamiaji, kuongeza wigo wa matumizi ya mfumo wa uhamiaji mtandao, ununuzi wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2024/2025. Naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2024/2025 yenye jumla ya shilingi 1,711,710,987,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 551,583,381,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi 870,429,138,000 ni mishahara na shilingi 289,698,468,000 ni fedha za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 285,635,968,000 ni fedha za ndani na shilingi 4,062,500,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE. MHANDISI HAMAD YUSSUF MASAUNI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/24 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2024/25.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba yangu katika Bunge hili. Natumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, nampongeza kwa kuendelea kuliongoza vema Taifa letu ikiwa ni pamoja na kusimamia amani, usalama, utulivu na mshikamano nchini.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Vyombo vya Usalama vilivyopo chini yake kwa kiasi kikubwa imenufaika na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Hatua hizo zinasaidia katika kuboresha utendaji wa Wizara ili kuleta tija na manufaa zaidi kwa nchi yetu ikiwemo kuzidi kuimarika kwa hali ya usalama nchini.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawapongeza na kuwashukuru Viongozi wote wa Kitaifa kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake na kwa miongozo wanayonipatia katika kuongoza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Viongozi hao ni pamoja na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza Mhe. Naibu Waziri Mkuu kwa uteuzi huo uliofanywa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Agosti, 2023.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru wewe binafsi Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Kuchaguliwa kwako kuwa Rais wa IPU ni heshima kwa Taifa letu na wanawake wote duniani. Aidha, namshukuru Mhe. Mussa Azan Zungu (Mb.), Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza vema Bunge lako Tukufu na kwa ushirikiano mnaoendelea kutoa kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kutekeleza majukumu yake.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** natumia fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote. Aidha, namshukuru kwa dhati Mhe. Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Jimbo la Namtumbo na Makamu Mwenyekiti Mhe. Vincent Paul Mbogo Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini na wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU). Kamati imechambua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara na kutoa ushauri uliosaidia kuboresha bajeti kwa mwaka 2024/25 na utendaji wa Wizara kwa ujumla. Kwa hakika najiona kuwa mwenye bahati kubwa kuwa sehemu ya Kamati hii makini.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine namshukuru Mhe. Rais kwa kufanya uteuzi wa Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tarehe 31 Machi, 2024 alimteua Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb.) kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia, tarehe 15 Machi, 2024 Mhe. Rais alimteua Ndugu Ally Senga Gugu kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii. Kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi nawapongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais katika

nafasi hizo. Katika muda mfupi wakiwa katika dhamana ya uongozi waliopewa wameonesha ushirikiano na umahiri mkubwa uliowezesha kuharakisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Mhe. Jumanne A. Sagini (Mb.) Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na Ndugu Kasper K. Mmuya Katibu Tawala wa Dodoma kwa mchango wao uliosaidia kuweka misingi ya mafanikio ya Wizara tunayoendelea kujivunia.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawapongeza Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Camillus M. Wambura; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee R. Nyamka; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John W. Masunga; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala kwa kutunukiwa nishani ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 24 Aprili, 2024. Pia, nawapongeza maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama waliotunukiwa nishani hizo.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Mhe. Rais, Bunge, wanafamilia na wananchi kwa ujumla kwa misiba mikubwa iliyotokea hapa nchini ikiwemo wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyefariki dunia tarehe 29 Februari, 2024. Aidha, nchi yetu pia ilipata msiba wa Waziri Mkuu Mstaafu Hayati Edward Ngoyai Lowassa aliyefariki dunia tarehe 10 Februari, 2024.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, natoa pole kwako na kwa Bunge lako kufuatia kifo cha Hayati Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, aliyefariki tarehe 01 Julai, 2023 na kifo cha Hayati Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani - Zanzibar aliyefariki tarehe 08 Aprili, 2024.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwa ndugu na wananchi wote waliopoteza ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali ikiwemo mafuriko yaliyotokea katika baadhi ya maeneo nchini pamoja na maporomoko ya udongo yaliyotokea katika Wilaya ya Hanang, Mkoani Manyara na eneo la Gombe Wilaya ya Mbeya Mjini, Mkoa wa Mbeya. Vilevile, natoa pole kwa askari wote

waliopoteza maisha na walioumia wakati wakitekeleza majukumu yao.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, kwa namna ya kipekee nawashukuru Viongozi Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waheshimiwa Wabunge na wananchi mbalimbali kwa kunifariji katika kipindi cha maombolezo ya msiba wa Baba yangu Mzazi Hayati Mzee Masauni Yussuf Masauni aliyefariki dunia tarehe 23 Februari, 2024. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

**Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2023/24**

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi 1,293,820,903,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 678,657,324,000 ni za Mishahara, Shilingi 510,135,630,000 za Matumizi Mengineyo na Shilingi 105,027,949,000 za Miradi ya Maendeleo. Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, Shilingi 100,233,364,000 ni fedha za ndani na Shilingi 4,794,585,000 ni fedha za nje.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 1,067,784,633,654.93 zimepokelewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutoka Wizara ya Fedha. Kati ya fedha hizo, Shilingi 594,556,472,454.20 ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi 409,937,438,597.31 ni za Matumizi Mengineyo na Shilingi 63,290,722,603.42 za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Fedha zilizopokelewa ni sawa na asilimia 83 ya bajeti yote ya Wizara iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 51,597,212,879.15 kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi, watoa huduma, wazabuni na wakandarasi. Kati ya fedha hizo, Shilingi 576,948,021.94 ni za NIDA, Shilingi 29,127,073,840.74 kwa ajili ya Jeshi la Polisi, Shilingi 17,901,528,033.14 za Jeshi la Magereza na Shilingi 3,991,662,983.33 kwa ajili ya Idara ya Uhamiaji.

**Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara ina lengo la kukusanya maduhuli ya Serikali jumla ya Shilingi 393,500,000,000. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 303,012,267,072 zimekusanywa sawa na asilimia 77 ya lengo. Ili kufikia lengo hili, Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo: kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa huduma za Wizara; kuimarisha ufuatiliaji wa vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo shughuli za kilimo na mifugo; kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa tozo za zimamoto na uokoaji; na kuendelea kuhakiki na kufuatilia Jumuiya zilizosajiliwa chini ya Wizara.

**B. MAENEO YA KIPAUMBELE KATIKA BAJETI YA MWAKA 2024/25**

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itatekeleza maeneo sita (6) ya kipaumbele yafuatayo: kuendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai; kukamilisha, kuendeleza na kuanza ujenzi wa ofisi, vituo na makazi ya askari; kuongeza vitendea kazi vya kisasa katika kutoa huduma ikiwemo magari, pikipiki, boti na helkopta; kuanza utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo Mradi wa Miji Salama (Safer Cities), Mradi wa Ukaguzi wa Magari wa Lazima (Mandatory Vehicle Inspection), Mradi wa Udhibiti wa Barabara Kuu (Highway Patrol); kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na kutumia nishati safi kwenye Magereza, Kambi za Wakimbizi na vyuo vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

## C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25

### Upandishaji Vyeo

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imewapandisha vyeo jumla ya watumishi 9,397 katika ngazi mbalimbali za uongozi. Kati ya hao, watumishi 7,239 ni wa Jeshi la Polisi, 1,255 wa Jeshi la Magereza, 35 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 828 wa Idara ya Uhamiaji na 40 wa NIDA. Hali hiyo imeongeza morali ya utendaji kazi kwa watumishi hao. Katika mwaka 2024/25 Wizara itawapandisha vyeo jumla ya watumishi 26,876. Kati ya hao, watumishi 53 ni wa Makao Makuu ya Wizara, 20,009 wa Jeshi la Polisi, 3,582 wa Jeshi la Magereza, 1,712 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 1,211 wa Idara ya Uhamiaji na 309 wa NIDA.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pongezi nyingi na shukrani kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa upandishwaji vyeo wa kihistoria kwa vyombo vya usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, kwa kuzingatia jinsia miongoni mwa aliowapandisha vyeo ni Naibu Makamishna wa Polisi sita (6) ambao ni wanawake. Upandishwaji vyeo wa aina hii ni wa kwanza kutokea katika historia ya nchi yetu.

### Ajira kwa Askari na Watumishi Raia

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nimshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuipatia Wizara na Vyombo vya Usalama ajira ili kuendelea kuimarisha usalama wa watu na mali zao. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imeajiri jumla ya watumishi 8,542. Kati ya hao, watumishi 7 ni wa Makao Makuu ya Wizara, 7,228 ni wa Jeshi la Polisi, 500 Jeshi la Magereza, 246 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 521 Idara ya Uhamiaji na 40 NIDA.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 4,857. Kati ya hao, watumishi 114 ni wa Makao Makuu ya Wizara, 3,068 ni wa Jeshi la Polisi, 613 Jeshi la Magereza, 425 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 517 Idara ya Uhamiaji na 120 NIDA.

**Mafunzo kwa Watumishi**

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Wizara, mafunzo ya kuwajengea uwezo yametolewa kwa maafisa, askari na watumishi raia 11,167. Kati ya hao, watumishi 86 ni wa Makao Makuu ya Wizara, 9,192 wa Jeshi la Polisi, 713 wa Jeshi la Magereza, 188 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 432 wa Idara ya Uhamiaji na 556 wa NIDA. Aidha, kati ya watumishi hao, watumishi 324 wamepatiwa mafunzo nje ya nchi, ambapo maafisa na askari 170 ni wa Jeshi la Polisi, 11 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 143 wa Idara ya Uhamiaji.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara imepanga kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi 10,640. Kati ya hao, watumishi 189 wanatoka Makao Makuu ya Wizara; 6,400 Jeshi la Polisi, 1,650 Jeshi la Magereza, 1,246 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 1,004 Idara ya Uhamiaji na 151 wa NIDA. Aidha, Shilingi 30,941,802,772 zimetengwa ili kuwezesha utolewaji wa mafunzo hayo kwa watumishi.

**JESHI LA POLISI**

**Hali ya Usalama Nchini**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** wajibu wa Jeshi la Polisi ni kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zao unaimarika na amani inatawala nchini ili kuwezesha wananchi kufanya kazi zao za kiuchumi na kijamii. Katika kutekeleza wajibu huo, Jeshi la Polisi hushirikiana na jamii na wadau wengine ili kuhakikisha uhalifu wa aina zote unadhibitiwa. Ushirikiano huu umewezesha nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 makosa makubwa ya jinai yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi yamepungua kutoka 45,485 hadi 43,146 sawa na asilimia 5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Uhalifu umepungua kutokana na Jeshi la Polisi kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kufanya doria, misako na operesheni za kubaini, kuzuia, kutanzua na kupambana na uhalifu katika maeneo ya mijini, vijijini, barabara kuu na mipakani. Aidha, elimu kwa umma juu ya utekelezaji wa dhana ya Ulinzi Shirikishi katika kudhibiti uhalifu inaendelea kutolewa.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya kesi 43,146 ziliripotiwa katika Vituo vya Polisi ikilinganishwa na kesi 45,455 zilizoripotiwa mwaka 2022/23. Kati ya hizo, kesi 16,173 zilipelekwa mahakamani, kesi 2,655 zilifungwa katika Vituo vya Polisi kwa sababu mbalimbali, kesi 167 zilihamishiwa Taasisi nyingine na kesi 24,151 zipo chini ya upelelezi.

**Mkakati wa Kuharakisha Upelelezi**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** vikao vya Haki Jinai vinaendelea kufanyika kwa lengo la kuharakisha upelelezi wa kesi na kujadiliana sababu za kesi kushindwa mahakamani na kukamilisha upelelezi kabla ya kukamata watuhumiwa kwa makosa yenye dhamana. Kwa wale ambao upelelezi umekamilika wanafikishwa mahakamani kwa wakati. Aidha, mafunzo na ukaguzi kwa vitendo umefanyika kwa wapelelezi 2,453 katika mikoa yote. Pia, ukaguzi wa pamoja wa Taasisi tatu (3) ambazo ni Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, TAKUKURU na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali umefanyika katika mikoa 35 ya Kipolisi.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Vikosi wanaendelea kutekeleza agizo la kukamilisha upelelezi kabla ya kukamata watuhumiwa. Watuhumiwa hao ni ambao makosa yao yanadhaminika kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. Aidha, kwa wale ambao upelelezi umekamilika wanafikishwa mahakamani kwa wakati.

**Hali ya Usalama Barabarani**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, jumla ya matukio ya usalama barabarani 1,463 yaliripotiwa ikilinganishwa na matukio 1,283 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hivyo, matukio 180 yameongezeka sawa na asilimia 12. Aidha, ajali zilizosababisha vifo zilikuwa ni 985 ikilinganishwa na 842 zilizotokea kipindi kama hicho mwaka 2022/23, ikiwa ni ongezeko la matukio 143 sawa na asilimia 14.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, watu 1,408 walipoteza maisha ikilinganishwa na watu 1,289 waliopoteza maisha kwa mwaka 2022/23 ikiwa ni ongezeko la watu 119 sawa na asilimia 9. Pia, watu 2,166 walijeruhiwa ikilinganishwa na watu 1,893 waliojeruhiwa kwa ajali mwaka 2022/23, ambapo ni ongezeko la watu 273 sawa na asilimia 14.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa sababu za ongezeko la ajali za barabarani ni pamoja na mwendokasi, uzembe wa watumiaji wa barabara, ubovu wa miundombinu ya barabara na uchakavu wa vyombo vya moto. Hatua zilizochukuliwa na Jeshi la Polisi katika kudhibiti ongezeko la ajali za barabarani ni udhibiti wa madereva wa magari ya abiria na mizigo kwa kuhakiki leseni zao na vyuo vinavyotoa mafunzo ya udereva sambamba na kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya barabara.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati mingine ni kuongeza doria za masafa katika barabara kuu (highway patrol) kwa ajili ya kupunguza ajali zinazosababishwa na makosa ya kibinadamu pamoja na ubovu wa vyombo vya moto. Jeshi la Polisi limepokea magari 43 kwa ajili ya kufanya doria kwenye barabara kuu na kuyasambaza katika mikoa mbalimbali ya Kipolisi ikiwa ni miongoni mwa hatua za utekelezaji wa mkakati huo.

**Programu ya Polisi Jamii**

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia kauli mbiu ya *"Polisi Jamii kwa Ulinzi na Usalama wetu"* elimu ya uhamasishaji juu ya masuala ya usalama na uzalendo kwa Taifa imeendelea kutolewa kwa jamii. Elimu hiyo imetolewa kwa kutumia vipindi 115 vya vyombo vya habari na mikutano ya hadhara 7,585. Aidha, elimu imetolewa katika shule za msingi na sekondari 7,470, nyumba za ibada 4,895 na vituo vya bodaboda 7,462 kupitia Maafisa wa Polisi Jamii, Wakaguzi na askari waliopo kwenye kata zote 3,956 na shehia zote 388. Nachukua fursa hii kuwapongeza askari kata wanaotekeleza majukumu yao kwa moyo wa kujituma na ubunifu wa hali ya juu kote nchi nzima. Kwa niaba yao leo tunaendeleza utaratibu wetu tuliojiwekea wa kuwatambulisha mbele yenu, kuwapongeza na tutawazawadia waliofanya vizuri zaidi kwa mwaka huu.

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na kuanzisha Polisi Kata/Shehia pamoja na utoaji elimu kwa jamii kumekuwa na mwitikio chanya katika kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu. Hali hiyo, imesaidia kupungua matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha na nguvu kutoka matukio 389 Aprili, 2023 hadi kufikia 290 Aprili, 2024 ikiwa ni kupungua kwa matukio 99 sawa na asilimia 25. Aidha, wananchi wanaendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kuruhusu mabasi ya abiria kusafiri saa 24.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, makosa ya ukatili wa kijinsia yameongezeka ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, makosa yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi yalikuwa 24,535 ikilinganishwa na makosa 21,317 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hili ni ongezeko la makosa 3,218 sawa na asilimia 13. Ongezeko hili limetokana na mmomonyoko wa maadili katika jamii, hususan makosa ya ubakaji na ulawiti ambapo kesi 5,865 zimefikishwa mahakamani.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa mikakati inayochukuliwa na Jeshi la Polisi ni kutoa elimu ya kuzuia ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto na wanawake. Kupitia Dawati la Jinsia

na Watoto, Jeshi la Polisi limetoa elimu hiyo kwa wananchi 1,953,218. Elimu hiyo imetolewa kupitia mikutano 168, midahalo 44, vyombo vya habari 73, nyumba za ibada 45, shule za msingi na sekondari 430 na vyuo 13. Aidha, elimu hiyo imeongeza ari kwa jamii kutoa taarifa za uhalifu na vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia.

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, Dawati hilo pia limefanikiwa kutoa mafunzo ya namna ya kushughulikia makosa ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa watendaji wa madawati ya jinsia na watoto 500 nchi nzima. Aidha, Jeshi la Polisi linaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa ofisi mbili (2) za Dawati la Jinsia na Watoto katika Wilaya ya Ikungi na Mkalama Mkoa wa Singida. Ofisi hizo zinatarajiwa kuzinduliwa na kuanza kutumika rasmi Juni, 2024. Shughuli hizo zimefadhiliwa na *SOS Children's Village Tanzania na UN WOMEN* kupitia Shirika la FARM AFRICA.

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi liliratibu Mkutano wa Jumuiya ya Polisi Wanawake Ukanda wa Afrika mwaka 2023 *(International Association of Women Police - IAWP)* uliofanyika tarehe 22 - 29 Julai, 2023 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulihudhuriwa na washiriki 2,073 kutoka nchi nane (8) ambazo ni Afrika Kusini, Botswana, Ethiopia, Ghana, Kenya, Malawi, Tanzania na Zimbabwe. Mkutano uliwawezesha washiriki wa dawati la jinsia na watoto kupata uelewa na kubadilishana uzoefu wa namna bora ya kushughulikia makosa ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

**Kushiriki katika Kuimarisha Ulinzi wa Amani Kikanda na Kimataifa**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika kupeleka askari kushiriki katika kuimarisha ulinzi na amani kwenye nchi nyingine. Ushirikiano huo unawezesha maafisa na askari kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani.

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 maafisa na askari 33 wamepelekwa kushiriki ulinzi wa amani

katika nchi zifuatazo: Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(United Nations Organization Stabilization Mission in the Democratic Republic of Congo - MONUSCO)* 19, Sudan Kusini *(United Nations Mission in South Sudan - UNMISS)* tisa (9) na Sudan *(United Nations Interim Security Force for Abyei - UNISFA)* wawili (2). Aidha, Maafisa wa Polisi watatu (3) wanafanya kazi kwa muda maalum (Secondment) kwenye Umoja wa Afrika (AU) mmoja (1) na UNMISS wawili (2).

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24 Jeshi la Polisi limefanyiwa tathmini na timu ya wataalam kutoka Umoja wa Mataifa ili kuangalia kiwango cha utayari wa kikundi cha Polisi (Formed Police Unit) kwenda kwenye kazi maalum ya ulinzi wa amani. Masuala yaliyoshauriwa kupitia tathmini hiyo ni pamoja na Jeshi la Polisi kununua vifaa maalum vinavyotumika wakati wa ulinzi wa amani. Kwa sasa Jeshi la Polisi linaendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa husika, ambavyo vitagharimu jumla ya Dola za Marekani 8,959,980 sawa na takribani Shilingi 22,892,748,900. Ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali utasaidia kuongeza ujuzi, maarifa na uzoefu kwa askari wetu pamoja na mapato ya fedha za kigeni kwa Serikali.

**Upatikanaji wa Vitendea Kazi kwa Jeshi la Polisi**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi, 2024 Jeshi la Polisi lilipokea magari 44 aina ya GWM kati ya magari 200 ambayo yanatarajiwa kupokelewa. Magari 156 yaliyobaki yanatarajiwa kuingia nchini wakati wowote. Aidha, Jeshi la Polisi limepata msaada wa magari matatu (3) na pikipiki 18 kutoka kwa wadau.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mhe. Rais ameridhia Jeshi la Polisi kupatiwa Shilingi 72,000,000,000 kwa ajili ya kununua magari ya polisi kuanzia ngazi ya Taifa hadi Vituo vya Polisi. Kati ya fedha hizo, Shilingi 15,000,000,000 zimeshapokelewa na taratibu za ununuzi zinaendelea kwa ajili ya kununua magari 147 ya Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wakuu wa Polisi wa Wilaya zote nchini.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024 Jeshi la Polisi limepokea jumla ya Shilingi 11,600,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa

boti 10 za kufanya doria maeneo ya bahari na maziwa kote nchini, pikipiki 19 za kuongoza misafara ya viongozi na magari 24, ambapo mzabuni ameshapatikana.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 jumla ya Shilingi 36,006,598,800 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari 181. Aidha, Shilingi 118,139,223,300 zimetengwa ili kununua vifaa vya kijeshi. Jeshi la Polisi litaendeleza juhudi za kupata vitendea kazi muhimu kwa kushirikiana na wadau kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

**Ulipaji wa Madeni na Fidia kwa Askari**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imetoa jumla ya Shilingi 25,000,000,000 kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi na wazabuni wa Jeshi la Polisi yaliyohakikiwa na kukubaliwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2000/01 hadi 2017/18. Kati ya fedha hizo Shilingi 15,000,000,000 ni kwa ajili ya watumishi na Shilingi 10,000,000,000 ni kwa ajili ya wazabuni. Aidha, katika kipindi hicho askari 95 walioumia wakiwa kazini wamelipwa fidia ya jumla ya Shilingi 356,827,500 kutoka katika Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi.

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi, Ofisi na Vituo vya Polisi**

**a) Miradi ya Jeshi la Polisi iliyokamilika**

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024 Jeshi la Polisi limekamilisha miradi 15 kwa kutumia Shililingi 9,279,758,501 kupitia fedha zilizowekwa katika Akaunti ya Amana zilizoidhinishwa katika bajeti ya mwaka 2022/23. Miradi iliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa jengo moja la nyumba za kuishi familia mbili (2) Mtwara; ujenzi wa uzio na mazingira ya nje awamu ya kwanza katika nyumba za makamishna Dodoma; ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe na kukamilisha ujenzi wa uzio wa Chuo cha Polisi Moshi; ujenzi wa nyumba moja (1) ya kuishi familia mbili Mkoa wa Kusini Pemba; na ukarabati wa ghorofa 28 katika Kambi ya Polisi Barabara ya Kilwa - Dar es Salaam.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine iliyokamilika ni: ukarabati wa nyumba tatu (3) za ghorofa kwa ajili ya makazi ya familia 12 za askari zilizopo Mwera (Mjini Magharibi); Kituo cha Polisi Daraja "A'' Ikungi na ghorofa za makazi ya askari Polisi Mkoa wa Singida; Kituo cha Polisi Daraja "A'' katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini (Dodoma); Kituo cha Polisi Daraja "B'' Wilaya ya Mkalama (Singida); Kituo cha Polisi Daraja "B'' Ludewa (Njombe); na Kituo cha Polisi Daraja "B'' Wilaya ya Mkoani, (Kusini Pemba).

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** vituo vingine vilivyokamilishwa ni: Kituo cha Polisi Daraja "B'' Makunduchi (Kusini Unguja); Kituo cha Polisi Daraja "C" Malindi kilichopo Mji Mkongwe (Mjini Magharibi); Kituo cha Polisi Daraja "C" Songambele, Urambo (Tabora); na Kituo cha Polisi Daraja "C" Malya (Mwanza).

**b) Miradi inayoendelea**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa nyumba nne (4) za makazi ya askari Kaskazini Pemba utakaogharimu Shilingi 263,435,134 upo kwenye hatua za awali za ujenzi. Aidha, Jeshi la Polisi limepokea Shilingi 514,921,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ambapo Shilingi 214,921,000 ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo manne (4) ya kuishi askari katika eneo la Makunduchi Mkoa wa Kusini - Unguja ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 75; na Shilingi 300,000,000 ni za kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "B" Mkuranga Mkoa wa Kipolisi Rufiji ambapo ununuzi wa vifaa unaendelea.

**c) Miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo, Jeshi la Polisi limepokea jumla ya Shilingi 6,468,664,544 kwa ajili ya kukamilisha miradi ifuatayo: Kituo cha Polisi Daraja "B" Kilolo – Iringa, Shilingi 400,000,000 ambao umefikia asilimia 60 na Vituo vya Polisi Daraja "C" vya Igurusi – Mbeya, Shilingi 35,000,000; Chang'ombe – Dodoma, Shilingi 265,000,000; na Mgeta – Mara, Shilingi 53,700,000.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayokamilishwa kupitia fedha hizo zilizopokelewa ni: Kituo cha Polisi Daraja "B" Namtumbo – Ruvuma ambao umefikia asilimia 75, Shilingi 398,000,000; kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "B" Misungwi – Mwanza, Shilingi 400,000,000 ambao umefikia asilimia 30; na kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "B" Kisarawe – Pwani, Shilingi 300,000,000 uliofikia asilimia 30.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** fedha hizo pia zitatumika kuanza ujenzi wa miradi ifuatayo: Vituo vya Polisi Daraja "B" katika Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Pwani - Shilingi 399,515,300; Ifakara – Morogoro, Shilingi 350,000,000; na Buhighwe – Kigoma - Shilingi 299,986,482; Vituo vya Polisi Daraja "C" vya Chukwani, Mjini Magharibi - Shilingi 62,679,000; Isaka, Shinyanga - Shilingi 100,000,000; Lupaso, Mtwara - Shilingi 115,000,000; Kengeja – Kusini Pemba - Shilingi 113,000,000.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine itakayoanza kutekelezwa ni: ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata Daraja "C" ambavyo ni: Tunza Road, Mwanza - Shilingi 158,000,700; Nanjilinji, Lindi - Shilingi 115,000,000; Kalya Uvinza – Kigoma kwa Shilingi 114,893,855; Naipanga, Nachingwea, Lindi - Shilingi 52,522,000; Sangambi, Mbeya - Shilingi 52,522,000; Changanyikeni, Dar es Salaam - Shilingi 115,000,000; na Kitangali, Newala, Mtwara - Shilingi 173,349,367.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** vituo vingine vya Kata Daraja "C" vinavyotekelezwa kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo ni: Karema – Katavi Shilingi 50,000,000; Kegonga Mkoa wa Kipolisi Tarime-Rorya, Mara - Shilingi 115,000,000; Matangatuani – Kaskazini Pemba, Shilingi 114,998,000; Katunguru – Mwanza, Shilingi 47,000,000; na Kambi Katoto Chunya – Mbeya, Shilingi 88,980,000.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya marejeo ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322 na kuandaa Rasimu ya Kanuni za Mfuko wa Tuzo na Tozo. Kuridhiwa kwa marekebisho hayo kutawezesha kurasimisha asilimia 60 ya mapato ya mfuko huo kutumika katika ujenzi wa miundombinu ya Jeshi la Polisi ikiwemo

ofisi, vituo na makazi kwa ajili ya Jeshi la Polisi kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi.

**Miradi ya Kipaumbele ya Jeshi la Polisi katika Mwaka 2024/25**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itatekeleza miradi ya kipaumbele ifuatayo: kumalizia ujenzi wa Vituo vya Polisi Daraja "C" vya Msomera, Tanga - Shilingi 220,000,000; Tumbatu, Kaskazini Unguja - Shilingi 209,454,230.01; na kuendeleza ujenzi wa Vituo vya Polisi Daraja "B" vya Bariadi, Simiyu - Shilingi 220,000,000; Masasi, Mtwara - Shilingi 798,000,000; Mvomero, Morogoro - Shilingi 90,251,000; na Mwera, Mjini Magharibi - Shilingi 50,000,000.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imekamilisha andiko la mradi wa ujenzi wa Vituo vya Polisi Daraja "C" vya ngazi ya Kata. Utekelezaji wake utaanza katika mwaka 2024/25 ambapo Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa zitajenga vituo vipya vya Polisi Kata 12 na kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata 77 vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** natumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa maelekezo haya ambayo yatasaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata katika mikoa yote. Aidha, namshukuru Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb.) Waziri wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na watendaji wake kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata na kuridhia ufanyike chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine ni: kukamilisha ujenzi wa uzio wa nyumba za Makamishna wa Polisi - Dodoma awamu ya pili - Shilingi 344,213,000; ujenzi wa *Rest House*, Arusha - Shilingi 139,000,000; kumalizia ujenzi wa ghorofa la kuishi familia 12 Buyekera, Kagera - Shilingi 1,000,000,000; kumalizia ujenzi wa Ofisi ya Kamanda

wa Polisi Mkoa Manyara - Shilingi 800,000,000; na ujenzi wa nyumba nne (4) za kuishi askari katika kambi ya Finya, Kaskazini Pemba - Shilingi 250,000,000.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine itakayotekelezwa katika mwaka 2024/25 ni: ujenzi wa nyumba nne (4) za kuishi askari kambi ya Mfikiwa, Kusini Pemba - Shilingi 250,000,000; ujenzi wa nyumba mbili (2) za kuishi askari katika kisiwa cha Tumbatu, Kaskazini Unguja - Shilingi 250,000,000; ujenzi wa kituo cha Polisi Bububu, Mjini Magharibi - Shilingi 250,000,000; na ujenzi wa maghorofa nane (8) ya kuishi askari na familia zao Dodoma - Shilingi 7,784,915,979.

**Kuboresha Mifumo ya TEHAMA**

***62.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi limetumia Shilingi 101,640,000 kwa ajili ya utengenezaji wa Mfumo wa Kupokea na Kuchakata Taarifa za Uhalifu kutoka kwa Wananchi (Crime Early Warning and Early Response System); na Shilingi 70,000,000 kwa ajili ya utengenezaji wa Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Kampuni za Ulinzi na Walinzi (Supervision of Private Security Companies). Pia, Shilingi 92,290,000 zimetumika katika kuboresha mfumo wa ulinzi wa jengo la Polisi Makao Makuu, Dodoma.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** mifumo hiyo imetengenezwa na wataalam wa ndani wa Jeshi la Polisi kwa gharama nafuu ikilinganishwa na gharama ambazo zingetumiwa na wataalam wa nje. Hivyo, imesaidia kuokoa gharama kwa Serikali na kujenga uwezo wa wataalam wetu.

***64.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea na utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, kwa kutumia wataalam wa ndani ya nchi, Jeshi la Polisi limetengeneza mfumo wa kielektroniki utakaounganishwa na Taasisi za Haki Jinai (Case File Management Information System). Hadi kufikia Aprili, 2024 Vituo Vikuu vya Polisi (Central Police Stations) katika mikoa 23 vilivyounganishwa kwenye Mkongo wa Taifa vinasomana na mfumo wa kielektroniki wa vituo vya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama. Kazi ya

kuunganisha mikoa mingine inaendelea. Katika mwaka 2024/25 Jeshi la Polisi litaendelea kujenga na kuboresha mifumo ya TEHAMA ikiwemo Mfumo wa Alama za Vidole (Automated Biometric Information System - ABIS) na ununuzi wa redio za masafa marefu na mafupi kwa jumla ya Shilingi 40,543,899,269.50.

**SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA JESHI LA POLISI**

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Serikali kwa lengo la kuimarisha usalama wa miji na majiji ili kuchochea shughuli za uwekezaji, utalii na ufanyaji wa biashara kwa wananchi na wageni. Aidha, rasimu ya muundo mpya wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi imeandaliwa ambayo itasaidia Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu yake ya msingi na Shirika kutekeleza shughuli za kibiashara ikiwemo miradi ya kimkakati. Miradi hiyo inayotekelezwa na Shirika ni pamoja na:

**a) Mradi wa Miji Salama (Safer Cities)**

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi una lengo la kuboresha mifumo ya usalama iliyopo nchini kwa kutumia teknolojia za kisasa ili kuhakikisha usalama wa watu na mali zao unaimarishwa. Katika utekelezaji wa mradi huu jumla ya Kamera 6,500 zenye Teknolojia ya Akili Bandia (Artificial Intelligency Technology) zinatarajiwa kufungwa katika maeneo ya viwanda, biashara, mikusanyiko ya umma, barabara za miji, hoteli, na huduma za jamii. Mradi utaanza kutekelezwa mwaka 2024/25 katika majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi utasaidia kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii kutokana na kuimarika kwa usalama katika miji na majiji nchini. Pia, mradi utasaidia katika utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai kuhusu matumizi ya teknolojia ya kisasa katika utendaji kazi wa Vyombo vya Usalama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu utatekelezwa kwa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani 145,200,000 kutoka Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Mkataba wa kibiashara (Commercial Agreement) kati ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi na mkandarasi umesainiwa. Utekelezaji wa mradi utaanza baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo wa Fedha (Financial Agreement) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya UAE.

**b) Mradi wa Ukaguzi wa Magari wa Lazima**

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi una lengo la kuhuisha mfumo wa ukaguzi wa vyombo vya moto nchini ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kupunguza ajali za barabarani zinazochangiwa na ubovu wa vyombo vya moto. Andiko la mradi lililoshirikisha wadau wote muhimu kwa lengo la kuwa na mradi wenye manufaa kwa Taifa limeidhinishwa katika hatua zote kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura ya 103 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2023.

**70.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huo utaanza kutekelezwa baada ya taratibu za kumpata mbia kukamilika. Gharama za mradi ni Dola za Marakeni 112,000,000 sawa na takribani Shilingi 286,160,000,000 na utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano (5). Utekelezaji wa mradi huu utasaidia kupunguza ajali na kuongeza ufanisi kama ilivyo azma ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa na lenye kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

**c) Mradi wa Udhibiti wa Barabara Kuu (Highway Road Patrol)**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muda mrefu kumekuwa na ongezeko la ajali za barabarani zinazochangiwa na tabia za kibinadamu na miundombinu mibovu. Kutokana na ongezeko hilo, Serikali imekuwa ikichukua hatua za kupunguza ajali zikiwemo upanuzi wa miundombinu ya barabara na elimu kwa watumiaji. Katika kuendeleza jitihada hizo, Serikali ina lengo la kuanzisha mradi wa kusimamia watumiaji

wa barabara kuu kupitia mifumo ya kidijitali. Mradi utawezesha kufuatilia mienendo ya madereva na kutoa taarifa za hali za usalama wa barabara kwa watumiaji ili kuchukua tahadhari.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** utafiti wa mradi umefanyika kwa kushirikiana na wadau na kubainisha maeneo yenye changamoto kubwa ikiwemo barabara ya Dodoma - Dar es Salaam ambapo kutafungwa kamera katika maeneo mbalimbali. Taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi imewasilishwa Kituo cha PPP kwa ajili ya uchambuzi. Mradi utatekelezwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na sekta binafsi.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** ipo miradi mingine inayotekelezwa na Shirika ikiwemo mafunzo ya usalama na umahiri wa matumizi ya silaha za moto za kiraia. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Shirika limetoa mafunzo ya umahiri kwa wamiliki wa silaha 3,500 wakiwemo wamiliki binafsi, kampuni za ulinzi na uwindaji. Katika mwaka 2024/25 Shirika litaendelea kutoa mafunzo hayo kwa kuwafikia walengwa wengi zaidi. ***Natumia fursa hii kuwaelekeza wamiliki wote wa silaha nchini kuhudhuria mafunzo husika na kufanyiwa tathmini ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.***

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine unaotekelezwa na Shirika ni usafirishaji na usindikizaji wa fedha na vito vya thamani. Shirika linafanya kazi ya usindikizaji fedha kwa Benki ya NMB kwenye matawi na vituo vya kutolea fedha (ATM) 18 katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, katika kuboresha utoaji wa huduma hiyo, Shirika limefanya uimarishaji wa kituo cha mawasiliano na ufuatiliaji (Control Centre) ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi hii. Katika mwaka 2024/25, Shirika litaendelea kuboresha utoaji wa huduma hiyo na kuongeza wigo kwa kuwafikia watoa huduma wengi zaidi.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika kupitia kampuni yake tanzu ya huduma za bandari (TPFCS Miscellaneous Port Services), imeanza kutoa huduma ya uhamishaji wa magari kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kupeleka kwenye bandari kavu. Ushiriki wa Shirika katika

kazi hii ni sehemu ya kuimarisha usalama wa mali za wateja. Aidha, kupitia kampuni hiyo Shirika litaendelea kutoa ajira za muda za madereva wanaoshiriki katika kazi hiyo.

## JESHI LA MAGEREZA

### Hali ya Ulinzi na Usalama Magerezani

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza linaendelea kuwapokea, kuwahifadhi na kuwapatia huduma wahalifu wanaoletwa magerezani kwa mujibu wa Sheria. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 jumla ya wafungwa na mahabusu 27,461 walikuwepo katika magereza yote nchini. Kati ya hao, wafungwa walikuwa 18,370 na mahabusu 9,091. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 91.8 ya uwezo wa magereza kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Hii ni hatua kubwa iliyofikiwa na Serikali ikilinganishwa na kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita ambapo mwaka 2019/2020 kulikuwa na jumla ya wafungwa na mahubusu 38,501. Hali hii imechangiwa na hatua zifuatazo:

**a)** **Matumizi ya Adhabu Mbadala:** matumizi ya adhabu mbadala yameendelea kuimarishwa kama nyenzo muhimu ya kudhibiti msongamano wa wafungwa magerezani. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 jumla ya wafungwa 621 walitolewa magerezani kupitia utaratibu wa Kifungo cha Nje (EML) na wafungwa 93 waliachiliwa huru kupitia huduma za Parole. Aidha, katika kipindi hicho elimu imetolewa kwa wajumbe 163 wa Parole katika mikoa nane (8) ambayo ni Dar es Salaam, Lindi, Pwani, Mara, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Mwanza. Elimu hiyo ililenga kuwajengea uwezo wajumbe hao kuhusu utekelezaji wa huduma ya Parole katika Jeshi la Magereza.

**b)** **Msamaha kwa Wafungwa:** Wizara inamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa msamaha wa jumla ya wafungwa 3,326 kupitia maadhimisho ya sherehe za kitaifa. Kati ya hao, wafungwa 2,244 waliachiwa huru katika siku ya Maadhimisho ya Sherehe ya miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara iliyofanyika tarehe 09 Desemba, 2023 na wafungwa

1,082 kupitia Maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 2024.

**c) Ushirikiano na Taasisi za Haki Jinai:** Wizara inaendelea kufanya maboresho ya mfumo wa Haki Jinai ambapo watuhumiwa ambao upelelezi haujakamilika na makosa yao yanadhaminika hukaa nje ya magereza kwa dhamana. Hatua hii ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**d) Huduma za Uangalizi wa Wafungwa wa Vifungo vya Nje:** katika kutekeleza Ibara Na. 120(J) ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 inayohimiza kupunguza msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani, huduma za uangalizi wa wafungwa wa vifungo vya nje zinaendelea kutolewa na Wizara. Jumla ya Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii 3,652 za watuhumiwa na wafungwa ziliwasilishwa mahakamani. Kupitia taarifa hizo, mahakama imewahukumu wafungwa 2,675 kutumikia adhabu zao kwenye jamii, kati ya hao wanaume 2,163 na wanawake 512. Aidha, wafungwa 2,365 waliungana na familia zao baada ya kumaliza kutumikia vifungo vyao. Kati ya hao wanaume 1,907 na wanawake 458.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hiyo ya wafungwa 2,675 kutumikia adhabu zao kwenye jamii imeiwezesha Serikali kuokoa jumla ya Shilingi 3,611,250,000 ambazo zingetumika kuwahudumia kwa chakula kama wangeendelea kukaa magerezani. Gharama hizo ni za kuwahudumia kwa chakula wafungwa hao kwa wastani wa Shilingi 5,000 kwa mfungwa kwa siku katika muda wa miezi tisa (9).

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, wafungwa 2,245 walipewa ushauri wa kisaikolojia na kufundishwa maadili ya jamii, 430 walifundishwa stadi za kazi na maisha. Aidha, wafungwa watano (5) waliokuwa wanatumia dawa za kulevya walipewa ushauri nasaha na matibabu na 2,365 walipewa ushauri nasaha kuwasaidia kuishi maisha mema katika jamii.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na wafungwa hao kushiriki katika programu za urekebishaji, pia walitekeleza miradi ya kimkakati ya utunzaji wa mazingira katika mikoa mitano (5) ambayo ni Dar es Salaam, Mbeya, Dodoma, Shinyanga na Kagera kwa kupanda miti 2,500, utunzaji wa bustani 14, upandaji na utunzaji wa vitalu vya miche ya matunda na vivuli. Vilevile, wafungwa hao wameshiriki katika shughuli za ujenzi wa madarasa matatu (3) na ofisi tatu (3) za walimu katika shule ya msingi Mwerani (Geita) na kusafisha eneo la Kituo Kikuu cha Mabasi Mkoa wa Shinyanga.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitoa elimu ya uhamasishaji kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii, Sura ya 291 na Sheria yaUangalizi wa Wafungwa, Sura ya 247 kwa wadau 1,500 wa Haki Jinai. Elimu hiyo pia ilitolewa kwa jamii kupitia vyombo vya habari vikiwemo vipindi vya redio, luninga, mitandao ya kijamii na magazeti. Aidha, katika Maadhimisho ya wiki ya Sheria ya mwaka 2024, elimu ilitolewa kwa jamii katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 jumla ya Shilingi 2,045,718,000 zimetengwa katika Idara ya Huduma za Uangalizi kwa ajili ya kazi zifuatazo: kuwasimamia na kuwafuatilia wafungwa 5,000 wanaotarajiwa kuwekwa chini ya Amri za Huduma kwa Jamii na Uangalizi; kufanya uchunguzi wa kijamii; kutoa elimu ya utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii, Sura ya 291 na Uangalizi wa wafungwa kwa wadau; kutekeleza Programu za Urekebishaji wa tabia za wafungwa; ununuzi wa pikipiki na vitendea kazi muhimu ikiwemo kompyuta na samani.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ambazo zitatatekelezwa ni: kutoa huduma za utangamano (Re-intergration) kwa jamii na wafungwa wanaoachiwa baada ya kumaliza kutumikia adhabu zao; kuendelea kutekeleza mradi wa utunzaji wa mazingira; na kuanzisha kanzidata ya wafungwa wa vifungo vya nje (Non-Custodial Offenders' Database Information System) ambao utakuwa unasomana na Mfumo wa Kielektroniki wa Mahakama. Aidha,

Wizara itaandaa kanuni za usimamizi wa wafungwa wanaomaliza vifungo vyao ili wasirudie makosa baada ya kurudi kwenye jamii.

**Kuimarisha Ulinzi na Usalama Magerezani**

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, ulinzi na usalama magerezani umeendelea kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kutumia vifaa vya usalama vya kielektroniki. Hadi kufikia Aprili, 2024 Jeshi la Magereza limepokea Shilingi 990,950,000 kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa vifaa vya usalama katika magereza matano (5) ambayo ni Gereza Arusha – Arusha, Isanga – Dodoma, Ukonga, Segerea na Keko – Dar es Salaam. Kazi ya ufungaji wa vifaa vya usalama unaendelea na utakamilika mwezi Juni, 2024.

**84.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25 Shilingi 1,000,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upekuzi magerezani. Vifaa hivyo vitafungwa katika Magereza matano (5) ambayo ni: Karanga - Kilimanjaro, Maweni - Tanga, lilungu - Mtwara, Uyui - Tabora na Ruanda - Mbeya.

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Magereza litajenga miundombinu itakayowezesha usikilizwaji wa mashauri ya wahalifu magerezani kupitia mfumo wa Mahakama Mtandao, hivyo kupunguza gharama za usafirishaji wa mahabusu kwenda mahakamani. Mpango huo utatekelezwa katika awamu tatu (3) na utahusisha magereza 43. Aidha, Shilingi 1,397,680,000 zimetengwa ili kuanza utekelezaji wa awamu ya kwanza ya huduma za mahakama mtandao utakaohusisha magereza 20.

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, magereza yatakayohusika kwenye awamu ya kwanza ni yafuatayo: Gereza Arusha - Arusha, Isanga - Dodoma, Bukoba - Kagera, Bangwe - Kigoma, Karanga - Kilimanjaro, Babati - Manyara, Musoma - Mara, Ruanda - Mbeya, Lilungu - Mtwara, Butimba - Mwanza, Ludewa – Njombe, Mkuza - Pwani, Bariadi - Simiyu, Maweni - Tanga, Uyui - Tabora, Geita na magereza mahabusu ya Lindi, Sumbawanga, Morogoro na Songea.

**Huduma za Urekebu**

**87.** ***Mheshimiwa* Spika,** programu za urekebu kwa wafungwa magerezani hutolewa kupitia huduma za kiroho, kisaikolojia na ushauri nasaha, elimu, michezo pamoja na stadi za kazi. Programu hizo zinalenga kuwaondolea wafungwa mawazo hasi yenye vichocheo vya uhalifu na kuwapatia elimu na ujuzi ili kuwarekebisha. Katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa programu hizo, Jeshi la Magereza linaboresha huduma za urekebu na mitaala ya mafunzo ili kuwajengea uwezo maafisa na askari wanaosimamia jukumu hilo.

**Maboresho ya Mitaala na Mafunzo ya Huduma za Urekebu kwa Watumishi**

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, maboresho ya programu za urekebu, hususan mitaala ya mafunzo kwa Jeshi la Magereza ni maelekezo mahususi ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi ya kuboresha mitaala ya mafunzo ya vyuo vya magereza imefanyika kwa kushirikiana na NACTVET, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Chuo cha Ustawi wa Jamii. Rasimu ya mitaala hiyo imewasilishwa NACTVET kwa ajili ya kupata idhini ya matumizi. Mitaala hiyo inatarajiwa kuanza kutumika katika vyuo vya Jeshi la Magereza mwezi Septemba, 2024.

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa usimamizi na utekelezaji wa huduma za urekebu magerezani wataalamu 88 wamehitimu mafunzo ya Sayansi ya Urekebishaji yanayotolewa katika Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Ukonga - Dar es Salaam (TCTA). Wataalamu hao wamepangiwa vituo vya kazi kwa ajili ya kuimarisha huduma za urekebu magerezani. Katika mwaka 2024/25 Shilingi 592,306,000 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo ya kuwaandaa walimu wa Vyuo vya Magereza ili kuendana na mitaala mipya na kuimarisha vyuo vya urekebu.

**Huduma za Urekebu kupitia Programu ya Elimu**

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, huduma ya elimu kwa wafungwa hutolewa magerezani kwa lengo la kuwapa nafasi wafungwa ambao wameshauriwa na kuonekena wana sifa na uwezo wa kujiendeleza kupitia programu za elimu zinazotolewa magerezani. Mafunzo hayo yanatolewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Huria Tanzania, Baraza la Mitihani ya Taifa, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na VETA.

**91.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2024 wafungwa 165 wameendelea kufundishwa na kuandaliwa kwa ajili ya kufanya mitihani ya Taifa kwa ngazi mbalimbali za elimu ikihusisha vyuo vikuu. Kati ya hao, wafungwa wawili (2) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo mmoja anasoma shahada ya sheria na mwingine shahada ya uzamili katika usimamizi wa miradi, 77 VETA, 07 Sekondari na 79 Shule ya msingi.

**Urekebu kupitia Stadi za Kazi**

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, stadi za kazi kwa wafungwa hutolewa kupitia shughuli za kilimo, ujenzi na viwanda vilivyopo magerezani. Wakati wa utekelezaji wa shughuli hizo wafungwa hufundishwa na kujengewa uwezo hatimaye kupata ujuzi wa shuguli husika.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa mwaka 2023/24 wafungwa 22,727 wamehusika katika shughuli za urekebu kupitia kilimo. Jumla ya ekari 7,257 za mazao zimelimwa, kati ya hizo, mahindi ekari 2,535, mpunga 747, alizeti 1,020, maharage 262 na 2,693 za mazao mengine. Matarajio ni kuvuna tani 4,420 za mahindi, 1,107.30 za mpunga, 975 za alizeti, 245 za maharage na 2,700 za mazao mengine. Lengo la programu hii ni kuwapatia ujuzi katika shughuli za kilimo na uzalishaji wa chakula cha wafungwa magerezani.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Jeshi la Magereza limeweka lengo la kulima ekari 12,159 za mazao. Kati ya hizo, ekari 5,812 zitalimwa mahindi, 2,325 mpunga, 3,018 alizeti, 754 maharage na 250 mbegu bora. Mavuno yanayotarajiwa ni tani 7,940.15

mahindi, 1,856.2 mpunga, 1,291 alizeti, 260.7 maharage na 93.95 mbegu bora za mazao mbalimbali.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Jeshi la Magereza limetenga Shilingi 3,805,523,000 kwa ajili ya uboreshaji wa shughuli za kilimo. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,378,523,000 ni kwa ajili ya ununuzi wa zana na mitambo ya kilimo, Shilingi 750,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa maghala matatu (03) katika magereza ya Butundwe – Geita, Kiabakari – Mara na Kitete – Rukwa na Shilingi 677,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo na viuatilifu.

**Matumizi ya Nishati Safi Magerezani**

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuondokana na matumizi ya kuni kwa kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu magerezani, Jeshi la Magereza linatekeleza mkakati wa nishati safi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 390,104,400 zimepokelewa kwa ajili ya kujenga mfumo wa gesi vunde (Bio-gas) katika Magereza ya Kimbiji na Wazo Hill – Dar es Salaam pamoja na Ngara – Kagera. Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa mifumo ya gesi vunde unaendelea na ujenzi wa mifumo hiyo imepangwa kukamilika mwezi Julai, 2024.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** zipo taasisi zinazoshirikiana na Jeshi la Magereza katika kutekeleza mkakati wa matumizi ya nishati safi ambazo ni Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kampuni ya PUMA, Kampuni ya Taifa Gesi na Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Kupitia ushirikiano huo, Kampuni ya Taifa Gesi imefunga mfumo wa gesi ya *Liquified Petroleum Gas* (LPG) katika Magereza ya Ukonga – Dar es Salaam na Butimba - Mwanza. Mifumo hiyo ipo katika hatua ya majaribio.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza limeandaa programu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2023/24 – 2025/26). Programu hii itagharimu Shilingi 35,446,711,475 na itatekelezwa kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Utekelezaji utafanyika katika vituo 211

vya Jeshi la Magereza vinavyohusisha magereza 129, kambi za magereza 47, vyuo vinne (4) na ofisi za magereza 31.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayotekelezwa kupitia Programu hiyo ni: ujenzi wa mitambo 126 ya bio-gas itakayogharimu Shilingi 24,097,939,565; usimikaji wa mifumo 56 ya LPG Shilingi 4,822,945,280; uboreshaji wa mfumo wa gesi asili katika Gereza Lilungu – Mtwara Shilingi 129,792,550; ununuzi wa tani 1,147 za Rafiki Briquettes na majiko 412 kwa gharama ya Shilingi 4,766,034,080; ununuzi wa mashine 61 za kutengeneza mkaa mbadala unaotokana na mabaki ya mazao (Charcoal Briquettes) Shilingi 1,630,000,000.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi 548,500,000 zitatumika kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi 280 wa Jeshi la Magereza kuhusu uendeshaji wa miradi ya nishati safi. Mradi huo utatekelezwa kwa mfumo wa kuchangia gharama ambapo REA itachangia asilimia 61.3 ya gharama za mradi na Jeshi la Magereza litachangia asilimia 38.7. Hati ya makubaliano ya utekelezaji wa program hiyo kati ya Jeshi la Magereza na REA imesainiwa tarehe 09 Aprili, 2024.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Jeshi limetenga Shilingi 1,477,000,000 kwa ajili ya kuwezesha matumzi ya nishati safi katika vituo 30 vya magereza ambayo ni Butimba – Mwanza, Uyui – Tabora, Isanga, Msalato na King'ang'a – Dodoma, Ukonga, Keko, Segerea, Wazo Hill na Kimbiji - Dar es Salaam, Lindi, Lilungu – Mtwara, Chuo Kiwira na Ruanda – Mbeya, Bariadi na Malya – Simiyu, Karanga – Kilimanjaro, Arusha – Arusha, Shinyanga na Kahama – Shinyanga, Maweni – Tanga, Kitai – Ruvuma, Mugumu, Tabora, Mahabusu Morogoro, Iringa – Iringa, Bwawani Sekondari, Chato – Geita, Ngara – Kagera, Ubena – Pwani. Fedha hizo zitatumika kununulia majiko ya gesi pamoja na kulipia gharama za uendeshaji wa mifumo hiyo.

**Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Magereza**

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Jeshi limefanya ukarabati katika magereza ya Tukuyu – Mbeya, Malya – Simiyu,

Gereza la Mahabusu Urambo – Tabora, Karakana ya Gereza Wami Vijana – Morogoro, Ukonga – Dar es Salaam, Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Ukonga – Dar es Salaam na Ofisi ya Magereza Mkoa wa Tabora. Jumla ya Shilingi 155,314,675 zimetumika kwa ajili ya ukarabati huo. Aidha, Shilingi 2,319,600,000 zimetolewa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa magereza 10 ambayo ni Kakonko – Kigoma, Kaliua na Igunga – Tabora, Karatu – Arusha, Kiabakari – Mara, Kilosa na Gairo – Morogoro, Kingurungundwa – Lindi, Msalato na Isanga – Dodoma.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa huduma za maji unaendelea kutekelezwa katika Magereza ya Ludewa – Njombe, Mbarali – Mbeya, Kiteto – Manyara na Kingurungundwa – Lindi. Kazi hii itakamilika mwezi Juni, 2024 na itagharimu jumla ya Shilingi 228,000,000.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Shilingi 4,022,125,000 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa magereza mapya mawili (2) katika Wilaya za Karatu – Arusha na Kilosa – Morogoro. Shilingi 6,491,794,000 zimetengwa kwa kazi ya ukarabati wa magereza manne (4) ya Butimba – Mwanza, Lilungu – Mtwara, Ukonga na Keko – Dar es Salaam.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Jeshi la Magereza limetenga Shilingi 147,881,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa nyumba tano (5) za maafisa na askari katika Gereza Kalilankulukulu - Katavi. Pia, Shilingi 187,319,000 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama katika magereza mawili (2) ambayo ni Gairo - Morogoro na Namajani – Mtwara.

**Upimaji wa Ardhi na Ulipaji wa Fidia**

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 1,495,111,477.51 zimelipwa kwa wananchi 201 wanaopisha maeneo yanayotarajiwa kujengwa magereza mapya katika Wilaya za Kishapu - Shinyanga, Ilemela - Mwanza na Nyasa –

Ruvuma. Aidha, Shilingi 200,000,000 zimetumika kwa ajili ya upimaji na uthamini wa ardhi katika maeneo 14 ya magereza.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Jeshi la Magereza limetenga Shilingi 492,940,000 kwa ajili ya upimaji na uthamini wa ardhi katika Magereza ya Urambo - Tabora, Kigongoni - Pwani, Kambi Kifaru - Kilimanjaro, Kambi Igumbilo - Iringa, Kambi Makele - Kigoma, Rorya – Mara, Busega - Simiyu na Ilemela – Mwanza.

**Ununuzi wa Vitendea Kazi kwa Jeshi la Magereza**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 6,545,568,600 zimepokelewa na kulipwa kwa mtoa huduma kwa ajili ya ununuzi wa magari 28. Kati ya hayo, magari 21 ni ya utawala na saba (7) ni ya kusafirisha mahabusu. Aidha, katika mwaka 2024/25 Shilingi 3,500,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari 12 yatakayotumika kwa shughuli za utawala na matatu (3) kwa usafirishaji wa mahabusu.

**SHIRIKA LA MAGEREZA (SHIMA)**

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imefanya maboresho ya kimkakati na kiuendeshaji wa Shirika la Magereza ili kujiendesha kibiashara. Maboresho hayo ni pamoja na kuhuisha mpango mkakati wa shirika, kuongeza uzalishaji na tija, kuimarisha mifumo ya utawala bora na kutoka kwenye faida ya Shilingi 162,165,859 mwaka 2021/22 hadi kufikia Shilingi 3,753,752,693 mwaka 2022/23. Shirika linaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya uzalishaji katika shughuli za kilimo na mifugo, viwanda vidogo vidogo, ujenzi na uchimbaji madini kama ifuatavyo:

**a) Shughuli za Kilimo na Mifugo**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Shirika limeboresha mazingira ya kilimo kwa kununua matrekta mapya kumi (10) aina ya *New Holland* (90HP) na zana zake kwa gharama ya Shilingi 1,000,000,000. Matrekta hayo yamepelekwa

kwenye miradi ya Kilimo Arusha, Isupilo – Iringa, Kwitanga – Kigoma, Kingolwira na Idete – Morogoro, Ludewa – Njombe, Mang'ola - Arusha, Mollo - Rukwa, Kitai - Ruvuma na Songwe – Mbeya.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** ununuzi wa zana hizo umewezesha kuongeza eneo la kilimo kutoka ekari 5,385 mwaka 2022/23 hadi ekari 7,400 katika msimu wa kilimo wa mwaka 2023/24. Mazao yaliyolimwa ni pamoja na mahindi ekari 5,420, mpunga ekari 1,030, maharage ekari 200, ngano ekari 400, alizeti ekari 230, miwa ekari 100 na kahawa ekari 20.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** makadirio ya mavuno ya mahindi ni tani 5,238, mpunga tani 543, maharage tani 125, ngano tani 400, alizeti tani 60, miwa tani 2,000 na kahawa tani 10 ikilinganishwa na msimu wa mwaka 2022/23 ambapo mavuno yalikuwa tani 2,785 za mahindi, tani 209 za mpunga, tani 18.9 za maharage, tani 17 za alizeti, tani 703 za miwa na tani 0.3 za kahawa.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Shirika limepanga kulima jumla ya ekari 10,760 za mazao ya kilimo ambalo ni ongezeko la asilimia 45 ikilinganishwa na ekari 7,400 zilizolimwa msimu wa 2023/24. Mazao yatakayolimwa ni kama ifuatavyo: mahindi ekari 6,530, mpunga ekari 1,300, maharage ekari 330, ngano ekari 500, alizeti ekari 300, miwa ekari 300 na michikichi ekari 1,500. Makadirio ya mavuno ni mahindi tani 7,272, mpunga tani 921, maharage tani 200, ngano tani 500, alizeti tani 108, miwa tani 7,500 na mafuta ya mawese tani 45.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea kuwekeza kwenye kilimo kwa kununua matrekta 10 na zana zake ambapo Shilingi 1,000,000,000 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2024/25. Aidha, Shilingi 500,000,000 zimepangwa kutumika katika kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji katika miradi ya kilimo Arusha na Mang'ola - Arusha. Pia, Shilingi 500,000,000 zitatumika kukamilisha ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao lililopo Kitai - Ruvuma na kuanza ujenzi wa maghala katika miradi wa kilimo Ludewa – Njombe, Kitengule – Kagera na Mang'ola - Arusha.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Shirika limechimba visima virefu sita (6) katika miradi ya Arusha na Mang'ola ili kuwezesha kilimo cha umwagiliaji. Shirika pia limetoa mafunzo kwa wataalam wa kilimo 30 kutoka kwenye miradi 15 ya kilimo. Mafunzo hayo yalihusu usimamizi wa mashamba kuanzia kipindi cha maandalizi ya kulima, utunzaji wa mazao hadi baada ya mavuno. Aidha, elimu ilitolewa kwa wataalam hao kuhusu uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya kilimo.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea kuboresha uzalishaji wa mifugo na miundombinu bora katika mashamba ya mifugo ya Kitengule – Kagera, Kingolwira – Morogoro, Mollo – Rukwa na Mugumu - Mara. Aidha, Shirika limejenga vituo vya unenepeshaji wa mifugo katika miradi ya Kitengule – Kagera na Mbigiri – Morogoro. Vituo hivyo vitakuwa na uwezo wa kunenepesha mifugo 400 kwa mwaka. Kujengwa kwa vituo vya unenepeshaji mifugo kutaongeza tija katika mnyororo wa thamani wa mifugo ikiwemo upatikanaji wa nyama na ngozi.

**b) Shughuli za Viwanda na Ujenzi**

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha vitendea kazi katika viwanda, Shirika limenunua mtambo wa kukausha chumvi unaoendelea kufungwa katika mradi wa Lilungu – Mtwara. Mtambo huo utaanza kutumika mwezi Juni, 2024 na utakuwa na uwezo wa kuchakata tani 15 za chumvi ghafi kwa siku.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia kikosi cha ujenzi, SHIMA linatekeleza miradi ifuatayo: ujenzi wa miundombinu ya kiwanda cha kuchakata bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro International Leather Company Limited wenye thamani ya Shilingi 3,628,199,924 umefikia asilimia 94 na umepangwa kukamilika mwezi Julai, 2024; ujenzi wa majengo ya Ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa wenye thamani ya Shilingi 1,477,104,202.08 umefikia asilimia 75; na ujenzi wa majengo ya Halmashauri ya Manispaa Singida wenye thamani ya Shilingi

354,362,894.84 umefikia asilimia 85. Miradi hii miwili inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2024.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Shirika litakarabati majengo ya viwanda vya samani Arusha na Ukonga - Dar es Salaam kwa gharama ya Shilingi 200,000,000. Pia, vitendea kazi vitanunuliwa kwa ajili ya Viwanda vya Samani Arusha, Ukonga - Dar es Salaam na Uyui - Tabora, Kiwanda cha Ushonaji Ukonga - Dar es Salaam, Kiwanda cha Sabuni Ruanda - Mbeya na Kiwanda cha Chumvi Lilungu – Mtwara. Fedha zilizotengwa kwa ununuzi wa vitendea kazi katika viwanda hivyo ni Shilingi 500,000,000.

**Ushirikishaji wa Sekta za Umma na Binafsi (Public Private Partnership**)

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeongeza miradi mipya ya Kokoto Msalato - Dodoma na Chokaa Wazo Hill - Dar es Salaam. Leseni za uchimbaji madini ya ujenzi katika Miradi ya Kokoto Msalato – Dodoma na Chokaa Wazo Hill - Dar es Salaam zimehuishwa na kufanya marejeo ya bei ili kuendana na bei elekezi kutoka Tume ya Madini. Marejeo haya ya bei yamewezesha ongezeko la mapato kutoka Shilingi 476,837,568 kwa mwaka 2022/23 hadi kufikia Shilingi 612,530,000 kwa kipindi cha kuanzia Oktoba, 2023 hadi Aprili, 2024. Inatarajiwa mapato hayo yataongezeka hadi kufikia takribani Shilingi 875,000,000 ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 83.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maelekezo ya Serikali kuhusu ushirikishaji wa sekta za umma na binafsi, Shirika limeandaa andiko la upembuzi wa awali wa mradi wa Kwitanga - Kigoma kwa ajili ya kilimo cha michikichi na kuzalisha mafuta ya kupikia. Katika mradi huo, ekari 808 zimepandwa miche ya michikichi bora aina ya Tenera. Lengo la mradi ni kulima ekari 4,000 za michikichi na kuwezesha kujengwa kiwanda cha kuchakata mafuta ya mawese kwa kushirikiana na wabia.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limesaini makubaliano ya ushirikiano na Bodi ya Sukari Tanzania na TARI Kibaha katika uendelezaji wa kilimo cha miwa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa

sukari nchini. Makubaliano hayo yatawezesha kuzalisha mbegu bora za miwa katika eneo la ekari 1,000 kwenye Mradi wa Kilimo Kiberege - Morogoro. Mbegu hizo pia zitasaidia wakulima wadogo kuongeza mavuno na kipato kutokana na mauzo ya miwa kwenye Kiwanda cha Sukari Kilombero. Utekelezaji wa makubaliano hayo utaanza msimu wa kilimo wa 2024/25.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maelekezo ya Serikali kuhusu ushirikishaji wa Sekta za Umma na Binafsi (PPP) katika uendelezaji wa rasilimali zilizopo kwa manufaa ya Taifa, Shirika limekuwa likitangaza fursa za ushirikiano zilizopo katika miradi ya Shirika kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija. Fursa hizi zinatangazwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na tovuti ya Shirika la Magereza, www.shima.go.tz.

## JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

### Huduma za Zimamoto na Uokoaji Nchini

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kuimarisha usalama wa watu na mali zao ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 limezima moto na kufanya uokoaji katika matukio 2,756 kwa kushirikiana na wadau. Baadhi ya matukio hayo ni: moto katika Soko la Mbuyuni Manispaa ya Moshi - Kilimanjaro; moto katika bweni la Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Ziba Wilaya ya Igunga - Tabora; na moto wa vibanda vya biashara eneo la Mnadani Kariakoo - Dar es Salaam.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** matukio mengine ambayo uokoaji umefanyika ni mafuriko na maporomoko ya udongo katika Kijiji cha Kateshi Wilaya ya Hanang – Manyara, Gombe Wilaya ya Mbeya Mjini, mafuriko katika Wilaya ya Rufiji na Kibiti – Pwani, eneo la Kisongo Jijini Arusha, mafuriko katika Halmashauri ya Mlimba, Wilaya ya Kilombero, Wilaya ya Morogoro Mjini, Wilaya ya Kilosa – Morogoro na Wilaya ya Kilwa – Lindi.

**Ukaguzi wa Kinga na Tahadhari ya Moto**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto ulifanyika kwenye maeneo 58,064 sawa na asilimia 83 ya lengo la mwaka 2023/24 la kukagua maeneo 70,000. Aidha, ramani za majengo 2,134 zimesomwa na kupitishwa baada ya kukidhi vigezo vya kinga na tahadhari ya moto na majanga mengine. Jumla ya Shilingi 9,919,243,405 zilikusanywa kutokana na shughuli hizo.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekamilisha maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ukaguzi wa Kinga na Tahadhari ya Moto kwa kutatua changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha majaribio. Mfumo huo umeanza kutumika katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Pwani na mafunzo yanaendelea kutolewa katika mikoa iliyobaki ili uweze kutumika nchi nzima. Katika mwaka 2024/25 Shilingi 341,259,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya mfumo huo kama vile kompyuta, *printer, scanner* na vifaa vya mtandao.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ikiwemo vipindi vya luninga 235 na redio 503. Aidha, klabu za zimamoto zimefunguliwa katika shule 151 kati ya hizo shule za msingi ni 81 na sekondari 70 zenye wanachama 10,856. Idadi hiyo inafanya jumla ya klabu za zimamoto kufikia 990 zenye wanachama 70,796 nchi nzima. Pia, skauti 1,352 wamefundishwa elimu ya kinga ya tahadhari ya moto na majanga mengine.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kipindi husika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeanzisha vikundi 14 vya wazimamoto wa kujitolea (fire volunteers) vyenye wanachama 178 katika Mikoa ya Katavi, Morogoro, Mtwara, Mwanza na Tanga. Vikundi hivyo vinasaidia katika utoaji wa elimu na kushiriki kwenye uokoaji majanga yanapotokea. Aidha, katika mwaka 2024/25, Shilingi 250,660,000 zimetengwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma na

uhamasishaji wa jamii kujiunga na vikundi vya wazimamoto wa kujitolea.

**Vitendea kazi kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha upatikanaji wa vitendea kazi ili kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji nchini. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea magari 28. Kati ya hayo, magari 15 ni ya shughuli za utawala na ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto kupitia fedha zilizotolewa katika bajeti ya mwaka 2022/23, magari 12 ya kuzima moto na uokoaji yamenunuliwa kupitia mkopo wa masharti nafuu uliotolewa na Serikali ya Austria na gari moja (1) la uokoaji ni msaada kutoka Serikali ya Ujerumani. Aidha, Serikali ya Japan imetoa msaada wa magari mawili (2) ya kuzima moto ambapo moja (1) limeshawasili nchini na jingine linatawasili kabla ya mwishoni mwa mwezi Mei, 2024.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Halmashauri ya Mji wa Tunduma imenunua gari moja (1) la kuzima moto ili kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji katika halmashauri hiyo. ***Naipongeza Halmashauri ya Mji wa Tunduma kwa jitihada hizo.***

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia bajeti ya mwaka 2023/24 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea Shilingi 1,873,917,900 kwa ajili ya ununuzi wa magari 11 ya utawala na ukaguzi. Magari hayo yatapokelewa katika mwaka 2024/25. Aidha, katika mwaka 2024/25 Shilingi 1,401,370,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari tisa (9) ya utawala na ukaguzi na Shilingi 500,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuzima moto na uokoaji.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha taratibu za upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu. Mkopo huo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 95 ulisainiwa tarehe 15 Februari, 2024 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya UAE. Aidha, Serikali imechangia Dola za Marekani milioni 5 sawa na

asilimia 5 ya gharama za mradi huo. Hivyo, ununuzi wote utagharimu Dola za Marekani milioni 100.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mkopo husika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litapatiwa vitendea kazi vya kisasa vitakavyopokelewa katika awamu nne (4) kwa kipindi cha miaka miwili (2) kuanzia 2024/25 hadi 2025/26. Awamu ya kwanza na ya pili itahusisha vifaa vya kuzima moto na uokoaji, mawasiliano na mafunzo, boti 23, magari 40 ya kubebea wagonjwa, *command cars* 30 na *mobile workshops* 6. Awamu ya tatu na ya nne zitahusisha magari 150 ya kuzima moto na uokoaji, magari matatu (3) ya kuzima moto wa kemikali (HAZMAT truck) na Helikopta moja (1).

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili vifaa husika viweze kuleta matokeo tarajiwa, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linahitaji kuwa na rasilimali watu inayotosheleza**.** Katika kuzingatia mahitaji hayo, mpango wa upatikanaji wa askari wa zimamoto 7,648 utakaotekelezwa kwa awamu tatu (3) kuanzia mwaka 2024/25. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa askari hao ikiwa ni pamoja na matumizi ya mitambo na vifaa vya kisasa vitakavyoletwa nchini.

**Uboreshaji wa Makazi ya Maafisa na Askari**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekamilisha ujenzi wa majengo sita (6) ya ghorofa kwa ajili ya makazi ya askari. Majengo hayo yamejengwa eneo la Kikombo Jijini Dodoma na yana uwezo wa kuishi familia 60. Katika mwaka 2024/25 Shilingi 2,500,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo mawili (2) ya ghorofa yenye uwezo wa kuishi familia 20 za askari katika eneo la Kikombo Jijini Dodoma.

**Ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji**

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa vituo vya Zimamoto na Uokoaji unaendelea katika mikoa saba (7) kwa gharama ya Shilingi 2,228,931,890.70. Hatua ya ujenzi iliyofikiwa hadi Aprili, 2024 ni kama ifuatavyo: Manyara asilimia 48; Njombe asilimia 62; Katavi asilimia 32;

Geita asilimia 22; Kagera asilimia 39; Simiyu asilimia 48 na Songwe asilima 50. Aidha, ujenzi wa vyumba vya kuhifadhia vifaa maalum katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam (Ilala), Dodoma na Tanga umefikia hatua zifuatazo: Ilala asilimia 97; Tanga asilimia 84; Arusha asilimia 86; na Dodoma asilimia 60.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 jumla ya Shilingi 2,600,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vituo saba (7) katika Mikoa ya Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Njombe, Simiyu na Songwe. Pia, Shilingi 236,521,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa viwanja vya ujenzi wa makazi ya askari na vituo vya zimamoto na uokoaji. Aidha, Shilingi 150,000,000 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya *Fire Hydrants* 140 katika mikoa mbalimbali nchini.

## IDARA YA UHAMIAJI

### Udhibiti wa Uingiaji na Utokaji wa Wageni na Raia Nchini

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji inaendelea kutekeleza jukumu lake la kulinda na kuimarisha hali ya usalama wa nchi kwa kusimamia na kudhibiti uingiaji, ukaaji na utokaji wa wageni na raia wa Tanzania nchini. Jukumu hili hutekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54, Rejeo la 2016; Sheria ya Pasipoti na Hati za Kusafiria ya Mwaka 2002; Sheria ya Uraia Sura ya 357, Rejeo la 2002 pamoja na Kanuni zake.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya wageni 1,695,350 waliingia nchini ikilinganishwa na wageni 1,143,645 walioingia katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hili ni ongezeko la wageni 557,705 sawa na asilimia 48. Aidha, jumla ya wageni 1,579,925 walitoka nchini ikilinganishwa na wageni 1,039,836 waliotoka katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Katika kipindi husika jumla ya wageni 412 walizuiliwa kuingia nchini kwa kutokidhi vigezo ikiwemo vya kiusalama. Pia, Watanzania 776 walirudishwa kutoka mataifa mbalimbali kutokana na kukiuka Sheria za Uhamiaji katika nchi husika.

**141.** ***Mheshimiwa Spika**,* kuongezeka kwa wageni kumetokana na jitihada za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu za kuvutia uwekezaji, utalii, biashara na shughuli nyingine za kijamii. Aidha, ili kuendelea kuvutia wageni, Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii Tanzania inaandaa mpango wa kuweka matangazo ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini kupitia Tovuti ya Idara ya Uhamiaji.

**Vibali vya Ukaazi kwa Wageni**

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, jumla ya vibali vya ukaazi 18,813 vilitolewa ambapo Daraja A ni 2,825; B – 12,460; na C – 3,528 ikilinganishwa na vibali 13,140 vilivyotolewa mwaka 2022/23 ambapo Daraja A vilikuwa 2,046; B – 8,032; na C – 3,062. Vibali vya Daraja A hutolewa kwa wawekezaji, Daraja B kwa waajiriwa na Daraja C kwa makundi mengine wakiwemo wanafunzi, watafiti na wagonjwa wanaokuja kupata matibabu nchini.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza wigo wa uwekezaji katika miradi mikubwa ya makazi (Real Estate) na kurahisisha ukaazi wa wageni katika makazi hayo, Kanuni za Uhamiaji za Mwaka 1997, zimefanyiwa marekebisho kupitia Tangazo la Serikali Na.428 la 2023. Marekebisho hayo yameweka vibali vipya vya ukaazi Daraja C11 kwa wanaotaka kununua nyumba za miradi hiyo.

**144.** ***Mheshimiwa Spika**,* pia, Idara ya Uhamiaji imetoa jumla ya Hati za Mfuasi 4,661 na Hati za Msamaha 756 ikilinganishwa na Hati za Mfuasi 4,123 na Hati za Msamaha 503 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, Visa 908,535 zilitolewa kwa wageni walioomba kuingia nchini kwa shughuli mbalimbali ikilinganishwa na Visa 767,942 zilizotolewa kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

## Pasipoti na Hati Nyingine za Safari

**145.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya Pasipoti 141,762 zimetolewa kwa Watanzania ikilinganishwa na Pasipoti 92,155 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati ya Pasipoti hizo, Pasipoti 426 zilikuwa za Kibalozi, 222 za Kiutumishi na 141,114 za Kawaida. Hati za Safari za Dharura 234,634 zimetolewa ikilinganishwa na Hati 256,471 zilizotolewa kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kwa mwaka 2024/25, Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa Pasipoti na Hati nyingine za safari kwa Raia wa Tanzania ili kuwawezesha kusafiri nje ya nchi.

**146.** ***Mheshimiwa Spika****,* kwa mujibu wa mkataba wa huduma kwa mteja wa Idara ya Uhamiaji, mwombaji wa pasipoti anayetimiza vigezo hupata pasipoti ndani ya siku saba za kazi kwa waombaji waliopo Dar es Salaam na Zanzibar. Aidha, kwa waombaji waliopo nje ya Dar es Salaam na Zanzibar hupata pasipoti ndani ya siku 14 za kazi.

## Operesheni, Misako, Doria na Ukaguzi

**147.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha hali ya usalama, Idara ya Uhamiaji imefanya operesheni, misako na doria za kawaida za kuwabaini wahamiaji haramu na wageni wengine wanaoishi nchini kinyume cha Sheria. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 jumla ya watuhumiwa 17,791 wa makosa ya kiuhamiaji walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

**148.** ***Mheshimiwa Spika****,* kupitia hotuba yangu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2023/24 nilitangaza kuondolewa kwa nchi ya Ethiopia katika orodha ya nchi zinazohitaji Visa Rejea. Kufuatia uamuzi huo, napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya Waethiopia 3,569 waliingia nchini kupitia vituo rasmi na 3,531 walitoka ikilinganishwa na Waethiopia 2,290 walioingia nchini na 2,364 waliotoka katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya Waethiopia 3,569 kuingia nchini kwa njia rasmi yamesaidia kukusanya mapato ya Dola za Marekani 178,450 sawa na takribani Shilingi 456,000,000 kutokana na huduma za Visa, kupungua kwa wahamiaji haramu waliokuwa wakitumia njia zisizo rasmi. Uamuzi huo pia umesaidia kupunguza msongamano magerezani ambapo kwa sasa raia wa Ethiopia waliopo magerezani ni 577 ikilinganishwa na 1,205 waliokuwepo mwaka 2022/23.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo mengine ni Serikali kuokoa Shilingi 8,565,600,000 ambazo zingetumika kugharamia chakula cha wafungwa raia wa Ethiopia kama wangefungwa magerezani kifungo kisichopungua miaka miwili (2) kwa mujibu wa Kifungu cha 45(2) Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 (wastani wa Shilingi 5,000 kwa siku 480). Pia, Serikali imeokoa Dola za Marekani 1,784,500 sawa na takribani Shilingi 4,460,000,000 kama wangekamatwa na kurudishwa kwao baada ya kutumikia vifungo vyao.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji itaendelea kuimarisha na kuboresha mifumo ya udhibiti na usimamizi wa uingiaji na utokaji wa watu ili kuhakikisha wanaingia nchini kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Idara inaendelea kutoa elimu kupitia kampeni ya "Mjue Jirani Yako" kupitia vyombo vya Habari kama vile radio na Televisheni. Elimu hiyo imetolewa kwa kushirikiana na watendaji kata katika Mikoa ya Kagera, Morogoro, Mtwara, Lindi na Rukwa na masheha katika Mikoa ya Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja na Kusini Unguja katika mikutano ya hadhara na shule za msingi.

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kudhibiti uhamiaji haramu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji imesaini makubaliano (MoU) na nchi za Angola, China, Indonesia na Zambia. Hatua hiyo itasaidia kudhibiti makosa ya kupangwa na yanayovuka mipaka pamoja na kubadilishana taarifa za kiintelijensia. Aidha, makubaliano hayo yatarahisisha uingiaji na utokaji wa raia na wageni kutoka mataifa husika kwa kuondoa gharama za malipo ya Visa kwa watu wanaotumia Pasipoti za Kibalozi na Kiutumishi. Nchi

nyingine 11 zinaendelea kukamilisha taratibu za ndani ili ziweze kusaini Hati za Makubaliano.

**Wageni Waliopewa Uraia wa Tanzania**

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya wageni 3,504 walipewa uraia wa Tanzania baada ya kukidhi vigezo stahiki ikilinganishwa na wageni 190 waliopewa uraia katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati ya hao, wageni 3,319 ni wahamiaji walowezi wasiohamishika wenye asili ya mataifa ya Comoro (147), Msumbiji (3,166), Burundi (5) na Rwanda (01); na wageni 185 ni kutoka mataifa mengine ya Afrika Kusini (1), Burundi (3), Congo (19), Cuba (1), India (80), Iran (1), Italia (1), Lebanon (6), Kenya (26), Msumbiji (1), Pakistan (17), Rwanda (3), Somalia (1), Syria (2), Uganda (1), Uingereza (1), Yemen (20) na Zimbabwe (1).

**Watanzania Waliopata Uraia wa Mataifa mengine**

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Watanzania 63 walipatiwa uraia wa nchi nyingine baada ya kuukana Uraia wa Tanzania ikilinganishwa na Watanzania 58 walioukana uraia wa Tanzania mwaka 2022/23. Nchi hizo ni: Botswana (1), Canada (15), India (2), Kenya (3), Marekani (5), Mauritius (1), Oman (25), Pakistan (1), Uganda (1) na Ujerumani (9). Kwa msingi huo, watu hao wanakosa sifa ya kuendelea kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia, Sura ya 357 Rejeo la 2002.

**Uboreshaji wa Vitendea Kazi kwa Idara ya Uhamiaji**

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 1,730,476,000 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi wa magari 11 na taratibu za ununuzi zimekamilika. Magari hayo yatatumika katika operesheni maalum, misako, doria, ukaguzi pamoja na shughuli za utawala katika wilaya zilizopo mipakani. Katika mwaka 2024/25 Shilingi 3,500,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari 20 ya Ofisi za Uhamiaji Wilaya.

**Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Idara ya Uhamiaji**

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2024 Idara ya Uhamiaji imepokea jumla ya Shilingi 1,264,719,641.55 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 200,208,006 ni kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara ambao umefikia asilimia 89.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi 130,000,000 ni za ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Mufindi; Shilingi 600,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba 12 za makazi ya wakufunzi katika Chuo cha Uhamiaji cha Raphael Kubaga, Tanga; na Shilingi 334,511,634.80 ni kwa ajili ya malipo ya mkandarasi wa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi.

**158.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25 Idara ya Uhamiaji inatarajia kuanza ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Songwe na ujenzi wa nyumba za makazi ya maafisa na askari watakaohudumia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato jijini Dodoma. Aidha, Idara ya Uhamiaji itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa ghorofa za makazi ya wakufunzi katika Chuo cha Raphael Kubaga mkoani Tanga. Jumla ya Shilingi 2,500,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo.

**159.** ***Mheshimiwa* Spika**, sambamba na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Idara ya Uhamiaji imepata ufadhili kutoka Shirika la Uhamaji Duniani (International Organization for Migration - IOM) wa kujengewa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Busega mkoani Simiyu kwa gharama ya Shilingi 250,000,000.

## MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

### a) Hali ya Usajili na Utambuzi wa Watu Nchini

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inaendelea kutekeleza Ibara ya 105(q) ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 inayohusu usajili na utambuzi wa watu.

Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 NIDA imesajili na kutambua jumla ya watu 880,347 sawa na asilimia 55 ya lengo la kusajili watu 1,597,827 kwa mwaka 2023/24. Kazi hiyo inaendelea kufanyika kupitia Ofisi za Usajili za Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa tangu kuanza kwa usajili na utambuzi wa watu imefikia 24,701,479 sawa na asilimia 78 ya watu 31,582,976 wenye umri kuanzia miaka 18 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Shilingi 2,932,768,570.77 zimetengwa kwa ajili ya kusajili na kutambua watu 2,389,290 wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, Shilingi 450,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza usajili na utambuzi wa watu kuanzia umri wa kuzaliwa. Usajili na utambuzi wa kundi hilo ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kutoa Namba ya Utambulisho ya Kipekee (Unique Identification Number). Namba hiyo itamtambulisha mtu wakati wa kupata huduma mbalimbali nchini. Pia, usajili huo utawezesha utekelezaji wa mipango ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiusalama.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatekeleza Mradi wa Tanzania ya Kidigiti (Digital Tanzania Project - DTP). Mradi una lengo la kutumia namba moja ya utambulisho katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kazi ya ujenzi wa mfumo wa utoaji wa namba moja ya utambulisho inaendelea.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, jumla ya Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) 751,677 zilizalishwa na kugawiwa kwa wananchi. Hivyo, kufanya jumla ya NIN zilizozalishwa kufikia 20,701,956 sawa na asilimia 84 ya idadi ya watu waliosajiliwa tangu kuanza kwa zoezi la usajili na utambuzi wa watu nchini.

**164.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuhakikisha watu wote wenye Namba za Utambulisho wanapata

vitambulisho vyao. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya vitambulisho 7,698,819 vimezalishwa na hivyo kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 20,578,325 sawa na asilimia 99 ya idadi ya Namba za Utambulisho 20,701,956 zilizozalishwa.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliandaa mkakati maalum kwa lengo la kuongeza kasi ya ugawaji na usambazaji wa vitambulisho kwa mkupuo. Mkakati huo ulizinduliwa mwezi Oktoba, 2023 mjini Musoma Mkoani Mara. Aidha, uzinduzi uliendelea kufanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kadri ya uzalishaji ulivyokamilika.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** mkakati huo umewezesha kusambaza vitambulisho 7,385,083 kwa wananchi kupitia Ofisi za Kata, Shehia, Vijiji na Mitaa. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa kila mwananchi mwenye namba ya Utambulisho Tanzania Bara na Zanzibar anapata Kitambulisho cha Taifa. **N*aomba nitoe rai kwa wananchi wote ambao bado hawajachukua vitambulisho vyao vya Taifa kufika katika ofisi za Serikali za Mitaa walipojiandikisha kwa ajili ya kuvichukua.***

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mikakati yake ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza ufanisi, ilitoa uamuzi wa kuziunganisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) ili kuwa na Taasisi moja inayoshughulika na matukio muhimu ya watu maishani. Uunganishaji huo utakwenda sambamba na usajili wa watu wenye umri chini ya miaka 18 na kutoa kitambulisho kimoja cha Taifa (Universal National Identification Card).

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji inaratibu uundwaji wa taasisi moja itakayosimamia usajili wa matukio muhimu ya watu katika maisha. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea kutoa ushirikiano stahiki ili kufikia azma hiyo ya Serikali ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza gharama za uendeshaji.

**b) Ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Kadighafi za Kuzalisha Vitambulisho**

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA imekamilisha rasimu ya andiko la awali (Pre-feasibility Study) kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha kadighafi. Kiwanda kinatarajiwa kujengwa kwa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) katika eneo la Chamakweza Halmashauri ya Chalinze, Mkoa wa Pwani. Kukamilika kwa kiwanda hiki kutawezesha Serikali kuokoa fedha za kigeni pamoja na kupunguza gharama na muda wa kuagiza kadighafi nje ya nchi. Aidha, ujenzi wa kiwanda husika utawezesha NIDA na taasisi nyingine za Serikali kupata kadighafi hapa nchini.

**c) Uunganishaji wa Mfumo wa Usajili na Utambuzi na Mifumo ya Taasisi Nyingine**

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 NIDA imeunganisha taasisi 21 katika mfumo wa usajili na utambuzi, hivyo kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa kufikia 107. Kati ya hizo, taasisi 48 ni za Serikali na 59 ni za binafsi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25 jumla ya Taasisi 35 za umma na binafsi zinatarajiwa kuunganishwa katika mfumo wa usajili na utambuzi ili kuwezesha ushirikishanaji wa taarifa na hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii.

**171.** ***Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwahamasisha watoa huduma kujiunga na Mfumo wa NIDA ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za wateja. Taarifa hizo, zitasaidia katika utambuzi wa wananchi kabla ya kutoa huduma na hivyo kupunguza udanganyifu ikiwemo ukwepaji wa kodi, utoaji wa mikopo na usajili wa laini za simu.*** Mpango huo ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuzielekeza Taasisi za Umma na Binafsi kutumia taarifa za wananchi zilizopo katika Rejista ya Usajili na Utambuzi ya NIDA ili kuepusha usumbufu kwa wananchi kuwasilisha taarifa zinazofanana kwa taasisi zaidi ya moja.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha usafirishaji wa taarifa za usajili na utambuzi kutoka ofisi za usajili za wilaya kwenda kituo cha uchakataji na uzalishaji wa vitambulisho, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 NIDA imeunganisha mtandao wa mawasiliano katika ofisi tisa (9) za usajili. Ofisi hizo ni Ngorongoro - Arusha, Buhigwe - Kigoma, Uyui - Tabora, Magharibi A, Magharibi B, Kaskazini A, Kaskazini B, Kusini Unguja na Micheweni - Zanzibar. Idadi hiyo imefanya jumla ya ofisi za usajili zilizounganishwa na mtandao kufikia 152 kati ya 153 zilizopo nchi nzima. Katika mwaka 2024/25 uunganishaji wa Ofisi ya Usajili ya Morogoro Vijijini iliyobaki utakamilishwa.

**HUDUMA KWA WAKIMBIZI**

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Huduma kwa Wakimbizi ina jukumu la kuwapokea, kuwasajili, kusimamia huduma na kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi na waomba hifadhi wanaoingia nchini.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, Tanzania inahifadhi jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi 249,803. Kati ya hao, 160,948 ni wenye asili ya Burundi, 88,257 wana asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na 598 ni kutoka mataifa mengine. Wakimbizi 200,071 wanaishi katika Kambi za Nyarugusu na Nduta - Kigoma. Wakimbizi 27,726 wanaishi katika Makazi ya Katumba na Mishamo - Katavi, Ulyankulu - Tabora na 21,508 wanaishi katika vijiji 73 vilivyopo Kigoma, 150 wapo eneo la Chogo - Tanga na 348 maeneo ya mjini.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya waomba hifadhi wapya 3,132 walipokelewa kutoka nchi za Afghanistani, Burundi, DRC, Cameroon, Eritrea, India, Misri, Syria, Palestina, Rwanda, Somalia, Sudani, Sudani Kusini, Ujerumani, Ukraine, Uturuki na Yemeni. Kati ya waomba hifadhi hao 2,951 walitoka DRC na 181 ni kutoka mataifa mengine.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama nchini itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika kambi na makazi ya wakimbizi kwa kufanya doria. Usimamizi huu unatarajiwa kuendelea kuboresha hali ya usalama katika maeneo hayo. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia huduma zote muhimu zinazotolewa kwa wakimbizi.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wakimbizi wanatafutiwa suluhisho la kudumu, Wizara itaendelea na zoezi la urejeshaji wa wakimbizi wa Burundi. Aidha, katika kikao cha 24 cha Pande Tatu baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Burundi na UNHCR kilichofanyika tarehe 30 Novemba, 2023 Jijini Dar es Salaam iliazimiwa kuwa zoezi la urejeshaji kwa hiari liingie hatua ya uhamasishaji wa pamoja ili kuongeza idadi ya wakimbizi wanaojiandikisha kwa ajili ya kurejea.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia uamuzi huo, Serikali imepanga kufunga kambi ya wakimbizi ya Nduta - Kigoma yenye wakimbizi wa Burundi 64,539 ifikapo tarehe 31 Desemba, 2024. Jumla ya Shilingi 1,731,219,000 zimetengwa katika mwaka 2024/25 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zinazohusu usimamizi wa wakimbizi na waomba hifadhi.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) imefanikiwa kuwatafutia wakimbizi 26,155 suluhisho la kudumu. Kati ya hao, wakimbizi 20,096 walirejeshwa kwa hiari nchini Burundi na wakimbizi 6,059 walihamishiwa nchi ya tatu za Marekani (5,734), Canada (279), Australia (43) na Finland (3).

**Utunzaji wa Mazingira katika Kambi na Makazi ya Wakimbizi**

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia jitihada za urejeshaji mazingira, jumla ya miti 507,850 ilipandwa katika kambi za wakimbizi na maeneo yanayozunguka. Majiko banifu 8,636 yalitengenezwa na kilogramu 317,000 za mkaa mbadala zilitengenezwa na

kugawanywa kwa wakimbizi ili kuendelea kupunguza matumizi ya kuni kama nishati ya kupikia.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba, 2023 Serikali ilisaini Mkataba na Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (United Nations Environment Program - UNEP) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa mazingira. Lengo la mradi ni urejeshaji wa mazingira kwa kupanda miti katika kambi za wakimbizi na vijiji vinavyozunguka vilivyoathiriwa kutokana na uwepo wa wakimbizi. Mradi pia utasaidia kuwezesha uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia matumizi ya nishati mbadala, utunzaji wa mazingira na utoaji wa elimu kuhusu matumizi bora ya ardhi ili kusaidia utunzaji wa mifumo ya ikolojia.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huo wa miaka mitano (2024 - 2029) wenye thamani ya Dola za Marekani 19,000,000 unafadhiliwa na Mfuko wa *Green Climate Fund* kupitia Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa. Mradi umeanza kutekelezwa mwezi Aprili, 2024 kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**USAJILI WA JUMUIYA ZA KIDINI NA ZISIZO ZA KIDINI**

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya Jumuiya 213 zilisajiliwa ikilinganishwa na Jumuiya 371 zilizosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati ya hizo, Jumuiya 95 ni za kidini na 118 zisizo za kidini. Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia utendaji wa Jumuiya zilizosajiliwa, kufanya ukaguzi pamoja na kufanya uhakiki wa Jumuiya hizo. Kupitia mazoezi ya uhakiki jamii ilipatiwa elimu kuhusu, aina ya taasisi na vikundi vinavyopaswa kusajiliwa, taratibu za usajili na kazi zinazofanywa na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya.

**184.** ***Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa watu wote kuhakikisha wanafuata taratibu zote za kisheria katika kusajili Jumuiya na kuepuka kuendesha jumuiya zisizosajiliwa kwa mujibu wa sheria, kwani kufanya hivyo ni kosa chini ya Kifungu cha 40 cha Sheria ya***

***Mabadiliko mbalimbali Na. 3 ya mwaka 2019 iliyoifanyia marekebisho Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337.***

**Kufanya Ukaguzi Shirikishi na Tathmini ya Vihatarishi kwa Jumuiya Zilizosajiliwa**

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Msajili imefanya ukaguzi na tathmini ya vihatarishi kwa Jumuiya 4,647, kati ya hizo, jumuiya 1,881 ni hai na jumuiya 2,766 zilibainika kuwa hazipo hai. Kifungu cha 20 cha Sheria ya Jumuiya, Sura 337 kinaitaka Ofisi ya Msajili kuzitangaza kwenye Gazeti la Serikali jumuiya za kiraia ambazo Msajili wa Jumuiya za Kiraia anazitilia mashaka kuwa haziko hai na kutoa muda wa miezi mitatu wa kuthibitisha uhai wake kabla ya kufutwa katika Daftari la Usajili. Katika kutekeleza matakwa hayo ya sheria, Awamu ya kwanza ya kutangaza Jumuiya 1,200 imefanyika tarehe 05 Januari, 2024 na orodha imewasilishwa kwa Mhariri Mkuu wa Gazeti la Serikali tarehe 13 Mei, 2024 kwa ajili ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali ili kuujulisha umma kuhusu kufutwa kwa usajili wa taasisi hizo. Jumuiya 1,566 zilizobaki zitatangazwa mwezi huu wa Mei, 2024.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 jumla ya Shilingi 880,386,000 zimetengwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Msajili. Wizara itaendelea kuziratibu na kuzisimamia Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini ili ziendelee kushirikiana na Serikali katika kudumisha amani, utulivu na usalama nchini. Aidha, Wizara inaendelea kuwahamasisha Viongozi wa Jumuiya za Kidini kuendelea kuliombea Taifa na Viongozi wa Kitaifa. ***Nachukua fursa hii kuwashukuru Viongozi wa Dini kwa kuitikia wito wa mwaliko wa kuhudhuria kwenye tukio hili muhimu. Hii ni ishara ya utayari wa Viongozi wa Dini na Taasisi zake kuendelea kushirikiana na Serikali katika kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa nchi yetu.***

**UDHIBITI WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU**

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu,

Sura ya 432. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, jumla ya waathirika 184 waliokuwa wakitumikishwa kuomba mitaani, kufanya kazi majumbani, kwenye mashamba, kuchunga mifugo na kwenye madangulo wameokolewa na kupewa huduma za kibinadamu. Kati ya hao, waathirika 122 walikuwa ni watoto na 62 walikuwa ni watu wazima. Aidha, wahalifu wanne (4) waliokuwa wakijihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu walihukumiwa kifungo gerezani na watuhumiwa 11 kesi zao ziko katika hatua mbalimbali za usikilizwaji.

**188.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mbinu za utambuzi na usimamizi wa waathirika, upelelezi na uendeshaji wa mashauri yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu, Wizara imetoa mafunzo kwa wadau 157 ikiwa ni sawa na asilimia 79 ya lengo la mwaka 2023/24 la kutoa elimu kwa wadau 200. Wadau hao ni pamoja na Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Polisi, Maafisa Kazi, Maafisa Uhamiaji, Maafisa Ustawi wa Jamii na watoa huduma kutoka taasisi zisizo za kiserikali. Mafunzo hayo yalitolewa katika Mikoa ya Geita, Kagera, Kigoma, Mara, Mjini Magharibi, Mwanza, Simiyu na Songwe.

**189.** ***Mheshimiwa Spika***, elimu kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu na madhara yake imeendelea kutolewa kwa umma kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, vipeperushi na maadhimisho ya Siku ya Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binadamu Duniani ambayo hufanyika tarehe 30 Julai, kila mwaka. Elimu hiyo imetolewa kupitia makongamano yaliyowahusisha Watendaji wa Kata na Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji, Masheha, Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, Viongozi wa Dini, Viongozi wa kisiasa, Wajumbe wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto na walimu. Makongamano hayo yamefanyika katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Kigoma, Kusini Unguja, Mara na Simiyu.

**190.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha udhibiti wa usafirishaji haramu wa binadamu katika pande zote za Muungano, Wizara imefungua Ofisi ya Sekretarieti Zanzibar. Ofisi hiyo ipo eneo la Dunga, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha, katika kutekeleza Ibara ya 6(3) ya Itifaki ya Palermo ya mwaka 2000

inayohimiza ushirikishwaji wa taasisi zisizo za kiserikali katika kudhibiti uhalifu wa aina hiyo, tarehe 30 Julai, 2023 Wizara ilizindua mtandao wa kupinga usafirishaji haramu wa binadamu (Tanzania Network Against Human Trafficking - TANAHUT).

**191.** ***Mheshimiwa Spika***, lengo ni kusaidia jitihada za Serikali katika kutoa huduma kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na kutoa elimu kwa umma. Mtandao huo unaundwa na mashirika 105 yasiyo ya kiserikali kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

**192.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, Wizara iliratibu mkutano wa ujirani mwema kati ya Mamlaka za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi. Mkutano huo ulifanyika tarehe 27 - 28 Februari, 2024 mkoani Kigoma ambao pamoja na mambo mengine, uliweka mikakati ya pamoja ya kudhibiti mitandao inayojihusisha na biashara ya kuwasafirisha raia wa nchi hiyo, hususan watoto wanaoletwa kutumikishwa hapa nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali imefanya mazungumzo na taasisi zinazohusika na kudhibiti usafirishaji haramu wa binadamu nchini Malaysia na kuweka mikakati ya pamoja ya kupambana na uhalifu huo.

**193.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka 2024/25 Wizara imetenga jumla ya Shilingi 1,759,824,000 kwa ajili ya kazi zifuatazo: kujenga nyumba salama moja kwa ajili ya kutoa hifadhi ya muda na ulinzi kwa waathirika na mashahidi wa usafirishaji haramu wa binadamu; kufanya operesheni za kusambaratisha mitandao inayojihusisha na uhalifu huo; kuokoa, kusaidia na kuwaunganisha waathirika na familia zao; kuandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu; na kutoa mafunzo kwa wadau na elimu kwa umma.

**194.** ***Mheshimiwa Spika**,* kazi nyingine ambazo zitatekelezwa katika mwaka 2024/25 ni: kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, kikanda na kijumuiya katika kupambana na usafirishaji haramu wa

binadamu; kununua vitendea kazi muhimu vikiwemo kompyuta na samani za ofisi; na kuanzisha Vikosi Kazi vya Mikoa vya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Vikosi kazi hivyo vitaundwa na wajumbe kutoka Ofisi ya Rais - Ikulu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji.

## D. SHUKRANI

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru Mhe. Daniel B. Sillo Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Ndugu Ally S. Gugu Katibu Mkuu na Dkt. Maduhu I. Kazi Naibu Katibu Mkuu kwa kunisaidia kusimamia vema utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, natoa shukrani zangu kwa Wakuu wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu nchini na kuwezesha wananchi kutekeleza shughuli zao za kijamii na kiuchumi. Viongozi hao ni: Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Camillus M. Wambura; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee R. Nyamka; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John W. Masunga; na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala. Pia, namshukuru Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Ndugu Ismail H. Rumatila.

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, natoa shukrani kwa Mhe. Balozi Khamis Kagasheki ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Parole na Inspekta Jenerali wa Polisi Mstaafu Saidi A. Mwema, Mwenyekiti wa Bodi ya SHIMA, pamoja na wajumbe wote wa bodi hizo kwa kusimamia vema bodi hizo na kuboresha utendaji kazi.

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** shukurani nyingine nazitoa kwa watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakiwemo Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Makamishna, Makamishna

Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Maafisa, Wakaguzi na askari kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**199.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natoa shukrani kwa nchi za Austria, Japan, Saudi Arabia, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Umoja wa Ulaya, Urusi, Jamhuri ya Watu wa China na Jamhuri ya Korea Kusini. Aidha, natoe shukrani kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni: IOM, UNDP, UNHCR, UNICEF, UNFPA, UN – Women na WFP. Taasisi za Elimu na Makampuni yafuatayo: Buzwagi Gold Mine, CAMARTEC, Chuo cha Uhasibu – Arusha, Vyuo vya Ustawi wa Jamii, NACTVET, North Mara Gold Mine, PUMA, REA, TAIFA GAS, TPA, TPDC, VETA, Taasisi za Kidini na zisizokuwa za Kidini, Vyombo vya Habari na wananchi kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu yake.

**200.** ***Mheshimiwa Spika***, mwisho na kwa umuhimu wa kipekee naishukuru kwa dhati familia yangu, Mke wangu na Watoto (Riziki, Asha na Bareek), ndugu, marafiki na jamaa kwa kunipa nguvu na moyo wa kutekeleza majukumu yangu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha,nawashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa ushirikiano na Imani kubwa wanayoendelea kunipa katika majukumu ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

## E. HITIMISHO

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea kuimarisha usalama wa watu na mali zao kupitia vyombo vya usalama vilivyopo chini yake. Jukumu hili litatekelezwa kwa kushirikiana na wadau muhimu wakiwemo wananchi katika maeneo yote nchini.

### Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2024/25

**202.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2024/25 Wizara imepanga kukusanya jumla ya Shilingi 403,300,000,000 kupitia vyanzo mbalimbali. Ili kuhakikisha kiasi hicho cha fedha kinakusanywa,

Wizara itaimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa maduhuli; kuimarisha huduma za mtandao (internet) katika Ofisi za Uhamiaji; kuongeza wigo wa matumizi ya mfumo wa Uhamiaji Mtandao (e-immigration); ununuzi wa vitendea kazi; na kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa jumuiya zilizosajiliwa chini ya Wizara ikiwemo ulipaji wa ada kwa wakati.

**Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2024/25**

**203.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba Bunge lako liidhinishe Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2024/25 yenye jumla ya **Shilingi 1,711,710,987,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 551,583,381,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Shilingi 870,429,138,000** ni Mishahara na **Shilingi 289,698,468,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, **Shilingi 285,635,968,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 4,062,500,000** ni fedha za nje.

**204.** ***Mheshimiwa Spika****,* naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO YA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, *Engineer* Hamad Yusuph Masauni. Nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi, Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iingie yote kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mapema leo hii asubuhi

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Fedha 2024/2025. Aidha, wasilisho hili naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na kuikubali kisha iidhinishe Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa niliyoiweka mezani mapema leo asubuhi imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni; sehemu ya kwanza inaonesha maelezo ya utangulizi na kubainisha msingi wa mawanda na muundo wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili iliyobainisha uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, sehemu ya tatu iliyoelezea uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, sehemu ya nne inayobainisha maoni ya ushauri pamoja na kuhitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2023/2024 na makadirio kwa mwaka 2024/2025. Sehemu hii inahusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa lengo la kufafanua hatua iliyofikiwa hadi mwezi Februari 2024. Ufafanuzi huo unagusa mambo matano yafuatayo: -

(i) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2023/2024;

(ii) Uchambuzi wa Taarifa ya Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;

(iii) Uchambuzi wa Hali ya Ukusanyaji wa Mapato;

(iv) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina;

(v) Hatua iliyofikiwa katika Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2023/2024. kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara hii ilipaswa kutekeleza jumla ya miradi 18 katika Mikoa mbalimbali nchini. Hata hivyo, kwa madhumuni ya masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi mitatu inayotekelezwa katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro na Pwani. Ufafanuzi wa hali ya Utekelezaji wa Miradi hiyo ni Kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hali ya Utekelezaji wa Miradi inakabiliwa na changamoto za kibajeti kubwa mbili: Moja ni baadhi ya miradi kutokupata kabisa fedha zilizoidhinishwa na Bunge na changamoto ya pili ni kutokupata fedha kwa wakati kwa miradi iliyopokea fedha. Kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni kuwa: -

(i) Si jambo jema kwa Miradi inayotekelezwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini ya Wizara hii kutopewa fedha za maendeleo kwa wakati;

(ii) Kukosekana kwa fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyoidhinishiwa fedha na Bunge ni jambo linalokwamisha lengo la kuwa na miradi inayotekelezwa na Wizara hii;

(iii) Utekelezaji wa miradi unaokwama kutokana na changamoto za kifedha unatatiza azma ya Serikali kuimarisha vyombo vinavyohusika na usalama wa raia na mali zao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo, upo umuhimu kwa Serikali kuendelea kuimarisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2023/2024. Aidha, uzoefu wa mkwamo wa utekelezaji wa miradi kwa mwaka wa fedha unaokwisha unastahili kutumika ili

kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Taarifa ya Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri. Wakati wa Kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kwenye Maeneo mbalimbali ya Mpango na Bajeti ya Wizara hii. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia ushauri unaotolewa, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri kuhusu uzingatiaji wa ushauri huo. ufafanuzi kamili kuhusu maelezo hayo ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 02.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Hali ya Ukusanyaji wa Mapato. Uchambuzi wa hali ya ukusanyaji wa mapato umezingatia mambo yafuatazo:-

(i) Ulinganisho wa hali ya ukusanyaji kati ya Februari 2023 na Februari 2024.

(ii) Ulinganisho wa kiasi kilichokusanywa na Makadirio kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 01;

(iii) Ulinganisho wa Kiasi kinachokusanywa kwenye kila fungu na mchango wa kiasi kilichokadiriwa kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 02.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa vigezo hivyo, Uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Kiasi kilichokusanywa hadi kufikia Mwezi Februari 2024 Machi, 2024 ni sawa na 63% ya lengo la mwaka lililopangwa;

(ii) Makusanyo ya Jeshi la Zimamoto yakilinganishwa na makadirio yalifikia 75%, Uhamiaji 63% na Jeshi la Polisi 62%. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshindwa kukusanya kiasi cha Shilingi 925, 000,000/= kutokana na

ukaguzi wa magari. Sababu zilizotolewa ni kutokukamilika kwa mazungumzo kuhusu Tozo hiyo itakavyokusanywa kupitia Ankara Jumuishi;

(iii) Makusanyo ya Jeshi la Magereza yaliyofikia 44% na Wizara Makao Makuu yaliyofikia 50% haya hayatoi matumaini ya kufikia lengo la makusanyo;

(iv) Makusanyo ya jumla kwa Wizara nzima yamefikia 63% pungufu kidogo ya kiwango kilichostahili. Hali hiyo imetokana na makusanyo hafifu katika Jeshi la Magereza na Wizara yenyewe;

(v) Makusanyo ya Jeshi la Zimamoto yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa 2.7%. lakini yamechangia kwa asilimia tatu kwenye kiasi kilichokusanywa hadi mwezi Februari, 2024;

(vi) Makusanyo ya Jeshi la Polisi, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa 28% na yamechangia 28% kwenye kiasi kilichokusanywa hadi mwezi Februari, 2024;

(vii) Makusanyo ya Jeshi la Magereza, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.4 lakini yamechangia 0.2% kwenye kiasi kilichokusanywa hadi mwezi Februari, 2024;

(viii) Makusanyo ya Wizara yenyewe, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa 0.12% lakini yamechangia kwa asilimia 0.10 kwenye kiasi kilichokusanywa hadi mwezi Februari, 2024; na

(ix) Makusanyo ya Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa 69%, taarifa ya makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo limeshachangia 69% ya kiwango kilichokusudiwa hadi mwezi Februari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kutoa matokeo yaliyotarajiwa iwapo fedha zinapatikana kama ilivyokusudiwa. Ili kujiridhisha na matokeo ya Bunge kuidhinisha Bajeti, Kamati ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa kuangalia mambo yafuatayo: -

(i) Kiwango cha jumla cha fedha kilichopatikana ikilinganishwa na jumla ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa Wizara hii kama inavyoonekana katika kielelezo namba tatu.

(ii) Uwiano wa aina ya matumizi wakati wa kupitisha bajeti ukilinganishwa na uwiano wa aina hizo kwa fedha zilizopatikana kama inavyoonekana katika kielelezo namba nne.

(iii) Uwiano wa bajeti za mafungu matano kama ilivyopitishwa na Bunge ukilinganishwa na uwiano wa fedha zilizopatikana kwa mafungu yote matano kama inavyoonekana katika kielelezo namba tano; na

(iv) Kiwango cha fedha zilizopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2024 ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo hivyo ni viashiria muhimu vya mwenendo wa kisera katika usalama wa raia na mali zao. Kwa msingi huo uchambuzi umebainisha yafuatayo: -

(i) Kiasi cha jumla ya fedha zilizopokelewa ni 55% ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara. Kiasi hicho kilipatikana katika kipindi cha robo ya tatu ya muda wa utekelezaji ambacho ni sawa na 75%;

(ii) Katika Bajeti ya Wizara iliyopitishwa na Bunge, kiasi cha matumizi ya uendeshaji *(OC)* kilikuwa ni 39% ya jumla ya

bajeti ya mafungu yote. Pia, upatikanaji wa fedha kwa matumizi ya aina hiyo umekuwa ni 41% ya jumla ya kiasi kilichopatikana kwa mafungu yote;

(iii) Kiasi cha fedha za miradi ya Maendeleo kilikuwa ni asilimia 8.1 ya bajeti yote ya Wizara iliyopitishwa na Bunge la Bajeti. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya hayo ni asilimia 4.1 ya kiasi chote kilichopokelewa;

(iv) Kiasi cha fedha kilichopatikana kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni 29% ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo;

(v) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halikupokea kiasi chochote kwa ajili ya miradi ya maendeleo ingawa jumla ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mafungu yote ni shilingi 33,630,972,628.91 hadi Februari, 2024;

(vi) Jeshi la Polisi (Fungu 28), Jeshi la Magereza (Fungu 29), Wizara yenyewe (Fungu 51) na Jeshi la Uhamiaji (Fungu 93) walipokea fedha za maendeleo chini ya 50%;

(vii) Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni 57% ya kiasi cha bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo.

(viii) Jumla ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote matano ni 91% ya jumla ya Bajeti ya Wizara nzima iliyoidhinishwa na Bunge, lakini, kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya matumizi hayo ni 68% ya jumla ya kiasi cha fedha zote kilichopokelewa na mafungu yote matano hadi Februari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba: -

(i) Kwa ujumla uendeshaji wa shughuli za kuhakikisha usalama wa raia na mali zao haukukabiliwa na changamoto kubwa. Hili limethibitishwa na taarifa za usalama wa raia zinazoonesha hali ya usalama kwa ujumla ni shwari na madhubuti;

(ii) Maandalizi ya kujiimarisha kwa shughuli za zimamoto na uokoaji kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 yanahitaji kufanyiwa kazi inavyostahili kabla ya kufikia mwezi Julai, 2024;

(iii) Mipango ya kuboresha huduma za na urekebu kwa lengo la kuongeza tija ya kuwa na magereza nchini, inafaa kuwekewa mkazo zaidi kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

(iv) Mipango thabiti ya huduma za uhamiaji, wakimbizi, uangalizi, vitambulisho vya taifa na usajili wa jumuiya ni miongoni mwa mambo yanayohitaji kuwekewa mkazo katika kipindi kilichobaki kabla ya kumaliza mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Ili kulijulisha Bunge hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri huo, Kamati ilipokea maelezo ya Mtoa Hoja kuhusu hatua iliyofikiwa katika kufanyia kazi ushauri huo. Uchambuzi wa maelezo hayo umeonesha kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri. Ufafanuzi wa kina unaonekana katika Kiambatisho Namba moja cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kulipa uzito wa kipekee suala la mahitaji ya watumishi katika Idara mbalimbali za Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetoa kibali cha ajira kwa Majeshi hayo. Kwa

kibali hicho, Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeajiri Askari 225, Fungu 28 – Jeshi la Polisi limeajiri Askari wapya 7,228, Fungu 29 – Jeshi la Magereza limeajiri Askari wapya 734 na Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji limeajiri Askari wapya 521.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzingatiaji wa ushauri huo, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kutoa fedha za maendeleo kwa wakati kwa mafungu yote ili kutekeleza kwa ufanisi miradi inayopangwa. Aidha, Wizara hii kutokupokea fedha za maendeleo kwa kiasi kinachostahili ni suala ambalo linaathiri utendaji wa vyombo vya ulinzi na usalama na taswira yake kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kamati ilichambua Mpango wa utekelezaji wa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa kulinganisha na majukumu ya msingi ya Wizara na vyombo vyake vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, uchambuzi umeonesha namna mipango iliyobainishwa na Wizara inavyoweza kuimarisha usalama wa raia na mali zao, utulivu na amani nchini, udhibiti wa uingiaji na utokaji nchini, usajlili wa Jumuiya, huduma za Vitambulisho vya Taifa na mambo mengine kuhusu majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi umeonesha mambo yafuatayo: -

(i) Kiasi cha mapato kinachokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kimeongezeka kwa asilimia tatu ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo, uzoefu wa ukusanyaji kwa mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kumudu kukusanya 63% hadi kipindi cha robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji;

(ii) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji yanategemea kufanikisha ongezeko la makadirio ya mapato lakini uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulionesha kuwa Jeshi la Uhamiaji halikuwa limefikia 75% wakati wa robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji;

(iii) Makadirio ya Makusanyo ya Fungu 28 – Jeshi la Polisi na Fungu 51 – Wizara yenyewe yanalingana na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokwisha;

(iv) Makadirio ya makusanyo kwa Fungu 29 – Jeshi la Magereza yamepungua kwa 47%. Uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha unaokwisha ulionesha umuhimu wa kupanga lengo kwa uhalisia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya matumizi kwa ajili ya maendeleo. Uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya maendeleo ulifanyika kwa kulinganisha na utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Aidha, ulinganisho ulifanyika ili kubaini uwiano wa miradi iliyopangwa kutekelezwa na shughuli za kawaida za uendeshaji. Kutokana na uchambuzi huo ilibainika kama ifuatavyo: -

(i) Matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa 17% ya jumla ya bajeti kama inavyoonekana katika Kielelezo Namba sita.

(ii) Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo yameongezeka kwa 175% ikilinganishwa na Makadirio ya mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Uwiano wa bajeti ya miradi ya maendeleo kwa bajeti nzima ya mafungu yote ya Wizara umeimarika kutoka asilimia nane ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi 17% ya bajeti yote kama inavyoonekana katika Kielelezo namba saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa ujumla. Uchambuzi kwa jumla wa makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, unaonesha yafuatayo: -

(i) Bajeti ya Wizara hii imeongezeka kwa 32% ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Makadirio ya matumizi ya aina zote katika Wizara hii yamezingatia umuhimu wa kufanikisha uimarishaji wa hali ya ulinzi, usalama, amani na utulivu nchini; na

(iii) Makadirio ya matumizi yaliyowasilishwa yasipoidhinishwa na Bunge kwa kiasi hicho au kwa nyongeza zaidi, majukumu ya Wizara hii yatakuwa mashakani na shughuli za umma nchini zitaingia matatani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri wa jumla. Kwa msingi huo, maoni na mtazamo niliyotoa, Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iweke utaratibu mzuri wa kuanza mapema maandalizi ya awali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuweza kuomba fedha za maendeleo Hazina kwa mafungu yote matano kwa wakati;

(ii) Serikali iendelee kuboresha hali ya vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii;

(iii) Serikali iendelee na mkakati wake wa kuboresha hali ya vifaa na vitendea kazi kwa Majeshi yote chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani;

(iv) Serikali iweke mikakati ya kupata hati ya umiliki wa ardhi katika maeneo yote yaliyopangwa au yanayotarajiwa kujengwa Ofisi za Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii;

(v) Pamoja na juhudi za serikali kuongeza ajira za Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Serikali iendelee kuviwezesha Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuajiri askari wengi zaidi ili kuimarisha utendaji kazi wa vyombo hivyo katika kuhudumia wananchi;

(vi) Serikali iboreshe matumizi ya teknolojia ya kisasa katika utendaji kazi wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya ndani. Kufanya hivyo kutasaidia Majeshi haya kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ambayo yanakua kwa kasi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri mahususi. Zaidi ya ushauri wa jumla, Kamati inao ushauri kwa kila Kifungu kulingana na yaliyobainika. Ushauri huo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Ili kufanikisha ustawi wa watu nchini kutokana na shughuli mbalimbali za jamii na umma, huduma za zimamoto na uokoaji zinahitaji kuendelea kuboreshwa. Kamati inashauri kuwa: -

(i) Serikali ihakikishe ujenzi unaoendelea wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika mikoa mbalimbali nchini unakamilika kama ilivyokusudiwa ili kupanua huduma za Jeshi hili katika maeneo hayo; na

(ii) Jeshi la Zimamoto na Ukoaji lijipange kutumia mbinu za kiteknolojia na za kisasa katika kupambana na majanga mbalimbali. Hili lifanyike sambamba na kutoa mafunzo mahususi ya kisasa ya zimamoto na uokoaji ndani na nje ya nchi kwa Askari wa Jeshi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu 28 – Jeshi la Polisi. Kwa kutambua nafasi ya Jeshi la Polisi katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kufanikisha amani, utulivu na ustawi katika Jamii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kusimamia inavyostahili katika kuhakikisha Askari wa Jeshi la Polisi wanazingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Miiko, Weledi na Maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wao;

(ii) Jeshi la Polisi lijikite katika matumizi ya vifaa vya kisasa vya kiteknolojia katika kukabiliana na uhalifu. Hatua hii iende sambamba na kutoa mafunzo ya kisasa kwa askari ili kuwawezesha kutumia vifaa hivyo katika utekelezaji wa majukumu yao; na

(iii) Jeshi la Polisi liendelee kuimarisha ushiriki wa jamii katika dhana nzima ya usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu 29 – Jeshi la Magereza. Ili kudhibiti amani katika jamii kwa kuimarisha huduma za magereza na kuboresha tija ya shughuli za urekebu magerezani, Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iendelee kutoa fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge. Aidha, upatikanaji wa fedha hizo ulingane na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija inayokusudiwa;

(ii) Jeshi la Magereza liandae mkakati wa kuboresha miundombinu chakavu kwenye baadhi ya magereza nchini kwa awamu ikiwa ni sehemu ya kuboresha mafunzo ya urekebu kwa wafungwa nchini;

(iii) Serikali iliwezeshe Jeshi la Magereza kupata magari hususan kwa ajili ya kusafirisha mahabusu. Kufanya hivyo kutakwenda sambamba na mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita wa kuimarisha mfumo wa Haki Jinai nchini;

(iv) Kama sehemu ya kuimarisha Mfumo wa Haki Jinai nchini, Jeshi la Magereza litekeleze kwa ukamilifu na ufanisi

mpango wa kuimarisha huduma za Mahakama Mtandao kwa kujenga vyumba maalum katika magereza 20 yaliyopangwa kufungwa mfumo huo katika mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu 51 – Wizara. Uchambuzi wa taarifa na makadirio kwa Fungu 51 umeipa kamati nafasi ya kushauri ifuatavyo: -

(i) Wizara iisimamie kwa karibu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* kuhakikisha kuwa inatekeleza mpango wa utambuzi wa watu kwa kutoa Jamii Namba kwa Raia Halali wa Tanzania, ikiwemo watoto kuanzia chini ya mwezi mmoja. Jamii Namba hiyo ndio itakuwa namba ya utambulisho wa wananchi katika kila eneo;

(ii) Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya *Parole* ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi katika utekelezaji pamoja na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kufanya marekebisho ili kuiboresha inavyostahili;

(iii) Serikali iandae mkakati wa kudhibiti mapema jumuiya zote zinazoendesha shughuli zake kinyume na malengo yaliyoainishwa wakati wa usajili;

(iv) Serikali iboreshe Muundo wa Idara ya Huduma kwa Wakimbizi kwa kuanzisha kitengo maalum cha kufuatilia wakimbizi waliopo nje ya makambi na makazi ya wakimbizi ili kitengo hicho kiweze kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mpango wa kuwatafuta, kuwatambua na kuwachukulia hatua za kisheria wakimbizi walio nje ya makazi na makambi ya wakimbizi;

(v) Wizara pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji zishirikiane na Wizara ya Fedha na kuainisha namna bora

ya Fungu 14, litakusanya maduhuli yatokanayo na tozo za ukaguzi wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji. Kwa upande wa Jeshi la Uhamiaji nchini, Kamati inashauri kuwa: -

(i) Serikali iendelee kuliwezesha Jeshi la Uhamiaji kupata vyombo vya usafiri ili kuwabaini wahamiaji wasio halali na kuwachukulia hatua stahiki kwa mujibu wa sheria;

(ii) Serikali iandae mkakati wa kuliwezesha Jeshi la Uhamiaji kufunga Mfumo wa Uhamiaji Mtandao katika Ofisi zote za Uhamiaji zisizo na mifumo hiyo sambamba na mfumo wa udhibiti wa mipaka kwenye ofisi na baadhi ya vituo vya kuingia na kutoka nchini;

(iii) Serikali iendelee na mkakati wa makusudi wa kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zaidi ya 1,000 katika mikoa mbalimbali ya mipakani ikiwemo kutumia mifumo ya udhibiti ya mipaka *(e-border)*; na

(iv) Uboreshaji wa Jeshi la Uhamiaji katika matumizi ya vifaa na vitendea kazi uende sambamba na kutoa mafunzo kwa askari ili waweze kutumia vifaa na vitendea kazi hivyo kwa ufanisi na kupata tija iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kutoa shukurani za Kamati kwa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mbunge, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na

Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote Kamati ilipokutana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi *(ndc)*. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili kujadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, kwa wasilisho hili, naliomba Bunge lako tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali kisha liidhinishe Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja pamoja na maoni na ushauri wa Kamati.

## 1.2 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja, zimeweka masharti yanayohusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilifanya uchambuzi na kupata maudhui ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na uchambuzi huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge yaliyohusu kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Kazi hiyo, ilifanyika kati ya tarehe 12 na 14 Machi, 2024. Nafurahi kulijulisha Bunge kuwa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulitumia matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi.

## 1.3 Mawanda ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, kama inavyofahamika, mawanda ya Taarifa ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara yanategemea muundo na majukumu ya Wizara inayohusika. Muundo na Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

umejengwa kwenye msingi wa Hati Idhini kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 383 na 385 la tarehe 7 Mei, 2021 pamoja na marekebisho yaliyofanyika kwa Tangazo la Serikali Na. 534 la tarehe 2 Julai, 2021.[1]

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii ilianzishwa na kupewa majukumu ya kushughulikia uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera zinazohusu usalama wa raia na mali zao, uhamiaji, wakimbizi na uraia nchini. Aidha, Wizara hii inahusika na utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Jeshi la Uhamiaji. Vilevile, Wizara imepewa wajibu wa kusimamia na kuratibu masuala ya Huduma za Wakimbizi, Vitambulisho vya Taifa, Usajili wa Jumuiya za Kidini na zisizo za kidini na Huduma za Uangalizi (Probation).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa wigo huo wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, uchambuzi uliofanywa na Kamati umejumuisha Mafungu matano (5) ya kibajeti ambayo ni:-

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Fungu 14 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; |
| (ii) | Fungu 28 | Jeshi la Polisi; |
| (iii) | Fungu 29 | Jeshi la Magereza; |
| (iv) | Fungu 51 | Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); na |
| (v) | Fungu 93 | Jeshi la Uhamiaji |

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilitengwa kwenye Mafungu hayo. Aidha, Bajeti inayoombwa na Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 nayo imetengwa kwenye Mafungu hayo. Kwa msingi huo, Uchambuzi unaozingatia

[1]Taz. https://www.moha.go.tz

mafungu hayo, umegusa wigo mpana wa dhima ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

### 1.4 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia urahisi wa kuelezea matokeo ya uchambuzi kwa namna inayoweza kueleweka kwa pamoja na masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge kuhusu Muundo wa Taarifa ya Kamati ya Bunge inayoingia Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya Kwanza inayoeleza maelezo ya utangulizi na kubainisha msingi, mawanda na muundo wa Taarifa;

(b) Sehemu ya Pili inayobainisha Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezajiwa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(c) Sehemu ya nne inayoelezea uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa fedha 2024/2025; na

(d) Sehemu ya Nne inayobainisha maoni na ushauri pamoja na kuhitimisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muundo huo, Kamati inaamini kuwa maudhui na mtiririko huu utakuwa na manufaa kwa Bunge na kwa Wabunge watakaopata fursa ya kuchangia katika hoja hii. Aidha, maoni na ushauri wa Kamati utapata msingi na kuwa rahisi kuzingatiwa na Bunge na Mtoa Hoja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/2024 NA MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Masharti ya Kanuni ya 117(1) na (2) ya Kanuni za Bunge yamebainisha idadi ya siku kwa ajili ya kutembelea miradi na kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti. Jumla ya siku zisizozidi saba zilipaswa kutumika kwenye ziara hizo na siku zisizozidi tisa zilipaswa kutumika kwa ajili ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji na Makadirio ya Bajeti. Nafurahi kulijulisha Bunge kuwa masharti hayo yalizingatiwa. Kwa kufanya hivyo, Kamati inaweza kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kulijulisha Bunge hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi iliyoidhinishiwa Fedha kwa mwaka 2023/2024;

(b) Kubainisha mwenendo wa upatikanaji wa fedha ulivyo ikilinganishwa na makusudio ya Bunge lilipopitisha Bajeti ya Wizara hiyo;

(c) Kulinganisha uzoefu unaojitokeza katika utekelezaji wa bajeti inayokwisha na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka unaofuata; na

(d) Kutoa ushauri utakaoliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo wajibu wa kuishauri Serikali wakati wa kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

## 2.2 Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya Taarifa inahusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa lengo la kufafanua hatua iliyofikiwa hadi kufikia Mwezi Februari 2024. Ufafanuzi huo unagusa mambo matano yafuatayo:-

(i) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2023/2024;

(ii) Uchambuzi wa Taarifa ya Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri;

(iii) Uchambuzi wa Hali ya Ukusanyaji wa Mapato

(iv) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

(v) Hatua iliyofikiwa katika Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mambo hayo manne yanatoa taswira muhimu kwa Bunge kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Bunge litakapotaarifiwa kuhusu mambo hayo, litakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kujadili hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliyoiweka mezani mapema leo hii.

### 2.2.1 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara hii ilipaswa kutekeleza jumla ya miradi 18 katika Mikoa mbalimbali nchini. Hata hivyo, kwa madhumuni ya masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi mitatu inayotekelezwa katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro na Pwani. Ufafanuzi wa hali ya Utekelezaji wa Miradi hiyo ni **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya Utekelezaji wa Miradi inakabiliwa na changamoto za kibajeti kubwa mbili: Moja ni baadhi ya miradi kutokupata kabisa fedha zilizoidhinishwa na Bunge na changamoto ya pili ni kutokupata fedha kwa wakati kwa miradi iliyopokea fedha. Kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni kuwa:

(i) Si jambo jema kwa Miradi inayotekelezwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini ya Wizara hii kutopewa fedha za maendeleo kwa wakati;

(ii) Kukosekana kwa fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyoidhinishiwa fedha na Bunge ni jambo linalokwamisha lengo la kuwa na miradi inayotekelezwa na Wizara hii;

(iii) Utekelezaji wa miradi unaokwama kutokana na changamoto za kifedha unatatiza azma ya Serikali kuimarisha vyombo vinavyohusika na usalama wa raia na mali zao kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mtazamo huo, upo umuhimu kwa Serikali kuendelea kuimarisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2023/2024. Aidha, uzoefu wa mkwamo wa utekelezaji wa miradi kwa mwaka wa fedha unaokwisha unastahili kutumika ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaokuja.

### 2.2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa Kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kwenye Maeneo mbalimbali ya Mpango na Bajeti ya Wizara hii. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia ushauri unaotolewa, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri kuhusu uzingatiaji wa ushauri huo. Maelezo kamili kuhusu maelezo hayo yanafafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 02**.

### 2.2.3 Uchambuzi wda Hali ya Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa hali ya ukusanyaji wa mapato yaliyokadiriwa umezingatia ulinganisho wa namna zifuatazo:-

(i) Ulinganisho wa hali ya ukusanyaji kati ya Februari 2023 na Februari 2024.

(ii) Ulinganisho wa kiasi kilichokusanywa na Makadirio kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 01**


**Kielelezo Na. 1 Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Makusanyo kwa kila Fungu**

| FUNGU | Makadirio ya Mapato kwa mwaka 2023/2024 | Makusanyo hadi Februari, 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **14 – Zimamoto** | 11,000,000,000 | 8,239,863,356.5 | 75 |
| **28 – Polisi** | 110,500,000,000 | 68,240,670,717.05 | 62 |
| **29 – Magereza** | 1,500,000,000 | 660,663,974 | 44 |
| **51- Wizara** | 500,000,000 | 249,730,654 | 50 |
| **93- Uhamiaji** | 270,000,000,000 | 170,174,953,905.7 | 63 |
| **JUMLA** | **393,500,000,000** | **247,565,882,605.25** | 63 |


(iii) Ulinganisho wa Mchango wa kiasi kinachokusanywa kwenye kila Fungu na mchango wa kiasi kilichokadiriwa kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 02.**

**Kielelezo Na. 2 Ulinganisho wa Makadirio ya Mchango wa Kila Fungu katika Mapato na Mchango halisi kwenye Makusanyo**

**MCHANGO WA KILA FUNGU WAKATI WA MAKADIRIO**




**MCHANGO WA KILA FUNGU KATIKA MAKUSANYO**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika**, vigezo vitatu vilivyotajwa, vimezingatiwa katika Uchambuzi kwa kuwa vinabainisha uthabiti wa makadirio na ufanisi wa juhudi za ukusanyaji wa mapato. Aidha, uchambuzi wa namna hiyo unaonesha sehemu zinazohitaji kuwekewa mkazo na sehemu zinazostahili kutumainiwa zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa vigezo hivyo, Uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Kiasi kilichokusanywa hadi kufikia Mwezi Februari 2024 Machi, 2024 ni sawa na **asilimia 63** ya lengo la mwaka lililopangwa**;**

(ii) Makusanyo ya Jeshi la Zimamoto yakilinganishwa na makadirio yalifikia **asilimia 75,** Uhamiaji **asimia 63** na Jeshi la Polisi **asilimia 62.** Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshindwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 925, 000,000/=** kutokana na ukaguzi wa magari. Sababu zilizotolewa ni kutokukamilika kwa

mazungumzo kuhusu Tozo hiyo itakavyokusanywa kupitia Ankara Jumuishi;

(iii) Makusanyo ya Jeshi la Magereza yaliyofikia **asilimia 44** na Wizara Makao Makuu yaliyofikia **asilimia 50** hayatoi matumaini ya kufikia lengo la makusanyo;

(iv) Makusanyo ya jumla kwa wizara nzima yamefikia **asilimia 63** pungufu kidogo ya kiwango kilichostahili. Hali hiyo imetokana na makusanyo hafifu katika Jeshi la Magereza na Wizara yenyewe;

(v) Makusanyo ya Jeshi la Zimamoto yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 2.7**. Taarifa zinaonesha yamechangia kwa **asilimia 3** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Mwezi Februari, 2024;

(vi) Makusanyo ya Jeshi la Polisi, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 28** na yamechangia **asilimia 28** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Mwezi Februari, 2024;

(vii) Makusanyo ya Jeshi la Magereza, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.4** lakini yamechangia kwa **asilimia 0.2** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Mwezi Februari, 2024;

(viii) Makusanyo ya Wizara yenyewe, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.12** lakini yamechangia kwa **asilimia 0.10** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Mwezi Februari, 2024; na

(ix) Makusanyo ya Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 69**, taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo limeshachangia **asilimia 69** ya kiasi kilichokusanywa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaweza kuongeza lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Jeshi la Polisi na Jeshi la Uhamiaji yanahitaji kuongeza juhudi kidogo ili kuboresha makusanyo yanayotakiwa. Kwa upande wa Jeshi la Magereza, juhudi kubwa inahitajika katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, kuna umuhimu wa kufanya tathmini ya lengo la makusanyo kwa upande wa Jeshi la Magereza na Wizara yenyewe ya Mambo ya Ndani.

### 2.2.4 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** bajeti inayoidhinishwa na Bunge hutoa matokeo yaliyotarajiwa iwapo fedha zinapatikana kama ilivyokusudiwa. Ili kujiridhisha na matokeo ya Bunge kuidhinisha Bajeti, Kamati ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa kuangalia mambo yafuatayo:-

(i) Kiwango cha Jumla ya fedha iliyopatikana ikilinganishwa na jumla ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa Wizara hii kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 03**.

**Kielelezo Na. 3 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na Kiasi cha Fedha iliyopatikana kwa kila Fungu**


| FUNGU | Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2023/2024 | Asilimia | Fedha iliyopatikana hadi Februari 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **14-ZIMAMOTO** | 56,247,435,000 | 4 | 29,358,164,968.29 | 4 |
| **28-Polisi** | 797,962,459,000 | 61 | 511,796,711,207.89 | 61 |
| **29-Magereza** | 260,694,221,000 | 20 | 169,365,816,211.79 | 20 |
| **51-Wizara** | 80,473,600,000 | 7 | 46,426,294,246.94 | 6 |
| **93-Uhamiaji** | 98,443,188,000 | 8 | 74,366,220,098.16 | 9 |
| **JUMLA** | **1,293,820,903,000** | **100** | **831,313,206,730** | **100** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara


(ii) Uwiano wa aina ya matumizi wakati wa kupitisha bajeti ukilinganishwa na uwiano wa aina hizo kwa fedha zilizopatikana kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 04**.

**Kielelezo Na. 4 Makadirio ya Uwiano wa Aina za Matumizi ukilinganishwa na Uwiano wa Upatikanaji wa fedha kwa Aina za Matumizi**

**Uwiano wakati wa Makadirio**




**Uwiano katika upatikanaji wa fedha**





**Chanzo:Randama ya Wizara 2024/2025**


(iii) Uwiano wa bajeti za Mafungu matano kama ilivyopitishwa na Bunge ukilinganishwa na uwiano wa fedha zilizopatikana kwa mafungu yote matano kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 05**;

**Kielelezo Na. 5 Uwiano wa Bajeti kwa kila Fungu ukilinganishwa na Uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa Miongoni mwa Mafungu hayo**

**Uwiano wakati wa makadirio**




**Uwiano katika upatikanaji wa fedha**




(iv) Kiwango cha fedha zilizopatikana hadi kufikia Mwezi Februari 2024 kikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023.

**Mheshimiwa Spika**, vigezo hivyo ni viashiria muhimu vya mwenendo wa kisera katika usalama wa raia na mali zao kwenye shughuli za umma kwa ujumla. Ulinganishaji unabainisha maeneo yanayohitaji msisitizo na ambayo yanaimarisha shughuli za umma, ustawi, amani

na utulivu nchini. Mambo hayo kwa ujumla ni sehemu ya mambo muhimu yanayostahili jicho la chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia hayo, Uchambuzi umebainisha yafuatayo:-

(i) Kiasi cha Jumla ya fedha zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia Mwezi Februari, 2024, ni **asilimia 55** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara. Kiasi hicho kilipatikana katika kipindi cha robo ya tatu ya muda wa utekelezaji ambacho ni sawa na **asilima 75**;

(ii) Wakati Bunge lilipoidhinisha Bajeti ya Wizara hii, Kiasi cha Matumizi ya Uendeshaji (OC) kilikuwa ni **asilimia 39** ya Jumla ya Bajeti ya Mafungu yote. Lakini upatikanaji wa fedha kwa matumizi ya aina hiyo umekuwa ni **asilima 41** ya jumla ya fedha kiasi kilichopatikana kwa Mafungu yote.

(iii) Kiasi cha fedha kwa ajili ya miradi ya Maendeleo kilikuwa ni **asilimia 8.1** ya bajeti yote ya Wizara wakati Bunge lililopitisha Bajeti. Lakini hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 fedha zilizopatikana kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 4.1** ya Jumla ya fedha iliyopokelewa na Wizara.

(iv) Kiasi cha Fedha kilichopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 29** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo.

(v) Jeshi la Zimamoto na uokoaji halikupokea kiasi chochote kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ingawa jumla ya fedha zilizopokewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Mafungu yote ni **Shilingi 33,630,972,628.91**

(vi) Jeshi la Polisi (Fungu 28), Jeshi la Magereza (Fungu 29), Wizara yenyewe (Fungu 51) na Jeshi la Uhamiaji (Fungu 93) walipokea fedha za maendeleo **chini ya asilimia 50.**

(vii) Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge kwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara yenyewe kilikuwa ni **asilimia 41 y**a Bajeti yote kwa miradi ya Maendeleo kwenye Mafungu matano. Lakini kiasi cha Fedha kilichopatikana kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara yenyewe ni **asilimia 62 ya** fedha za miradi ya maendeleo zilizopatikana kwa mafungu yote matano.

(viii) Kiasi cha Fedha kilichopokewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni **asilimia 57** ya kiasi cha bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo.

(ix) Jumla ya Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote matano ni **asilimia 91** ya jumla ya bajeti ya Wizara nzima iliyoidhinishwa na Bunge. Lakini kiasi cha fedha kilichopokewa kwa ajili ya matumizi hayo ni **asilimia 68** ya jumla ya kiasi cha cha fedha zote kilichopokewa kwa mafungu yote matano.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni wa kuridhisha. Uchambuzi umeonesha kuwa kwa Mafungu yote, Wizara imepokea zaidi ya asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Mishahara na matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, uchambuzi umeonesha kuwa kuna mtiririko wa fedha usioridhisha. Kwa mfano, Fungu 28- Jeshi la Polisi, Fungu 29 Jeshi la Magereza na 93 Jeshi la Uhamiaji yamepata fedha za maendeleo chini ya asilimia 50. Aidha, Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halikupata kabisa Fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba:

(i) Kwa ujumla uendeshaji wa shughuli za kuhakikisha usalama wa raia na mali zao haukukabiliwa na changamoto kubwa. Hili limethibitishwa na taarifa za usalama wa raia zinazoonesha hali ya usalama kwa ujumla ni shwari na madhubuti;

(ii) Maandalizi ya kujiimarisha kwa shughuli za zimamoto na uokoaji kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 yanahitaji kufanyiwa kazi inavyostahili kabla ya kufikia mwezi Julai 2024;

(iii) Mipango ya kuboresha huduma za na urekebu kwa lengo la kuongeza tija ya kuwa na magereza nchini inafaa kuwekewa mkazo zaidi kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

(iv) Mipango thabiti ya huduma za uhamiaji, wakimbizi, uangalizi, vitambulisho vya taifa, usajili wa Jumuiya ni miongoni mwa mambo yanayohitaji kuwekewa mkazo katika kipindi kilichobaki kabla ya kumaliza Mwaka wa fedha 2023/2024.

### 2.2.5 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Ili kulijulisha Bunge hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa Ushauri huo, Kamati ilipokea maelezo ya Mtoa Hoja kuhusu hatua iliyofikiwa katika kufanyia kazi ushauri huo. Uchambuzi wa maelezo hayo umeonesha kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri. Ufafanuzi wa kina unaonekana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kulipa uzito wa kipekee suala la mahitaji ya watumishi katika Idara na Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Taarifa iliyowasilishwa ilieleza kuwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali imetoa kibali cha ajira kwa Majeshi hayo. Kwa kibali hicho, Fungu 14 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeajiri Askari wapya 225, Fungu 28 – Jeshi la Polisi Askari wapya 7,228, Fungu 29-

Jeshi la Magereza Askari wapya 734 na Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji Askari wapya 521.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na uzingatiaji wa ushauri, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kutoa fedha za maendeleo kwa wakati kwa mafungu yote ili kutekeleza kwa ufanisi miradi inayopangwa. Aidha, Wizara hii kutokupokea fedha za maendeleo kwa kiasi kinachostahili ni suala ambalo linaathiri utendaji wa vyombo vya ulinzi na usalama na taswira yake kwa umma.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge yalitaka uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha unaoisha ili uzoefu wake utumike kwa mwaka wa fedha unaofuata. Aidha, uchambuzi wa makadirio kwa mwaka wa fedha 2024/2025 unafanyika kwa madhumuni ya kuhusianisha na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za umma chini ya Wizara hii. Kwa madhumuni hayo uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:

(i) Mpango unaolengwa kutekelezwa na wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Malengo ya ukusanyaji wa mapato;

(iii) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida; na

(iv) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

### 3.2 Uchambuzi wa Mpango wa Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ulilenga kubaini iwapo, fedha zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge zinawezesha tija ya majukumu ya Wizara hii. Kufikia azma hiyo, Kamati ilichambua Mpango wa utekelezaji wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kulinganisha na majukumu ya msingi ya wizara na vyombo vyake vyote.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa**,** uchambuzi umeonesha namna mipango iliyobainishwa na Wizara inavyowezesha kuimarisha usalama wa raia na mali zao, utulivu na amani nchini, udhibiti wa uingiaji na utokaji nchini, usajlili wa Jumuiya, huduma za vitambulisho vya Taifa na mambo mengine kuhusu majukumu ya Wizara hii.

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii umefanyika kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Ulinganisho wa lengo la mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na ukusanyaji ili kuona uhalisia wa lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Uwiano wa mchango wa makadirio kwa kila Fungu ikilinganishwa na uzoefu wa mchango wa makusanyo ya kila Fungu kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

(iii) Uwiano wa bajeti ya matumizi kwa lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ukilinganishwa na hali ilivyokuwa kwa ukusanyaji na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Lengo ni kujiridhisha zaidi na maeneo yanayohitaji msisitizo katika ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Uchambuzi yanaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Kiasi cha mapato kinachokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kimeongezeka kwa **asilimia 3** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo, uzoefu wa ukusanyaji kwa mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kumudu kukusanya **asilimia 63** hadi kipindi cha robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji.

(ii) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji yanategemewa kufanikisha ongezeko la makadirio ya mapato. Lakini uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulionesha kuwa Jeshi la Uhamiaji halikuwa limefika asilimia 75 wakati wa Robo ya tatu ya Kipindi cha Utekelezaji.

(iii) Makadirio ya Makusanyo kwa Fungu 28 - Jeshi la Polisi na Fungu 51- Wizara yenyewe yanalingana na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokwisha.

(iv) Makadirio ya Makusanyo kwa 29 – Jeshi la Magereza yamepungua kwa **asilimia 47.** Uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha unaokwisha ulionesha umuhimu wa kupanga lengo kwa uhalisia zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, hali ya vitendea kazi na upungufu wa rasilimaliwatu vinaendelea kuwa changamoto. Uzoefu wa hali katika kipindi cha miaka mitano unaonesha kuwa, mambo hayo yamekuwa yakiathiri makusanyo ya mapato. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, changamoto hizo zisipofanyiwa kazi lengo la makusanyo linalowekwa linaweza lisifikiwe.


### 3.3.1 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Makadirio ya bajeti ya Maendeleo ulifanyika kwa kulinganisha na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, ulinganisho ulifanyika ili kubaini

uwiano wa miradi inayopangwa kutekelezwa na shughuli za kawaida za uendeshaji. Kutokana na uchambuzi huo ilibainika kama ifuatavyo:-

(i) Matumizi kwa ajili ya Miradi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa asilimia 17 ya jumla ya Bajeti kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 06.**

**Kielelezo Na. 6 Mchanganuo wa Aina za Matumizi kwa Asilimia ya Jumla ya Bajeti inayokadiriwa**





***Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025***

(ii) Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo yameongezeka kwa asilimia 173 ikilinganishwa na Makadirio kwa mwaka wa fedha 2023/2024;


(iii) Uwiano wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Bajeti nzima ya Mafungu yote ya Wizara umeimarika kutoka asilimia 8 Mwaka 2023/2024 hadi asilimia 17 ya bajeti yote kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 07**.

**Kielelezo Na. 7 Ulinganisho wa Uwiano wa Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ukilinganishwa na uwiano wa makadirio ya Bajeti hiyo kwa Mwaka 2024/2025**

**Makadirio kwa mwaka 2023/2024**




**Makadirio kwa mwaka 2024/2025**




### 3.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ujumla

**Mheshimiwa Spika,** Mbali na uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya uchambuzi wa jumla wa makadirio kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Wizara hii imeongezeka kwa **asilimia 32** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo halitakuwa na mantiki iwapo Wizara haitahakikisha kuwa, Mafungu yote yanakamilisha taratibu za awali za kuomba fedha kwa wakati

na kwamba HAZINA itatoa fedha zinazohusika kama inavyostahili.

(iii) Makadirio ya Matumizi ya aina zote katika Wizara hii yamezingatia umuhimu wa kufanikisha uimarishaji wa hali ya Ulinzi, Usalama, Amani na utulivu nchini; na

(iv) Makadirio ya Matumizi yaliyowasilishwa yasipoidhinishwa na Bunge kwa kiasi hicho au kwa nyongeza zaidi, majukumu ya Wizara hii yatakuwa mashakani na shughuli za umma nchini zitaingia matatani.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA HITIMISHO

### 4.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi ulioelezewa katika Taarifa hii, umejenga msingi wa jumla wa mtazamo wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja. Aidha, Mtazamo huo unazingatia matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji na ufuatiliaji wa kawaida wa shughuli za Wizara hii. Kwa msingi huo, Kamati ina mtazamo ufuatao:-

(i) Makadirio ya matumizi ya fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo yatakuwa na mantiki ikiwa Wizara kupitia Taasisi zake zitaweka utaratibu mzuri wa kuanza na kukamilisha taratibu za awali mapema ili kuweza kuomba fedha hizo HAZINA kwa wakati. Kushindwa kukamilisha taratibu hizo mapema si jambo lenye afya kwa miradi ya Maendeleo;

(ii) Juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara hii ni jambo la kupongezwa na kujivunia. ili kuendelea kuimarisha utendaji utakaozingatia matumizi ya teknolojia mtiririko wa fedha kwa ajili

ya vyombo hivyo ni suala la kupewa umuhimu stahili wakati wote kwa kuzingatia mipango iliyopo;

(iii) Pamoja na juhudi za Serikali katika kutatua changamoto ya Uhaba wa vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii, changamoto hiyo isipoendelea kupatiwa utatuzi, utendaji utaendelea kuathirika;

(iv) Uamuzi wa Serikali wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Polisi kwenye kata mbalimbali nchini kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI unastahili kuendelezwa na kuungwa mkono. Uamuzi huu unaongeza tija katika azma ya kuimarisha utulivu, amani, usalama, misingi ya haki na kuweka mustakabali wa jamii katika ngazi za chini kiutawala;

(v) Matumizi ya vifaa vya kisasa na vya kidijitali yanahitaji kuzingatiwa ipasavyo wakati wa Ujenzi wa Ofisi za Vyombo vya Ulinzi vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kufanya hivyo kwa sasa ni jambo linalowezesha vyombo hivyo kuendelea kuwa madhubuti na kwa sasa na badaye kama ilivyobainishwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 katika ukurasa wa 155-160;

(vi) Kitendo cha kushindwa kukusanya maduhuli kwa maelezo kuwa Taasisi za Serikali hazijakubaliana namna ya kukusanya ni jambo lisilofaa kwa kuwa hali hiyo inasababisha Serikali kukosa mapato yanayostahili; na

(vii) Ujenzi wa ofisi za Majeshi yaliyochini ya Wizara unaondelea katika sehemu mbalimbali nchini usipofanyika sambamba na upimaji wa maeneo hayo na kupata hati, utaendelea kuwa chanzo cha migogoro kwa wakati ujao.

### 4.2 Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi wa Maoni na mtazamo niliyotoa, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iweke utaratibu mzuri wa kuanza mapema maandalizi ya awali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuweza kuomba fedha za Maendeleo HAZINA kwa mafungu yote Matano kwa wakati.

(ii) Serikali iendelee kuboresha hali ya vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Kufanya hivyo, kutaboresha utendaji kazi wa Majeshi haya katika kukabiliana na uhalifu pamoja na majanga mbalimbali na hivyo kuboresha hali ya usalama wa raia na mali zao.

(iii) Serikali iendelee na mkakati wake wa kuboresha hali ya vifaa na vitendea kazi kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kufanya hivyo kutaongeza ufanisi wa Majeshi hayo katika utendaji kazi ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli.

(iv) Serikali iweke mikakati ya kupata Hati ya Umiliki wa ardhi katika maeneo yote yaliyopangwa au yanayotarajiwa kujengwa Ofisi za Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Mkakati huu uende sambamba na kupata Hati kwa maeneo yote yenye Ofisi za Majeshi hayo yasiyo na Hati.

(v) Pamoja na juhudi za serikali kuongeza ajira kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Serikali iendelee kuviwezesha Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuajiri Askari wengi zaidi ili kuimarisha utendaji kazi wa vyombo hivyo katika kuhudumia wananchi.

(vi) Serikali iboreshe matumizi ya teknolojia ya kisasa katika utendaji kazi wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya ndani. Kufanya hivyo kutasaidia Majeshi haya kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ambayo yanakuwa kwa kasi Duniani.

### 4.3 Ushauri Mahsusi

**Mheshimiwa Spika**, Zaidi ya Ushauri wa jumla, Kamati inao ushauri kwa kila Fungu kulingana na yaliyobainika. Ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

### 4.3.1 Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

**Mheshimiwa Spika**, Ili kufanikisha ustawi wa watu nchini kutokana na shughuli mbalimbali za jamii na za umma, Huduma za Zimamoto na uokoaji zinahitaji kuendelea kuboreshwa. Kamati inashauri kuwa:

(i) Serikali ihakikishe Ujenzi unaoendelea wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Mikoa mbalimbali nchini unakamilika kama ilivyokusudiwa ili kupanua huduma za Jeshi hili katika maeneo hayo. Kufanya hivyo kutaboresha utendaji katika kutoa huduma za Zimamoto na Uokozi nchini; na

(ii) Jeshi la Zimamoto na Ukoaji lijipange kutumia mbinu za kiteknolojia na za kisasa katika kupambana na majanga mbalimbali. Hili lifanyike sambamba na kutoa mafunzo mahsusi ya kisasa ya zimamoto na uokozi ndani na nje ya nchi kwa Askari wa Jeshi hili.

### Fungu 28- Jeshi la Polisi

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua nafasi ya Jeshi la Polisi katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kufanikisha amani, utulivu na ustawi katika Jamii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kusimamia inavyostahili katika kuhakikisha Askari wa Jeshi la Polisi wanazingatia Sheria, Kanuni, taratibu, miiko, weledi na maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wao;

(ii) Jeshi la Polisi lijikite kwenye matumizi ya vifaa vya kisasa vya kiteknolojia katika kukabiliana na uhalifu. Hatua hii iende

sambamba na kutoa mafunzo ya kisasa kwa Askari ili kuwawezesha kutumia vifaa hivyo katika utekelezaji wa majukumu yao; na

(iii) Jeshi la Polisi liendelee kuimarisha ushiriki wa Jamii katika dhana nzima ya Usalama wa Raia na mali zao. Kufanya hivyo kutasaidia Jeshi hilo kupata taarifa fiche kwa wakati na hivyo kuimarisha mapambano dhidi ya uhalifu katika Jamii.

**4.3.2 Fungu 29- Jeshi la Magereza**

**Mheshimiwa Spika**, ili kudhibiti amani katika jamii kwa kuimarisha huduma za magereza na kuongeza tija ya shughuli za urekebu magerezani, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha Ujenzi wa Magereza mapya mawili pamoja na kukarabati Magereza manne kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali iendelee kutoa fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge. Aidha, upatikanaji wa fedha hizo ulingane na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija inayokusudiwa.

(ii) Jeshi la Magereza liandae mkakati wa kuboresha miundombinu chakavu kwenye baadhi ya magereza nchini kwa awamu ikiwa ni sehemu ya kuboresha mafunzo ya urekebu kwa wafungwa nchini. kufanya hivyo kutasaidia kufikia tija iliyokusudiwa katika utoaji wa mafunzo ya urekebu.

(iii) Serikali iliwezeshe jeshi la Magereza kupata magari hususan kwa ajili ya kusafirisha mahabusu. Kufanya hivyo kutakwenda sambamba na mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita ya kuimarisha mfumo wa Haki Jinai nchini.

(iv) Kama sehemu ya kuimarisha mfumo wa haki jinai nchini Jeshi la Magereza litekeleze kwa ukamilifu na ufanisi mpango wa kuimarisha huduma za Mahakama Mtandao kwa kujenga

vyumba maalum katika Magereza 20 yaliyopangwa kufungwa mfumo huo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 4.3.3 Fungu 51- Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa taarifa na makadirio kwa Fungu 51 umeipa kamati nafasi ya kushauri ifuatavyo:-

(i) Wizara iisimamie kwa karibu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuhakikisha kuwa inatekeleza mpango wa utambuzi wa watu kwa kutoa Jamii Namba kwa Raia halali wa Tanzania ikiwemo watoto kuanzia chini ya mwezi mmoja. Jamii Namba hiyo ndio itakuwa namba ya utambulisho wa mwananchi katika kila eneo.

(ii) Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Parole ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi katika utekelezaji pamoja na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kufanya marekebisho ili kuiboresha inavyostahili.

(iii) Serikali iandae mkakati wa kudhibiti mapema Jumuiya zote zinazoendesha shughuli zake kinyume na malengo yaliyoainishwa wakati wa usajili. Kufanya hivyo kutasadia kudhibiti madhara ambayo yanaweza kutokea hali hiyo isipodhibitiwa mapema.

(iv) Serikali iboreshe muundo wa Idara ya Huduma kwa Wakimbizi kwa kuanzisha kitengo maalum cha kufuatilia wakimbizi waliopo nje ya makambi na makazi ya wakimbizi ili kitengo hicho kiweze kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mpango wa kuwatafuta, kuwatambua na kuchukua hatua za kisheria kwa Wakimbizi walio nje ya makazi na makambi ya wakimbizi.

(v) Wizara pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji zishirikiane na Wizara ya Fedha na kuainisha namna bora ya Fungu 14 litakusanya maduhuli yatokanayo na Tozo za ukaguzi wa magari. Kufanya hivyo kutasaidia kuongeza mapato ya Serikali.

### 4.3.4 Fungu 93 - Uhamiaji

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Jeshi la Uhamiaji, Kamati inashauri kuwa:

(i) Serikali iendelee kuliwezesha Jeshi la Uhamiaji kupata vyombo vya usafiri ili kuwabaini wahamiaji wasio na vibali na kuwachukulia hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria;

(ii) Serikali iandae mkakati wa kuliwezesha Jeshi la Uhamiaji kufunga mfumo wa uhamiaji Mtandao katika Ofisi zote za Uhamiaji zisizo na mifumo hiyo sambamba na mfumo wa udhibiti wa mipaka kwenye ofisi na baadhi ya vituo vya kuingia na kutoka nchini. kufanya hivyo kutasaidia kuongeza ufanisi wa Jeshi hilo kwa kutumia vifaa vya kisasa;

(iii) Serikali iendelee na mkakati wa makusudi wa kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zaidi ya 1000 katika mikoa mbalimbali ya mipakani ikiwemo kutumia mifumo ya udhibiti mipaka (e-border). Kufanya hivyo itakuwa ni sehemu ya kudhibiti uingiaji wa wahamiaji haramu pamoja na bidhaa za magendo nchini; na

(iv) Uboreshaji wa Jeshi la Uhamiaji katika matumizi ya vifaa na vitendea kazi uende sambamba na kutoa mafunzo kwa Askari ili waweze kutumia vifaa na vitendea kazi hivyo kwa ufanisi na kupata tija iliyokusudiwa.

### 4.4 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Cosato David Chumi, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dr. Alfred James Kimea, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Minza Simon Mjika, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Maimuna Salum Mtanda, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Eng. Hamadi Yusuf Masauni (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb), pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (*ndc*). Aidha, napenda kuishukuru Sekretariat ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani

ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Vita Rashidi Kawawa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

15 Mei, 2024

**KIAMBATISHO NA. 01: UFAFANUZI WA HALI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI MITATU ILIYOKAGULIWA**

| A | FUNGU/ MRADI NA. | UFAFANUZI | MAELEZO KUHUSU HALI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | **Fungu 29**<br><br>Mradi Na. 6305 | Ujenzi wa Gereza la Wilaya na Ofisi za Jeshi la Magereza katika Wilaya ya Gairo unaotekelezwa na Jeshi la Magereza | (i) Mradi utagharimu kiasi cha Sh. Shilingi **Bilioni 8.2**;<br><br>(ii) Mradi ulianza kutekelezwa Mwezi Aprili, 2023;<br><br>(iii) Mpango wa Utekelezaji umwekwa kwa Awamu Nne;<br><br>(iv) Mradi unatekelezwa kwa utaratibu wa Force Accounts;<br><br>(v) Awamu ya kwanza imekamilika kwa kiasi cha **Shilingi 378,600,000/=;**<br><br>(vi) Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Bajeti iliyotengwa ni **Shilingi 183, 531,000/=** kwa ajili ya mradi huu; |

| A | FUNGU/ MRADI NA. | UFAFANUZI | MAELEZO KUHUSU HALI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | | (vii) Hadi tarehe 13 Machi, 2024 Kamati ilipotembelea mradi huu (**Miezi mitatu kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha ujao**) hakuna kiasi chochote cha fedha kilichopokewa;<br><br>(viii) Mradi unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-<br>(i) Ukosefu wa fedha ambao unakwamisha utekelezaji na kutatiza madhumuni ya ujenzi; na<br>(ii) Ukosefu wa maji utakwamisha tija iliyokusudiwa na mradi kwa kusababisha Mahabusu na Wafungwa kukosa huduma ya maji |
| 2. | **Fungu 51**<br><br>Mradi Na. 6501 | Usajili na utambuzi wa watu katika Wilaya mbalimbali nchini. Mradi huu unajumuisha:<br>(a) kuunganisha na kuwezesha mawasiliano kati ya vituo vya usajili vya Wilaya na Kituo cha Taarifa<br><br>(b) kuunganisha Taasisi za Umma na Binafsi katika Mfumo wa | (a) Mradi ulitengewa kiasi cha Shilingi **41,094,585,000/=**<br><br>(b) Hadi kufikia Februari, 2024 kiasi cha **Shilingi 15,894,277,762/=** kilikuwa kimetumika kwa ajili ya usajili na utambuzi, uunganishaji wa mifumo ya NIDA na taasisi nyingine, ujenzi wa ofisi na vituo vya kanzi data.<br><br>(c) Hadi tarehe 14, Machi, 2024 NIDA ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 19,990,185,324/=** kwa ajili ya Mradi huu. |

| A | FUNGU/ MRADI NA. | UFAFANUZI | MAELEZO KUHUSU HALI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | | Usajili na Utambuzi. | (d) Hadi wakati Kamati inakagua utekelezaji, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ulifikia kadiri ya asilimia 49 ya bajeti iliyotengwa. |
| 3. | **Fungu 28**<br><br>Mradi Na. 6582 | Mradi huu unahusu ujenzi wa Nyumba Tatu za Makamishna wa Jeshi la Polisi jijini Dodoma. | (a) Mradi ulianza kutekelezwa Mwezi Machi, 2023 kwa uratatibu wa Force Accounts<br><br>(b) Mradi huu utahitaji Shilingi 1,050,000,000/= ambapo kila nyumba inagharimu shilingi 350,000,000/=<br><br>(c) Kamati ilipokagua utekelezaji wa mrdadi huu ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 80<br><br>(d) Mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Mei, 2024 |

## KIAMBATISHO NA. 02: UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

### Maelezo ya Jumla

Wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambapo maelezo ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

i) **Serikali imetoa zaidi ya asilimia 70 ya fedha za maendeleo kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Kamati inashauri kiasi hicho cha fedha kiakisi uhalisia kwa Mamlaka hiyo kuongeza kasi ya kuandikisha na kugawa Vitambulisho vya Taifa hasa ikizingatiwa kuwa vitambulisho hivyo kwa sasa vimeungwanishwa na huduma muhimu mbalimbali.**

Katika kuongeza kasi ya usajili, mwaka 2022/23 Serikali ilitoa fedha **Shilingi 46,018,603,665.35** sawa na **asilimia 75** kwa ajili ya utekelezaji shughuli za maendeleo. Kutolewa kwa fedha hizo, kuliwezesha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo usajili na utambuzi, uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa pamoja na kununua Kadighafi za kuzalisha Vitambulisho vya Taifa 13,514,251 ambazo hadi kufikia Februari, 2024 zilikuwa zimeshapokelewa. NIDA katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 imezalisha vitambulisho 7,668,561 hivyo kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa kutoka kuanza kwa zoezi usajili na utambuzi mwaka 2012 kufikia 20,548,067 sawa na asilimia 98.9 ya Namba za Utambulisho za Taifa (NIN) zilizozalishwa na kugawiwa kwa wananchi. Aidha, katika kipindi hicho pia imesambaza vitambulisho 7,385,083 na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyosambazwa kufikia 19,743,367 sawa na asilimia 96 ya vitambulisho vilivyozalishwa.

ii) **Wizara iweke utaratibu wa kufuatilia mtiririko wa fedha za maendeleo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mafungu yake yote matano.**

Wizara imeweka utaratibu wa kufuatilia utolewaji wa fedha za maendeleo kutoka Hazina kila mwezi. Hadi kufikia Februari, 2024 fedha zilizotolewa kwa Wizara ni jumla ya Shilingi 30,091,917,752. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: Fungu 28 Jeshi la Polisi imepokea jumla ya Shilingi 4,781,611,786 kati ya Shilingi 27,093,000,000 sawa na asilimia 17.6; Fungu 29 Jeshi la Magereza Shilingi 1,695,111,000 kati ya Shilingi 16,369,600,000 sawa na asilimia 10.4; Fungu 93 Idara ya Uhamiaji Shilingi 2,995,195,641.55 kati ya Shilingi 8,240,525,000 sawa na asilimia 36.3; Fungu 51 Makao Makuu ya Wizara Shilingi 629,814,000 kati ya Shilingi 2,200,000,000 sawa na asilimia 28.6; na NIDA Shilingi 19,990,185,324.36 kati ya Shilingi 36,400,000,000 sawa na asilimia 54.9. Hata hivyo, Mwezi Machi, 2024 NIDA ilipokea Shilingi 5,000,000,000 na hivyo kufanya fedha zote zilizipokelewa hadi sasa ni Shilingi 35,091,917,752 sawa na 33.4 ya bajeti yote ya fedha za maendeleo kwa mwaka 2023/2024.

iii) **Serikali izingatie umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo na kupatikana kwa tija ya miradi inayotekelezwa chini ya mafungu yote ya Wizara hii.**

Serikali imekuwa ikitoa fedha za maendeleo kulingana na mapato ya Serikali yaliyokusanywa na kwa kuzingatia mahitaji ya kitaifa. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Serikali imetoa jumla ya Shilingi 35,091,917,752 ambazo ni fedha za ndani sawa asilimia 33.4 ya bajeti yote ya maendeleo kwa mwaka 2023/2024. Pia, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 7,950,000,000 nje ya bajeti kwa mchanganuo ufuataoo: Jeshi la Polisi Shilingi 6,000,000,000 za ununuzi wa redio za mawasiliano; na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Shilingi 1,950,000,000 kutoka kwenye Mfuko wa Ustawishaji Makao Makuu Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto Mji wa Serikali – Mtumba. Hivyo, kufanya fedha zilizopokelewa na Wizara kwa ajili ya Miradi ya maendeleo kuwa jumla ya Shilingi 43,041,917,752.

iv) **Wizara iisimamie kwa karibu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwemo kuongeza kasi ya uandikishaji na ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa kuendana na mahitaji.**

Wizara imeendelea kuisimamia NIDA kwa kutoa maelekezo na miongozo mbalimbali ili kuhakikisha inatekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Uanzishwaji wake. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 NIDA imesajili na kutambua watu 530,433. Kasi ya ugawaji wa vitambulisho imeongezeka kwa kutumia ofisi za Kata, mitaa, vijiji na Shehia ili kufikia lengo la kuhakikisha kila mwananchi aliyekidhi vigezo anapatiwa kitambulisho.

**v) Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Parole ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kufanya marekebisho.**

Wizara kupitia Jeshi la Magereza imefanya mapitio ya Sheria ya Parole, Sura ya 400 ili kuzingatia mahitaji ya sasa na Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai. Maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho ni pamoja na maeneo yafuatayo:

(a) Kifungu cha 4 inapendekezwa kifanyiwe marekebisho kwa kupunguza muda wa sifa ya Parole kutoka Kifungo cha kuanzia miaka 4 na kuwa miaka 3 ili kutoa nafasi kwa wafungwa wa vifungo kuanzia miaka 3 kunufaika na Parole kwa kuwa hawaguswi na sheria nyingine zinazotoa vifungo mbadala;

(b) Kifungu cha 4(a) inapendekezwa kiandikwe upya kwa kuruhusu mfungwa anayetumikia kifungo cha maisha na ambaye amekaa gerezani kwa muda usiopungua miaka 25 tangu alipohukumiwa au atakapofikisha umri wa miaka 65 na akiwa ametumikia miaka 15 ya kifungo. Inapendekezwa kifungu hiki kisomeke "*Life Imprisonment, shall not be placed on parole until he has served at least 25 years of his sentence; provided that he may be placed on parole when he has*

*reached the age of 65 and he has served at least 15 years of his sentence*";

(c) Kifungo cha 4(b) kiboreshwe kwa kuongeza makosa ya usafirishaji haramu wa bindamu, utakatishaji fedha, uhujumu uchumi, ugaidi na makosa ya mitandao kuwa hawatonufaika na Parole;

(d) Kifungu cha 6 kiboreshwe kwa kuandikwa upya na kuondoa mamlaka ya kutoa au kutotoa Parole kutoka kwa Waziri Mwenye Dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuwa chini ya Bodi ya Taifa ya Parole. Aidha, Waziri Mwenye Dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi awe ni mamlaka ya Rufaa kwa mfungwa asiyeridhika na maamuzi ya Bodi ya Parole ya Taifa;

(e) Kuondoa maneno ***"Principal Commissioner of Prisons***" popote lilipotumika kwa kuwa cheo hicho hakipo kwa sasa na kutumia neno "***Commissioner General of Prisons"***; na

(f) Kuwekewa kifungu kipya kitakachoweka muda usiozidi mwezi mmoja wa kushughulikia maombi ya Parole na au rufaa katika kila ngazi.

**vi) Wizara ifanye tathmini ya Mfumo uliopo wa usajili wa Jumuiya za Kidini kwa lengo la kuona kama mfumo na utaratibu uliopo unakidhi mazingira ya sasa ambapo kumekuwa na Jumuiya nyingi ambazo zimesajiliwa lakini zinaendesha shughuli zake kinyume na malengo ya Jumuiya hizo.**

Wizara imefanya tathmini ya Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Jumuiya za Kidini na kubaini mapungufu ya kimuundo yanayoathiri usimamizi wa Jumuiya hizo. Aidha, tarehe 14 Oktoba, 2023 Wizara ilifanya kikao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kujadili namna ya kuimarisha mfumo wa usajili na usimamizi wa Jumuiya nchini. Katika kikao hicho, iliazimiwa kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe

kuwa Ofisi za Wasajili Wasaidizi zinaanzishwa katika ngazi ya Wilaya kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa usajili na usimamizi wa Jumuiya katika ngazi za wilaya.

Kwa sasa Wizara inaendelea na majadiliano na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuona namna bora ya kuimarisha ushirikiano ili kuongeza tija na ufanisi katika mfumo wa usajili na usimamizi wa Jumuiya nchini. Ni matarajio yetu kuwa hadi kufikia mwezi Mei, 2024 mazungumzo haya yatakuwa yamefikia hitimisho. Sambamba na jitihada hizo, Andiko la Maboresho ya Muundo wa Ofisi ya Msajili limeshaandaliwa na linaendelea kufanyiwa kazi ndani ya Wizara kabla ya kuwasilishwa Ofisi ya Rais UTUMISHI kwa hatua zaidi.

**vii) Serikali iandae mkakati maalumu wa kuwatafuta, kuwatambua na kuchukua hatua kwa Wakimbizi walio nje ya makazi na makambi ya wakimbizi.**

Kupitia vyombo vya ulinzi na usalama, wakimbizi watoro wamekuwa wakichukuliwa hatua za kisheria na kukamatwa. Aidha, Wizara imeandaa Mkakati Maalumu ambao ni endelevu wa kukabiliana na changamoto hiyo ya kiusalama na kuchukua hatua za kisheria za kukabiliana nazo. Utekelezaji wa mkakati huo umeanza na kazi zinazoendelea kufanyika ni pamoja na:

(a) Kutoa elimu kwa Viongozi wa Mikoa na Wilaya zilizo na Makazi ya Wakimbizi wa Burundi walioingia nchini mwaka 1972 kuhusu athari za kijamii na kiusalama zinazosababishwa na uwepo wao;

(b) Kusajili waomba hifadhi wapya kuanzia umri wa miaka sita (6) katika kanzidata ya NIDA kuepusha kundi hilo kujipatia nyaraka mbalimbali za utambulisho wa utaifa wa Tanzania kwa njia ya udanganyifu. Hadi kufikia Februari, 2024 waomba hifadhi wapya 7,751 kutoka nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wamesajiliwa;

(c) Kushiriki katika mazoezi ya kubaini udanganyifu wa wakimbizi wanaotaka kuajiriwa katika baadhi ya vyombo

vya ulinzi na usalama ambapo wakimbizi 18 walibainika na hatua stahiki zimechukuliwa; na

(d) Kushiriki zoezi la uhakiki wa wananchi waliokuwa na changamoto za Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN), Mkoani Kagera. Katika uhakiki huo uliohusisha wananchi 803, watu 26 walibainika kuwa ni wakimbizi waliosajiliwa hapa nchini. Hatua stahiki zimeendelea kuchukuliwa kwa wahusika ikiwemo kufungiwa kwa Vitambulisho hivyo.

***viii) Serikali iendelee kutoa elimu ya kimkakati kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutoa taarifa za uhalifu kwa wakati ikiwa ni sehemu ya jamiii kuchukua hatua dhidi ya uhalifu pamoja na umuhimu wa kuwa na ulinzi shirikishi katika makazi kama sehemu ya kukabiliana na uhalifu.***

Idara ya Uhamiaji inaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya athari za kuhifadhi wahamiaji haramu kupitia Kampeni ya "MJUE JIRANI YAKO", ambayo hutolewa kwa njia ya vyombo mbalimbali vya habari kama vile radio, magazeti, na Televisheni pamoja mikutano warsha, semina mbalimbali kwa makundi mbalimbali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi februari jumla ya ya vipindi 77 vilirushwa katika vyombo mbalimbali vya Habari na mikutano ya madiwani 58 na semina 205 katika mashule na vikundi vya mgambo zilifanyika. Aidha, Idara ya Uhamiaji inatoa elimu hiyo kupitia maonesho mbalimbali ya Kitaifa kama vile Siku ya Sheria na Wanawaka Duniani.

***ix) Serikali iendelee kuyawezesha Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi vitendea kazi kwa kuzingatia mahitaji halisi na kwa wakati.***

Serikali imeendelea kuiwezesha Idara ya Uhamiaji kwa kuipatia vitendea kazi ikiwemo magari. Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Idara ya Uhamiaji ilitengewa **Shilingi bilioni 3.89** kwa ajili ya kununua magari 23 na tayari kiasi cha **Shilingi bilioni 1.73** kwa ajili ya ununuzi wa magari 11 zimepokelewa na kulipwa. Aidha, Idara ya Uhamiaji inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kupata kiasi cha fedha kilichosalia kukamilisha ununuzi wa magari yaliyopangwa kununuliwa katika mwaka wa fedha 2023/24.

***x) Serikali iandae Mpango Mkakati wa muda mrefu wa kutoa mafunzo ya Uokozi Majini (divers) kwa Askari wengi zaidi pamoja na ununuzi wa vifaa vya uokozi kwa kuzingatia mahitaji halisi.***

Katika jitihada za kukabiliana na changamoto ya uhamiaji haramu kupitia majini, Idara ya Uhamiaji ipo katika maandalizi ya kuanzisha Kikosi ambacho kituo cha kwanza kitakua MOA Mkoani Tanga. Katika hatua hizo tayari Idara imewapatia mafunzo ya wanamaji askari 25 na wamehitimu walihitimu mafunzo hayo mwezi Januari katika Chuo cha Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM).

***xi) Serikali pamoja na Mamlaka zake kuja na Mpango Mkakati wa muda mrefu na unaotekelezeka utakao hakikisha kwamba nchi yetu haindelei kuwa na wahamiaji haramu.***

Idara ya Uhamiaji inaendelea kudhibiti na kusimamia mipaka kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa sanjari na kupambana na watu wanaojihusisha usafirishaji wa binadamu magendo. Aidha, Serikali imeondoa sharti la Visa Rejea kwa Taifa la Ethiopia ili kuwawezesha vijana wa Taifa hilo wenye Pasipoti halali kupata Visa kwa utaratibu wa kawaida. Hatua hii inalenga kupunguza kwa kiwango kikubwa changamotio ya Wahamiaji haramu kutoka nchi ya Ethiopia ambao wamekuwa wakiingia nchini kwa makundi. Pamoja na hatua hiyo, Idara ya Uhamiaji kupitia mikutano na vikao mbalimbali vya kikanda na ile ya ujirani mwema imeendelea kuimarisha ushirikiano katika mapambano dhidi ya wahamiaji haramu.

***xii)*** **Jeshi la Magereza liandae mkakati wa kuanzisha na kutekeleza kilimo cha mazao ya chakula ikiwemo kilimo cha umwagiliaji. Mkakati huo uwe ni sehemu ya huduma ya urekebu na kujitosheleza kwa chakula.**

Jeshi la Magereza tayari lina mkakati wa Mapinduzi ya Kilimo (2023/2024 – 2028/2029) unaolenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa mitambo na zana za kisasa za kilimo. Magereza saba (7) ya kimkakati yameshabainishwa, kati ya hayo magereza

matatu (3) yameshafanyiwa upembuzi yakinifu wa awali wa skimu za umwagiliaji. Utekelezaji wa awali utaanzia kwenye eneo la **ekari 3,300** ambapo mazao makuu ya chakula ambayo ni mahindi, mpunga, maharage na alizeti yatalimwa zaidi ya mara moja kwa mwaka. Mahindi yatalimwa kwenye eneo la **ekari 1,500** kwenye magereza ya Kitete – Rukwa, Kalilankulukulu – Katavi na Kiabakari – Mara kwa eneo la ekari 500 kwa kila shamba. Zao la maharage litalimwa kwenye eneo la ekari 1,000 kwenye magereza ya Ilagala – Kigoma na King'ang'a – Dodoma ekari 500 kwa kila shamba. Mpunga utalimwa Pawaga ekari 500 na Alizeti italimwa Ushora ekari 300. Matarajio ya mavuno ni tani 14,175 za mahindi, tani 5,063 za mpunga, tani 2,000 za maharage na tani 540 za Alizeti. Mavuno hayo yatasaidia kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia chakula cha wafungwa na mahabusu magerezani.

Mahitaji ya chakula cha wafungwa 35,000 kwa mwaka katika mazao hayo ni tani 7,515 za mahindi, tani 1,692 za mchele, tani 1,411 za maharage na tani 378 za mafuta ya kula.

Aidha, katika mwaka 2023/2024 Jeshi la Magereza limetenga **Shilingi 4,760, 000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati huo kwa kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo sambamba na huduma ya Urekebu na kujitosheleza kwa chakula. Ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 1,500, 000,000.00** ni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji Gereza Kitete-Nkasi na **Shilingi 3,260,000,000.00** ni kwa ajili ya ununuzi wa zana za kisasa za kilimo.

**xiii) Serikali iliwezeshe Jeshi la Magereza kupata magari hususani kwa ajili ya kusafirisha mahabusu pamoja na magari kwa ajili ya shughuli za utawala ambapo kwa sasa mahitaji halisi ni magari 800. Upatikanaji wa magari hayo, pamoja na mambo mengine, utasaidia mahabusu kupata nafasi ya kusikiliza kesi zao kwa wakati uliopangwa na hivyo kuamuliwa mapema.**

Katika mwaka 2023/2024 Jeshi limetenga kiasi cha **Shilingi 6,691,416,000.00** kwa ajili ya kununua magari arobaini (40) yatakayo tumika katika shughuli za utawala na kusafirishia mahabusu. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Fungu 29 limepokea

kiasi cha **Shilingi 4,615,568,600.00** kwa ajili ya ununuzi wa magari ishirini na nane (28) kati ya hayo magari kumi na nane (18) ni kwa ajili ya utawala na magari kumi (10) ni kwa ajili ya kusafirishia mahabusu ambapo malipo ya magari hayo yameshafanyika. Upatikanaji wa magari hayo utasaidia mahabusu kupata nafasi ya kusikiliza mashauri yao kwa wakati uliopangwa.

xiv) **Jeshi la Magereza lilishiriki kikamilifu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kupanda miti na kuitunza katika magereza yote katika miji ambayo magereza hayo yapo. Aidha, kufanya hivyo kunaweza kuwa pia ni sehemu ya huduma za urekebu.**

Jeshi la Magereza linaendelea kushirikii katika kukabilina na mabadiliko ya tabia nchi kwa kupanda miti na kutunza mazingira. Katika mwaka 2023/2024 Jeshi lilikuwa na lengo la kupanda miti 1,500,000 ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2024 jumla ya miti 1,009,440 imepandwa katika maeneo mbalimbali ya magereza yakiwemo makambi.

Aidha, Jeshi linaendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kupunguza matumizi ya kuni kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia na kujielekeza katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 jumla ya vituo sita (06) vya magereza vimeanza kutumia nishati safi ya kupikia. Vituo hivyo ni Gereza Ukonga, Keko, Chuo TCTA – Dar es Salaam, Shule ya Sekondari Bwawani – Pwani, Gereza Lilungu na Namajani – Mtwara na Gereza Mpanda.

*xv)* **Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mkakati wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Majeshi ambayo hayajapimwa; kufanya hivyo kutaepusha migogoro baina ya wananchi na majeshi**.

Katika jitahada za kutekeleza mkakati wa upimaji wa maeneo ya magereza nchini, Jeshi la Magereza katika mwaka 2023/2024 limetenga **Shilingi 2,145,111,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya upimaji na ulipaji wa fidia. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,945,111,000.00** ni kwa ajili kuwalipa fidia wananchi wanaopisha maeneo yatakayojengwa Magereza mapya katika Wilaya za

Kishapu – Shinyanga, Ilemela – Mwanza na Nyasa – Ruvuma, Chamwino – Dodoma na Kaliua – Tabora na **Shilingi 200,000,000.00** ni kwa ajili ya Kufanya upimaji na uthamini wa ardhi katika maeneo 14 ya Magereza ambayo ni Chuo Kiwira – Mbeya, Chalinze – Pwani, Namtumbo – Ruvuma, Nanyumbu – Mtwara, Hanan'g – Manyara, Muleba – Kagera, Liwale – Lindi, Kalambo – Rukwa, Mlele – Katavi, Ikungi – Singida, Bahi – Dodoma, Wazo Hill, Kambi Kimbiji na Mvuti – Dar es Salaam.

Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi 1,695,111,477.51** zimepokelewa kwa ajali ya kutekeleza jukumu la upimaji maeneo ya Magereza na kulipa fidia. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,495,111,477.51** zimetumika kulipa fidia kwa wananchi 201 wanaopisha maeneo yatakayojengwa Magereza mapya katika wilaya za Kishapu-Shinyanga, Ilemela-Mwanza na Nyasa – Ruvuma na kiasi cha **Shilingi 200,000,000.00** kimepokelewa kwa ajili ya upimaji na uthamini wa ardhi katika maeneo 14 ya Magereza unaendelea.

**xvi) Serikali iendelee kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuajiri askari wengi zaidi ili kuimarisha utendaji kazi wa vyombo hivyo.**

Katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa askari, Serikali imeendelea kuajiri askari wapya kwa awamu kwa kila mwaka wa bajeti ambapo mahitaji halisi ni 29,796 na waliopo kwa sasa ni 14,592. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Jeshi la Magereza imeajiri askari wapya 734. Vilevile Jeshi limepata kibali cha kuajiri askari wengine 500 ambapo taratibu za kuajiri askari hao zinaendelea.

**xvii) Dhana ya Polisi Jamii itekelezwe kwa ukamilifu katika kupambana na uhalifu hususani katika makazi ya watu**

Jeshi la Polisi limeendelea kudumisha dhana ya Polisi Jamii kwa kuendelea kusogeza huduma za Polisi kwa wananchi kwa kuwapanga Polisi kata **3956** na sheikia **388** nchi nzima, kuhuisha miradi ya Polisi Jamii ikiwemo Ulinzi Shirikishi, Ulinzi Jirani na Familia yangu haina muhalifu kwa lengo la kudumisha mahusiano kati ya Polisi na jamii na kuendelea kutoa elimu/mafunzo kwenye Shule,

Vyuo, Makanisa na Misikiti na kupitia mikutano ya hadhara kama mkakati wa kubaini na kuzuia uhalifu kwa kushirikiana na wadau wengine ndani ya jamii husika kwa kufanaya mikutano ya hadhara **7,585**, Vikao vya ndani **436**, Vyombo vya habari (Televisheni, Redio, Makala na Vipeperushi) **115**, Maonyesho (Sabasaba na Nanenane), Makongamano, utoaji wa elimu katika nyumba za ibada **4,895**, Shule za Msingi na Sekondari **7,470,** Vituo vya bodaboda **7,462.** Huduma za polisi zimesogezwa kwa kupanga askari katika kata **3956** na shekhia **388.**

**xviii) Askari wa Jeshi la Polisi wasimamiwe inavyostahili ili kuzingatia Sheria, taratibu, miiko, weledi na maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wao**

Jeshi Polisi limeendelea kusimamia nidhamu za askari kwa kuimarisha madawati ya maadili na malalamiko amabayo yamefikishwa hadi katika ngazi ya Wilaya. Pia mitaala ya mafunzo ya maadili imeboreshwa, umeanzishwa mpango wa kutoa elimu pamoja na kuanzisha mifumo ya kupokea malalamiko kidigitali.

**xix) Usalama barabarani kutozingatiwa ipasavyo kwa sheria za usalama barabarani na matumizi duni ya teknolojia za kisasa katika kudhibiti usalama barabarani mambo yanayochangia ongezeko la ajali za barabarabani.**

Jeshi la Polisi kupitia Shirika la uzalishaji mali la Polisi "police cooperation sole" linatekeleza mradi wa udhibiti wa Barabara kuu (high way patrol) Mradi unaolenga kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usalama barabarani kwa watumiaji wa Barabara kuu nchini kwa kutumia mifumo ya kidijitali. Mradi unatekelezwa kwa njia ya ubia "unsolicited". **HATUA ZA UTEKELEZAJI:** Andiko la Mradi lipo tayari pamoja na "Feasibility study" imefanyika. Andiko la mradi limepelekwa PPP Centre linasubiri kujadiliwa 25 Machi, 2024. Aidha, mradi wa ukaguzi wa magari wa lazima (Manadatory Vehicle inspection) umewasilishwa katika kikao cha steering Commitee cha wizara ya fedha

***xx)*** **Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji unaoendelea katika mikoa mbalimbali nchini uzingatie upatikanaji wa eneo kubwa ambalo litakidhi ujenzi wa miundombinu ya kisasa na mahitaji ya baadae.**

Jeshi linaendelea na utaratibu wa upatikanaji wa maeneo makubwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo pamoja na nyumba za makaazi ya Askari unaokidhi miundombinu ya kisasa na mahitaji ya baadae. Aidha, kwa sasa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo yatakuwa na ukubwa wa mita za mraba **6000** na yale ya makaazi ya Askari yatakuwa na ukubwa wa mita za mraba **30000**.

***xxi)*** **Jeshi *la Zimamoto na Uokoaji lijipange kutumia mbinu za kiteknolojia na za kisasa katika kupambana na majanga mbalimbali. Kufanya hivyo, kutasaidia jeshi hilo kutoa huduma katika miradi mikubwa ya kimkakati na kupambana na majanga kwa mbinu za kisasa zaidi.***

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea na utaratibu wa kuwapatia mafunzo ya kisasa Maafisa na Askari ili kuendana na kasi ya ukuaji wa tekinolojia. Hadi kufikia Februari, 2024 Jumla ya Maafisa na Askari **178** wamepatiwa mafunzo kati ya hao Maafisa na Askari **167** wamepatiwa mafunzo ya kitaalamu ndani ya nchi na **11** nje ya nchi. Pia, Jeshi linaendelea kupitia michoro na kutoa ushauri elekezi kuhusiana na kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto na mengine hususan kufunga mifumo ya kisasa ya kung'amua na kuzima moto (Automatic alarm and Detection and Suppression Systems) katika miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo mradi wa SGR na upanuni wa viwanja vya ndege. Aidha, Serikali imekamilisha taratibu za upatikanaji mkopo wa magari ya zimamoto na uokoaji na vifaa vya kisasa ambavyo vitasaidia jeshi kutumia mbinu za kiteknolojia katika kupambana na majanga mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Tuna wageni ambao wameingia ndani ya Bunge, hao majina yao pengine hayakufika hapa kwangu kwenye kiti. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ambao ni; *DCF* Charo Mangare, Kamishna wa Oparesheni Jeshi la Zimamoto

na Uokoaji; *SACF* Yusufu Semtena, Kaimu Kamishna wa Usalama wa Umma, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Ndugu Emmanuel Kihampa, Msajili wa Jumuiya za Kiraia, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na Ndugu Sudi Mwakibasi, Mkurugenzi wa Idara ya Huduma kwa Wakimbizi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba kuna Naibu Makamishna, Maafisa na Askari wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wengi tu ambao wamealikwa na wapo na sisi hapa na wengine wapo nje wanaangalia usalama wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni Viongozi wa Dini, Wenyeviti wa CCM Mikoa, Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Mjini Zanzibar wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Ndugu Talib Ali Talib. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Mjini Zanzibar wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Ndugu Hamidi Mbwana Said. *(Makofi)*

Tunao Waheshimiwa Madiwani wa Jimbo la Kikwajuni tunao hapa na Mabalozi wa Jimbo la Kikwajuni tunao hapa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Wajumbe wa Baraza la Usalama Barabarani wapo humu ndani, pia tunao humu ndani Wajumbe wa Mabaraza ya Kisheria na tuna wageni mbali mbali kutoka katika asasi mbalimbali za kiraia ambazo zinapewa usajili na Wizara ya Mambo ya Ndani. Karibuni sana nyote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nadhani nimemaliza majina ya wageni, tunakwenda kwenye hatua sasa ya uchangiaji. Nina majina mengi sana. Idadi ya watu waliotaka kuchangia ni wengi sana, kwa hiyo ili tuweze kuchangia wengi basi nitawapa dakika sita isipokuwa kwa wale ambao hawajachangia kabisa.

Sasa tutaanza uchangiaji na nitamwita kwanza kabisa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwanza niende kwa haraka haraka, nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni. Pamoja naye nimpongeze Ndugu yangu Mheshimiwa Sillo kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi hiyo na tunamtakia kila la kheri katika kutimiza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameendelea kuiheshimisha nchi na kipekee katika taasisi na hivi vyombo ya ulinzi kwa sababu nchi yetu imeendelea kuwa ni kisiwa cha amani na wananchi wanafanya shughuli zao bila matatizo yoyote. Kipekee pia niipongeze Wizara kwa usimamizi mzuri wa vyombo ambavyo vipo chini na mamlaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina eneo moja ambalo ningetaka nianze nalo, ni kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*. Tarehe 15 Disemba, 2023, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji ilitoa tangazo la kuunganisha taasisi ambazo zinashabihiana ama zinafanana zikiwa katika eneo moja ama katika maeneo tofauti. Miongoni mwa taasisi hizo ilikusudiwa kuunganishwa kwa taasisi ya *NIDA* pamoja na *RITA*. Kwa kuangalia kwa mtazamo wa juu ni kwamba taasisi hizi zote mbili zinahusika kwa namna moja ama nyingine na suala la usajili na utambuzi, lakini ukienda kwa undani zaidi unagundua kwamba majukumu yake kuna mahali yanafanana na kuna mahali yanaachana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niishauri Serikali kwamba eneo hili ni vyema tukalitazama kwa mapana kwa sababu *RITA* inasajili ndoa na vizazi; lakini ukija kwenye *NIDA* inaanza kutambua, kwa maana pia ina *component* ya uraia na hapa inahusika na suala zima la uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwangu mimi naona kwamba *NIDA* ni chombo cha kiusalama wa nchi zaidi; hivyo ni vizuri tukalitazama hili jambo kwa mapana makubwa ili kuhakikisha kwamba chombo hiki tunakiimarisha zaidi. Ingependeza zaidi kwamba badala ya kuvitenganisha ni vizuri tukavitenganisha kwa majukumu. Kwa mfano suala la usajili na

utambuzi likawa chini ya *NIDA* na tukawaongezea pia pamoja na kusajili vizazi, vifo, ndoa, uasili watoto; na haya mambo mengine ya udhamini, ufilisi na mirathi yakabaki kuwa chini ya *RITA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaweza tukajifunza hata kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wanacho chombo kinachoitwa *ZCSRA* ambacho kinatekeleza majukumu ya usajili wa vifo, vizazi, ndoa, talaka pamoja na utambuzi wa watu na kutoa vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu, pia katika Mataifa mengine kama vile Rwanda, Botswana na Afrika Kusini majukumu haya yanafanywa na Ofisi za Kabidhi Wasii Mkuu, kwa maana mambo ya udhamini, ufilisi na mirathi. Kwa hiyo tukijifunza hapo tunaweza tukaona kwamba tunaweza bila kuunganisha tutatenganisha tu majukumu. Kwamba yale yanayofanywa na *RITA* yakaenda moja kwa moja kwenye *NIDA* ili *NIDA* ianze kusajili, kama ambavyo Kamati imesema, katika hatua ya kwanza ya mwezi mmoja baada ya mtoto kuzaliwa. Kwa hiyo hilo naliomba sana tulitazame katika muktadha huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ziko baadhi ya Nchi ikiwemo Kenya, Zambia, Singapore pamoja na Botswana pia eneo hili lipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, kama ilivyo hapa kwetu kwamba *NIDA* ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Hiki ni chombo cha kiusalama na kwa hiyo ni vyema kikabaki kuendelea kuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ajili ya suala zima la usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nataka nizungumzie jambo moja tu linaohusu mahabusu, hasa wale ambao wanakamatwa na Majeshi Usu ambayo tumeyaanzisha. Mara nyingi majeshi haya siku hizi yanakamata na yanapokamata kwa sababu hayana mahabusu wanakwenda kuwaweka katika mahabusu hizi za polisi, ambapo polisi hawana mamlaka na hawa mahabusu ambao wamekamatwa *either* na *TANAPA, TAWA* ama na *TFS,* kwa mifano hiyo. Kwa hiyo ninachojaribu kuomba ni kwamba, Watanzania wanatambua kwamba Jeshi la Polisi limeanzishwa kwa ajili ya usalama wa raia na mali zao, kwa hiyo hiki ni chombo cha wananchi ambacho kinakamata kwa

muktadha wa kiraia. Sasa, haya majeshi yapo ambayo yanapamabana na ujangili, yapo ambayo yanapambana na uhalifu na yapo ambayo yanapamba na uvamizi. Kwa hiyo hata namna ya ukamataji ni tofauti na Jeshi la Polisi linavyofanya. Kwa hiyo nashauri na hili lipo pia katika Taarifa ya Haki Jinai, kwamba suala la kukamata liendelee kubaki chini ya mamlaka ya Jeshi la Polisi na hivi vyombo vingine vikamate kupitia Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shangazi. Nimwite sasa Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mheshimiwa Aleksia Kamguna atafuata na Mheshimiwa Mariam ajiandae.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii asubuhi ya leo kuwa mchangiaji wa pili kwenye hotuba hii ya taarifa ambayo ameiwasilisha Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ambaye ni Mheshimiwa Masauni. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia hata leo hii nikaamka mzima. La pili, nikushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa umaridadi wako wa kusimamia kiti vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa nina makosa makubwa sana nisipompongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyofanya kazi kwa kipindi kifupi tokea kuwa madarakani, hususani kwenye Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa mambo makuu matatu, hususani kwenye Wizara hii. Moja tumeshuhudia zaidi ya magari 181 ambapo 71 sasa hivi tayari yameshagawiwa kila wilaya. Kwa hiyo mpaka sasa hivi ninavyozungumza ma-*OCD* wetu wa wilaya huko wanatembea na magari kwa neema hii ya Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana pia Mheshimiwa Rais, kwenye zima moto nako pia tumeambiwa kuna magari zaidi ya 150, nayo yapo njiani kwa ajili ya kusaidia huduma

hii ya zimamoto nchini kwetu, kwamba kila wilaya itapata gari. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais nampongeza sana vile vile kwa huduma ya *TEHAMA*. Tunaambiwa sasa hivi takribani kwenye mipaka yote ya nchi hususani kwenye eneo la *airport* nako tutapata vifaa vipya ambavyo vitakwenda kwa ajili ya kuzuia uhalifu wowote ambao unategemewa huenda ukatokea katika nchi yetu. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea Jimbo la Chaani Mkoa wa Kaskazini Unguja. Ni miaka mingi sana hapa tangu tuingie tukiwa tunalalamika, hususani Mkoa wetu wa Kaskazini Unguja, kuhusiana na vituo vya polisi. Tuna vituo zaidi ya vitatu tu kwenye mkoa mzima wa Kaskazini Unguja ambapo ukiangalia kwenye Wilaya ya Kaskazini B tuna kituo kimoja tu cha polisi. Kituo hicho kimejengwa tokea enzi za ukoloni na kina daraja C. Naomba sana kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Masauni aangalie Wilaya hii ya Kaskazini B; huduma ya kipolisi kwenye vituo vya polisi bado tupo nyuma sana. Tuna kituo kimoja tu kwenye wilaya nzima, kuna vijiji kadhaa zaidi ya ambavyo mimi sivijui idadi yake vinafuata huduma kutoka kwenye...

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kaka yangu hapa pamoja na mchango wake mzuri anaochangia. Katika Wilaya ya Kaskazini B vijiji vinavyotembea masafa marefu ni Kichungwani, Kichwele, Mchanjarike, Mwembemajogoo na Kitope Ndani. Hawa wote wanatembea masafa marefu kufuata Kituo cha Polisi Mahonda.

**MWENYYEKITI:** Mheshimiwa Usonge unapokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge jirani yako hapo?

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa kwa mikono miwili na bahati nzuri naye pia anatokea Mkoa wetu wa Kaskazini Unguja, kwa hiyo nimpongeze sana. Naomba sana wilaya hii tuiangalie kwa jicho la kipekee, tuongeze idadi kubwa vya vituo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa huu wa Kaskazini Unguja una idadi kubwa sana ya wananchi na pia kwenye uwekezaji wa hoteli nao pia unaongoza, lakini huduma ya kipolisi bado ipo nyuma. Kwa hiyo naiomba sana Wizara katika bajeti hii tuongezewe walau kituo kimoja kwenye Wilaya ya Kaskazini B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Wilaya ya Kaskazini A Unguja. Wilaya ya Kaskazini A Unguja nako tuna vituo viwili tu vya polisi. Nako pia tunashukuru sana, kwa sababu katika bajeti iliyopita walitenga fedha tukaenda kukamilisha lile jengo ambalo sasa hivi lina *grade* B. Kwa hiyo naiomba sana Wizara, mara hii twende tukakiangalie Kituo cha Polisi cha Lungalunga ambacho kipo kwenye Jimbo langu la Chaani. Kituo hiki tokea enzi za ukoloni hadi leo hii, nikimpitisha pale Mheshimiwa Waziri hawezi akaamini au akaniambia hiki ni kituo cha polisi. Kituo hakina hadhi kabisa, kituo kimekaa kama kibanda cha kuku. Naomba sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana hapa nilizungumza sana kuhusiana na Kituo hiki cha Polisi kilichokuwepo Chaani Lungalunga kwenye bajeti yake na wakatenga bajeti zaidi ya milioni 80, lakini mpaka leo hii ninavyozungumza hakuna hata thumni iliyokwenda pale kwa ajili ya kukitengeneza kituo cha polisi. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kituo kile kimekaa kimkakati ukitoka Mahonda ukija Chaani pale, maana yake ndiyo unaingia kwenye eneo la uwekezaji na eneo ambalo tayari kuna *population* kubwa ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la pili la Pwani Mchangani. Kuna kituo kimejengwa na wawekezaji, ni kituo kizuri chenye hadhi, lakini hadi leo hii ninavyozungumza kituo kile mwekezaji tayari ameshafikia ukomo, tunamshukuru kwa jitihada zake, lakini kinahitaji baadhi ya vifaa, navyo ni, kumaliziwa kupigwa rangi, milango, madirisha pamoja na vifaa vya kiofisi.

*Gap* kubwa mwekezaji huyu ameshalitoa, kwa hiyo naomba sana Wizara twende tukamalizie kile kituo cha Pwani Mchangani ili kuwasaidia wananchi wa Pwani Mchangani na maeneo yote ya jirani pale kupata huduma ya kipolisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni Matemwe, nako ndiyo hivyo hivyo, kwamba kuna *population* kubwa na uwekezaji nao umeshamiri. Kuna eneo kabisa la Serikali limeshatolewa, wameshapewa polisi kwa ajili ya kujenga kituo cha polisi. Kwa hiyo naiomba Wizara kwenye bajeti hii twende kule tukakiangalie Kituo hicho cha Matemwe kuweza kujengwa kwa haraka ili wananchi, wawekezaji pamoja na wageni mbalimbali kuweza kupata huduma za kipolisi kwenye eneo hilo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umeisha.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Aisee! Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, nimwombe Mheshimiwa Mariam Omary Said ajiandae.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi asubuhi ya leo. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanamke wa kwanza kwa kushika nafasi. Tunasema kila siku mwanamke umpe kazi aifanye. Kama tunaweza tukafanya kazi ngumu leo Mheshimiwa Rais amedhihirisha kwamba kweli wanawake tunaweza. Tunaomba huyu mama tuzidi kumuunga mkono hatimaye kazi iwe rahisi siku zote za maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wizara, Waheshimiwa Mawaziri pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ulinzi, maana bila ya wao sisi amani Tanzania isingekuwepo, tunawashukuru sana kwa kazi ngumu ambayo wanaifanya katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatoa pole kwa Watanzania wote kwa mafuriko ambayo yametupata, hasa Mkoa wa Morogoro. Jamani mafuriko myasikie tu. Katika Tanzania sidhani kama kuna mkoa ambao umeathirika kama Mkoa wa Morogoro, maana hata helikopta zinashindwa kwenda kutua kwa ajili ya kutupelekea misaada. Kwa hiyo tunaomba Serikali hicho kilio wakisikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu Jeshi la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto ni jeshi ambalo lina msaada mkubwa sana katika nchi yetu lakini ukiliangalia jeshi hili lina changamoto nyingi, japo kwa hivi karibuni tumepata magari 12 ambayo yana uwezo mkubwa sana katika nchi hii. Hata hivyo magari 12 ni machache ukilinganisha na ukubwa wa nchi yetu, lakini si haba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jeshi hili, pamoja na kazi wanayoifanya ya zimamoto na uokoaji bado lina upungufu, halina ofisi, ofisi zao zipo katika hali mbaya. Hivi jamani Serikali, mtu anatoka nyumbani kwakwe anakwenda ofisini, anafanya kazi ngumu halafu anafika kwenye ofisi ambayo haijulikani ilivyo. hali mbaya, huyo mtu si inampunguzia *morale* ya kazi jamani? Kwa hiyo Serikali tujitahidi tuwaangalie wale watu wapate ofisi nzuri na hatimaye wazidi kuwa na moyo wa utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jeshi hilo pia kuna tatizo la rasilimali watu. Kwa sasa hivi hapa tunavyoongea kuna wafanyakazi wa zimamoto na uokoaji ambao wapo kazini, hasa upande wa uokoaji kwa njia ya maji wapo 77 tu; ukilinganisha na nchi kubwa ya Tanzania, watu 77 hawatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kwamba ambao wanategemea kuwaajiri ni 246 na kwamba bado wapo kwenye mpango wa 425, huo ni mpango, hawajui kama wataajiriwa, haijulikani kama hawataajiriwa. Jamani kazi ngumu kama hii kweli bado wanasema kwamba watu 77 ndio waliopo kazini na hao wengine 246 hatuna uhakika kama wote waliopo kwenye mafunzo wataajiriwa au hawataajiriwa. Kwa hiyo naishauri Serikali iajiri hawa watu. Tanzania tuna bahari kubwa ya Hindi, tuna

mabwawa, tuna maziwa, yote yanahitaji hawa watu wa uokoaji wa majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kuzungumzia matatizo ya barabarani; Jeshi la Polisi kuna shida, kuna zile njia za *service*, tunaita *service roads,* unakuta asubuhi kipindi cha kwenda kazini, nachukulia mfano Dar es Salaam au kwenye miji, unakuta kwamba ile njia ya *service road*, askari wanazuia wanasema watu wasipite katika zile barabara, wakati barabara kubwa ina msongamano mkubwa. Sasa huwa najiuliza hizo barabara za *service roads* zimewekwa kwa ajili ya watu gani kupita na zinatakiwa watu wapite wakati gani? Labda hilo wangetuelewesha kwamba ni watu gani wanatakiwa kupita, nani wakati gani wanatakiwa kupita ili watu wafahamu kwa sababu usumbufu unaokuwepo ni mkubwa mno bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba mnapoweka *service road* maana yake zile barabara kuu zimekuwa zimelemewa hatimaye zinajengwa zile za pembeni ziweze kutoa huduma kupunguza msongamano lakini matokeo yake polisi wanawashika na wanawatoza faini watu, sasa sijajua sababu ni zipi na kusudio ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine ni la kuhusu bodaboda; katika bodaboda utakuta kwamba bodaboda na bajaji kwenye hizi *service roads* na hizo barabara kubwa wanapaki yale magari. Kama mtu anaendesha gari hawezi kuona kulia hawezi kuona kushoto na askari yupo pale amesimama anawaona wale watu waliosimama. Sasa najiuliza wale askari wako pale barabarani kwa ajili ya kumwangalia nani? Tunataka ajali itokee ili wao waseme wameona, wakati watu wamesimama pale hawawezi kuwakemea kwamba hizi barabara mtu anatakiwa aangalie kulia na kushoto mbele na nyuma lakini askari wapo. Sasa kazi yake ya kusimama pale barabarani ni nini? Ni kuwaruhusu watu ili wapate matatizo zaidi au kuwasaidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nataka kuzungumzia suala la bodaboda kupita kwenye taa zinazowaka; bodaboda ni kero, hatusemi kwamba watoto wetu wasiendeshe bodaboda, vijana

wetu wanajiajiri lakini askari wako pale bodaboda wanapita wakati taa ni nyekundu. Wale vijana ni nguvu kazi ya Taifa, wale vijana wanagongwa kila siku, tunatumia madawa mengi katika kuwatibia wale vijana na pia, Taifa linapoteza nguvu kazi...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimpe taarifa mchangiaji anayechangia vizuri kuhusu bodaboda. Bodaboda kwa tafiti ambayo nimeifanya, ninavyokuwa nazunguka na na-*drive*, bodaboda wengi unakuta wameng'oa zile *site mirror* zao, kwa hiyo hata ukim-*mute* lazima ageuke kukuona, *by the time* anafanya hivyo anapata ajali. Kwa hiyo, ni lazima Jeshi la Polisi liangazie sana na litoe elimu toshelezi kwa bodaboda hawa ili tuweze kunusuru maisha yao lakini na yale ya abiria ambao anakuwa amewabeba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, unaipokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa?

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hiyo Taarifa kwa mama yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda hao ukiangalia ni vijana wetu tumewaruhusu, kweli wanapata kibali wafanye ajira, lakini ile ajira sasa inakuwa ni shubiri sio ajira tena kwao kwa sababu wanakufa. Wale Polisi wa Barabarani wanawaangalia hawajali kama kuna mtu amepita kushoto, amepita kulia, wakati wao wana usemi wao unaosema kwamba tii sheria bila shuruti, sasa wale wanapopita kwenye taa je, wale wanatii zile sheria na kwa nini wanawaacha? Sasa hapo tuwaelewe vipi wale askari walioko barabarani, ina maana wale hawawaoni na wale wanaosimama kandokando ya barabara wanazuia barabara hawawaoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaongea nao mara nyingi, jamani kwa nini wale wanazuia pale barabarani watu hawaoni vizuri ikitokea ajali, wanakwambia mama au Mheshimiwa sisi wale wametushinda. Sasa wanawashindaje wakati sheria zipo? Tunaomba kwa Mheshimiwa Waziri, hili walifanyie kazi wale, wote walioko kandokando ya barabara waondolewe wawekwe kwenye vituo vinavyotakiwa ili hata wale wanaoendesha magari ni haki yao na hata wanaotembea kwa miguu pia ni haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu jambo lingine ambalo huwa linanitatiza kwenye hizi barabara zetu kubwa zenye kuanzia barabara mbili na kuendelea yaani barabara za lami, unaweza kukuta kuna malori makubwa, lakini yale malori yaliyoko pale yanapita kushoto na yanapita kulia, kwa hiyo wale wenye magari madogo labda kama ni *saloon car* au kama ni mabasi ambayo wanataka waende kwa haraka hawawezi wakaenda kwa sababu lori liko kushoto, lori liko kulia kama vile wanafanya kusudi kuzuia watu wasipite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza mbona nchi za wenzetu kuna utaratibu kwamba kama wewe unajiona mwendo wako ni mdogo au malori wapite kushoto kwa sababu miendo yao ni midogo, wenye magari ya kwenda kasi wapite kulia ili kumfanya kila mmoja afike sehemu yake akafanye kazi. Tunapoteza muda mwingi sana barabarani kwa uzembe na askari wapo. Kwa nini tusipitishe sheria kwamba magari ya mwendo fulani yapite kushoto magari ya mwendo fulani wapite kulia ili yule mwenye haraka aende afanye kazi akazalishe na yule mwenye mwendo mdogo kama wa lori aende taratibu naye afike kwenye safari yake anayokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kuuliza hilo swali nikaambiwa hiyo sheria haipo, kwa hiyo tunamsubiri nani aje atuletee hiyo sheria, sio sisi ndio tunatunga hiyo sheria ya Watanzania baada ya kuona tunaenda kwa wakati? Kwa sababu lazima kila jambo linalofanyika tulifanye kufuatana na wakati tulionao. Haiwezekani wewe unatoka nyumbani kwako unajua unaenda kazini, unafika baada ya nusu saa, lakini unafika

baada ya masaa matatu eti kwa sababu lori moja liko kushoto moja liko kulia na liko mbele yenu, mnafanyaje mtapita wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani naomba hilo aliangalie ili hatimaye tuweze kufika mapema kwenye sehemu zetu za kazi, tuzalishe badala ya kupoteza muda na kuleta ajali ambazo hazina msingi kwa sababu wengi watajiona kwamba mbona lori linanichelewesha ngoja nijaribu kupita pembeni matokeo yake tunaleta ajali. Askari wapo na kama haliwezekani, kuanzia sasa hivi tutunge sheria na tutoe mafunzo kwa watu ili waelewe. Kama nchi nyingine wanaweza sisi tunashindwa nini? Naomba hili tulifanyie kazi na tulichukue kuanzia sasa hivi ili tupunguze ajali za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kuzungumzia kuhusu hizi safari za usiku; safari za usiku ni safari nzuri ambazo vijana wengi wanapenda hasa wafanyabiashara, zinawafikisha kwa wakati, lakini hizi safari zina madhara yake. Madhara ni makubwa kwa sababu kwa usiku ukiangalia barabara zetu hazina taa utakuta ajali zinatokea nyingi. Mchana pia tunaona ajali nyingi, lakini usiku ajali ni nyingi zaidi kwa sababu uwezo wa kuona ni mdogo na pia askari wanakuwa ni wachache, hawapo. Sasa kama mchana tunaona askari ni wengi usiku askari ni wachache, sasa kama hatujajipanga tukafikia hapo, naona hii inasababisha hatari sana kwa Taifa. Tujipange tuweke askari wengi usiku ili kulinda usalama wa watu wanaotembea usiku. Sijasema kwamba watu wa usiku wasitembee la hasha ila tuwe waangalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nimwite Maryam Omar Said, Mheshimiwa Kasalali Mageni ajiandae.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kusema neno katika hoja hii iliyoko mezani. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kadri wanavyofanya kazi, lakini uongozi mzima wa Wizara hii ikiwemo Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shida mbili au tatu katika Wizara hii, mojawapo, ni mara nyingi sana huwa nasimama hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi, nikiulizia *either* vituo vya polisi ama majengo ya askari wetu Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwa asilimia kubwa kila atakayesimama hapa kuchangia basi hoja kubwa itakuwa ni vituo vya polisi, majengo ya makazi, askari wetu hali haziridhishi. Mkoa wa Kaskazini Pemba tuna vituo vitatu vya polisi, kituo kimoja kinabeba Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Mkoa wa Kaskazini Pemba, kituo kiko Wete pale. Hali ya lile jengo ni mbaya hairidhishi na mara zote tukisimama hapa kuuliza unaambiwa tunafuatilia tunasubiri fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, fedha ndio kama hizi hakuna fedha nyingine itakayokuja ikawa mahususi, hebu tunakuomba na sisi Mkoa wa Kaskazini tuone, tena tuone kwa jicho la huruma. Kwa mfano, kuna nyumba inayokaliwa na familia karibia 12 na zaidi ya Jeshi la Polisi. Askari Polisi hawa wanakaa katika mazingira magumu. Jengo ni bovu ninavyokwambia kipindi hiki cha mvua ni kama chujio, bora ukakae kwenye mwembe kama ile nyumba wanayoishi. Hili ni Jengo linaitwa *Like Kilimanjaro* liko karibu Uzunguni kule Wete Pemba, hili jengo haliridhishi, hali ni mbaya mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo ukija kwenye utendaji wa Jeshi la Polisi, tukija kwenye usafiri wa magari, Mkoa wa Kaskazini pale Makao Makuu kuna gari moja tu la *OCD*, gari moja la *OCD*, hebu niambie Mheshimiwa Waziri gari hili moja litafanya kazi vipi, kule mhalifu ameshaiba, huku huyu ameshalawitiwa, gari hilo moja litafanya kazi vipi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri katika haya magari ambayo nimesikia hapa akiyataja, hebu na siye atuangalie kwa jicho la huruma, atupatie angalau gari moja watuongezee angalau gari moja tuwe na mawili. Badala ya gari moja, hakuna hata pikipiki moja inayofanya kazi. Angalau hata ikitokea emergency ukaambiwa askari yule atafika kwa pikipiki, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niingie katika usalama barabarani. Mheshimiwa aliyenitangulia amezungumzia sana bodaboda. Bodaboda ni vijana wetu, tunawapenda sana na sisi wengi hapa, mtu anakujia Mheshimiwa naomba unipatie

bodaboda ili nijiwezeshe kimaisha sawa, lakini sasa imekuwa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie, wenzetu Rwanda walipoanzisha bodaboda walikuja kujifunza kwetu Tanzania, twende Rwanda tukaangalie, bodaboda anavaa *helmet* pamoja na abiria wake, bodaboda anavaa *uniform* pamoja na abiria wake wana kile kikoti cha *blue*, bodaboda hazidishi abiria zaidi ya abiria wake mmoja, bodaboda anasimama kwenye mataa mpaka taa imruhusu, sisi tunashindwa wapi? Wapi sisi tunashindwa? Kama wale walikuja kusoma kwetu wakaenda kuboresha kule kwao sisi tuliosomesha kipi tunashindwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza vijana wengi, juzi hapa tulisikia kati ya watu wengi ambao wanahatarisha maisha yao wanakuwa katika hali ngumu kule *MOI* wodini ni bodaboda. Hawa hawana bima, asilimia kubwa hawana bima na ukizingatia hao hao bodaboda asilimia kubwa hawana leseni. Niwaulize watu wa usalama barabarani wanafanya kazi gani? Ni sheria gani inayomruhusu mtu aendeshe chombo barabarani akiwa hana leseni? Hii sheria tumeitoa wapi? Namwomba Mheshimiwa Waziri, hiki Kitengo cha Usalama Barabarani hebu kiangaliwe sana bado kuna mapungufu makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda nataka nilisemee kidogo suala la kitambulisho cha Taifa pale *migration.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam, bahati mbaya muda wako umeisha.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, sasa nimwite Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mheshimiwa Martha Festo Mariki ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa

uhai na uzima, lakini nitumie fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amir Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye kuboresha vyombo vilivyochini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia, nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri Kaka yangu Masauni kwa kazi nzuri anayoifanya akisaidiana na Mheshimiwa Sillo, Wizara inakwenda vizuri sana, nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha hayo naomba nitumie nafasi hii kushauri machache kwenye hii Wizara nyeti na hasa nitashauri kwenye Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu Polisi na Vitengo vyao vyote wanafanya kazi nzuri sana. Mimi kama mdau wao kazi wanayoifanya ni nzuri sana inahitaji kupewa moyo na kusahihishwa pale wanapokosea kwa sababu nao ni binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wahudumu wao kwenye maslahi yaani Serikali na Bunge tunaopitisha bajeti, naomba niishauri Wizara iangalie sana maslahi ya askari polisi, waangalie mishahara yao, waangalie *allowance* zao, kwa sababu tumekutana na changamoto huko wanasema *ration allowance* kuna wakati inalipwa tarehe 40 badala ya kulipwa tarehe 15 na nafikiri kuna mambo mengi kwenye maslahi ya askari ambayo Mheshimiwa Waziri naomba sana ayaangalie. Askari wetu wanafanya kazi nzuri na sisi tufanye kazi nzuri kuwapatia maslahi mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jeshi la Polisi nakumbuka Mheshimiwa Rais akiwa anazungumza nao pale Kilwa alizungumza kuhusu kero ya kikokotoo kwa askari wetu. Kikokotoo kipo cha aina mbili, kuna kikokotoo ambacho kiko kwa watumishi huku, lakini Mheshimiwa Rais alisema Jeshi la Polisi linatakiwa liwepo kwenye utaratibu wa majeshi mengine. Majeshi mengine hayaingii kwenye huu utaratibu wa kikokotoo wa utumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe Wizara ifahamu kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Rais alielekeza yale

maelekezo kama Amiri Jeshi Mkuu na maelekezo ya Amir Jeshi Mkuu yanatakiwa yatekelezwe sio yajadiliwe. Niwaombe Wizara na niwatake wakatekeleze maelekezo haya, wakaangalie namna bora ya kuliondoa Jeshi la Polisi kwenye mambo haya ya kikokotoo wakati tunashughulika na kuondoa watumishi, lakini askari polisi wanatakiwa waingie kwenye utaratibu wa majeshi ili waachane na hii kero ya kikokotoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunayo changamoto ya makazi ya askari polisi. Kwenye Wilaya ya Kwimba ambako mimi natoka, askari wana tatizo kubwa la makazi. Kwa hiyo, naomba Wizara watuongezee bajeti ya kujenga makazi ya Polisi kwenye Wilaya ya Kwimba, lakini na nchi nzima. Vitendea kazi kama magari Wilaya ya Kwimba ina majimbo mawili, lakini gari zima linalotembea tena kwa kusukumwa ni moja, sasa askari wetu watafanyaje kazi kwenye mazingira hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Masauni, najua ni msikivu, askari bado wanahitaji vitendea kazi. Askari kata wanahitaji pikipiki, askari polisi mbali na vitendea kazi tatizo la *uniform* ni kubwa. Wanajishonea *uniform* zao, sasa utaratibu wa kawaida unataka askari ajishonee *uniform* zake, unataka makazi yake yawe ya chumba kimoja na jiko halafu maslahi yake sio mazuri, mwisho wa siku tunawavutia hata kuingia kwenye hizo tunazozisema rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafika wakati sisi tunalalamika tu wao wanakula rushwa, lakini hatuangalii mazingira wanayofanyia kazi. Ni wajibu wetu kama Serikali kuhakikisha askari wetu wanakuwa na mafuta ya kutosha kwenye vituo vya polisi ikitokea kuna mhalifu wanawasha gari wanaenda kukamata. Sasa mtu ameenda kushtaki kuna mhalifu, polisi wanamwomba mafuta kwa sababu hawana hayo mafuta. Sasa hayo mafuta ya kujaza kwenye gari yeye ayatoe wapi. Kwa hiyo kuna vitu lazima tuvichukulie *very serious*. Hizi rushwa na kero za vituoni wakati mwingine tunasababisha sisi kwa kutokuhudumia vizuri Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimwite Mheshimiwa Martha Festo Mariki na Mheshimiwa Asha Juma Mshua ajiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema, lakini kipekee zaidi nimpongeze sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa letu la Tanzania, lakini nimpongeze zaidi kwa jinsi ambavyo ameendelea kuboresha Wizara hii ya Mambo ya Ndani ukizingatia Wizara ya Mambo ya Ndani ndio Wizara ambayo inatusababisha sisi wananchi tuweze kukaa katika hali ya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia, naipongeza sana Kamati inayoshughulikia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa jinsi ambavyo wameendelea kuishauri Wizara kuangalia namna nzuri ya kuboresha ili Wizara hii iweze kufanya vizuri katika kuboresha usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia suala la gari la zimamoto katika Mkoa wetu wa Katavi. Naishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuleta magari ya zimamoto nchini, lakini katika maeneo mbalimbali. Ni dhahiri kabisa Mkoa wangu wa Katavi ni takribani zaidi ya miaka kumi tumekuwa hatuna gari la zimamoto. Tumekuwa tukitumia gari ambalo ni la *airport* na unaweza ukaona jinsi gani Mkoa wa Katavi tulivyo katika hali ya hatari pale inapotokea siku ndege inatua katika Mkoa wetu wa Katavi, Wilaya ya Mpanda na inapojitokeza shida ya moto katika Mkoa wetu wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari tunalolitegemea ni ambalo linatumiwa na *airport*. Tunaomba sana, Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Mheshimiwa Waziri wetu, katika mgawo wa magari yaliyokuja utupe kipaumbele sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi ili tuweze kupata gari la zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana pia Serikali inayoongozwa na Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutenga pesa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vituo vya polisi nchini pamoja na kujenga Vituo vya Polisi Kata katika maeneo yote nchini. Tunaipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunaiomba sana Serikali, katika Mkoa wangu wa Katavi tunacho Kituo cha Polisi katika Wilaya yangu ya Mpanda. Ni kituo ambacho ni cha miaka mingi na ni chakavu. Naiomba sana Wizara iweze kuangalia namna ya kutenga pesa kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mpanda, kwani ni kikongwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza sana Wananchi wa Wilaya yangu ya Tanganyika kwa kuonesha juhudi zao binafsi kwa kutoa nguvu kazi zao, kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Tanganyika. Hata hivyo, kwa kuwa, wananchi wameanzisha ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Tanganyika kwa nguvu zao binafsi, naiomba sasa Wizara iweze kutukumbuka sisi wananchi wa Wilaya ya Tanganyika kwa kutenga pesa kwa ajili ya umaliziaji wa Kituo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuna changamoto kubwa katika makazi duni ya Polisi katika Mkoa wetu wa Katavi na vilevile, katika maeneo yote nchini. Naiomba Wizara, Polisi wanafanya kazi nzuri sana katika Taifa letu la Tanzania, hata hivyo, ni dhahiri kwamba, wamekuwa wakikaa katika makazi ambayo hayaridhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwapa motisha Polisi hawa, naiomba Serikali, tunajua kwamba, imetenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Polisi katika maeneo ya Dodoma, Arusha pamoja na Dar es Salaam, lakini ukiangalia kwa

mikoa ya pembezoni makazi yao ni duni sana na hayaridhishi. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana tuwakumbuke Polisi, hususani katika mikoa ya pembezoni. Kwa kweli, makazi wanayokaa hayaridhishi, lakini pia, tuwakumbuke Polisi hawa katika maslahi mbalimbali kwa kweli, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukawalaumu Jeshi la Polisi kwamba, wananingia katika rushwa, ni kwa sababu makazi wanayokaa ni duni na hata maslahi yao pia, ni duni. Naiomba sana Serikali kwa kuwa, Polisi hawa wanatumia nguvu kubwa sana kuhakikisha sisi pamoja na mali zetu tunakuwa salama, basi ni wakati wa kuboresha mazingira yao, ili yaweze kuwa safi na salama, lakini pia, na masilahi yao tuweze kuyaangalia ili Polisi wetu waweze kufanya kazi katika mazingira yaliyo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusiana na suala la Sayansi na Teknolojia katika majeshi yetu yote nchini likiwepo Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto pamoja na Jeshi la Uhamiaji. Naiomba sana Wizara, ni muda na wakati sahihi kabisa wa kutenga pesa, kwa ajili ya kuwekeza kwenye Sayansi na Teknolojia katika Jeshi letu hili la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi anapokwenda kutoa malalamiko yake pale anapokuwa amepata shida, badala ya wao kuandika katika makaratasi, basi ziwepo *camera* na vitendea kazi maalum ambavyo vinarekodi. Rekodi hiyo iweze kutunzwa, ili hata mtu anapokwenda katika hatua ya mahakama, awe na kumbukumbu nzuri na kuepusha ubabaishaji wa kubadili yale maelezo katika makarastasi ambapo mara nyingi watu wanakuwa wanaonewa katika kesi na hawapati haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri, kuna *clip* ambayo ilikuwa inasambaa mtandaoni ikionesha mama analalamika kwamba, mtoto wake amelawitiwa, amekwenda kutoa malalamiko yake katika Jeshi la Polisi, lakini Jeshi letu la polisi kwa kweli, halikumtendea haki mama yule. Kama jambo lile lilikuwa ni kweli, naiomba Wizara ya Mambo ya Ndani waweze

kufuatilia jambo hilo ili kuhakikisha akinamama hawa ambao ni wahanga wakubwa kwa watoto wao ambao wamekuwa wakilawitiwa waweze kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana mama anakwenda katika Jeshi letu la Polisi kutoa malalamiko yake, lakini kesi ile inakuwa inapigwa danadana na hapati haki yake. Naomba sana Jeshi la Polisi liweze kushughulikia malalamiko hayo. Pia, katika Mkoa wetu wa Katavi naomba sana tupate Wilaya ya Kipolisi. Tunapata adha kubwa wananchi kwenda katika Wilaya ya Inyonga, ni mbali. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, lakini ninampongeza sana *RPC* wangu wa Mkoa wa Katavi, ni mwana mama. Kwa kweli, anaupiga mwingi na anashughulika na vijana wale wa damu chafu. Nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita Mheshimiwa Asha Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, wewe Mheshimiwa Mwantum Dau nyamaza hapo. Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za kimaendeleo kwa Nchi yetu ya Tanzania. Napongeza sana kwa kuridhia bajeti hii ambayo ina mchango mkubwa kwa usalama wa wananchi, mali zetu na utulivu ambayo ni chachu ya maendeleo kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, *Engineer* Hamad Masauni, ambaye ameimudu vyema Wizara hii na sisi wana-Jimbo la Kikwajuni na dada zake

ametuheshimisha sana. Vilevile, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi anavyofuata nyayo na mambo kule Wizara ya Mambo ya Ndani yanakwenda bila shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza timu nzima ya Wizara kuanzia Makatibu Wakuu, Wakuu wa Vyombo vya Wizara hii na watendaji wote kwa sababu, mara hii mambo yenu yamekuwa mazuri hata malalamiko yamepungua sana. Kwa hiyo, mnaupiga mwingi pokeeni maua yenu Wakuu wa Vyombo na Watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze mchango wangu kwa taasisi hii ya Magereza. Nimeona hapa kumependekezwa kiasi kikubwa cha pesa kama shilingi 990, 000,104 kwa ajili ya kuandaa mitandao ya *biogas* (gesi vivunde) kwa kushirikiana na *Taifa Gas* na *REA*. Hata hivyo, ninapendekeza kwamba, waweze kutumia njia ya vinyesi vya watu na wanyama. Kwa kuwa, magereza mengi yana mifugo mingi, hivyo ni wakati mzuri wa kwenda na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu ambaye amekuwa katika harakati kubwa za kuwezesha kuwa na matumizi endelevu ya hii nishati bila kukata miti na hivyo, kutunza mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, magereza yetu ni hazina kubwa ya kuonesha mfano wa matumizi ya nishati endelevu ya gesi ya kinyesi cha wafungwa na ng'ombe. Mifano ya matumizi ya kinyesi hiki ipo katika nchi jirani, unaweza kwenda kusoma kule Rwanda ambako shughuli zote za kimagereza zinatumia nishati hii. Kwa kutumia hii nishati ya vinyesi itapunguza gharama ambazo mtaingia katika mikataba mtakayoiweka baina ya *REA* na hiyo taasisi nyingine. Kwa kufanya hivi pia, itasaidia kuhifadhi mazingira katika zile sehemu za magereza kwa kupata nishati ya kutosha, kwa ajili ya matumizi mengine kama vile kuchemsha maji na kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mavi ya ng'ombe au kinyesi cha ng'ombe, kama nilivyosema kwa vile magereza mengi yana mifugo kwa hiyo, ni kupata tu hii teknolojia ambayo ina msaada mkubwa na itapunguza gharama nyingi. Mitambo ya kuchakata gesi hii inapatikana kwa bei nafuu hapa nchini. Kwa mfano, hata

sisi wenyewe kwenye shamba letu, *Msonge Farm,* tuna ng'ombe sita na tunapata gesi ya kutosha ya kutumia kwenye mambo yetu, kuwashia taa na kufanya mambo yote yanayohitaji gesi. Kwa hivyo, kwa magereza jambo hili litakuwa zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninalo kuhusu magereza ni kwamba, hawa watu wanafanya kazi kubwa sana, lakini mazingira yao wanayokaa ni hafifu na masilahi yao pia, ni madogo. Kwa hiyo, ninapendekeza wale askari wa magereza waboreshewe masilahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusu magereza. Magereza mengi huko wilayani yamechoka sana mpaka yanavunja moyo, kwa mfano Gereza la Lushoto. Ninaiomba Serikali ifanye mapitio na kuyajenga upya magereza yote nchi nzima, ili kidogo yawe na sura ya kuwafanya wahalifu wasipende kuja kufungwa kwenye magereza kama yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu naomba niwe na hayo tu, lakini napongeza sana mambo ambayo yanafanywa na Wizara hii. Kwa kweli, mnaupiga mwingi, pokeeni maua yenu. Naunga mkono hoja, ahsanteni.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha. Nilimuita Mheshimiwa Grace Tendega, atafuatiwa na Mheshimiwa Anania Tadayo.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri, *Eng.* Masauni, Naibu Waziri Mheshimiwa Sillo, Makamishna Jenerali wote pamoja na watendaji wa Wizara hii. Karibuni sana kwenye kamati yetu na hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa *Eng.* Masauni kwa Mradi wa *Safer City*. Ule Mradi wa ukianza, hizi hoja ambazo zinazungumzwa hapa kuhusu bodaboda na mambo mengine zinaweza zikaisha, mradi huu utasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameandika katika hotuba yake kwamba, watafunga kamera 6,500. Wale ambao tulikuwa Rwanda tuliona, pale bodaboda wapo na unaweza ukakuta hakuna askari kabisa kwa sababu, kuna mambo ya *Artificial Intelligence* ambayo yamewekwa pale, kwa ajili ya kuangalia na ku-*monitor* mtandao mzima wa waendeshaji wa magari, bodaboda na waendeshaji wengine katika miji na mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mradi huu ukitekelezeka haya yote ambayo tunazungumza hapa yatakuwa ni ndoto. Kwa hiyo, nakupongeza na ninaomba Wizara ya Fedha, inasikia, watoe fedha kwa Wizara hii. Fedha za maendeleo katika Wizara hii zinakwenda kidogo sana, hawa ni watendaji wetu wa majeshi. Tuna majeshi hapa, hawa hawazungumzi wanatekeleza tu kwa hiyo, kama fedha haziendi tutashindwa kufika mbele na kutekeleza majukumu ambayo tumewapangia. Kwa hiyo, unaona katika maoni ya Kamati sisi tumesema tunaomba fedha zitolewe ili waweze kufanya kazi zinazokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie majeshi yetu, wakiwa hawapewi fedha wanapata changamoto zipi? Tukianza na madeni. Kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, 2020/2021 mpaka 2022, Jeshi letu la Magereza walienda kuhakiki wafanyakazi ambao wana madai. Hata hivyo, wafanyakazi wale walipohakikiwa wakaambiwa watalipwa, lakini walilipwa kidogo na sio pesa zote ambazo walikuwa wametarajia kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana nasema Wizara ya Fedha iwalipe Magereza na Uhamiaji. Iwape pesa za maendeleo, ili waweze kulipa malimbikizo ambayo wanajeshi na askari wetu wanadai. Kwa hiyo, unakuta kwamba, wale wamefanya kazi kwa pesa zao, wametumia pesa zao, wanadai kwa miaka mitatu, minne, lakini hawajazipata, wana watoto na familia kwa kweli, inatia uchungu kwa hawa watendaji. Tukiwajali watumishi wetu watafanya kazi nzuri kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya likizo kwa Jeshi la Polisi na majeshi mengine yote bado ni changamoto sambamba na upandishaji wa vyeo. Angalieni upandishaji wa vyeo, ili waweze

kupanda. Wanakwenda kwenye mafunzo, basi muwapandishe kulingana na hitaji linavyotakiwa, mtu anapata motisha anapokuwa amekwenda kwenye mafunzo na anaporudi anapanda cheo. Kupanda cheo ni kupata mshahara mzuri na kuendelea kufanya kazi kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni ajira na ikama. Jeshi la Zimamoto lina askari wapya 225, polisi 7,228, Magereza 734 na Uhamiaji 521, hiyo ni ikama mpya. Hata hivyo, ukiangalia Jeshi la Magereza peke yake wanahitaji askari 29,796, lakini waliopo ni 14,592. Bado tuna hitaji la watumishi 15,000 na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri wa Utumishi aajiri watu waende kwenye haya majeshi, wanapata shida. Pia, katika ajira mnatakiwa ku-*consider* askari wanawake kwenye haya majeshi. Kwa mfano, Jeshi la Magereza unakuta kuna wafungwa wa kike, wajawazito, wenye watoto, wanaowahudumia ni wale wanawake walioko pale. Kwa hiyo, tunaomba muongeze idadi ya wanawake katika jeshi letu, ili waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nawapongeza Jeshi la Zimamoto, wanafanya kazi kubwa. Wamejenga nyumba za makazi nzuri kabisa, lakini hawa kwa mwaka huu wa fedha hawakupata kabisa fedha za maendeleo, ni sifuri kabisa. Pamoja na kutopata kabisa fedha za maendeleo bado wamekuwa wakifanya kazi kubwa, tumekwenda kuona nyumba za wafanyakazi wa ngazi ya chini ambazo wamezizindua, wamefanya vizuri kabisa, ninawapongeza jeshi hili. Hata hivyo, muendelee kukusanya maduhuli, ili muweze kupata fedha zaidi za kuweza kuendesha shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naupongeza uhusiano wa Jeshi letu la Polisi na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuweza kuungana, ili kujenga Polisi Kata. Hiki ni kitu kizuri sana kwa sababu, tuko kule tuna wananchi na kwenye kata hakuna nyumba za Polisi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tendega, malizia.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mahusiano yao hayo yatatusaidia sana kuendeleza Jeshi la Polisi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Tadayo, mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Mohammed Said Issa.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naanza kwanza kwa kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa jinsi ambavyo ameweka kipaumbele katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati kwa hiyo, ninayo fursa ya kuona mambo makubwa ambayo yanendelea katika Wizara hii nyeti. Pili, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na timu yake nzima bila kuwasahau Makamishna wetu wanne ambao wanasimamia majeshi yetu haya manne kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya kwa kuiheshimisha na kuiweka salama nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni nyeti sana. Tunapozungumzia mambo mengi na makubwa yanaanzia katika Wizara hii. Kwa mfano, suala la haki jinai ambalo limepewa kipaumbele sana na Serikali ya Awamu ya Sita linaanzia katika Wizara hii na kuishia Wizara hii. Mhalifu anaanzia Polisi na akitiwa hatiani anakwenda magereza na kote huko ni ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hata suala la uchumi na masuala yote tunayotamba kwenye nchi hii kama utalii, wawekezaji na masuala ya diplomasia yote hayo na hata wageni wakiingia *airport* mtu wa kwanza wanayekutana nae ni wa Uhamiaji, wa Wizara hii na siku ya kuondoka ni wao ndio wanamuaga na barabarani wanakutana na *traffic*. Kwa hiyo, ni Wizara ambayo inabeba sura ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa suala la maafa ambalo kwa mwaka huu, nadhani hatujapata somo dogo, tumepata somo kubwa sana. Kabla hatujafikiria kupeleka

magodoro na chakula wanaotangulia ni watu wa uokoaji. Kwa hiyo, Wizara hii ni nyeti na ndiyo maana naungana na wote wanaosema fedha za kutosha zipelekwe kwa wakati, fedha za matumizi ya kawaida pamoja na za matumizi ya maendeleo, hasa katika suala zima la mafunzo na kujengewa uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii, kwa ajili ya huu Mradi wa Kesi Mtandao ambao unaendelea. Ni mradi ambao utaharakisha upatikanaji wa haki wakati kesi inapofunguliwa pale Polisi na Ofisi ya *DPP* wanaona kinachoendelea. Hii itarahisisha na kuleta ufanisi mkubwa katika masuala ya haki jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo Mradi nyeti wa *Safer City* ambao utatusaidia sana kuleta usalama. Mradi huu utasaidia kuweka utofauti wa kiusalama ukilinganisha na nchi ambazo zina vibaka wengi na watu kupata shida ya kunyang'anywa vitu njiani. hii itatokana na kufungwa kwa kamera ambazo zitasaidia kufanya kila kitu kionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi ya mwisho ambayo siyo ndogo, ni kubwa, ni jinsi ambavyo Jeshi la Polisi linaweza kusimamia vizuri maandamano ya vyama vya siasa ambayo yameruhusiwa na Serikali ya Awamu ya Sita. Wanafanya kazi kubwa ya kutuheshimisha na wamekuwa wadau wakubwa wa demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisahau kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa ajili ya Gari la Uhamiaji ambalo aliniahidi katika Bunge hili. Nadhani Mwanga sasa tunakwenda vizuri na tutaacha kutembea na vidumu vya mafuta na *oil* kwenye gari ambalo lilikuwa na hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote haya bado changamoto ambazo zimetajwa na wenzangu, kama vile uduni wa makazi ya askari na mazingira yao ya kutendea kazi, ni mambo ambayo lazima yatiliwe mkazo ikiwa ni sambamba na madai yao yalipwe kwa wakati. Hatupendi kuwa na askari ambao wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zito kidogo la kudhibiti kambi za wakimbizi, ili wasipenye huko mitaani, halafu baadaye wakajichanganya na sisi wakawa hatari kwa usalama wetu. Kwa mfano wenzetu wa Malaysia ukiacha hii *my card,* ile *smart card* yao inaitwa *my card* ya Kitambulisho cha Taifa wana nyingine wanaita *My PR* ambayo wanapewa wageni wanaokaa kwa muda mrefu. Inawezekana kabisa pia tukatengeneza kitambulisho kwa ajili ya hawa wakimbizi ambao wamekaa muda mrefu ili atakapoomba kitambulisho chetu cha *NIDA* asomeke kule kwenye kile kitambulisho chake kama mkimbizi asiweze kutuchanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimevutiwa sana na hoja ya Mheshimiwa Shangazi juu ya suala la *RITA* na *NIDA*. *RITA* kama ambavyo tunafahamu inasimamia mambo ya vizazi, vifo, ndoa, ufilisi na udhamini. Hapa wanahitajika wasomi wa sheria pamoja na ustawi wa jamii, ukija *NIDA* masuala ya vitambulisho vya Taifa ni masuala ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni Wizara ya Katiba na Sheria ikiwa na msuli wa kutosha wa kiusalama wa kusimamia *NIDA* na wala sioni Wizara ya Mambo ya Ndani ikiwa na ubobezi wa kutosha wa kisheria wa kusimamia *RITA*. Kwa hiyo suala la kuunganisha hizi Taasisi mbili liangaliwe kwa umakini sana kabla hatujafikia mwisho wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungefikiria kukua zaidi kama wenzetu wa Malaysia nilisema kwamba wao kitambulisho chao cha *NIDA* pamoja na kuwa ni kitambulisho cha mtu lakini pia kinatumika kama *ATM card*, kama *driver's license*, kama *medical insurance* na kadhalika tufikirie kukua zaidi kuliko kuunganishwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nimwite sasa Mohamed Said Issa, mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitie neno kwenye Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Sitapoteza muda kwanza nianze kwa Kituo cha Polisi Jimbo la Konde kilichopo pale Konde Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari nimeshapata kuungwa mkono kwa sababu nitashika shilingi na watu wataniunga mkono. Hii ni kwa sababu Mheshimiwa Waziri katika bajeti tatu zilizopita zote ameniahidi kwamba kituo kile kinakwenda kujengwa pamoja na nyumba za makazi wa polisi pale. Kwa hiyo leo nitamshikia shilingi Mheshimiwa Waziri. Sasa nimwombe tu kabla sijashika shilingi leo alielezee Bunge hapa kwamba kituo kile kinakwenda kutengenezwa na isiwe tena ni hadithi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, mchango wangu wa pili nataka nizungumzie suala zima la ubaguzi. Leo Vyombo vya Ulinzi na Usalama vipo hapa kwa hiyo ningetamani sana kulielezea jambo hili. Sisi Wazanzibar tumekuwa tukibaguliwa kwenye mitandao, kwenye vyombo vya habari, kwenye mikutano hatujui sababu ni nini? Sasa jambo hili nilitamani nilichangie mimi leo ili Vyombo vya Ulinzi na Usalama vijue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tumekuwa tukisikia Mheshimiwa Rais akibaguliwa kwa Uzanzibar wake na mwisho anaambiwa kwamba amekopeshwa kutoka kule Zanzibar. Hili jambo si sahihi, mimi kama Mzanzibar kwa sababu siku yoyote naweza kuwa Rais wa nchi hii. Sasa naweza kuja kubaguliwa kama anavyobaguliwa Mheshimiwa Rais jambo hili si sahihi, naomba vyombo vyetu hivi vikemee siyo jambo sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyobaguliwa Mheshimiwa Rais kwa kuambiwa kwamba anatawala nchi ambayo siyo ya kwake, amekopeshwa hivihivi ndio anaweza kubaguliwa na mtu mwingine yoyote. Sasa jambo hili kama

Mzanzibar anachaguliwa na hii ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Anatropia.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nataka nimpe taarifa mchangiaji anayeongea vizuri sana. Sisi tunaamini ni raia wamoja, ni nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini katika hali ya kusikitisha Mheshimiwa Mbunge alisimama hapa Bungeni akisema; "Wanaotoka Bara wapatiwe *passport* ya kwenda Zanzibar." Sasa nataka kusema sisi ni nchi moja hatuhitaji *passport* ya kwenda Zanzibar au kuja Tanganyika, hiyo ndiyo taarifa yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo Taarifa siipokei.

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza sijakuuliza. Unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hiyo siipokei kwa sababu jambo hilo liko hadharani kila mtu amesikia kuna kikundi cha watu akiwemo Mwenyekiti Mbowe amekuwa akimbagua Rais pamoja na na kikundi chake. Sisemi CHADEMA ndiyo wanaofanya hivyo lakini wako watu hawa wamekuwa wakimbagua Rais pamoja na mimi mwenyewe kwa kuweka hii hoja ya *passport*…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** … Hii ni hoja yangu mimi Mbunge huku nililetwa kuchangia kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Konde…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** …Wananchi wa Zanzibar lakini na Watanzania sasa jambo hili si sahihi…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza sasa yeye siyo Mzanzibar yeye ni Mtanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa unaipokea Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kunambi?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei, Tanzania ni Muungano wa nchi mbili…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** …Zanzibar imeungana na Tanganyika ikiwa ni nchi mbili huru na mimi naamini kwamba ndani ya Tanzania kuna Tanzania bara (Tanganyika) na Zanzibar kwa hiyo siipokei. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** …Niacheni niendelee na hili suala la *passport* naomba mnipe muda niwaelezee vizuri sina nia ya kuvunja Muungano, sina nia ya kero za Muungano.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** …jambo hili mnalichukulia kama mzaha…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa zinatosha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa, kwa mujibu wa Kanuni Taarifa mwisho ni tatu. Taarifa ya mwisho Mheshimiwa Condester.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunataka kumweleza mwenzetu kwamba sisi Watanganyika na Wazanzibar ni kitu kimoja toka tumepata uhuru na wakati mwingine watu wakikosa hoja wanatafuta hata ambacho hakina sababu kusema. Kwa hiyo yule alikosa hoja na Watanzania wote tunajua alikuwa anasema hayo. Kwa hiyo yeye aridhie kwamba yeye ni Mtanzania mwenzetu hayo mambo yeye atulie tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Kwanza hili suala la kumbagua Rais huyu kwa sababu eti amekuwa Rais kutoka Zanzibar, nataka nitoe mfano mmoja CHADEMA kilimweka mgombea hapa Hayati Edward Lowassa na mgombea mwenza alikuwa ni Babu Juma Duni Haji. Tuseme leo angekuwa Rais Babu Juma Duni Haji wangesema wamemkopa?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo siyo sahihi ubaguzi huu hatuutaki na suala hili nililosema la *passport* nifuateni niwape *clarification* mtaelewa tu. Sikuwa na nia ya ubaguzi Wazanzibar waingie huku kwa *passport* Watanzania

Bara waingie kule kwa *passport* na hakuna tatizo ni suala tu la kulinda visiwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa Said muda wako wa kuchangia umekwisha

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu. Tumefika mwisho wa kipindi chetu hiki cha kuchangia lakini kabla hatujaondoka tuna majina hapa ya wageni mahiri na mashuhuri sana ndani ya ukumbi wetu ambao ningependa niwatambulishe kwa niaba yenu.

Tuna Wenyeviti wa CCM wa Mikoa kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na kwa umuhimu wake ningependa niwataje na tuwatambue. Tuna Ndugu Loy Thomas Sabaya, Mwenyekiti wa Mkoa wa Arusha. Kuna Ndugu Abbas Zuberi Mtemvu, Mwenyekiti Mkoa wa Dar es Salaam; Tuna Ndugu Adam Omari Kimbisa, Mwenyekiti wa Mkoa wa Dodoma; na Ndugu Nicholaus Kasendamila Nabayo, Mwenyekiti wa Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Daudi Yassin Mlowe, Mwenyekiti wa Mkoa wa Iringa; Ndugu Nazir Mustapha Karamagi, Mwenyekiti wa Mkoa wa Kagera; Ndugu Iddi Hassan Kimanta, Mwenyekiti Mkoa wa Katavi; Ndugu Jamal Abdalah Tamim, Mwenyekiti wa Mkoa wa Kigoma; Ndugu Patrick Pata Boisafi, Mwenyekiti wa Mkoa wa Kilimanjaro; Ndugu Hassan Mohamed Jarufu, Mwenyekiti wa Mkoa wa Lindi; Ndugu Peter Toima Kiroya, Mwenyekiti wa Mkoa wa Manyara; Ndugu Patrick Adkin Mwalunenge, Mwenyekiti wa Mkoa wa Mbeya; Ndugu Joseph Peter Masinga, Mwenyekiti wa Mkoa wa Morogoro; Ndugu Talib Ali Talib Mwenyekiti wa Mkoa wa Mjini; Ndugu Said Mussa Nyengedi, Mwenyekiti wa Mkoa wa Mtwara; na Ndugu Michael Lushinge Masanja, Mwenyekiti wa Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Katika Wenyeviti pia tunao Ndugu Silafu Jumbe Maufi, Mwenyekiti wa Mkoa wa Rukwa; Ndugu Odo Killian Mwisho, Mwenyekiti wa Mkoa wa Ruvuma; Ndugu Mabala K. Mlolwa, Mwenyekiti wa Mkoa wa Shinyanga; Ndugu Martha Moses Mlata, Mwenyekiti wa Mkoa wa Singida; Ndugu Shemsa Mohamed Seif, Mwenyekiti wa Mkoa wa Simiyu; Ndugu Radwell Tullo Mwampashi, Mwenyekiti wa Mkoa wa Songwe; na Ndugu Rajab Abdallah Abdulrahman, Mwenyekiti wa Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Kuna jina la Mwenyekiti wa Mkoa wa Njombe hapa limekuwa *ticked,* lakini najua angekuwa humu ndani na siamini kama yupo kule, naamini hayupo.

Waheshimiwa Wabunge tutaanza na wachangiaji wafuatao mchana, tutaanza na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, tutakuja na Mheshimiwa Tarimba Abbas, halafu tutakuja na Mheshimiwa Enosy Swalle.

Baada ya kusema hayo, nasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.12 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea, namwita mchangiaji wetu wa kwanza mchana huu, nilisema atakuwa Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Abbas, Mheshimiwa Swalle ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufanya kazi ni suala la kikatiba na ni haki ya kila mtu au raia wa nchi hii, katika kuifahamu na kuifafanua nadharia hii ndiyo maana Serikali ilipoona kwamba haina ajira za kutosha za kuajiri vijana na wananchi wote iliamua kurasimisha baadhi ya biashara zikiwemo biashara za bajaji na bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge na Kaka zangu Makamanda, wakati mwingine busara na hekima umuhimu wake huishinda sheria. Ndugu zetu hawa bodaboda ni ulezi wetu huu; sisi tukiwa kama viongozi ni lazima tuwalee. Bodaboda wana viongozi wao, bodaboda wana usajili wao na wanavyo vituo vyao na vinaeleweka. Namna bora ya kusimamia haki na heshima kwa vijana hawa, ni vizuri sana na ipo kila sababu ya kutumia viongozi wao na kuwapa elimu juu ya usimamizi wa misingi bora ya utekelezaji wa sheria bila ya shuruti, hususan katika masuala yanayohusu barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwapa elimu itakuwa ni bora zaidi kuliko kila wakati Jeshi la Polisi kushughulika nao kwa njia za kufanya hizi doria za kuwashtukiza, kwa sababu doria hizo mara nyingi zinakuwa siyo za kujenga, badala yake tunawajengea usugu vijana wale. Kazi rahisi ilikuwa ni kuwapa elimu juu ya sheria za barabarani, lakini tunapita njia ngumu kwa mambo yaliyorahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine ukamataji wanaofanyiwa vijana wale unakuwa siyo wa halali na unashusha hadhi na heshima na utu wa mtu. Ieleweke kazi ya bodaboda ni kazi kama ajira nyingine na jamii ya bodaboda ni jamii ambayo ni sawasawa na jamii ya wafugaji, tunatofautiana katika majukumu na mazingira ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona Askari wanaenda kukamata bodaboda kwa kuvizia na kwa kunyatianyatia au kwa kushtukiza, basi jua kuna kasoro katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi. Ukiona taratibu za uvamizi wa vituo vya bodaboda zimekithiri basi elewa kwa wenye kuelewa wataelewa kwamba

kuna hitilafu katika mifumo ya ufuataji wa misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke ya kwamba dhamira ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwenda kujenga vituo katika maeneo ya vijiji na Kata, kushusha vituo katika maeneo ya wananchi ni kuhakikisha wanawashirikisha wananchi katika dhana nzima ya Posili Jamii au Polisi Shirikishi. Utaendaje kuitekeleza dhana hii wakati una mkakati wa kupanga doria za kushtukiza? Hatimaye wananchi hao wakiwa wanabugudhiwa na hizo doria usitarajie kwamba wananchi hao watatoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kimoja, nina mfano mzuri wa matukio mengi sana hususan kule Kaskazini maeneo ya Nungwi. Bahati kule ukuaji wa miji umeongozeka na panapokuwa na ongezeko la ukuaji wa mji basi vijana na biashara ya bodaboda inakuwa inakithiri. Vijana wangu wa maeneo yale wamekuwa hawana furaha wala hawaifurahii kazi ile ya bodaboda kutokana na adha na bugudhi za Jeshi la Polisi, kwa misingi gani? Wakati mwingine utakuta Jeshi la Polisi wanawavizia, wanajificha kabisa katika vichaka ili wawakamate hali ya kwamba hawana sare ama *uniform*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine unaweza ukawakuta Jeshi la Polisi linakusanya vyombo vyao hali ya kwamba vyombo viko maskani vijana wametulia, wanavichukua na kuvipeleka katika Kituo cha Polisi, baadae kituo kile kinageuka kuwa karakana badala ya kuwa kituo cha kushughulikia raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kwa kusema kwamba unapohisi Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa kuvizia vizia na linafanya kazi kwa kudowea dowea hawa raia maana yake kuna kasoro katika Jeshi la Polisi. Kuna kasoro kubwa ndani ya Jeshi la Polisi kwa watendaji wadogo wanaoenda kusimamia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine Jeshi la Polisi lina kawaida ya kuwakimbiza bodaboda, bodaboda kasajiliwa, chombo chake kinaeleweka na kijiwe chake kinaeleweka, kuna haja gani ya kumkimbiza wakati wana viongozi wao? Kitu

ambacho kimekuwa kikisababisha migogoro na ajali nyingi barabarani, wakati mwingine tunawalaumu vijana, lakini hata Jeshi la Polisi kwa misingi hiyo kwa sababu wale vijana hawana pa kusemea, tunakuwa tunawabebesha lawama zisizokuwa za msingi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simai muda wako umekwisha ni kengele ya pili.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Tarimba Abbas.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti, Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kwanza kwa haraka sana niweze kuchukua nafasi hii kupongeza juhudi za kitaifa kuipongeza klabu ya *Young Africans* kwa kuweza kuchukua ubingwa mapema zaidi na hivyo kuashiria kumalizika kwa ligi ingawa kuna watu wanahangaika na ushindi wa pili na ushindi wa tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Nilikuwa nikiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Ukurasa wa 53 hadi 59, Waziri anazungumzia zaidi masula ya uzimaji wa moto. Hata ukiangalia ujenzi wa vituo na kuleta magari, nashukuru kuna juhudi kubwa sana ya Serikali katika kuongeza uwezo wa jeshi hili katika kukabiliana na majanga ya moto. Sijaona sana ni kwa kiasi gani jeshi hili linapewa nyenzo za uokoaji, eneo la uokoaji mimi sijaliona zaidi ya uzimaji wa moto, sasa tuzungumzie hayo hayo ya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nizungumzie changamoto ambazo ziko Dar es Salaam. Tunakumbuka mwaka 2021 Soko la Kariakoo lilipoungua. Vilevile, kule Jimboni kwangu Kinondoni katika Kata ya Magomeni kuna nyumba mbili ziliungua pale na pale hatuko mbali sana na kituo cha magari ya Zimamoto kinachoitwa *Fire* ni karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto za barabara zetu kuwa finyu na msongamano wa magari inapotokea matatizo ya moto siyo rahisi sana kwa magari yale ya Zimamoto hata kama ni mazuri kiasi gani kuweza kuwahi kufika katika eneo ambalo nyumba zinaungua ili kuweza kusaidia kuokoa hata mali zilizobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikifuatilia hata wakati taarifa hii ya kuungua kwa soko la Kariakoo inatolewa kulikuwa na sababu karibu 10 ambazo zinaonesha jinsi matatizo ya majanga haya yanavyotokea, lakini mimi nikachukua moja lile wanasema kutokuwepo kwa chemba za maji, wanaita *fire hydrants*. Mheshimiwa Waziri ameizungumzia katika *paragraph* ya 138, amelizungumzia suala hili kwa uchache sana lakini hii kitu ni muhimu sana. Magari ya Zimamoto yanapofika katika nyumba zinazoungua wakimaliza maji ambayo wameyachukua katika magari yao inabidi watafute kizimba cha maji kilichopo karibu, sasa kwa Dar es Salaam vizimba vya maji ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Aprili mwaka 2013 kuna taarifa ilitolewa na wakati ule kulikuwa na bwana mmoja ni Kamishna anaitwa Fikiri Sala alisema kwamba, "Dar es Salaam *fire hydrants* 1,268 hazifanyi kazi" na taarifa zilizopo ni kwamba nyingine zimefukiwa na nyingine watu wamejenga juu, wengine wajenga ndani ya nyumba na kadhalika. Hili ni kosa la kijinai kabisa kuweza kufanya vitendo ambavyo vinafanya *fire hydrants* ipotee na isiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa hiyo walisema kwamba *fire hydrants* mwaka 2013 zinazofanya kazi ni 74 tu. sasa utaona hali ilivyo ngumu ingawa taarifa zilizopo sasa hivi wamezihuisha, ahsante sana kwa kuzihuisha na kufikia 108 lakini ni ndogo sana. Sasa nikiangalia fedha ambazo Mheshimiwa Waziri

anaziomba shilingi milioni 150 kwa Tanzania nzima mimi naona Serikali bado haijaingiza nguvu katika suala zima la kutengeneza *fire hydrants.* Hii ni hatari kwa sababu tutakuwa tumerudi kulekule kwenda kumalizia kuokoa nyumba isiungue sana lakini mali hazitokuwepo kwa sababu magari yakimaliza maji lazima yatafute *fire hydrants* na vizimba hivi sasa hivi havipo pale Dar es Salaam havifanyi kazi na kwa hali hiyo naiomba Serikali itilie mkazo suala la kujenga vizimba. Sasa sijui Waziri atapokuja atatueleza nini juu ya kuhakikisha kwamba shilingi milioni 150 inakwenda kujenga vizimba wapi na wapi kwa sababu bila hivyo hataweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi sana kuhusiana na biashara ya bodaboda. Biashara ya bodaboda ni biashara muhimu sana. Hadi ilipofika Februari mwaka 2003, naomba tufahamu kwamba tumetumia dola za kimarekani milioni 136.7 sawa na shilingi bilioni 319 kwa ajili ya kuagiza pikipiki. Hiyo ni *industry* kubwa sana. Kuna ma-*graduates* wanafanya kazi mule ndani, lakini kutokana na umuhimu wa biashara hii mbona Serikali haionekani kuisaidia hii biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini iisaidie? Tunaiachia ijiendeshe yenyewe na ndiyo maana Wabunge wengi wakisimama wanalalamikia utaratibu wa usimamizi wa sheria za barabarani, hamzisaidii. Nakumbuka nilivyoingia Bungeni mara ya kwanza kabisa niliuliza swali linalohusiana na masuala ya bodaboda. Ukweli ni kwamba Serikali mnatuambia tu, mnatutoa barabarani kwamba mnatoa elimu, hata hiyo elimu tangu imechukua miaka mitatu tangu itolewe, hata chuo kikuu mtu amesha-*graduate*. Ni lini basi atakaa aelezwe umuhimu wa ufuataji sheria za usalama za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 2007 iko wazi kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha hoja yako.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimissha kwa kuiomba Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba biashara ya bodaboda inaendeshwa vizuri ili

watu wasiendelee kupata ajali. Nataka ujue pale Muhimbili Moi watu 280 kwa mwezi wanapelekwa kama majeruhi wa pikipiki ni watu wengi sana hao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo naiomba Serikali ikija hapa itueleze ni kitu gani kinawazuia wasiweze kusimamia sheria za usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba Abbas. Sasa namwita Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle aweze kutoa mchango wake, baada ya hapo atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mheshimiwa Haji Amour Haji ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza niungane na Wabunge wenzangu wote kuvipongeza sana vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu nikiwa kama Mjumbe wa Kamati hii ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vikiongozwa na makamanda wetu kwa maana *CGI, CGP, CGF* na *IGP* wanafanya kazi nzuri sana kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi hapa mmesema miaka ya nyuma malalamiko juu ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama yalikuwa makubwa sana. Sasa hivi wote mmeshuhudia hata vyama vya upinzani vinapongeza kazi nzuri ya vyombo vya ulinzi na usalama. Hii maana yake tunakokwenda ni kuzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuwaambia Waheshimiwa Wabunge wenzangu hata mipango ya Wizara hii ya Mambo ya ndani ni mipango mikubwa. Tumeshuhudia kwenye

Taarifa ya Mheshimiwa Waziri hapa wanakusudia kufunga kamera kwenye miji yote kulinda usalama wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Waheshimiwa Wabunge tuwaunge mkono na sisi kama Kamati tuko pamoja na Wizara hii na vyombo vyote vya ulinzi na usalama. Naomba nichangie maeneo mawili au matatu kwa mchana huu wa leo. Sehemu ya kwanza nakubaliana sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri juu ya mipango ya Serikali ya kununua magari ya askari wetu na kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya majeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie eneo maalum kuhusu wizi wa mtandao. Dunia inakwenda mbele sana. Zamani wizi mkubwa ulikuwa ukifanyika kwa kutumia nguvu, *SMG,* kuteka magari na kadhalika, sasa hivi wizi mkubwa upo kwenye mitandao. Hili nataka niliombe Jeshi la Polisi wakishirikiana na watu wa Wizara ya TEHAMA wafanye kazi mahsusi usiku na mchana, kupanga mipango ya kudhibiti uhalifu wa mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naviamini vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Juzi tumeshuhudia pale Makutupora watu wa Mizinga wamezindua bomu la kufukuza tembo nchini. Sina mashaka ya kwamba vyombo vyetu vinao uwezo wa kukaa na kutafuta njia bora ya kudhibiti wizi wa kutumia mitandao. Hata *BOT* walitoa taarifa miezi miwili iliyopita kwamba benki nyingi sasa hivi zinaibiwa fedha siyo kwa unyang'anyi bali kwa kutumia mitandao. Nafahamu kazi nzuri imeanza naomba jambo hili lipewe mkazo kwa vyombo vyote vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba niseme kuhusu bodaboda. Wabunge humu ndani ya Bunge wamesema na inaonekana kama kuna lawama kidogo kwa baadhi ya askari wetu kwamba pengine wanawaonea watu wa bodaboda. Mtazamo wangu ni tofauti kidogo, nadhani vijana wetu wa bodaboda pamoja na elimu ambayo wanapewa lakini wengi hawana leseni za kuendesha bodaboda. Kinachotokea ni nini? Wakiona askari wakati fulani wanakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Bunge tulitunga Sheria kusema kwamba bodaboda walipie leseni shilingi 70,000. Nina ombi kwa

Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa. Wakati wa bajeti ya fedha hili jambo nitalisema na ikibidi nitashika shilingi. Serikali ilete sheria humu ndani ya Bunge, tupunguze gharama ya watu wa bodaboda kupata leseni. Sasa hivi leseni ya bodaboda ni shilingi 70,000, sawasawa na leseni ya dereva wa *Grade C*. Ni vema gharama hii ya leseni ya bodaboda ikashuka angalau mpaka 20,000 ili bodaboda wote wapate mafunzo mazuri wafanye kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni muhimu pia hao bodaboda wote wakapewa namba maalum za kwenye vituo vyao. Watambulike kwamba bodaboda fulani anafanya kazi kwenye kituo fulani ili Jeshi la Polisi lisilazimike kuwakimbiza badala yake liwabaini kwa namba zao na sehemu ambako wanafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu kwa mchana huu, nataka niseme kidogo kuhusu Magereza. Naona muda wangu umekwisha lakini rai ni kwamba watu wa Magereza katika vyombo vyote ndiyo ambao wanapata fedha kidogo sana ya kuendesha taasisi yao. Niiombe Serikali wawaongeze fedha watu wa magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Swalle. Nimwite sasa Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Chombo hiki cha Polisi ndiyo kimepewa dhamana ya usalama na ulinzi wa mali na raia wa Tanzania. Wana dhamana hiyo ili wazalishe amani na utulivu na wakishazalisha amani na utulivu wananchi waweze kufanya kazi zao kwa amani, weledi na uhuru na tuweze kuliletea Taifa letu maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili waweze kuzalisha hiyo amani na utulivu, ni lazima na wenyewe wawe na amani na utulivu. Kwa sababu kama ilivyo kawaida, hutegemei kwamba utapata nyanya chungu kwenye mwembe. Mwembe unatoa embe na nyanya chungu zinatoa nyanya chungu. Sasa ili sisi tupate amani na utulivu, raia na mali zetu tuwe salama, ni lazima polisi na wao wawe na amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tumesomewa bajeti ya Wizara nzima kwa ujumla kwamba wamepelekewa 55% na hii 55% wamepelekewa robo ya tatu, maana yake ni Januari pale Februari. Ina maana hawa polisi kuanzia mwezi Julai mpaka Januari waliishi vipi? Wamefanya kazi zao vipi? Magari yao yametembea kwa vipi? Wamelipa *bill* kitu gani, maji na umeme? Wale tuliowapeleka kule *cell* wamekula kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba kama tunataka kufanya kazi zetu kwa amani na utulivu na tunategemea tupate zao kutoka kwa polisi hatuna ujanja ni lazima tuwekeze kwao kama ambavyo ukitaka kupata maziwa mengi kwenye ng'ombe lazima umlishe. Tunataka amani na utulivu wa Taifa letu uwe kwa asilimia kubwa na 100%, lazima tuwekeze, bajeti yao iende kwa 100% na iende kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalalamika hapa namna ambavyo polisi wanafanya kazi. Tunalalamika namna ambavyo watoto wetu wako kwenye *risk*, watoto wa shule sasa hivi wako kwenye *risk*. Watoto mitaani wanapita wamelewa, yaani polisi wangekuwa tu wana kazi nyingine ya kuchunguza hata vile viashiria vya uovu kwenye nchi, viashiria vya hatari kwa raia, maana wao ndiyo wanatuangalia usalama wetu na viashiria vya hatari kwa watoto wetu; hana hata mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi Kata yupo lakini hawezi, kata zetu tunajua, kuna kata nyingine unakwenda kilomita 80 kata moja. Polisi Kata anakwendaje? Polisi wanapataje muda wa kuzunguka zunguka hata kwenye shule na taasisi kuona usalama uliopo kwenye shule hiyo kama nusu mwaka nzima hawajapelekewa hata shilingi kwa ajili ya kuendesha shughuli zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi wanakuwa *frustrated*, hawana amani na utulivu. Leo hawa tuna *think tank* ambao ni polisi, hawa wengi karibu wanastaafu. Ni vile tu wanaishi kwenye *chain* ya *command*, kwamba mambo yao ni amri lakini wengi wao unaweza kuwaona *serious* ukajua ndiyo tabia ya polisi kuwa *serious* lakini kumbe hawana utulivu. Kikokotoo peke yake kimewachanganya kwanini haya mambo ya sera hizi mnakwenda ku-*impact* kwa polisi, yaani hawa mkishawachanganya na sisi wote tunachanganyikiwa, utulivu wetu unakuwa hatarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwanza polisi wawe *regarded* kama majeshi mengine kwa sababu *salute* wanapiga kama majeshi mengine. Polisi wasichukuliwe kama watumishi wa kawaida. Ile biashara ya kikokotoo wawe *regarded* kama majeshi mengine. Tunashukuru kwamba hicho kikokotoo wamesema kwamba watakishughulikia lakini hawa polisi tunataka jeshi la kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaambiwa sasa hivi majambazi hawaibi tena kwa mitutu wanatumia akili, ndiyo hicho alichokuwa anasema Mheshimiwa Swalle. Wanatumia akili zaidi ndiyo maana wanaiba kidijitali, wanaiba kwenye mitandao siyo tena wanakujia na mapanga na nondo. Hao wa mapanga na nondo ni vibaka wale ambao bado hawaja-*graduate* kwenye ule uhalifu wa hali ya juu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa polisi wetu nao wanatakiwa wawe na *IQ* kubwa zaidi. Leo hii katika Jeshi la Polisi, mimi nina polisi wangu Iringa pale. Iringa sisi tuna bahati nzuri ya kuwa na vyuo vikuu vingi, wamesoma, wana vyeti, wana *degree*, wana *masters*, wakipeleka kwa mabosi wao hawavitambui vile vyeti, wanavikataa kwa sababu tu hawakupata kibali kwa bosi kwamba akasome. Tunataka polisi ya aina gani? Kijana kajitolea mwenyewe polisi kasoma wewe hutaki ku-*accept*, kutambua mchango wake kwamba huyu sasa ana *masters*, huyu ana *degree*, kwa sababu wewe huna, hapana. Tunataka jeshi lenye weledi na Kamati imeelekeza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima polisi waangaliwe wawe na amani. Kwa makazi yale wanayokaa, nyumba zile wanazolala. Mimi polisi wangu pale wana hati hati ya kugongwa na *cobra* kwa sababu kwanza wako porini lakini nyumba zenyewe zimejengwa tangu ukoloni. Polisi hata kwa kulala, wengine wana-*enjoy* futi sita kwa ngapi. Nyumba za polisi, leo tuondoke twende Kituo Kikuu cha Polisi cha Dodoma tuangalie nyumba za polisi, ndiyo mfano *capital city*, tukaangalie makazi ya askari, tuangalie jinsi yalivyo. Pale watapata usingizi wenye amani ipi ili watuzalishie sisi amani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapata utulivu upi? Nilikuwa naongea na akinamama wangu pale wa *Line Police*, tunaongea mambo yetu ya *VICOBA* na vitu vingine. Wakasema tunapata changamoto kubwa sana, sisi waume zetu hata kurudi kulala huku wanaona tabu. Wengine wanajiingiza tu kwenye *shift* za usiku siyo kwa sababu wamo, ila kwa sababu pa kulala panachekesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuwezi kuwa na chombo ambacho tunategemea kilinde amani ya nchi yetu, Waziri wetu, Mheshimiwa mwenye dhamana ya fedha umewanyima robo mbili hawana hela. Nawapongeza Watanzania, endeleeni kuwawezesha polisi kwa sababu kama mambo yenyewe ndiyo haya, tupeane tu hela mitaani humo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Msambatavangu, muda wako umeisha.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimwite sasa Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuata Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi leo nitakuwa na mambo mawili…

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, TAARIFA.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mchango umekwisha kwa mujibu wa Katiba hatuwezi kuruhusu.

Endelea Mheshimiwa Haji. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi hii na mimi niweze kuzungumza mambo mawili matatu yanayohusiana na Wizara ya Mambo ya Ndani. Kabla ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo alikuwa anayalea majeshi yetu haya yaliyokuwa katika Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nizungumze wazi kwamba hakuna kazi ambayo ni ngumu sana kama kazi ya ulinzi. Kazi ya ulinzi ni kazi moja ngumu sana na ni kazi ambayo inahitaji weledi. Kwa kweli, nasema wale wanaoongoza yale majeshi, wanaoongoza askari wetu, wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, pamoja na watendaji wao wote ni watu ambao wanatakiwa wawe na hekima kubwa sana kwa sababu ni kazi ngumu na ni kazi inayohitaji hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite katika mchango wangu hapa, kwa leo nizungumzie suala la Jeshi la Polisi. Kwa kweli, nizungumzie katika masuala yanayohusiana na hizi kamisheni za kipolisi. Jeshi la Polisi lina kamisheni nane, katika kamisheni hizo nane mimi nitaziangalia kamisheni mbili tu katika kuzitolea mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamisheni ya kwanza ambayo nitaweza kuizungumzia ni suala la kamisheni ya ushirikishwaji wa jamii pamoja na ile kamisheni iliyokuwepo kwa upande wa Zanzibar. Kwa nini nimesema nitazichagua kamisheni hizi mbili? Kwanza, katika suala la kamisheni ya ushirikishwaji wa jamii, kuna tasnia moja ambayo ni muhimu sana; nimejaribu kuangalia katika hotuba ya kibajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi nikasema kwamba hii tasnia inaachwa na ni tasnia ambayo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tasnia hii ni tasnia ya ulinzi wa kampuni binafsi ambayo nayo tukiangalia kwa upande wa nchi yetu wanatoa msaada mkubwa sana. Sasa, nikawa najaribu kuangalia shughuli muhimu hasa zinazofanywa katika hizi kamisheni zetu. Hasa nikaiangalia hii kamisheni ya ushirikishwaji wa jamii, nikajaribu kuziangalia zile *task* au zile kazi zilizopo pale ambazo kubwa zaidi zinazungumzia masuala ya ulinzi wa kijamii hasa upande wa polisi jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nikawa najiuliza haya makampuni ya ulinzi, katika uwasilishwaji wa bajeti yetu, hasa wanaingia kwa upande gani? Wakati mwingine nasema kwamba ni kampuni ambazo zimekuwa kama yatima. Kwa nini nasema ni kama yatima? Kwa sababu hata katika ule mchango ambao upo kwa upande wa Jeshi la Polisi unaozungumzia suala la mapato ambayo yanaingia katika Jeshi la Polisi sikuona kama kuna mchango wowote, hasa wa kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa upande wa Tanzania tuna karibu kampuni binafsi 2,000 mpaka 3,000. Kampuni hizi kwa kawaida huwa zinasajiliwa na Jeshi la Polisi na wanaposajiliwa maana yake kuna vibali. Kibali unaposajili kampuni mara ya kwanza unatoa shilingi 300,000. Tujiulize kwa upande wa Tanzania nzima, tuna kampuni kama 2,000 mpaka 3,000 ni kiasi gani ambazo zitakuwa zimeingia? Mbali na hivyo, sikuweza hata kuona mchango wao ukizungumzwa katika hii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumza katika hali ya haraka haraka kabla muda wangu haujaisha, ni suala la vibali. Wakati mwingine, *IGP* yupo hapa; tunaona kwamba hizi kampuni ni za kibiashara na kama hizi ni kampuni za kibiashara maana yake zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria za kibiashara (Kampuni ambazo zinaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za kibiashara).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna pande mbili, kuna upande wa Zanzibar na kuna upande wa Bara ambazo zote zinasimamiwa na Jeshi la Polisi. Hata hivyo, kitu ambacho kilikuwa kizito na cha urasimu zaidi ni pale unapoomba kibali cha ulinzi.

Maana yake kufungua kampuni ya ulinzi, kibali kile ni mpaka taarifa zije Dodoma wakati Zanzibar kuna kamisheni ambayo ina mamlaka ya kufanya shughuli hizo pale lakini inaachwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi pengine ningeliomba Jeshi la Polisi kupitia kamisheni ya Zanzibar, kuhusu shughuli za vibali. Kwa vile taratibu za kibiashara kwa upande wa Zanzibar zinakidhi haja, wapewe mamlaka ya kuweza kutoa vibali kupitia ruhusa ya *IGP* wa Tanzania. Kuliko ile kwamba taarifa zao zichukuliwe Zanzibar kuja upande wa Dodoma, zinachukua siyo chini ya mwezi mmoja mpaka miezi mitano. Jambo hilo mimi nitaliomba Jeshi la Polisi waweze kufanya hivyo ili kuondoa urasimu uliokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika hivi vibali, kampuni maana yake itakuwa na kibali mama. Shida inayojitokeza ni kwamba kila unapokwenda kufungua taasisi nyingine katika mkoa unatakiwa uwe na kibali kipya ambapo vile vibali vyote maana yake vinafanya kazi moja. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji, muda wako umeisha, hitimisha.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante mengine nitaandika kwa maandishi kwa sababu mchango ulikuwa mrefu. Naomba kuunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia hali ya uzima hivi sasa. Pia, niwashukuru Wajumbe wenzangu waliokuwamo humu katika Bunge hili Tukufu, ambao sasa hivi wataweza kunipigia makofi mengi humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda sana kumshukuru Waziri wangu Mheshimiwa *Engineer* Masauni pamoja na Naibu

wake. Mheshimiwa *Engineer* Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kweli unaifanyia kazi hii Wizara. Tutasema yeye ni *big up* na wala asitokee mwingine, siku zote namwombea dua ukae hapo hapo ili uiendeleze Wizara hii uifanyie kazi vizuri. Mama hakufanya vibaya, kakurejesha hapo kakuona wewe mpiganaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninalotaka kuzungumza hapa, ulikuwa wewe pamoja na Mheshimiwa Sagini, na yeye namshukuru. Kwa hiyo, sasa hivi Mkoa wa Kusini unang'ara na kesho kutwa utazidi kung'ara, hasa katika sherehe za mwaka kesho kutwa. Watalii wengi watakwenda kule na wataiona Makunduchi ilivyokuwa imegeuka. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea Makunduchi kuna nyumba moja ya makazi ya polisi bado haijaguswa kabisa. Nyumba moja umeijenga lakini bado haijaisha, Mheshimiwa Waziri nakuomba Serikali ichukue jitihada zile nyumba zimalizike. Ndiyo maana nikasema kwamba kule kutang'ara. Kwa hiyo, mimi naishukuru sana Serikali yangu kwa jitihada zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya Mkoa wa Kusini vimekwishakumalizika na kingine amekifungua *DC* juzi na sasa kinafanya kazi huko Makunduchi. Mheshimiwa Waziri, Kituo cha Dunga nacho tayari kimeshafunguliwa, kinafanya kazi lakini kina changamoto. Pale mbele ikinyesha mvua kuna tope, tena pale inakuwa kero kubwa. Pia, kuna eneo pale limalizwe kununuliwa ili liwekwe maeneo ya kuwekea magari. Pia, hawana gari, gari lao mpaka waende Tunguu, wapige simu hadi lije huku kama kumetokea uhalifu basi tayari uhalifu unakuwa umeshaharibika, kwa sababu gari halipo Dunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jitihada za pale Dunga waweke mambo madogo madogo, choo cha nje hakuna hapo Dunga. Watu wanaingia ndani wanaenda kutuchafulia Kituo kama kile kilivyokuwa kinang'ara namna ile, kweli ni vizuri vile? Siyo vizuri. Mheshimiwa Waziri jitahidi na yale madogo madogo uyatengeneze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Jambiani nao hawana gari na makazi pale. Kimekwisha lakini nyumba za makazi hakuna. Kituo cha Paje, kimeshakuwa kuukuu kuu sana, naomba nacho kifanyiwe ukarabati. Ukitegemea ukanda ule ndiyo ukanda wa watalii zaidi: Paje, Jambiani mpaka Michamvi, upande ule watalii wanakwenda wengi sana. Kwa hiyo, namwomba Waziri, Kituo kile kipo nje, kipo wazi, akifanyie kazi Mheshimiwa Waziri ili nacho kipate kung'ara. Kusini ipate kung'ara kuliko inavyong'ara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Sillo na yeye pia aje Kusini atembee aone maendeleo ya Kusini yalivyo. Mheshimiwa Sillo, jamani nawapa *big up* wanafanya kazi vizuri sana. Askari wangu, wanafanya kazi vizuri sana, usalama barabarani waufanyie kazi vizuri sana. Jamani, mnafanya kazi kubwa na mnapiga kazi kwa hiyo mimi nawapa hongera zenu mfanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hizo pongezi, sina la kusema. Nakushukuru Waziri wangu pamoja na Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anapiga kazi kubwa sana katika Wizara zake. Ahsante sana kwa mwanamama yule, Mungu amjaalie heri, ampe baraka, hekima na busara ya kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa atafuata na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu. Kwa dakika jinsi zilivyo chache naomba nikimbie mchaka mchaka. Mheshimiwa Waziri tunashukuru Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, jengo letu la Kituo cha Polisi cha Wilaya linaelekea ukingoni, lakini tunachoomba ni *furniture*. Katika bajeti hii tunahitaji *furniture* ili tuingie kwenye lile jengo na

askari wetu wakae sehemu salama, tulivu, yenye hadhi ili waweze kutekeleza wajibu na majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu fidia. Mheshimiwa Waziri, eneo lile lilichukuliwa wananchi wakiwa hawajalipwa fidia. Jengo limekamilika na tunakaribia kuingia. Wananchi wa Wilaya ya Chemba waliotoa eneo lile kwa ajili ya jengo la Kituo cha Polisi, Wilaya ya Chemba tunaomba, michakato yote ilishakwisha, sasa akija hapa atuambie fidia ile tunalipa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na vituo viwili tulivyonavyo Wilaya ya Chemba. Nimekuwa nikiuliza maswali ya msingi hapa, nimeuliza na maswali ya nyongeza hapa kuhusiana na Kituo cha Kwa Mtoro pamoja na Mrijo. Tuliomba magari, bajeti iliyopita aliniahidi tungepata gari kwenye hivi vituo viwili, lakini mpaka leo hakuna gari. Tuliomba fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa vituo vile mpaka leo ni kimya. Wananchi tumepambana lakini bado ukarabati wa majengo yale mawili, yaani Kituo cha Mrijo pamoja na Kwa Mtoro, bado vina changamoto kubwa. Kwa hiyo tunahitaji fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa vituo vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kituo kingine ambacho kimejengwa kwa nguvu za wananchi, Kituo cha Mondo, kiko pale, na tuna askari yuko pale. Watusaidie pia hiki kituo, waongeze fedha hiyo ili tuweze kukamilisha kile kituo na hatimaye tuweze kutoa huduma stahiki kwa wananchi wetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba kulisemea suala la polisi kata. Tunashukuru Serikali waliliona hilo na wameamua kusogeza huduma ya usalama wa raia na mali zao kwenye maeneo ya wananchi wanakokaa. Hata hivyo watu hawa wa polisi kata hawana vitendeakazi, hawana hata usafiri. Tukio linatokea askari anaambiwa, lakini hana pikipiki wala baiskeli; atembee kwa miguu mpaka aende akafike eneo la tukio mhalifu alishaondoka. Kwa hiyo askari hawa wanashindwa kufanya kazi na wako kule. Mwisho wa siku wananchi wanaona wamekwenda pale si kwa ajili ya kazi kwa sababu wakifika pale

wanapoitwa hawafiki kwa wakati. Naomba na kushauri kuwa polisi kata wetu ambao wako kwenye kata zetu kwenye halmashauri zote nchini wapewe usafiri, kwa maana ya pikipiki ili waweze kutimiza wajibu na majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la posho za safari kwa askari wetu wote na kwa majeshi yote. Posho hizi moja ni kidogo, lakini pili hazitolewi kwa wakati. Kwa mfano tuna Kituo cha Polisi Mrijo na tuna Mahakama ya Mwanzo Mrijo. Mhalifu huyu akikamatwa na akipelekwa Mahakamani, akikutwa na hatia polisi anatakiwa kumchukua huyu mhalifu ampeleke Kondoa Magereza. Anatumia gharama zake, amsafirishe mtuhumiwa ama mshtakiwa yule, ajisafirishe yeye mwenyewe, amlishe na ahakikishe kwamba amemfikisha kwenye mikono salama. Gharama hizi hawa askari wakija kuziomba wanakaa miaka na miaka hawalipwi hizi stahiki zao. Kwa hiyo tunaomba sana Mheshimiwa Waziri, posho za maaskari wetu ziongezwe, lakini pia ziwe zinatolewa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana pia na suala la hela za uhamisho. Mimi nina askari kadhaa waliokuwa Wilaya ya Chemba, wamehamishwa wamepelekwa kwenye maeneo mbalimbali, lakini hadi leo hawajalipwa stahiki zao za uhamisho. Tunaomba walipwe hela zao za uhamisho. Kama Serikali haiwezi kulipa fedha za uhamisho, hatuna sababu ya kuwahamisha watu hawa kwa sababu hatuwatendei haki. Wewe umeamua kuniondoa, nipe changu, nisepe tumalizane, lakini watu hawa hawataki kuwalipa, ni kwa nini? Wana miaka minne hadi miaka mitano hawajawalipwa hela zao za uhamisho. Kwa hiyo naomba sana na Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie kwamba, ni lini watalipa fedha za uhamisho za askari wetu ili na wao waweze kuona kwamba wanapotoa huduma wanathaminiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *OC*. Halikadhalika *OC* hizi zinatolewa *flat rate*. Haijalishi eneo hili ni kubwa kiasi gani na kwamba anahudumiaje, ni hiyo hiyo moja. Kwa hiyo suala hili nalo pia liangaliwe, hizi *OC* zinapotolewa, waangalie na maeneo. Leo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ina kata 26, vijiji 114, vitongoji 432, haiwezekani kwenye *OC* huyu ukampa shilingi

milioni na wa Dodoma Mjini ukampa shilingi milioni, sijui na wapi ukampa shilingi milioni, haiwezekani! Watu hawa wana mahitaji makubwa na yanatofautiana. Kwa hiyo tuangalie tunapokwenda kutoa suala zima la *OC*, tuangalie, tutoke kwenye *flat rate* twende sasa tukaangalie na ukubwa wa maeneo yao husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la magereza. Wilaya ya Chemba hatuna gereza. Kama nilivyosema, watuhumiwa wakipatwa na hatia tunatoa kule tunawapeleka Kondoa. Hizo gharama ni kubwa, tunahitaji gereza katika Wilaya ya Chemba ili na sisi watu wetu wanapokutwa na makosa mbalimbali, basi waweze kuhudumiwa kwenye eneo lao husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimwombe Mheshimiwa Waziri, tuna magari mawili pale, la *OCD* pamoja na *OC-CID*. Yale magari ni hoi bin taaban. Juzi wamesafiri, wameishia njiani wameshindwa kufika kwenye eneo la tukio, tairi zimepasuka. Hivi hata tairi ya shilingi 250,000, Wizara hawawezi kuwasaidia hawa watu wakapata tairi? Tunawaomba tafadhali tuwatendee haki. Watu hawa wanafanya kazi kubwa na kwenye mazingira magumu, wanalihudumia Taifa lao. Kwa hiyo zile stahiki zao zinazohitajika na vitendea kazi vyao tunaomba wapatiwe ili waweze kutimiza wajibu na majukumu yao wakiwa na roho kunjufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunti. Namwita sasa Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza moja kwa moja kwa kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa upendo wake mkubwa aliouonesha kwa vijana wa Kitanzania. Baada tu ya Waziri wetu Mheshimiwa Masauni kumshauri kuwa vijana wanaomba ajira, lakini vigezo vya

kwamba mpaka wawe na cheti cha JKT ndicho kikwazo, Mheshimiwa Rais kwa sababu ni msikivu, ni mama na ni mlezi amekubali na sasa vijana wanaomba kazi wakiwa wako huru kabisa. Tunampongeza kwa kweli, tunamshukuu sana Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu Masauni, pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kutoa pesa nyingi kwa Mkoa wetu wa Mara kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya ujenzi wa nyumba za askari wetu. Mkoani kwetu Mara, ukija pale Musoma Mjini panang'ara, yaani ukipaangalia ni maghorofa ya polisi ambayo yameng'ara. Kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. Wanasema kwamba mwenye nacho huongezewa, basi namwomba Mheshimiwa Waziri wetu, hata kwa Askari Magereza atuongezee pia pale maghorofa kusudi Mkoani kwetu Mara paendelee kung'ara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba sasa gereza lijengwe pale Wilaya ya Butiama kwa sababu ni wilaya ya mfano. Taifa zima linajua, ulimwengu mzima unajua kwamba Butiama ndiko alikotokea muasisi wa Taifa hili la Tanzania, Mkombozi wa Taifa la Tanzania na kwa hiyo panapaswa kuwa ni wilaya ya mfano, kwa hiyo ni wilaya ambayo miundombinu yake mbalimbali inapaswa iangaliwe. Kwa kweli hili nimwombe Mheshimiwa Waziri Masauni aliangalie kwa jicho la pili, naamini kabisa mama yetu kipenzi, mama yangu mimi Chifu Hangaya anasikia, atakwenda kufanya mambo katika Wilaya ya Butiama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu kuwasemea hawa ndugu zetu wa Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto kwa sababu inajulikana wazi kabisa kwamba mishahara yao kwa kweli ni midogo ukilinganisha na hali halisi ya maisha ya sasa ya Tanzania. Sasa ukiwaongezea tena na kikokotoo mambo yanakuwa siyo shwari. Unaweza ukakuta hata ndoa zao nyingi tunasikia zinavunjika na askari wengine wanajinyonga ni kwa sababu tu ya hali ngumu ya maisha. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu anapomshauri Mama, Mama huwa anasikia, basi aende

akamshauri tena kuhusiana na hili kwamba aliangalie suala la kikokotoo kwa majeshi haya. Tunajua mama analishughulikia na tunajua atafanya jambo. Kuhusiana na masuala ya ongezeko la mishahara na mambo mengine, tunajua kabisa mama ni mlezi, kuna jambo anafanya. Naamini kabisa siku moja mambo yatakuwa vizuri, kwa hiyo wasiwe na wasiwasi kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kipekee kabisa, kwamba Mkoa wa Mara ni mkoa uliokaa kimkakati, lakini ni mkoa wenye matukio mengi kama inavyojulikana, kwa hiyo ni mkoa ambao tunapaswa kuwa na magari mengi ya kipolisi. Kwa hiyo magari haya ya polisi yatakapokuja basi mimi naomba Mkoa wa Mara uwe ni kati ya mikoa ya mfano na uwe ni mkoa wa upendeleo ambao wataanza kuyapeleka magari haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwenye suala la risiti. nimevuta kidogo nimeshindwa kuliongelea vizuri, suala la risiti, risiti zinakatwa, kwa mfano mimi nikiwa nimepoteza kadi yangu ya benki, nikiwa nimepoteza kadi yangu labda ya gari, kadi mbili, nikienda Kituo cha Polisi, nalipia shilingi 3,000 ya kadi ya benki, nalipia shilingi 3,000 ya kadi na *NIDA* lakini napewa risiti ya shilingi 1,500 peke yake. Sasa swali langu, zile pesa nyingine zinakwenda wapi? Basi tuangalie kwa wale wenzetu ambao kidogo hawana uaminifu, waangalie hizi pesa ziingie Serikalini kwa sababu tunajiuliza. Labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa pia atuelezee kwamba hizo pesa nyingine huwa zinakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee zaidi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri sana anayoifanya, lakini nampongeza sana *RPC* wetu wa Mkoa wa Mara kwa kazi nzuri anazozifanya, Mkoa wa Mara umetulia tulii. Nampongeza sana *IGP*, Tanzania sasa imetulia, ina utulivu wa kutosha na naamini kabisa yeye anafanya kimyakimya, lakini mambo yanakwenda. Nawapongeza sana Jeshi la Polisi na Majeshi mengine kwa ujumla, Mwenyezi Mungu awabariki sana kwa kuleta utulivu Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa…

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Namwita sasa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niwe mchangiaji jioni ya leo. Naomba kumtanguliza Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais wetu ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu, naomba tu nipige saluti kwake, kwamba amefanya kazi nzuri sana katika kuiongoza nchi hii na kuhakikisha kwamba usalama unapatikana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu Masauni kwa kazi nzuri, lakini pia nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Sillo kwa kuteuliwa kuingia katika Wizara hii, tunajua wameitendea haki. Pia nawapongeza wakuu wote wa vyombo vya usalama bila kumsahau *Commissioner General* dada yetu Dkt. Anna Makakala ambaye anatuwakilisha sisi wanawake hapo juu kabisa katika jeshi, anatenda haki. Sasa hivi pasipoti zinapatikana kwa haraka sana, hongera sana, lakini pia hatugongi tena mihuri *airport,* kwa hiyo ni *big up* kabisa katika kazi yake. Pia nampongeza *RPC* wetu wa Mkoa wa Iringa kwa kazi nzuri na askari wote wa Mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi katika Mkoa wa Iringa. Kwanza kuna uhaba mkubwa sana wa askari katika vituo vya polisi, lakini pia kuna uhaba wa magari katika mkoa wetu, pia hawana hata fedha kwa ajili ya mafuta na kwa hiyo wanapata shida sana. Tuna magari ambayo

hayatengenezeki kwa sababu hawana *OC* za kutengeneza magari, kwa hiyo magari yanachukua muda mchache sana kuharibika kwa sababu hayafanyiwi ukarabati mkubwa. Tunaomba Mkoa wa Iringa uletewe pesa za kutosha. Pia makazi ya askari, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mjini, kwa kweli ni changamoto kubwa sana. Tunaomba Mkoa wa Iringa tuangaliwe, nyumba nyingi zijengwe kwa sababu askari wengi wanaishi uraiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja sasa katika Jeshi la Magereza, pia waangaliwe posho zao na makazi yao. Naomba sasa Serikali iangalie uwezekano wa kuhamisha Gereza la Kihesa Mgagao. Hili gereza libadilishiwe matumizi kwa sababu Tanzania tuna dhana kubwa sana ya kulinda historia za wenzetu. Pale kulikuwa ni kambi ya wakimbizi, kuna Waheshimiwa Marais ambao walitetea nchi zao, kwa mfano Nelson Mandela na Walter Sisulu walikaa pale. Sasa hivi tunaomba lile gereza liondoke ili tuweke historia. Kuna makaburi pale. Tayari Waheshimiwa Wabunge waliopita wote walikuwa wameomba kwamba lile gereza lihamishwe na wakakubaliana kwamba litafutwe eneo ili wale mahabusu, kwa sababu pale kuna mahabusu tu, waondolewe ili pale tuendelee kutengeneza historia za wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi zinataka kuja kutembelea katika kile kituo ambacho waliishi, wanashindwa kuja kwa sababu kuna gereza. Kwa hiyo naomba na ikiwezekana Mheshimiwa Waziri aje Kihesa Mgagao aje aone ili tufanye utaratibu wa kuhamisha lile gereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna tatizo hilohilo la magereza. Kuna mwingiliano mkubwa sana katika gereza la mkoa, pia kuna mwingiliano katika hospitali ya mkoa, kuna changamoto kubwa sana. Sasa hivi, hakuna nyumba za madaktari lakini kunatakiwa majengo mengi yawepo katika hospitali yetu ya mkoa. Kutokana na ule mwingiliano unaweza ukakuta wafungwa wanatolewa kwenye gereza upande mwingine na *ambulance* inaingia hospitali. Kwa hiyo kunakuwa kuna shida sana, kuna wagonjwa wanapata matatizo makubwa. Iringa kuna eneo kubwa kule Mlolo, naomba ikiwezekana Serikali itoe pesa. Tayari tulishaanza

huo mchakato, gereza lihamie Mlolo, kuna eneo kubwa kule ili kupisha uendelezaji wa Hospitali ya Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kupongeza sana Serikali kwa ujenzi wa Jengo la Polisi Kilolo. Naomba sasa waongezee zahanati za polisi na magereza ambazo zinasaidia sana huduma kwa wananchi. Basi nao wapewe dawa na vifaa vya matibabu ili waendelee kuwasaidia raia ambao wapo karibu na kambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi la Zimamoto, nawapongeza sana. Napongeza kwamba wamepatiwa magari ya zimamoto. Naomba Mkoa wa Iringa uangaliwe katika hayo magari. Tunayo mazao ya misitu katika Wilaya za Kilolo na Mufindi ambako moto unatokea kila wakati. Wananchi na hata Serikali wanapata hasara kwa sababu ya moto wa kila wakati. Kwa hiyo naomba kila wilaya kuwepo na gari la zimamoto ili inapotokea moto wowote iweze kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ajali nyingi sana katika Mito ya Ruaha na Lukosi, watoto wamekuwa wakipata tatizo kubwa. Hakuna vyombo vya uokozi katika Jeshi la Zimamoto. Juzi tu pale Mahenge kuna mtoto wa miaka 15 amezama kwenye maji na wameshindwa kumuokoa kwa sababu hakuna vifaa. Kwa hiyo naomba hili liangaliwe, tuletewe vifaa vya uokozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuendelea kulipongeza Jeshi la Polisi, lakini naomba sasa hivi tujengewe vituo vingi vya polisi kwani vimechakaa sana. Tunaomba tuletewe gari pia katika Kituo cha Polisi ya Ruaha Mbuyuni, kimekuwa kikifanya kazi kubwa sana lakini hakuna gari la polisi. Kuna ajali nyingi zinatokea pale katika Mlima Kitonga. Pia imekuwa ikisaidia mpaka Jimbo la Mikumi pamoja na Jimbo la Kibakwe. Kwa hiyo naomba sana gari la polisi katika Kituo cha Ruaha Mbuyuni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Namwita sasa Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Juma Othman Hija ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa dakika sita hizi ili kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani. Naanza kwa kushukuru kama wenzangu walivyoshukuru, nasema tunashukuru mara zote ili tuombe tena. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maboresho yake makubwa katika Wizara ya Mambo ya Ndani na hasa katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona na nilisoma sehemu kwamba Jeshi la Polisi, lile shirika la uzalishaji mali lilikuwa linafutwa, lakini Mheshimiwa Rais kwa busara zake, ameacha kulifuta ili liboreshwe, liweze kuendeleza askari wetu. Kwa hiyo nashukuru sana kwa maboresho haya ya *modernization* ambayo Mheshimiwa Rais anayafanya mpaka huko kwenye mambo ya TEHAMA na kama nitapata muda, nitaisema huko baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa dhati kwa kweli. Nilimwomba hapa aje Jimboni kwangu Kilombero, amefika, tukatembea na tukafanya ziara hadi usiku. Mheshimiwa Waziri Masauni akafika Gereza la Idete usiku, akasema lazima nifike niangalie mazingira ili niweze kuyaona na kuyaelewa. Mheshimiwa Waziri pia akafika Kituo cha Polisi Kidatu, akafika Mwaya na akafika Ifakara Mjini. Nataka kukiri hapa leo kwamba mambo yangu yote niliyomwomba, nimeyaona leo yakifanyiwa kazi na chini ya *OCD* wetu Nkuba, kwa kweli yanasimamiwa vizuri sana. Mheshimiwa Waziri ametusaidia na Serikali imetusaidia tumepata shilingi 802,000,000 za ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilombero. Ni wilaya kongwe sana, lakini ilikuwa haina kituo, tumepata. Nimemwambia Katibu Mkuu

wa Wizara hapa atusaidie ili michakato ikamilike na hati ile irudi kule ili *OCD* aweze kujenga kituo kile kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuhusiana na maombi yangu. Tulitembelea Kituo cha Polisi cha Tarafa ya Mang'ula ambacho kiko Kata ya Mwaya, kwa kweli ni Kituo cha Polisi cha Mbao. Mheshimiwa Waziri aliingia pale ndani akasaini vitabu. Kwa hiyo naendelea kumsisitiza kwamba Kituo cha Polisi cha Kidatu na cha Mwaya ni muhimu sana tukavijenga upya. Mimi kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani, tumeshapata tayari maeneo ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, nataka kwenda kama na-*mention* hivi. Sisi tunamwomba Mheshimiwa Waziri gari la zimamoto kwa sababu Ifakara ipo katikati ya Jimbo la Mlimba, Jimbo la Ulanga na Jimbo la Malinyi. Akitupatia gari la zimamoto pale Ifakara, atakuwa amelisaidia Jimbo la Mlimba, ameisaidia Ulanga na ameisaidia Malinyi na alifika kwenye ziara sehemu zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba atu-*note* katika *list* ya magari yake ya zimamoto. Tunaomba atusaidie kuboresha Ofisi yetu ya *NIDA* pale Wilaya ya Kilombero ambayo ipo Ifakara, tunaomba pikipiki kwa watu wetu na askari wetu wazuri wanaofanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie changamoto ya Wizara hii ni kubwa tunajua, mimi nikiangalia nyumba za askari wangu naona changamoto ni kubwa. Hapa Dodoma tu Makao Makuu ya Nchi ukienda hapo Polisi ukitazama mabanda ambayo askari anakaa huwezi kuamini. Hii yote ni mizigo ambayo sisi tunambebesha Waziri, kila mfuko wake utakapotuna ajaribu kukumbuka askari wetu ili wafanye vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ifakara tulikuwa tunasemwa kwenye mambo ya mitandao tangu afande *IGP* atuletee afande Nkuba na *RPC* – Morogoro kasi ile ya vijana waliokuwa wanasemwa semwa wizi wa mitandao imekwisha. Vijana sasa hivi wanajishugulisha na bodaboda, wanajishughulisha na bajaji na uendeshaji wa kirikuu. Mheshimiwa Waziri, ikimpendeza hata

mwakani tunaweza tukakubaliana vijana hawa wasamehewe mambo ya faini faini. Maana yake nilikaa nao Ifakara pale kwa Churu, wengi wanalalamika faini zimekuwa nyingi na askari akamati bila makosa, makosa yapo lakini vijana wetu hawa ni muhimu kuwaangalia namna gani tunaweza tukawasaidia ili waweze kufanya kazi yao ya kuachana na mambo mengine na tabia mbaya kujiwezesha katika kutafuta kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kwenda moja kwa moja katika *Modernization* ya Jeshi la Polisi ambalo Mheshimiwa Rais analisimamia na wewe unasimamia, mfumo huu wa kuboresha kuunganisha Mahakama, Jeshi la Polisi na *DPP* ni mfumo muhimu sana. Katika dunia ya wenzetu sasa hivi ukipata tatizo unaenda Polisi, unazungumza Polisi unarekodiwa *video* bila mtu kuandika. *DPP* kule anaona, Mahakama inaona inarahisisha hata katika mambo ya kutoa hukumu, huu mfumo ni mzuri na uendelee kuboreshwa. Mshirikiane na mkongo wa Taifa ambao upo chini ya Wizara ya Habari na Mawasiliano ambao mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, tuliomba huu mkongo urudishwe kwa Serikali ili iweze kutoa huduma hiyo ya kiteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani sasa hivi unaenda Polisi unatumia saa zima askari anaandika kwa mkono kwa kalamu kwenye karatasi hii ni dunia ya wapi? Hii dunia imeshapitwa na wakati, tuachane nayo. Nimeona katika ukurasa wa 27 kuhusu kuboresha shirika hili alilosema Waziri la uzalishaji mali wa Jeshi la Polisi, nasisitiza hata huu Mradi wa Tehama wapewe hili shirika ili waweze kuuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameanza katika mikoa michache Mradi wa Miji Salama ya Kiteknolojia na Kufunga Kamera, lakini katika miji waliyoanza Morogoro wameiacha, sasa Morogoro ndiyo katikati ya kiungo hapa huwezi kwenda mikoa 17 kwa barabara kama hujapita Morogoro. Kwa hiyo, nasisitiza na Morogoro waiweke, nasisitiza Mradi wa *High Way Speed, Road Patrol Camera* uboreshwem dunia tunayoenda sasa hivi siyo dunia ya kujaza Polisi barabarani. Wizara ifunge kamera za kisasa, wapunguze askari wetu wakaendelee kusaidia wananchi huko walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza sana kwamba Mheshimiwa Waziri nikiunga mkono hoja yake, mzigo huu ni mkubwa, mimi nataka nyumba za Polisi, kila Mbunge anataka nyumba za Polisi. Dodoma hapa yenyewe nimesema kuna nyumba, ni aibu kabisa, napita pale nauliza haya mabanda ya nani wanasema ya Polisi, kweli ni shida sana. Tunambebesha Mheshimiwa Waziri, mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru sana, ikimpendeza Mheshimiwa Waziri afanye tena ziara aje katika Jimbo la Kilombero. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Juma Othman Hija ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa nzuri anayoifanya pamoja na timu yake katika kuhakikisha kwamba wanaendelea kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta hii ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nchi yetu sasa imendelea kuwa na amani utulivu wa kutosha na hatimaye hata waganga njaa mitaani wameendelea kufanya mikutano kwa amani kubwa. Japokuwa wameendelea kumtukana Mheshimiwa Rais wetu, lakini sisi wenye akili timamu tuko vizuri kuhakikisha kwamba tunaendelea kumlinda Mheshimiwa Rais wetu na kuhakikisha kwamba mwaka 2025 mpaka 2030 tutaendelea kuwa naye. Niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais, amekuwa mtulivu sana hatujawahi kusikia hata siku moja akitoa majibu kwa watu ambao hawajitambui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Magereza – Lindi, kwa sababu muda hautoshi, lakini niseme tu kwamba kwanza jambo la kwanza nimwombe Mheshimiwa Waziri ama Naibu Waziri kuja Lindi kufanya ziara maalum ya kutembelea majengo ya Magereza pamoja na nyumba za watumishi wa Magereza na nyumba za watumishi wa Polisi. Maana yake

yawezekana mimi nikisema hapa Mheshimiwa Waziri hatonielewa, kwa hiyo nimwombe afanye ziara rasmi ya kuja Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, bajeti ya 2023/2024 walitenga fedha milioni 800 kujenga majengo ya utawala ya ofisi za Magereza katika mikoa mitano ikiwepo Lindi. Sasa tuko robo ya mwisho wa mwaka, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba fedha hizi zinakuja ili tuboreshe kujenga ofisi ya Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini magereza ya Lindi ni magereza kuu. Magereza ambayo wale wafungwa waliohukumiwa kunyongwa maana yake wanakaa pale kusubiria. Wafungwa walioshindikana katika maeneo mengine wanaletwa pale, wafungwa wa muda mrefu, wanaletwa pale Lindi lakini hali ya magereza ya Lindi ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabati yametoboka, jua likiwaka wanalo kwenye mabweni, mvua zikinyesha wanaendelea kutaabika wafungwa hawa. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kuhakikisha tunapata fedha kwenda kukarabati ili kuweka hali salama. Pia Magereza ile haina uzio maana yake mabwenini mtu akichomoka akapanda juu ya ukuta anaondoka zake. Ndiyo magereza ya kwanza ya aina hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aje Lindi athibitishe hayo na aone namna ya kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wake za Polisi pamoja na Polisi wanawake wameniomba kwamba, tunaomba tupate hali ya utulivu, amani kuhakikisha kwamba tunapata nyumba safi na salama ili waweze kuishi vizuri na familia zao. Najua kwamba kuna changamoto nchi nzima Tanzania, kila kona nyumba za Polisi ni mgogoro, nyumba zilizokuwepo ni za muda mrefu zimepitwa na wakati. Mheshimiwa Masauni ana kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba anatafuta fedha ili kuboresha nyumba za maaskari wetu waweze kukaa salama na wapate utulivu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wametupatia fedha zaidi ya bilioni moja kujenga Kituo cha Polisi Daraja A na ni kituo cha mfano Kanda ya Kusini ambacho

kimekamilika. Changamoto iliyopo *furniture* za kisasa hatuna na jengo limeshakamilika, ni Mheshimiwa Masauni kujiandaa kuja kufanya uzinduzi kuhakikisha jengo lile akishatupatia *furniture* linaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa nyingine, tumejenga majengo ya Mahakama ya kisasa ya watoto ya wilaya na mkoa, tumejenga jengo la uhamiaji, tuna ofisi za TAKUKURU nzuri za kisasa, lakini changamoto kubwa ni vitendea kazi, hawana magari wale wenzetu wa TAKUKURU, wengi wana magari yao binafsi, kwa hiyo, wanatumia hayo, lakini Maafisa Uhamiaji ni changamoto hawana magari, Zimamoto changamoto hawana magari, hawana majengo ya ofisi wala vifaa vya uokoaji. Sisi tuliokuwa kanda ya pwani ya bahari ni changamoto, tunapata na kunatokea matukio mengi ya ajali. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba maeneo hayo anayatazama kwa jicho la huruma kuhakikisha vifaa hivi vinapatikana ili maafisa wetu wajisikie amani kuwa na vyombo vya usafiri ili waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afisa Uhamiaji anapotoka kwenda wilayani kuangalia maendeleo ya kazi zake ni mbaya sana kuona anakwenda stendi kupanda basi ili asafiri, ni changamoto. Kwa hiyo, hebu tuwape heshima zao maafisa hawa wapate magari ili waweze kusimamia kazi zao vizuri ili wajisikie amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, najua kwamba wameendelea kufanya kazi nzuri, bajeti yao ina mambo mengi, mambo ya maendeleo, mambo makubwa ya mapinduzi katika nchi yetu. Niendelee kuwapongeza sana maaskari wetu wa Jeshi la Ulinzi na Usalama, wanaendelea kutufanyia kazi nzuri, ni wazalendo wa kweli japokuwa mazingira yao ya kazi siyo salama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Juma Othman Hija, atafuatiwa na Muharami Shabani Mkenge na Mheshimiwa Minza Simon Mjika ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JUMA OTHMAN. HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Niungane na wenzangu jioni hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwepo hapa leo tukiwa hatujambo, Mwenyezi Mungu *In Shaa Allah* aendelee kutupa afya njema kutekeleza wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nami sina budi kuungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia kwa namna anavyofanya kazi za kutuletea maendeleo katika nchi yetu. Mheshimiwa Rais amekaa muda mfupi lakini mambo ambayo ameyafanya ni mengi sana, sote Watanzania hatuna budi kuendelea kumwombea kheri Mwenyezi Mungu ampe wepesi wa kutekeleza mambo yake haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa namna walivyowasilisha, walivyotayarisha hotuba hii na hatimaye kuiwasilisha kwa ufasaha zaidi. Hotuba ya mara hii ni hotuba ya viwango kabisa. Hotuba yao ya mara hii ina vipaumbele sita, bajeti yao ya mara hii ina vipaumbele sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika vipaumbele hivyo kipaumbele namba mbili kinasema kwamba nanukuu kukamilisha, kuendeleza ujenzi vituo na makazi ya askari. Kipaumbele hiki ndicho ambacho mimi kwa leo nitakuwa nachangia katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kushukuru sana Serikali yetu hii ya muungano kwa kuendeleza kituo chetu cha Kisiwa cha Tumbatu. Kituo kimefika hatua nzuri kama 60%, sasa hivi kimeshakamilika lakini kituo hiki kama Serikali haitojenga makazi basi ubora wa kituo kile hautaonekana, ni lazima Serikali ijenge makazi kwa wananchi wale. Bila ya makazi kutokana na jiografia ya pale, basi kile kituo kitakuwa kipo tu vilevile, hakina kazi yoyote. Kwa hivyo tunaomba kwamba Serikali ichukue juhudi ya makusudi kujenga makazi katika Kituo cha Polisi cha Tumbatu kwa ajili ya mustakabali wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika katika Jimbo langu kuna vituo viwili; kimoja hicho cha Tumbatu ambacho ni kipya

lakini pia kuna Kituo cha Mkokotoni ambacho ni cha zamani sana, nacho vilevile hali ya makazi ya pale ni mbovu sana kiasi ambacho inasikitisha sana. Kwa hivyo, kwa dhana ile ile naomba kituo kile nacho kifikiriwe makazi ya askari wetu pale Mkokotoni, wajengewe maslahi mapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tumbatu sisi tuna wananchi wa kule tumetenga eneo makusudi la kuwapa askari kama hamna eneo. Kwa sisi tumetenga eneo makusudi kwa ajili ya makazi ya maaskari pale kwa hivyo, hamna haja ya kuja Tumbatu wakanunua eneo, sisi kule maeneo hatuuzi, wao waje tuwakatie wajenge makazi ya maaskari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *forum* zetu za kuelezea maendeleo ya Serikali hii ni sehemu ya pili. Moja hapa Bungeni lakini nyingine ni katika maeneo yetu ya kazi, unapotokezea mradi wa kazi katika eneo lako kwa mfano kama hiki Kituo cha Polisi. Sehemu ile ni sehemu muhimu sana kwa Mbunge kuwepo pale kuelezea na kuisifu Serikali yetu, haipendezi hata kidogo kuona kwamba hii Wizara ya Mambo ya Ndani inakwenda katika sehemu ya mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kama kwangu mie wamekwenda wameweka jiwe la msingi katika Kituo cha Polisi cha Tumbatu, uongozi hauna habari kwa maana ya mimi kama Mbunge sina habari pale. Kitendo kile hakina afya hata kidogo kwa maslahi yetu na maslahi ya Taifa, ni lazima tushirikishwe, tunaambiwa tu kila siku kwamba sisi Wabunge tufuatilie miradi, tusimamie, tuelekeze na hamna wenyeji. Kitendo kile cha kutia jiwe la msingi katika Kituo cha Tumbatu cha Polisi bila kushirikishwa Mbunge na wengine na mambo mengine hakina afya kwa Taifa hili. Kwa hivyo, tunaomba, Mheshimiwa Waziri ni miongoni mwa Mawaziri wazuri, anachapa kazi sana sana. Sasa asiruhusu mambo haya madogo madogo yakamtia doa, jaribu kuyashikilia sana haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi, kwa haya yangu machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge atafuatiwa na Mheshimiwa Minza Simon Mjika, na Mheshimiwa Naibu Waziri, Daniel Baran Sillo ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii. Kwanza kabisa, kwa haraka haraka maana yake muda hautoshi, ningependa kumpongeza Amir Jeshi wetu Mkuu Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya na kuyaongoza Majeshi yetu. Pili ningependa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Makamanda wote ambao wanaongoza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika suala zima la Jeshi letu la Zimamoto. Kweli kabisa Jeshi hili kwa sasa Serikali iko haja na umuhimu mkubwa wa kuliangalia kwa kiwango cha juu sana, kwa sababu sasa hivi dunia inakumbwa na mabadiliko ya tabianchi. Hali inakuwa mbaya ya mafuriko na majanga mengineyo, Jeshi hili sasa umefika wakati linatakiwa lipewe nguvu za ziada ili liweze kumudu kazi au kasi ya uokoaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wizara wanajitahidi. Juzi tu Jeshi hili limepokea magari 12 mapya kwa ajili ya uokoaji, magari haya ni ya kisasa kabisa ambayo yanahitajika yaende sehemu mbalimbali katika nchi yetu kwenda kufanya kazi ya uokoaji pamoja na kuzima moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe angalizo moja kwa wenzetu wa Jeshi la Zimamoto, magari haya ni ya kisasa zaidi na yameletwa ili yaje kufanya kazi kwa ajili ya uokoaji, kwa hiyo basi wahakikishe kwamba wanayatazama na kuyatunza magari haya. Magari haya kwa sasa yako chini ya uangalizi wa *supply,* basi wakae na wao kujifunza waone ni jinsi gani ambavyo wanaweza kuyatumia magari yao. Kujifunza mitambo yake inavyofanya kazi ili kesho na kesho kutwa tusiyakute magari haya yako ubaoni yamechakaa kwa muda ambao haukukusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiachilia mbali magari haya ya Zimamoto bado kuna changamoto kubwa katika Jeshi letu la Polisi. Jeshi la Polisi lina changamoto ya usafiri, magari mengi ya Jeshi la Polisi yamechakaa hayafanyi kazi, mengi yamekuwa *stranded,* yamekaa hayana mpango wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali itenge bajeti kwa ajili ya kuyafufua haya magari, tusitegemee wafadhili kutufufulia haya magari au kututengenezea, kwa sababu ni hatari kabisa kabisa Jeshi la Polisi kuwa linasaidiwa kila mara. Kama alivyozungumza mzungumzaji aliyepita jirani yangu hapa, Jeshi la Polisi linatakiwa sasa hivi lielekee katika kujitegemea, Serikali ilipe nguvu Jeshi hili liweze kuhudumia vifaa vyake, kwa sababu leo anapotokea mtu mtaani analisaidia Jeshi la Polisi kwa chochote kile, kesho mtu huyo akifanya kosa Jeshi hili la Polisi litashindwa kumdhibiti kwa sababu limekuwa ni mfadhili wao. Kwa hiyo, niwaombe ndugu zangu, Serikali pamoja na Wizara wachukulie umuhimu sana kutoa huduma katika majeshi yetu haya na hususan Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari yatakapochakaa watenge bajeti na fungu kabisa la kufanya *service* haya magari. Tunajua Serikali inajitahidi na inapambana kuhakikisha magari mapya yanapatikana na kweli tunaona juhudi za Serikali, tunaona juhudi za Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya. Jeshi la Polisi sasa hivi linapata magari ya kisasa na mapya, lakini wachukulie umuhimu huu wa kufanya *service* magari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Makamanda wetu wa Polisi wa Mikoa, wanafanya kazi kubwa sana hususan kama kamanda wangu wa Polisi wa Mkoa wa Pwani. Nampongeza kwa kazi kubwa anayoifanya Mkoa wa Pwani sasa hivi umetulia, matukio ya uhalifu yamepungua kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza *OCD* wangu wa Bagamoyo pamoja na Chalinze kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika Wilaya yetu ya Bagamoyo, kwa kweli hali ya usalama imekuwa nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda niwapongeze wenzetu wa Jeshi la Polisi kwa kweli, hawa makamanda au Polisi Kata wanatusaidia kwa kiasi kikubwa sana katika nchi yetu. Leo hii katika kata nyingi sana uwepo wa Polisi Kata unasababisha kuwepo kwa amani kwa kiasi kikubwa sana. Wanajitahidi sana tunatakiwa tuwapongeze, tuwape ushirikiano na ikiwezekana tuwaongezee vile vitu ambavyo wanavihitaji ili kufanya kazi zao kwa weledi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la pale Jimboni kwangu Bagamoyo. Bagamoyo tuna changamoto ya gari, hakuna gari ambalo ni zima, ni gari la siku nyingi na limekuwa bovu. Sambamba na hilo, tunahitaji ikiwezekana Wizara ifikirie kutupatia boti la polisi, ili liweze kuangalia maeneo ya bahari kwa sababu, maeneo ya Bagamoyo ni hatarishi ambayo, wakimbizi au wahamiaji wengi haramu wanapata uchochoro wa kupita na pia, magendo mengi yanapitishwa. Askari hawa wa Bagamoyo wakipatiwa boti, watakuwa na uwezo wa kufanya kazi ya kupita baharini katika maeneo yote, ili kuhakikisha wahamiaji haramu pamoja na magendo hayafanyiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri limejionesha hapa kwamba, Serikali inakusudia kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto. Suala la ukaguzi wa vyombo vya moto ni muhimu sana, ajali nyingi zinatokea katika nchi yetu kutokana na magari kuwa mabovu. Kwa hiyo, hili suala ambalo Wizara inakusudia kulifanya kwa kupitia Jeshi la Polisi ni suala la msingi na ninawapongeza sana katika jambo hili ambalo mnakusudia kulifanya. Kwa kweli, ukipita barabarani huko magari mengi ni mabovu kwa hiyo, Serikali ina kila sababu kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa magari ili tuweze kunusuru wananchi wetu katika suala zima la usalama barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni ambao wapo ndani ya Bunge letu waliotutembelea kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* tuwaone. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata. Namwita sasa Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mheshimiwa Naibu Waziri, ajiandae.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake za pekee, kutuwezesha jioni hii njema kuingia katika Bunge hili. Pia, namshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika nchi yake. Mungu aendelee kumbariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nazidi kuvipongeza hivi vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri ambazo wanafanya. Ningewezakutaja majina ya mtu mmoja mmoja, lakini kwa sasa siwezi kulingana na muda. Nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Masauni, kwa kazi nzuri ambazo anafanya pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Sillo, ahsanteni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza moja kwa moja kwa upande wa Jeshi la Polisi, linafanya kazi nzuri sana nchini Tanzania. Linafanya ulinzi wa mipaka yetu na raia, usalama wa wananchi na kila kitu, wanafanya kazi nzuri, lakini kwa kweli, kuna kitu kimoja ambacho tunawafanyia, naona wakati mwingine hata raha ya kazi wanaikosa, hawana makazi mazuri. Kwa kweli, wana nyumba za ajabu, nyumba ambazo ni za zamani, zimepitwa na wakati, lakini ndizo wanazokaa. Inabidi Waziri Masauni, kaka yangu, naelewa yeye ni msikivu, tunaomba awajengee nyumba askari wetu ili waweze kuwa na utulivu wa akili kuanzia nyumbani mpaka kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia katika Mkoa wangu wa Simiyu. Nashukuru sana kwamba, viongozi wetu wanafanya kazi nzuri, lakini kuna wilaya moja kongwe, Wilaya ya Maswa ni ya siku nyingi sana kwa kweli, ina nyumba za ajabu sana, zimechoka na

ni fupi kama vibanda, tunaomba waweze kujengewa nyumba ambazo ni nzuri. Kwa kweli, tunawafanya wanakaa katika mazingira ambayo siyo rafiki. Mtu anapofanya kazi, basi utulivu uanzie pale anapoishi, anapolala na anapotoka kwenda kazini anakuwa vizuri. Tunaomba maaskari wetu wawajengee nyumba nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari nyingine ni ya kikokotoo. Kikokotoo kwa upande wa Jeshi la Polisi tunaomba wakiondoe, lakini siyo kwa Polisi tu, bali pia, kwa wafanyakazi wengine wote, hii ni kero. Unashangaa mtu kafanya kazi Serikalini muda wa miaka 35 au 40, mwisho wa siku anakuja kupata shilingi milioni 28 kwa kweli, hiyo siyo sawa. Mtu apewe haki yake yote apange utaratibu wa mambo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, viongozi wetu hawa tunaamini wanafanya kazi vizuri, lakini pia, hawana magari. Magari yao mengi ni chakavu na hawana hata hela za *service*. Muda mwingi wanahangaika, hawana hata matairi ya gari, *service* hakuna, mafuta ni shida, tunaomba *OC* inapoenda hawa watu wapate mahitaji yao muhimu, ili waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda upande wa Jeshi la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto wanafanya kazi vizuri sana chini ya kiongozi wetu John Masunga. Juzi tu hapa tumeona kuna magari 11 yametolewa, tunamshukuru sana Rais wetu. Mbali na magari haya, pia, kuna nyumba sita za ghorofa ambazo wanakaa wanajeshi 60. Hizi ni nyumba ambazo ni nzuri na zimejengwa kwa shilingi bilioni 7.1 kwa kweli, ni nyumba nzuri na wanaokaa mle ni askari wa chini wa kawaida kabisa. Kwa hilo, kwa kweli, namshukuru sana Mheshimiwa Masauni kiongozi wetu wamefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia katika Mkoa wangu wa Simiyu kwa kweli, hatuna magari ya Askari Polisi. Hawana magari kabisa, tunaomba magari yapelekwe. Rais wetu amesema magari ya zimamoto yanaletwa kwa nchi nzima, tunamshukuru sana mama yetu, nchi nzima kuanzia Wilaya na Mikoa yake wote tutapata magari hayo. Magari hayo yatasaidia utendaji wa kazi

wa maaskari wetu maana wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini wakipata yale magari watafanya kazi vizuri, mambo yote yataenda vizuri na tutaendelea kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wafanyakazi wa Jeshi la Magereza ni kwamba, Magereza ni chombo ambacho kinafanya vizuri sana, kule wanawafundisha wafungwa. Sasa hivi urekebu wanajifunza mambo mbalimbali, lakini hawana vitendea kazi na miundombinu imechoka. Magereza nyingi ni za siku nyingi, hata Gereza letu la Mkoa wa Simiyu, Wilaya ya Meatu, ni gereza ambalo kwa kweli, limechoka, ni kama banda. Mheshimiwa Waziri afike kule ajifunze, aone, siyo nyumba ni banda tu limejengwa hata mfungwa akiamua kufanya vurugu mle anatoka kwa sababu, hata ukuta wenyewe haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aiangalie sana Wilaya ya Meatu tupate magereza ambayo ni nzuri hata wafungwa wanapokaa mle, wakae sehemu ambayo ni safi na salama. Kwa sababu, binadamu yeyote yule hata kama ana makosa anatakiwa kukaa sehemu iliyo salama, lakini gereza hili halina hata bwalo la chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu la Magereza tunaona jinsi linavyofanya kazi, wanalima na sehemu nyingine wanajihudumia chakula wao wenyewe, lakini kwa ajili ya kukosa miundombinu mizuri ndiyo maana hata vyakula hawaivishi. Mvua zinanyesha sana, lakini hatuna mabwawa ya kuhifadhi maji, basi naomba magereza wachimbiwe mabwawa, kwa ajili ya kufanyia shughuli zao za kilimo. Waweze kulima muda wote, wakati wa kiangazi na wakati wa masika, ili waendelee kufanya uzalishaji mkubwa. Watakula kile chakula na kingine wanaweza wakauza wakaongeza kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AMINA BAKAR YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya hasa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, Jeshi la Polisi lisimamie vyema usalama barabarani kwa kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani hasa kwa vyombo vya moto vikiwemo bodaboda wamekuwa wakivunja sheria sana bila kujali usalama wao na raia wengine na kupelekea ongezeko la ajali barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalishauri Jeshi la Polisi wasimamie inavyostahili ili waweze kuzingatia sheria, taratibu, miiko, weledi na maadili ya Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kuviwezesha vyombo vyo ulinzi na usalama kwa kuajiri askari wengi zaidi ili kuimarisha utendaji kazi wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika Taifa letu. Nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kuendelea kuliombea Taifa letu baraka, amani, upendo na mshikamano kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu pamoja na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi wanavyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020

hadi 2025, hongera sana Mheshimiwa Rais na waandamizi wako wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Wizara hii ya Mambo ya Ndani na vyombo vyetu vyote vya ulinzi na usalama nchini. Pia naipongeza pia Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na maoni ya Kamati yetu ya Bunge yaliyowasilishwa mbele ya Bunge letu leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kuondoa kigezo cha uhitimu wa mafunzo ya JKT kwa vijana wetu kujiunga kwenye majeshi yetu yote kwa kuwa siyo vijana wote nchini wenye sifa mbalimbali wamefanikiwa kupata mafunzo ya JKT nchini. Hivyo basi tunaiomba Serikali iangalie kwa mapana suala la urefu wa kimaumbile kwa vijana waombaji kama sifa mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua urefu wa binadamu ni maumbile aliyomjalia Mwenyezi Mungu hivyo basi katika sura nyingine kigezo hiki kinaweza kuwa kinyume na haki za binadamu kwa kuwa ni zaidi ya uwezo wake wa sifa na jitihada zake binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono 100% na naomba kuwasilisha.

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya kwa kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingozea uweledi katika kazi na utendaji kazi wa Jeshi la Polisi, kwa mfano, kusimamia maandamano ya vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa ujenzi wa vituo vya polisi nchini, Serikali imejenga vituo vya polisi maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano jengo la polisi la Mkoa wa Kaskazini Unguja, Kituo cha Polisi Tumbatu na hata Mkoa wa Kusini Unguja pia kumejengwa jengo la polisi la mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali na Wizara ya Mambo ya Ndani, changamoto iliyopo ni vituo vingi nchini Bara na Zanzibar vilijengwa muda mrefu hivyo vinahitaji ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vituo vingine vimejengwa tangu ukoloni kwa mfano, Kituo cha Polisi Mahonda na Mfenesini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa vituo vya polisi katika mkoa wa Kaskazini Unguja, Wilaya ya Kaskazini B kuna maeneo muhimu kama Kichakani, Mwembemajogoo, Kichwele, Kichungwani, Mbaleni na Kitope Ndani. Wananchi wa maeneo haya wanapata tabu kufuata huduma ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Masauni, na Naibu Waziri Naibu Waziri, Mheshimiwa Sillo kwa kuteuliwa, tuna imani naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pongezi nyingi kwa makamanda wote na watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kulinda amani nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi katika Mkoa wetu wa Iringa zipo changamoto nyingi, tunaomba kupatiwa pesa ya kutosha. Moja, uhaba mkubwa wa askari katika vituo vyetu vya polisi; pili, uhaba mkubwa wa magari na fedha za mafuta na matengenezo ya magari; na uhaba wa vitendea kazi kama *computer* kwa ajili ya matumizi katika mifumo ya ofisi; na kuhusu makazi ya askari, nyumba ni chakavu sana na pia askari wengi wanaishi uraiani kwa kukosa nyumba katika makambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Magereza; changamoto kubwa tunaomba Serikali ihamishe Gereza lililopo Kihesa Mgagao katika Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna dhana ya kulinda historia za wenzetu, hili eneo lilikuwa ni Kambi ya Wakimbizi wa Kusini mwa Afrika, kuna viongozi wa nchi waliishi pale kama Nelson Mandela, Thabo Mbeki, Walter Sisulu na kadhalika. Siyo haki eneo hilo Serikali iondoe hilo gereza kwa sababu yapo maeneo mengi katika Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi la Zimamoto, kwana hawana makazi ya askari na hawana ofisi za wilaya, magari ya zimamoto kwa sababu tunayo misitu katika Wilaya ya Kilolo na Mufindi ajali za moto kila wakati na tuna Mlima Kitonga tunahitaji *crane,* ajali ni nyingi mlimani na vifaa vya uokozi vya majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi kwa majeshi yetu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu kwa kulishauri Jeshi la Polisi kupitia Kamisheni zake nane wawe na Kamisheni tisa kwa makampuni mahsusi itakayosimamia tasnia ya makampuni za ulinzi binafsi hivyo itapelekea ufanisi na tija kwenye tasnia hiyo za kamponi binafsi za ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi hutembea umbali mrefu zaidi ya kilometa 15 kwenda Mahonda au Mfenesini kufata Kituo cha Polisi. Wilaya ya Kaskazini A pia kuna changamoto ya Kituo cha Polisi cha Chaani Lungalunga, eneo hili kituo ni kichakavu na hakifanyi kazi saa 24 . Hivyo wananchi wanapata tabu sana, wanatembea zaidi ya kilomeeta 17 kwenda Polisi Mkokotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine vifaa vya kutendea kazi Polisi wa Usalama Barabarani, hawana vifaa bora kama magari, pikipiki, *uniform* na *radio call.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ushauri wangu kwa Jeshi la Polisi, Serikali ianzishe mpango maalumu wa kujenga vituo vya polisi ambavyo ni muhimu. Pia Serikali itenge fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa vituo vya polisi vya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP,* Kamishna wa Polisi wa Zanzibar na Wakuu wote wa Vyombo vya Usalama kwa kuendelea kulinda nchi yetu, kudumisha amani na utulivu Bara na Zanzibar.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi maalumu; tunaomba kujengewa makazi ya polisi katika Kituo cha Polisi Iringa Mjini.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ukiukwaji wa sheria za barabarani kwa kasi sana. Hivi pikipiki kubeba watu watatu mpaka wanne ni ruksa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari ya Serikali hasa STL/STK bado *speed* zao siyo nzuri na uendeshaji wa hovyo hasa ku-*overtake* na kupita upande usiostahili unaendelea. Dodoma inaongoza kwa fujo za bodaboda. Pia magari mabovu yenye kelele na moshi yanaendelea kupita barabarani bila woga wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vibaka na wabakaji wameendelea kuumiza watoto na wanawake. Kila mwezi taarifa za ubakaji zinatolewa na vyombo vyetu. Serikali iongeze nguvu ya ulinzi kwa watoto.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kutambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambavyo vipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Pia nimpongeze Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini kwa

kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ili asaidiane na Mheshimiwa *Engineer* Masauni kuwahakikishia Watanzania usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani itusaidie kufanya maboresho kwenye Vituo vidogo vya Polisi vya Bassotu, Balangdalalu na Endasak kimiundombinu ipi kupatiwa usafiri ili wafanye kazi zao kwa ufanisi. Wilaya ya Hanang ina kata 33, ninashauri Wizara ya Mambo ya Ndani iige kama walivyofanya wenzao wa TAMISEMI kwa kuwapatia watendaji wa kata usafiri wa pikipiki hivyo askari kata nao wapatiwe pikipiki. Hali hii usafiri pia ni mbaya sana ngazi Wilaya, tunaomba tupatiwe magari wilayani ili kuboresha utendaji kazi wa Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Jeshi la Zimamoto Wilaya ya Hanang ni mbaya sana, hakuna askari wa kutosha, hawana usafiri ba hakuna gari la Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha atuhakikishie Wana-Hanang kupata watumishi waliowezeshwa vitendea kazi. Tumejifunza wakati wa maporomoko ya udongo, mawe na magogo Mlima Hanang kuwa Idara ya Zimamoto Wilaya ya Hanang ina mapungufu makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo niwapongeze sana watumishi wachace tulionao wanavyojitolea na kwa kushirikiana na Wana-Hanang wengine walifanya kazi kubwa kuokoa maisha ya Wana-Hanang wengi kipindi kile cha maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize kupatiwa gari la Zimamoto kwa kuwa Hanang ipo njia kuu ya Arusha kwenda Singida na magari mengine yamekuwa yakiungua yakiwa safarini mfano siku ya Jumapili gari iliyobeba *cement* iliungua moto wilayani kwetu ikiwa na mifuko 600 na sehemu kubwa wataalamu waliopo wilaya wakabaki kuhangaika kwa kukosa gari la Zimamoto. Hivyo Hanang tupewe kipaumbele kwenye magari ya Zimamoto zinazonunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Hamad Masauni na Naibu wake Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye majukumu ya ulinzi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa leo utahusu changamoto za mdau muhimu wa kusafirisha abiria ambao ni bodaboda na ushauri wa nini kifanyike kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya bodaboada ni biashara inayokuwa kwa kasi sana hapa nchini Tanzania. Hii ni kwa sababu vijana wengi wameamua kuingia kwenye biashara ya bodaboda kutokana na ukosefu wa ajira. Hivyo basi, kazi ya kusafirisha abiria kwa kutumia bodaboda imekuwa ni fursa kwa vijana kutokana na ukosefu wa usafiri wa magari kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto ya barabara, kwenye maeneo mengine ya makazi, hii ndiyo njia pekee ya watu kufika makwao. Bodaboda hutumika pia kwenye shughuli za kisiasa kwani zimekuwa zikinogesha misafara ya wanasiasa wetu wakiwa katika majukumu yao ya kutembelea maeneo mbalimbali, lakini pia bodaboda zimekuwa usafiri mbadala ikiwa mtu ana haraka na hataki kukwama katika changamoto ya msafara wa magari barabarani. Vilevile wafanyabiashara pia wanatumia bodaboda kuwachukulia wateja wao bidhaa za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli huu, ni vyema kundi hili liangaliwe kwa jicho la pekee ili wasaidiwe kuboresha huduma zao kwa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu huu wa bodaboda, waendeshaji wa vyombo hivi hukabiliana na changamoto nyingi. Hivyo basi Wizara ya Mambo ya Ndani ikishirikiana na wadau wengine wanahitaji kuja na mikakati ya

kitaifa ili kukabiliana nazo. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Baadhi ya waendesha magari huwadharau sana bodaboda. Utakuta bodaboda ipo barabarani, gari inaipigia honi kwa fujo itoke au utakuta gari inataka kuingia barabara kuu wakiona bodaboda hawasubiri, wanaingia tu na kusababisha ajali. Ikumbukwe vyote ni vyombo vya moto, vina haki ya kutumia barabara na vinalipia mapato ya Serikali. Aidha, bodaboda inakuwa imebeba roho za watu pia. Hilo nalo linahitaji kuangaliwa, kwani vitendo hivi husababisha ajali na vifo.

(ii) Waendesha bodaboda wengi huwa wanakamatwa na polisi na kuandikiwa faini kwa kutofuata sheria za usalama barabarani na kuhatarisha maisha yao na ya watumia njia kwa miguu na hata kusabaisha mtafaruku na usumbufu kwa waendesha magari.

(iii) Waajiri walio wengi hawawapi mikataba madereva wa bodaboda inayowapa haki zao kimkataba. Wale wenye mikataba, sehemu kubwa haina haki ya kupata bima za afya na kuweza kujiwekea akiba. Mikataba inaonesha kulinda maslahi ya mwenye chombo badala ya maslahi ya dereva wa bodaboda.

(iv) Hapa nchini hakuna mfumo rasmi na rafiki wa kuwakagua madereva wa bodaboda kama wamekidhi vigezo vya kufanya hiyo kazi.

(v) Baadhi ya abiria wanaowapa huduma huwa wanakuwa wezi na sio abiria wa kweli. Katika maeneo mengi hapa nchini, waendesha bodaboda wengi wameibiwa na kuporwa pikipiki na watu wanaojifanya kuwa abiria, lakini baadaye wanawageuka na kuwapora kwa kuwatishia kuwafanyia mambo mabaya ikiwa ni pamoja na kuwatoa uhai.

(vi) Changamoto nyingine ni ajali kuongezeka. Hii inasababishwa na vijana wengi kutokujua sheria za barabara. Kuna vijana wanaamini ukishajua kuendesha bodaboda mtaani unaweza pia kuendesha barabarani. Hii hupelekea waendeshe pikipiki barabarani bila kuwa na uelewa kuhusu sheria za barabara. Ajali nyingi zimepelekea vifo na ulemavu wa kudumu kuongezeka. Taarifa zinaonesha kwamba 70% ya majeruhi wa ajali za barabarani wanaopokelewa *MOI* wanatokana na ajali za bodaboda.

(vii) Changamoto nyingine ni ya waendesha bodaboda kupata vishawishi vya ngono. Kuna abiria ambao ni wanawake wakipanda pikipiki hawataki kulipa na kuwaambia waendesha bodaboda kuwa wanaweza kulipa kwa kufanya ngono hasa abiria ambao wanawachukua usiku kutoka sehemu za starehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto zilizotajwa hapo juu, ni vyema Wizara ya Mambo ya Ndani ikaweka umuhimu mkubwa kwenye watoa huduma hawa ambao kwa mawazo yangu ndiyo inayosafirisha watu wengi kuliko vyombo vingine vyote vya usafiri hapa nchini na kutoa ajira za vijana wetu wengi na huchangia kwenye pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto ya bodaboda hapa chini, ninaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Idara ya Usalama Barabarani ishirikiane na *LATRA* ili kuwe na usajili wa vituo rasmi vya bodaboda katika maeneo yote nchini (vijijini na mijini). Kwenye hivi vituo, kuwe na ukaguzi wa madereva pamoja na pikipiki mara kwa mara na kwa yule asiyekidhi vigezo asiruhusiwe kupakia abiria hadi pale atakaporekebisha kasoro zake. Ni vyema Idara ya Usalama Barabarani itoe mafunzo maalumu ya uendeshaji salama wa bodaboda.

(ii) Bodaboda hufika katika maeneo yote ya vijijini na mijini. Kuna maeneo mengine askari huzuia bodaboda kuingia sehemu za miji mikuu. Hivyo basi, kama kuna

sera yoyote itakayotungwa kuzuia bodaboda zisifike maeneo fulani, hili inabidi liangaliwe kwa umakini mkubwa kwani inaweza kuathiri kwa kiwango kikubwa kuyafikia maeneo hayo.

(iii) Pikipiki nyingi za bodaboda kwa sasa zina cc125-150. Pikipiki hizi hukimbia sana na hiki ndicho chanzo cha ajali nyingi. Napendekeza Serikali iweke sheria kwa pikipiki za kusafirishia abiria zisiwe na nguvu zaidi ya cc100.

(iv) Askari wa Usalama Barabarani wahamasishe raia kukataa kupanda abiria zaidi ya mmoja (mishikaki) kwa sababu udhibiti wa chombo *(control)* hupungua kwa dereva akipakia abiria zaidi ya mmoja, hivyo ni rahisi kupata ajali ukiwa uko kwenye mshikaki endapo itatokea dharura yoyote.

(v) Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na ile ya Uchukuzi na wadau wengine ianzishe *clinics* za kutoa elimu. Katika *clinic* hizo, yafuatayo yapewe kipaumbele:-

(a) *Clinic* hizi zitoe elimu mara kwa mara kwa waendesha bodaboda kuhusu usalama barabarani.

(b) *Clinic* kwa wamiliki wa bodaboda ziwaelekeze kwamba mtu wanayempa chombo cha usafiri ana leseni.

(c) Waendesha bodaboda wazingatie sheria za barabarani na kutotumia kilevi chochote muda wa kazi.

(d) Vijana wafundishwe kujihami ili wasiambukizwe au kuambukiza VVU.

(e) Kwa kuwa changamoto kubwa ya kazi ya bodaboda ni ajali, *clinic* hizi ziwafundishe umuhimu

na namna ya kupata bima za afya na kujiunga na Mifuko ya Pensheni ili akiba hizi zije kuwasaidia uzeeni. Bima za Afya zitakuwa msaada mkubwa katika usalama wao pale inapotokea changamoto ya ajali au kuugua.

(f) *Clinic* hizi zitoe elimu kwa madereva bodaboda ili waweze kuepukana na kundi la kulaumiwa. Kundi bodaboda linafahamika kama linalovunja sheria za barabarani na kufanya vurugu, hasa pale mwenzao anapopata ajali. Wengi hujichukulia sheria mkononi ikiwa ni pamoja na kuua watu na kuchoma magari hata kama kosa ni la bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa Mheshimiwa Waziri hongera kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia bajeti yake Mji wa Geita hauna gari kubwa la Zimamoto, gari kubwa liko Uwanja wa Ndege wa Chato na Mji wa Geita pamoja na Mji Mdogo wa Katoro una watu wengi na huduma hii ni ya muhimu sana haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wilaya ya Geita ina majimbo matatu, watu takribani milioni 1.7, wilaya nzima haina gari la polisi na hivi sasa gari yao imeharibika, wanazunguka mtaani kuchangisha pesa za matengenezo, naomba tupewe magari matatu; tupate gari moja kwa kila jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, jimbo la Geita Mjini lina *influx* kubwa sana ya watu, kutokana na wingi huo wa watu kumekuwa na wimbi kubwa la vijana wa bodaboda nadhani ni vyema utaratibu wa kuwasimamia hawa vijana uandaliwe kuondoa ajali nyingi, tuanzishe mafunzo na usajili wa vituo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba polisi kata wapewe usafiri, wanatia huruma.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia hutoba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa letu ikiwa na utulivu na salama pamoja na kusimamia amani mshikamano. Pia ninapenda kumpogeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, minapenda kumpogeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi wa malori makubwa barabarani, polisi ni lazima kuweka vituo maalumu kwa ajili ya ukaguzi wa malori hayo kwa sababu hivi sasa imekuwa kero kubwa kwa madereva ambao wanaenda safari ndefu hapa nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iweke nembo *(sticker)* maalumu ambayo itaonesha kwamba tayari gari hiyo imeshakaguliwa ili kuondoa usumbufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vituo vya Polisi ambavyo vinajengwa hivi sasa, tunaomba Wizara kuimarisha zaidi ili kujenga vituo vya kisasa vya polisi kwa ajili ya sasa na baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyombo vya usafiri hasa kwa Idara ya Usalama Barabarani, tunaomba Wizara kwa kitengo hiki iwapitie vyombo vya usafiri, kina ukosefu wa vitendea, kwa sababu idara hii ndio inayotoa huduma barabarani pale zinapotokea ajali inachukua muda mrefu, askari huchelewa kufika kwenye matukio hayo. Hata wale *DTO* hawana kabisa vyombo vya usafiri. Tunaomba Wizara katika mpango wake wa kuleta magari hayo iwakumbuke Idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wastaafu wa polisi, tunaomba maslahi yao ya kustaafu wasicheleweshewe mafao hayo wakati wa kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nimeshamwita Naibu Waziri, Daniel Baran Sillo. Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye hoja yetu hii ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Awali ya yote naungana na wenzangu waliotangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na hatimaye leo kuwa katika Bajeti ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka huu wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayofanya na pia, kwa maelekezo yake mahususi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kuboresha majeshi ambayo tunayasimamia. Pia, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye anamsadia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mwenyekiti wa Kamati yetu ya NUU, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Vicent na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Ushauri na maelekezo ambayo wanatupatia sisi Wizara hii hakika umekuwa ni msingi mzuri wa utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wetu, Mheshimiwa *Engineer* Masauni, kwa kazi kubwa na uongozi wake mahiri ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ndani ya Nchi. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunajiita ni kijiji kimoja chini ya

Mwenyekiti mmoja, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, nakuhakikishia nitakuwa msaidizi wako mahiri sana katika kutenda kazi. Pia, nawapongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na watendakazi wote walioko chini ya Wizara hii. Halikadhalika navipongeza vyombo ambavyo vipo chini ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia hoja hii ni Wabunge 24. Pia, Mwenyekiti wetu aliwasilisha Hoja ya Kamati, tunampongeza sana yeye pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote. Nawahahikikishia kwamba, hoja zenu zote tumezichukua, tunazithamini, tunaziheshimu sana na tutazifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kutoa ufafanuzi kwa hoja chache na nianze na hoja ya kwanza kuhusu Jeshi la Zimamoto. Hoja hii imetoka kwa Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum, ambaye alizungumzia habari ya changamoto ambazo zipo katika Jeshi hili la Zimamoto ambazo ni upungufu wa rasilimalli watu hasa waokoaji wa majini, vitendea kazi pamoja na vituo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inaendelea kuboresha mazingira ya Ofisi kwa kujenga na kukarabati vituo vya zimamoto na uokoaji. Katika Mwaka wa Fedha unaokuja 2024/2025, Jeshi linaendelea na ujenzi wa vituo saba katika Mkoa wa Geita, Manyara, Katavi, Songwe, Njombe, Kagera na Simiyu, ambapo miradi hii imetengewa kiasi cha shilingi 2,600,000,000 katika Mwaka wa Fedha unaokuja 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina jumla ya Maafisa na Askari 104 hawa ni kwa ajili ya ukokoaji majini. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Jeshi limepata kibali cha kuajiri askari wapya 246 ambapo kati ya hao, askari 25 wapo kwenye mafunzo ya uokoaji majini. Vile vile, katika Mwaka wa Fedha huu unaokuja 2024/2025 Jeshi limepanga kuajiri askari wapatao 425.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo kazi kubwa inafanyika katika Wizara hii. Juzi, tarehe 13 mwezi wa tano, Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Mheshimiwa Rais alizindua nyumba sita za Makazi ya Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji zenye thamani ya shilingi bilioni 7.1. Sambamba na nyumba hizo pia, Mheshimiwa Waziri alizindua magari 12 ya zimamoto ambayo yamegawanywa katika mikoa mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge Martha Mariki. Yeye amesema katika Mkoa wa Katavi hakuna gari la zimamoto na kwamba, Jeshi liwekeze katika sayansi na teknolojia na liwe na vifaa maalum badala ya kutumia karatasi katika kurekodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepata mkopo wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 95. Kupitia mkopo huo Jeshi litapata magari 150 ya zimamoto na uokoaji, magari haya yatakwenda kwenye wilaya na mikoa yote hapa nchini ambayo haina magari ya zimamoto, ukiwepo Mkoa wa Katavi ambao amesema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, amezungumza habari ya gari la Mkoa wa Iringa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wilaya zipo 139, magari yapo 150. Kwa hiyo, mikoa yote ambayo haina magari itapata magari ya zimamoto na uokoaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sayansi na teknolojia, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kuboresha shughuli zake kwa kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetenga jumla ya fedha kiasi cha shilingi 345,259,900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie. Shilingi 345,259,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizi mbalimbali za sayansi na teknolojia. Aidha, baadhi ya majukumu ikiwemo ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto umeanza kufanyika kwa kupitia

mifumo ya kitaalam na kupitia mradi huu wa mkopo nafuu, kama nilivyosema hapo awali kutoka Falme za Uarabuni, Jeshi linatarajia kusimika miundombinu ya mawasiliano katika vituo vikuu na kamandi 30 za zimamoto na uokoaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega, ambaye amezungumzia mambo kama matano hivi. Jambo la kwanza ni Jeshi lizingatie ulipaji wa malimbikizo ya madeni ya likizo. Pili ni, upandishaji wa vyeo kwa askari wetu. Tatu ni, ajira zinazotolewa na Jeshi letu zizingatie idadi ya wanawake. Nne, ajira zinazotolewa na Jeshi la zimamoto na uokoaji kwanza zizingatie ikama na wanawake. Tano, zimamoto haijapata fedha ya maendeleo na sita ni zimamoto iendelee kukusanya maduhuli, ili iweze kupata pesa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Jeshi kupitia Wizara ya Fedha, linaendelea na uhakiki wa madeni ya watumishi, wazabuni na watoa huduma yenye thamani ya shilingi 2,591,188,845.4. Jeshi likishakamilisha uhakiki huu litawasilisha Wizara ya Fedha, kwa ajili ya malipo ya madeni haya ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu upandishwaji wa vyeo. Jeshi linaendelea kuhakikisha kwamba, maafisa na askari wanapandishwa vyeo mara baada ya kufuzu mafunzo. Aidha, katika Mwaka huu wa Fedha wa 2024/2025, Jeshi linatarajia kuwapandisha vyeo maafisa na askari 1,224. Hii ni hatua kubwa sana na ya kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu ajira; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Jeshi limepanga kuajiri jumla ya askari 425 ambapo ajira hizo zitazingatia pia, idadi ya wanawake, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni kuhusu fedha za maendeleo. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Jeshi lilipokea shilingi 12,865,150,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha hizo pia, zimetumika kugharamia malipo ya

awali ya asilimia tano ya mkopo wa Dola Milioni 95, kama nilivyosema, kutoka *Abu Dhabi Export Trade Agency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, jeshi linaendelea na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali ambapo hadi Mwezi, Aprili 2024, limekusanya jumla ya shilingi 9,919,243,405 sawa na 90.17% ya lengo la Mwaka wa Fedha uliopita 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni juu ya Jeshi la Magereza ambayo ilitoka kwenye Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati yetu ya NUU. Moja, ilikuwa ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iweke utaratibu mzuri wa kuanza mapema maandalizi ya awali ya kuchochea miradi ya maendeleo. Ushauri huu umepokelewa na Wizara. Ninakuhakikishia pamoja na kamati yako kwamba, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea kufanya mawasiliano ya karibu na Hazina, kwa ajili ya kupatiwa fedha za maendeleo kwa wakati ili kuhakikisha kwamba, miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa wakati kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya Kamati ilikuwa ni Serikali iendelee kuboresha hali ya vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Serikali inatambua ukubwa wa tatizo la usafiri kwa Majeshi yetu yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Katika jitihada hizo Serikali imekuwa ikitenga fedha, kwa ajili ya kununua vyombo vya usafiri, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 shilingi 6,691,419,000 zilitengwa na jumla ya magari 25 yameshalipiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, shilingi 3,540,000,000 zimetengwa ili kununua magari ya Jeshi la Magereza, kwa ajili ya shughuli za utawala na usafirishaji wa mahabusu. Kwa hiyo, namtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba, maelekezo ya kamati sisi tunayasikiliza kwa umakini mkubwa, ili kuboresha utendaji kazi katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni Serikali iendelee na mkakati wake wa kuboresha hali ya vifaa na vitendea kazi kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 3,260,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa zana za Kilimo. Aidha,

kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi 2,378,523,000 ili kununua mitambo na zana za Kilimo. Maboresho haya ya ununuzi wa zana za kilimo, yatasaidia sana kuboresha upatikanaji wa maduhuli kwa sababu, Jeshi la Magereza linategemea sana shughuli za kilimo katika utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali vilevile imetakiwa iweke mikakati ya kupata hati za umiliki wa ardhi katika maeneo yote yanayotarajiwa kujengwa na yanayomilikiwa na Jeshi la Magereza hapa nchini. Serikali imeandaa mkakati wa kuhakikisha maeneo yote yanayomilikiwa na Jeshi la Magereza yanapimwa na kupatiwa hatimiliki. Nitatoa mfano, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilitenga shilingi 500,000,000 na mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga shilingi 200,000,000 na katika bajeti hii inayokuja ya 2024/2025 Serikali imetenga shilingi 492,940,000. Hata hivyo, mpaka sasa Jeshi la Magereza limeshapata hatimiliki 66 na kufanikisha kukamilisha kupima maeneo 144 ambayo yanasubiri hatimiliki. Aidha upimaji wa maeneo 40 yaliyobaki pia unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja kuwa, Serikali iboreshe matumizi ya teknolojia ya kisasa katika utendaji kazi wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Serikali imeendelea kuboresha matumizi ya sayansi na teknolojia kwa Jeshi la Magereza katika mifumo ya ulinzi na upekuzi. Kufikia Mwezi Aprili, 2024, Magereza 10 zimefunga mifumo ya *CCTV Camera*. Aidha, Magereza Kuu tatu zinatarajia kufungwa mifumo hiyo katika Mwaka huu wa Fedha unaoendelea 2023/2024. Vile vile Jeshi la Magereza linatarajia kusimika mifumo ya upekuzi *(Work through Scanner)* katika Magereza tano katika Mwaka wa Fedha unaokuja 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilitoka Fungu 29 - Jeshi la Magereza, lakini hii kutoka kwa Kamati ya NUU ambapo Kamati ilitaka pia fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi ma magereza mapya mawili pamoja na ukarabati wa magereza manne katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati umepokelewa na ukarabati na ujenzi wa magereza mapya kwa

Mwaka wa Fedha 2023/2024, umepokelewa na utazingatiwa katika mwaka wa fedha unaokuja na kuhakikisha kuwa fedha inapatikana kwa wakati ili miradi iweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni Jeshi la Magereza liandae mkakati wa kuboresha miundombinu chakavu kwenye baadhi ya magereza nchini. Jeshi la Magereza tayari limeshafanya tathmini na kuainisha mahitaji halisi ya ukarabati wa magereza pamoja na ujenzi wa magereza mapya ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yatakarabatiwa magereza manne ambayo yametengewa shilingi 6,491,792,000. Naomba niyataje magereza hayo: ni Gereza la Butimba lililoko Mwanza, Lilungu ambalo liko Mtwara, Ukonga na Keko, Dar es Salaam. Aidha, kulingana na mkakati huu wa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Jeshi la Magereza litakamilisha magereza mawili ambayo ni Gereza la Kilosa na Gereza la Karatu ambayo yametengewa shilingi 4,022,125,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine, Serikali iwezeshe Jeshi la Magereza kupata magari hususan kwa ajili ya kusafirisha mahabusu. Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inanunua magari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imetoa shilingi 1,930,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa magari ya mahabusu. Kwa Mwaka wa Fedha unaokuja wa 2024/2025, Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa magari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu kwenda Mahakamani na kurudi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kama sehemu ya kuimarisha Mfumo wa Haki Jinai nchini. Jeshi la Magereza litekeleze kwa ukamilifu na ufanisi mpango wa kuimarisha Huduma za Mahakama Mtandao. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Jeshi la Magereza limezingatia ushauri huu wa Kamati na litahakikisha kuwa vyumba 20 vya Mahakama Mtandao vinajengwa kama ilivyopangwa kwenye Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika eneo hili imetengwa fedha shilingi 1,397,680,000 katika mwaka wa fedha kama nilivyosema 2024/2025. Kwa hiyo, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge

wote kwamba hoja zenu kama mlivyosema, hoja zote tumezipokea na tutazifanyia kazi kila hoja na kuhakikisha kwamba tunazifanyia kazi na kuzitolea ufafanuzi kwa kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema maneneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kwa uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu:-

(i) Raia na mali zao wataendelea kuwa salama kupitia Jeshi la Polisi;

(ii) Uongozi na ujenzi utaendelea kuimarishwa kupitia Jeshi la Magereza;

(iii) Uokoaji wa maisha na mali utaendelea kupitia Jeshi la Zimamoto na uokoaji; *(Makofi)*

(iv) Usalama wa wahamiaji na masuala ya Hati ya Kusafiria na kuboresha mipango yote ya wahamiaji iko salama ndani ya uongozi wa Mama Samia Suluhu Hassan; na

(v) Vitambulisho vya Taifa vitatolewa kupitia *NIDA* katika uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo. Nimwite sasa mtoa hoja, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na afya njema. Vilevile, kwa mara nyingine tena

ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, kwanza kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa letu hili na kuendelea kudumisha amani na utulivu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumshukuru sana kwa kuendelea kuwa na imani na mimi katika nafasi hii. Namshukuru tena Mheshimiwa Daniel Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini lakini pia Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa umahiri wake mkubwa ambao ameuonesha kwa muda mfupi tu toka ameaminiwa kwenye Wizara hii. Kwa kweli amekuwa na msaada mkubwa sana kwangu na hata ninyi ni mashahidi. Maeneo mengi ambayo leo tulitakiwa tuyatolee ufafanuzi, ameweza kuyatolea ufafanuzi kwa umahiri mkubwa. Hivyo, kuifanya kazi yangu hapa leo kuwa siyo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, watumishi wote na askari wote walio chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Bunge chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, kwanza kwa jinsi ambavyo amewasilisha taarifa yao vizuri na hoja zilizotulia kweli kweli. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wale ambao walipata nafasi ya kuchangia walikuwa ni Wabunge kama 23. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa kama muda ungekuwa wa kutosha Wabunge wengi wangeweza kuchangia lakini hawa waliochangia wachache wamewawakilisha. Basi pamoja na taarifa ama hoja za Kamati baada ya zile ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezitolea ufafanuzi na nitaomba nichukue nafasi hii kuzitolea ufafanuzi baadhi ya hoja hizo. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zote

ambazo wamezitoa, hata zile ambazo hatutapata nafasi ya kuzitolea ufafanuzi hapa, tumezichukua na tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo nimeliona katika michango ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, ni dhahiri kabisa kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo tumeisikia hapa inakwenda sambamba na Dira ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia *4R* zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema hayo kwa sababu ukiangalia michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo imechangiwa hapa, mingi imejikita katika kuhakikisha na kuona Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Vyombo vyake inaendelea kuimarika na kufanya kazi zake vizuri ili hatimaye iweze kutoa huduma bora kwa wananchi. Maeneo ambayo nadhani Waheshimiwa Wabunge wameyagusia ili kutimiza azma hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, wamegusia sana katika eneo la kuangalia haki na stahiki za askari wetu. Vilevile, wamegusia katika maeneo ya kuhakikisha kwamba vyombo vyetu vya usalama vinakuwa na miundombinu bora na ya kisasa katika kutekeleza majukumu yake, ikiwemo nyumba za askari za kuishi, vilevile na vituo vya askari vya kufanyika kazi na Vyombo vyote vya Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo nimeona Waheshimiwa Wabunge wameigusia ni eneo la kuhakikisha kwamba askari wetu wanapata vitendea kazi vya kisasa na vilivyo bora ikiwemo: vyombo vya usafiri, mifumo na miradi mbalimbali ya TEHAMA ya kuweza kurahisisha utekelezaji kazi wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ni miongoni mwa mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyagusia na ni mambo hayo hayo ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akiyapigania na akituelekeza tuyasimamie. Ushahidi wa hayo ni pale ambapo Mheshimiwa Rais alipoamua kwa makusudi kuunda Tume ya Haki Jinai. Baada ya kuunda Tume ya Haki jinai ambayo

imetoa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hizi zote zilizoelezwa hapa Bungeni na nyinginezo ambazo nitapata nafasi ya kuzifafanua, kuna mambo ambayo Mheshimiwa Rais ameshaanza kuyafanya kwa vitendo hata kabla Tume hii haijaundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea alivyoingia madarakani siku ya kwanza, jambo la kwanza kubwa Mheshimiwa Rais alilolifanya ni kuhakikisha anaongeza Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutoka shilingi bilioni 937 kufikia shilingi trilioni 1.2 kwa muda wa mwaka mmoja. Waheshimiwa Wabunge leo ni mashahidi, nimesoma bajeti hapa ikiwa na shilingi trilioni 1.7. Tafsiri yake ni kwamba, Mheshimiwa Rais kwa muda wa miaka mitatu ameitoa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutoka shilingi bilioni 937 kuja shilingi trilioni 1.7. Hiyo inadhihirisha ni dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kuona mabadiliko makubwa yanatokea katika Wizara hii hususan Vyombo vyake vya Usalama vilivyopo katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge wakalikumbuka. Ni kweli bado Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia juu ya changamoto ya baadhi ya miradi kutokukamilika au baadhi ya fedha kutokufika kwa wakati. Nikiri kwamba, katika eneo la kuwezesha Vyombo vyetu vya Usalama, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejitahidi sana. Mbali na fedha hizi ambazo zimetengwa kwenye bajeti ambazo kwa mfano katika bajeti ya mwaka jana iliyokuwa karibu takribani shilingi trilioni 1.29, mpaka Mwezi wa Aprili, fedha ambayo ilikuwa imetoka ni shilingi 1,000,068,000,000/= ambayo ni sawasawa na 83%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba hiyo haitoshi, fedha hii 83% imetoka katika kipindi cha mpaka mwezi Aprili lakini kuna fedha ambayo ni nje ya bajeti ya kiasi cha shilingi bilioni 127, zimetoka nje ya bajeti. Kwa hiyo, kwa kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Serikali ya Awamu ya Sita imejitahidi sana kuviwezesha Vyombo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha hiyo, zaidi ya shilingi bilioni 51 zimeelekezwa mahususi kwa ajili ya kulipa madeni, madeni ya askari na madeni ya wazabuni. Madeni haya ni ya muda mrefu, lakini kwa mfano katika mwaka huu pekee, Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 15 kupunguza deni la shilingi bilioni 77 la Jeshi la Polisi, katika deni ambalo limehakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Tume ya Haki Jinai ambayo pamoja na mapendekezo mengine imetoa mapendekezo ya namna gani ambavyo stahiki na haki za Jeshi la Polisi zitakavyoimarishwa, kuboreshwa na kupatia ufumbuzi wa kudumu changamoto ya maslahi ya askari wetu. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kazi hiyo inaendelea vizuri. Tume ambayo imepewa kazi ya kufanya uhakiki imeshakamilisha kazi yake na sasa hivi andiko hilo limewasilishwa katika mamlaka husika katika ngazi mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kutolewa maoni ili baadaye litolewe uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba, malengo haya ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha anaongeza mishahara, posho, na haki na stahiki za askari wetu lakini hata ile hoja ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikiwagusa Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Rais alishaitolea maelekezo, hoja ya kuangalia stahiki zao kwenye upande wa pensheni kwa maana ya kikokotoo na yenyewe inakwenda kupatiwa suluhisho kwenye mchakato huu ambao tunakwenda nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza kwamba, mbali na mambo ambayo Tume ya Jinai imefanya lakini kuna mambo ambayo Mheshimiwa Rais ameyatekeleza kupitia bajeti yetu. Kwa mfano katika eneo la upandishaji wa vyeo, katika upandishaji wa vyeo, katika mwaka 2020/2023 watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wa Vyombo vyote 9,397 wamepandishwa vyeo. Mwaka huu tunakwenda kupandisha vyeo watumishi 26,876 kwa bajeti hii ambayo nimetoka kuisoma leo ikiwa Waheshimiwa Wabunge wataipitisha na naamini wataipitisha kwa mambo haya yalivyo makubwa na mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mafunzo; takribani askari 11,000 na watumishi 11,167 wamepata mafunzo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, mwaka huu tunazungumzia zaidi ya 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ajira, ajira 8,542 katika mwaka uliopita, mwaka huu tunazungumzia ajira zaidi ya 4,857. Yote haya yana lengo la kuhakikisha kwamba tunasaidia askari wetu waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia sana. Wako Wabunge ambao wamelalamika kwamba kuna upungufu wa magari katika majimbo yao. Wako Wabunge ambao wamelalamika katika majimbo yao kuna upungufu wa vituo vya polisi. Wako Wabunge ambao wamelalamika kuna changamoto ya uchakavu wa nyumba na upungufu wa nyumba za askari kwenye majimbo yao.

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba niwakumbushe, kupitia bajeti ambayo nimeisoma leo hii kuna kazi kubwa sana imefanyika katika eneo hili. Nikianzia kwa upande wa vyombo vya usafiri peke yake; nilisema hapa leo asubuhi, Jeshi la Polisi limepokea magari, kwanza tumepokea magari 44 aina ya *GWM* kati ya magari 200. Magari 156 kati ya haya 200 yanatarajiwa kuingia wakati wowote kuanzia sasa hivi. Tunatarajia hata kabla ya mwaka huu haujamalizika tunaweza tukapokea magari hayo 156 ili kutimiza idadi ya magari haya 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shilingi bilioni 72 ambazo Mheshimiwa Rais ameridhia zitoke kwa ajili ya kununua magari mengine. Kati ya fedha hizo, tayari shilingi bilioni 15 tumeshaagiza magari yanayogharimu shilingi bilioni 15 ambayo ni magari 147. Magari haya tunatarajia yaende kwenye ofisi za polisi mikoa na ofisi za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, juzi wakati tunazindua kituo cha kisasa hapa Dodoma - Mtumba, aliweza kuzindua mchakato wa makabidhiano ya magari kwa ajili ya Ma-*OCD*. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wanatoka

katika majimbo yale ambayo yana changamoto ya wakulima ambapo tulitumia fursa hiyo kuweza kuwapata magari yale. Yako magari mengine ambayo yameshakwenda katika wilaya na sehemu ya magari machache ambayo yamebakia yatakwenda kumaliza wilaya zote na hivyo Waheshimiwa Wabunge katika wilaya zenu zote Ma-*OCD* wenu sasa watakuwa na magari ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, Wabunge wamezungumzia kuhusu changamoto ya mafuta. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa ni kwamba utaratibu ambao tumeshaanza kuutekeleza wa mafuta kufikia mikoani sasa haupo. Sasa hivi mafuta moja kwa moja yanakwenda kwa Ma-*OCD* ili magari haya yaweze kutumika vizuri. Kana kwamba hiyo haitoshi, katika Bajeti ya Mwaka 2023/2024, zilitengwa shilingi bilioni 11.6 kwa ajili ya ununuzi wa boti 10 na kazi hiyo ya manunuzi inaendelea vizuri. Boti hizo zitasambazwa katika maeneo mbalimbali yenye changamoto katika bahari pamoja na maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimenunuliwa pikipiki 24, kuna pikipiki ambazo ni kwa ajili ya misafara ya viongozi, kuna pikipiki ambazo zinakwenda kwenye kata. Nitalizungumzia hili baadaye nitakapozungumza mkakati wa Polisi Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, jumla ya shilingi bilioni 36 ambazo zitanunua magari mengine 181 zimeshatengwa pamoja na shilingi bilioni 118 kwa ajili ya kununua vifaa mbalimbali vya kijeshi. Shilingi bilioni 40.5 kwa ajili ya kununua mifumo mbalimbali ya TEHAMA ikiwemo redio za masafa mafupi na masafa marefu. Kwa kweli mambo ni mengi sana ambayo yamefanyika katika kuhakikisha kwamba tunaimarisha vyombo vyetu vya usalama katika nyanja zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande makazi, Jeshi la Polisi limekamilisha miradi 15 ya ujenzi. Ni kweli ninatambua kuna maeneo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia hapa, kwamba maeneo yao yana changamoto ya makazi. Ninataka niwahakikishie kwamba, kwa yale maeneo ambayo mmezungumzia bado kuna changamoto ya vituo vya polisi

ambayo mmezungumza leo katika hili Bunge, bajeti ya matumizi ya Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka ujao hatujaikamilisha. Nawahakikishia kwamba tutachukua na tutaingiza katika bajeti ijayo. Ni kweli ni maeneo ambayo ni ya msingi na tutayaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kama nilivyosema mwanzo kwamba, tumekuja na mkakati kabambe wa kuimarisha ulinzi katika ngazi za chini. Imani yetu ni kwamba, tukiimarisha ulinzi katika ngazi ya kata itasaidia sana kupunguza changamoto ya uhalifu. Kwa sababu, kwenye kata ndiyo wahalifu wote wanaanzia kuishi lakini kwenye kata ndiyo kwenye taarifa zote za uhalifu. Ndiyo maana tukaja na mpango kabambe wa kupeleka askari kata, tena askari hawa wenye elimu ya chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hiyo ya kuendelea kusambaza askari hawa inaendelea lakini hata upelekaji wa vyombo vya usafiri, tumepata fedha tayari kwa ajili ya kununua pikipiki kama nilivyoeleza, zitakazokwenda katika kata. Najua safari hii ni ndefu, lakini safari ni hatua, tumeshaanza na naamini kabisa tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tumeamua kuja na mkakati wa ujenzi wa vituo vya polisi katika kata. Nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake aliyoyatoa alipokuja kwenye shughuli ya Jeshi la Polisi. Alitutaka mimi na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tukae pamoja na kuangalia uwezekano wa kuzishirikisha halmashauri zetu katika kujenga vituo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na timu yake yote. Tulikaa tukakubaliana na Mheshimiwa Rais kama nilivyoeleza katika hotuba yangu kwamba tumeanza mkakati mwaka huu. Tutaanza mkakati wa ujenzi wa Polisi Kata kupitia halmashauri zetu. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge niliwaahidi hapa mwaka jana na niliwahamasisha kwamba waanze kujenga vituo vya polisi katika maeneo yenu na sisi tutavimaliza. Katika mkakati huu wa TAMISEMI, vituo vyote ambavyo Waheshimiwa Wabunge

mmeshiriki pamoja na wananchi katika kupeleka nguvu zenu ndivyo ambavyo tutaanza navyo. Karibu vituo vya polisi 77 tunaanza navyo katika mwaka huu wa fedha, lakini tutajenga vituo vingine vya polisi 12 vya ngazi ya kata kupitia utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo ambapo kupitia maboresho ambayo tunaendelea nayo kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi, tunatarajia kujenga vituo vya ziada vya kata ili kuweza kuchangia jitihada za kazi nzuri ambayo itafanywa na halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, wale ambao wataamua kuhamasika tena safari hii kuanza ujenzi wa vituo kata katika majimbo yao niwaahidi kwamba, mara ambapo tutakuwa tunaanza awamu ya pili ama awamu ya tatu ya ujenzi wa vituo hivi, aidha kupitia kwa utaratibu wa halmashauri ama utaratibu wa Mfuko wa Tuzo na Tozo kupitia Shirika la Uzalishaji la Jeshi la Polisi tutawapa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge walilizungumza ni hoja ya kuimarisha utendaji kazi ama kulifanya Jeshi la Polisi liwe la kisasa. Nataka nichukue fursa hii kulipongeza sana Jeshi la Polisi, Jeshi la Polisi limeanza kutumia mifumo katika kufanikisha azma hii, katika lengo hilo matumizi ya mifumo yameshaanzishwa, zaidi ya mifumo 22 sasa hivi ya Jeshi la Polisi inaitumia kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake mbalimbali ikiwemo katika maeneo ya haki jinai, katika usalama barabarani, masuala ya utawala, mfumo wa manunuzi ya umma, mfumo wa ukusanyaji wa madeni na hata mifumo mingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kulipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kuimarisha uwezo wa askari wetu katika kufanya majukumu haya. Mifumo hii imesimamiwa na kutayarishwa na Askari Polisi wenyewe. Mifumo hii inakwenda kusaidia sana, nitoe mfano wa mfumo mmoja ambao umeweza kusaidia sana kutatua changamoto ama malalamiko yaliyokuwa

yakilalamikiwa kwa muda mrefu kwenye vituo vyetu vya polisi, mfumo ambao unaitwa *case file information system*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mfumo huu ambao umeandaliwa na wataalam wetu wa ndani ya Jeshi la Polisi unasaidia kuhakikisha kwamba mtu yeyote ambaye anakwenda kuhudumiwa katika Jeshi la Polisi taarifa ambazo anazitoa zinasomeka katika vyombo vyote wa kijinai, ikiwemo Ofisi ya Mkurugenzi wa mashtaka, Mahakamani na kadhalika ili kuepusha malalamiko ya muda mrefu ya wananchi kubambikiwa kesi, wananchi kutozwa rushwa na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi mfumo huu umefungwa katika maeneo vituo 23, lakini lengo letu ni kuhakikisha kwamba mfumo huu unasambaa maeneo yote ya nchi nzima. Ni imani yetu kwamba katika mwaka huu wa fedha tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba mfumo huu unaendelea kusogea katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfumo mwingine ambao kuna malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na changamoto ya rushwa kwa Askari wetu wa Barabarani, wakati huo walipokuwa wakipokea tozo na faini za barabarani kwa njia ambazo zilikuwa siyo za kisasa. Kupitia mfumo wa *TMS* sasa hivi kumekuwa na udhibiti mkubwa sana wa maduhuri ya Serikali, ingawa siyo lengo hilo, lakini imesaidia kupunguza malalamiko ya wananchi katika eneo hili la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze ni hoja ambayo imeibuka ama imeibuliwa na Mheshimiwa Mbunge wa Konde. Niliona hoja hii isingekuwa sawa kuiacha bila kuzungumza. Mheshimiwa Mbunge wa Konde amezungumzia hoja mbili, moja ni hoja ya suala la uhalifu wa mtandaoni na akagusia kuihusisha hoja hiyo na masuala ya ubaguzi. Hoja ya pili alizungumzia suala la *passport*, nadhani hili ilitoka kama taarifa lakini akaendelea kusisitiza mtazamo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba Jeshi la Polisi litaendelea kuhakikisha kwamba linasimamia sheria na sheria ni msumeno na hakuna mtu ambaye yupo juu ya sheria.

Matendo yote ambayo yanafanyika kupitia mitandao, ni kweli uhalifu wa mitandaoni ni masuala ambayo yamekuja kutokana na kasi ya utanuzi wa teknolojia, hivyo inahitaji tufanye kila jitihada kuhakikisha kwamba tunawezesha Askari wetu ama Jeshi la Polisi kuweza kukabiliana na aina hiyo mpya ya uhalifu na kazi hiyo inafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya kuhakikisha kwamba tunajenga uwezo kwa askari wetu ili kuweza kuwa na uweledi katika kukabiliana na matatizo ya uhalifu wa mitandao, pia tunafanya jitihada kuhakikisha kwamba tunawasaidia na kuwawezesha Askari kuwa na vifaa vya kisasa kukabiliana na changamoto hizo. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba sheria zote zinazohusu uhalifu wa mtandaoni ikiwemo *Cyber Crime Act* na nyenginezo ni sheria ambazo zimetungwa na Bunge hili Tukufu na tutaendelea kuzisimamia. Hivyo mtu yeyote ambaye anakiuka sheria hizo Jeshi la Polisi linaendelea kuchukua hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza hatua zinaendelea kuchukuliwa, kwa hiyo hakuna mtu ambaye atavunja sheria hizi akadhani kwamba tutamfumbia macho. Niendelee kutoa tahadhari kwa wananchi, iwe wa ndani ya nchi ama nje ya nchi kuhakikisha wanaendelea kutii sheria za nchi vinginevyo sheria itachukua mkondo wake, inawezekana isiwe leo lakini ikawa kesho, kwa kadri ambavyo hali ya upelelezi itakavyokamilika sheria itachukua mkondo wake, hivyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba asidhani kwamba Jeshi la Polisi linafumbia macho aina yoyote ya uvunjifu wa sheria za mitandao ambazo zipo wazi kabisa kwenye sheria hizo zilizoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya *passport* ambayo ameizungumza, kwanza lazima Mheshimiwa Mbunge na wananchi wafahamu kwamba *passport* ni *identity* ya nchi na ni mali ya wananchi, *passport* inaku-*identify* wewe kama ni raia wa nchi gani na *passport* hii nimezungumza ni ya wananchi na wananchi wana haki kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 17(1) inatoa uhuru wa mwananchi kwenda anapotaka. Kwa hiyo, raia yeyote wa Tanzania alipo popote ana haki ya kwenda anapotaka na

ndiyo maana *passport* hatuitumii kwa ajili ya matembezi au mizunguko ya ndani ya nchi kwa sababu ni *identity* ambayo ni ya Taifa inayoitambulisha nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapotoa hoja kwamba zamani kulikuwa kuna *passport* tuirudishe, nadhani ni kukosa uelewa, hakujawahi kuwa na *passport*. Kilichokuwepo ni matumizi ya hati maalum kwa ajili ya masuala ya usalama na hati hizo mpaka leo zinatumika, tofauti ni mabadiliko ya wakati tu. Kwa mfano, leo ukitaka kusafiri kwenda kutoka Zanzibar kuja Dar es salaam au kutoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam au kutoka hata Mkoa mmoja kwenda mwingine unavyoenda kukata tiketi utaambiwa utoe kadi yako *NIDA* haina maana kwamba ile ni *passport*, ile ni *identity* ya kiusalama. Kwa hiyo nataka hii ieleweke kwamba siyo sawa kuhamasisha au kujenga taswira katika jamii miongoni mwa Watanzania ndani ya nchi moja, kwamba kuna matumizi ya *passport* na mipaka baina ya sehemu moja na sehemu nyingine, Tanzania ni nchi moja na Watanzania ni wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa ilikuwa ni hoja ya udhibiti wa taasisi za kidini ambazo zinakiuka sheria. Ni kweli kuna taasisi ambazo aidha zinakiuka sheria ambazo hazijasajiliwa rasmi ambalo ni kosa kisheria, lakini kuna taasisi ambazo zimesajiliwa lakini zinakiuka sheria. Tumeshaanza kuchukua hatua, tumeanza uhakiki wa kuchukua hatua kwa zile taasisi zote ambazo zinatekeleza majukumu yao kinyume na Katiba zilizosajiliwa, mbali na kuchukua hatu kupitia Ofisi ya Msajili tunaendelea kutoa elimu kupitia semina na mafunzo mbalimbali kwa Watendaji wa Serikali katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Mitaa juu ya umuhimu wa kufuatilia kwa karibu mienendo ya jumuiya za kiraia zilizopo kwenye maeneo yao na kubainisha taarifa kwa ofisi za Msajili wa Jumuiya juu ya tabia na mienendo hatarishi ya jumuiya zilizopo nchini ili hatua stahiki ziweze kuchukulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Jumuiya, Sura Namba 337, kwa lengo la kuboresha muundo wa ofisi ya msajili, kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi wa ofisi hii katika kufuatilia na kusimami mienendo na uendeshaji

wa jumuiya za kiraia katika ngazi za wilaya ili kudumisha amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na taratibu za kuandaa mwongozo wa usajili na usimamizi wa jumuiya za kiraia nchini unaobainisha nafasi na wajibu wa Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa jukumu la usajili na usimamizi wa jumuiya hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mwongozo huo pamoja na mambo mengine unabainisha mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa na ofisi za Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya katika utekelezaji wa jukumu hilo ikiwemo kuwa na ajenda ya kudumu kwenye Kamati za Usalama za Wilaya pamoja na Mikoa kuhusu tabia, mienendo na uendeshaji wa jumuiya za kiraia zilizopo kwenye maeneo yao na zile zinazoomba usajili kwa lengo la kudumisha amani, utulivu na usalama wa Taifa letu. Mwongozo huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa robo ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambazo Waheshimiwa Wabunge walizizungumzia ilikuwa ni hoja inayohusu Idara yetu ya Uhamiaji. Serikali inaendelee kuliwezesha Jeshi la Uhamiaji kupata vyombo vya usafiri ili kuwabaini wahamiaji wasiyo na vibali na kuchukuliwa hatua. Tumezungumzia katika Jeshi la Magereza na Jeshi la Zimamoto, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia kwa kina kabisa jinsi ambavyo Serikali ilijipanga katika kuhakikisha inawezesha vyombo vyetu hivyo kwenye eneo la usafiri na mimi nilizungumzia kwenye Jeshi la Polisi. Hata kwa upande wa Uhamiaji, Serikali imetenga shilingi bilioni 3.3 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuwezesha Idara ya Uhamiaji kupata magari 18 ikiwa ni mkakati wa kuimarisha udhibiti wa wahamiaji haramu nchini na kuwachukulia hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kwamba hakuna chombo ambacho kimeachwa, Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto, Jeshi la Uokoaji kuna uwekezaji mkubwa ambao unaendelea kufanyika katika maeneo yote ikiwemo maeneo ya vyombo vya usafiri

katika kusaidia utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi kupitia vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo limezungumzwa kuhusu Idara ya Uhamiaji, kwamba Serikali iendelee na mkakati wa kuliwezesha Jeshi la Uhamiaji kufunga mfumo wa uhamiaji mtandao katika ofisi zote za uhamiaji zisizo na mfumo huo sambamba na mfumo wa udhibiti wa mipaka kwenye ofisi za baadhi ya vituo vya kuingia nchini. Mkakati wa kuboresha mfumo wa Uhamiaji mtandao katika ofisi ambazo hazina mfumo umezingatiwa katika bajeti ya mwaka 2024/2025, ambapo Serikali imetenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uhamiaji mtandao ili kuendelea kujenga mtandao huo katika vituo ambavyo havijafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo inahusu Idara ya Uhamiaji ni hoja ambayo inahusu mkakati wa kudhibiti mianya ama njia zisizo rasmi zaidi ya 1,000 katika Mikoa mbalimbali ya mipakani, ikiwemo kutumia mifumo ya udhibiti wa mipakani *(E-border)* kufanya hivi kwani itakuwa ni sehemu ya udhibiti wa uingiaji na utokaji wa wahamiaji haramu pamoja na bidhaa za magendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Idara ya Uhamiaji inaendelea kudhibiti njia zisizo rasmi zinazotumiwa na wahamiaji haramu, tumefanya ufuatiliaji na kubaini njia zisizo rasmi 1,029, kazi inayoendelea hivi sasa ni kufanya uchambuzi ili kuamua maeneo gani yanaweza kuanzishwa vituo rasmi vya kuingia na kutoka nchini na kufungwa mifumo ya udhibiti wa mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni jitihada za kudhibiti njia zisizo rasmi za Idara ya Uhamiaji imepata kibali cha kuajiri askari wapya 400. Nilizungumzia pale idadi ya ujumla wake ya askari wote walioajiriwa katika vyombo vyote lakini kwa upande wa Uhamiaji kwa mwaka huu tunatarajia kuajiri askari 400, askari hawa watakapomaliza mafunzo yao wataweza kutawanywa katika sehemu mbalimbali ikiwemo katika maeneo ya mipaka pamoja na kwenye Kikosi cha Uhamiaji Wanamaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwenye Uhamiaji ilikuwa ni hoja ya uboreshaji wa Jeshi la Uhamiaji katika matumizi ya vifaa na vitendeakazi, kwamba uendane na kutoa mafunzo ya askari ili waweze kutumia vifaa na vitendea kazi hivyo kwa ufanisi na kupata tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Uhamiaji limeendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari ili waendane na matumizi ya vifaa na vitendeakazi wanavyovitumia katika utoaji wa huduma ambapo kwa mwaka 2023/2024, jumla ya Maafisa na Askari 432 walipatiwa mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia hoja yangu naomba nichukue nafasi hii kusisitiza katika eneo moja ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia sana. Nichukue nafasi hii kwanza kuendelea kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutupa moyo Wizara yetu kwa yale ambayo tunayasimamia na mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza ama yale ambayo tumewasilisha katika taarifa yetu wameendelea kuyaunga mkono, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo makubwa ambayo yanakwenda kuleta mabadiliko makubwa sana ya utendaji kazi katika vyombo vyetu vya usalama, hususan Jeshi la Polisi ambapo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia kwa umahiri mkubwa ni eneo la matumizi, naomba hili nimalizie kwa kulisisitiza niligusia, lakini naomba nimalizie kwa kusisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la matumizi ya TEHAMA na wapo ambao walifikia kulilaumu Jeshi la Polisi juu ya namna ambavyo wanashindwa kudhibiti changamoto ya bodaboda na wakajaribu kutoa mfano na baadhi ya nchi ambazo pengine kuna nidhamu ya bodaboda. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mifano ya nchi ambazo mmetoa na hata zile ambazo hamjatoa zenye utiifu wa sheria kwa watumizi wa vyombo vya usalama barabarani wakiwemo bodaboda zimeshaanza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza kwenye bajeti kwenye miradi ya kimkakati kuna miradi mikubwa kadhaa ambayo tunaona inakwenda kuleta mabadiliko makubwa katika Jeshi la Polisi. Moja katika miradi ambayo nimeizungumza ni mradi wa Miji Salama, mradi huu utahusisha ufungaji wa *camera* 6,500 kwa kuanza na Majiji manne. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba miradi hii ikiwemo mradi wa *highway road patrol* ambao unakwenda kuweka mifumo ya kisasa kwenye barabara kuu, inakwenda kutatua chanagmoto ya uvunjifu wa sheria za usalama barabarani, lakini inakwenda kusaidia kupunguza ajali na kubwa zaidi inakwenda kusaidia kuimarisha usalama na kuwasaidia askari wetu kuweza kufanya kazi kwa weledi zaidi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutuelewa na kutuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bado dakika zangu zimebakia nitaomba pia nisisitize mambo mengine ya muhimu machache sana. Moja katika jambo ambalo nimeomba nisisitize sana japokuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameligusia kidogo ni mapinduzi makubwa ambayo tunakwenda kufanya kwenye Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeshuhudia hivi juzi tulimwakilisha Mheshimiwa Rais, katika kukabidhi magari 12 mapya ya kisasa ya zimamoto. Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakilalamika sana kuhusu changamoto hii. Nilimsikia Mheshimiwa Martha, Mbunge wa Viti Maalum Katavi, akizungumzia juu ya changamoto ya gari la Zimamoto katika Mkoa wa Katavi, anasema kuna gari moja lipo *Airport* inakuwaje, leo moto ukitokea na huku ndege inatua, kwa kweli ni changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuchukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Amiri Jeshi Mkuu kwa kufanya mapinduzi makubwa sana kwenye Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, ambayo hayajawahi kufanyika katika historia ya nchi hii. Tunazungumzia ununuzi wa magari 150, boti 23, helikopta moja na vifaa vingine mbalimbali vya kuzima moto. Haya mambo ni mambo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu vifaa hivi vitakapokuwa vinawasili na nimshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuweza kusaidia kufanikisha upatikanaji wa mkopo huu. Mwaka wa Fedha 2024/2025, tutaanza kupokea magari haya ya ziada, mwaka 2025/2026 tunamalizia awamu ya mwisho ya upokeaji wa vifaa na magari haya ya kisasa. Mara yatakapowasili mikoa yote na wilaya takribani nyingi zitaweza kupata vifaa vya kisasa. Jitihada zinaendelea kuhakikisha kwanza tunaongeza idadi ya askari wa kuzima moto lakini pia, tunawajengea uwezo ili waweze kutumia vifaa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tumeanzisha mkakati kabambe wa kuhamasisha watu binafsi kujitolea kushiriki katika shughuli mbalimbali za uokozi na uzimaji moto kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu. Niipongeze mikoa ambayo tayari imeshaanza kutekeleza wito huo na ni imani yangu kwamba, mikoa mingine itaendelea kutuunga mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hitimisha kwa kuomba hela.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nishukuru sana kwa mara nyingine tena Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao na kama ambavyo nimewaahidi kwamba, yale ambayo hatujapata nafasi ya kuyafafanua, basi tutaweza kuyafanyia kazi na kuyawasilisha kwa maandishi. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hatujakusikia. Hiyo hoja haijasikika, hebu rudia.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, nasikia hujaomba hela. Nilikuwa nimesema omba hela. Kwa hiyo, tukamilishe kwa kuomba hela. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Bunge lako Tukufu liridhie shilingi 1,711,710,987,000 ambazo kati ya fedha hizo, shilingi 551,583,381,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 870,429,138,000 kwa mishahara na shilingi 289,698,464,000 ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na kuungwa mkono. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI- KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management Division*………………Sh. 24,987,361,000

**MWENYEKITI:** Nina majina ya watu hapa ambao wameomba maelezo. Kuna majina ya watu kama wanne kwa hiyo, nitaanza na mmoja mmoja. Mheshimiwa Athuman Almas Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, pamoja na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Mheshimiwa *Engineer* Masauni, lakini naomba ufafanuzi wa jambo mmoja muhimu sana nalo ni kuhusu Sekta ya Ulinzi Binafsi. Sekta ya Ulinzi Binafsi ilianzishwa hapa nchini mwaka 1980 ambapo kulikuwa na makampuni mawili. Leo tuna kampuni zaidi ya 2,500 zinazoajiri askari walinzi zaidi ya 850, lakini hakuna sheria iliyoanzisha makampuni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitangaze, nina-*declare interest* kwamba, nilileta Muswada wa Sheria ya Ulinzi Binafsi ambayo ingezaa Mamlaka ya Sekta ya Ulinzi Binafsi *(Private Security Industry Authority),* ambayo ingeyapanga makampuni haya katika madaraja mbalimbali na kuyafanya yatambulike kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika tangu Sheria hiyo ilichukuliwa na Serikali haijarudishwa hapa Bungeni tangu mwaka 2017 mpaka leo. Makampuni haya yanafanya kazi kwa tabu sana, 80% ya mapato yao yanatumika kama …

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni haya…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige, endelea.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni yanafanya kazi kwa tabu sana. 80% ya mapato yao yanatumika kwa ajili ya kulipa shughuli za kuendeshea na inayobakia ndogo sana ndiyo waweze kujikimu. Kumekuwa na matatizo katika kesi zote za *CMA,* 90% au zaidi ni kesi za makampuni ya ulinzi binafsi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige, kwa ngazi hii ni jambo moja mahususi la kisera. Jambo gani unalotaka litolewe ufafanuzi?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja mahususi la kisera ni kutaka kupata Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi Nchini.

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashika shilingi kama sitapata maelezo mazuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Mheshimiwa Maige, upo kwenye Kampuni za ulinzi?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Chama cha Waajiri Nchini *(ATE)* ambayo ndani yake kuna Sekta hii ya Ulinzi Binafsi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, tuendelee Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Almas Maige, amekuwa akizungumzia hoja hii kwa muda mrefu. Bahati nzuri mimi na yeye tumeshakaa na nimeshamweleza hatua ambayo Serikali tunachukua. Nilimwambia kwamba, kuna hatua fulani ambazo kimsingi za kisheria lazima tuzifuate kabla ya kufikia kuweza kuwasilisha Muswada huo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Almas Maige, aamini kwamba, *commitment* ya Serikali katika kufanikisha jambo hili ipo pale pale na yale ambayo nimezungumza naye mimi na yeye pembeni yaendelee kusimama. Nimhakikishie kwamba, michakato hiyo itakapo kuwa imekamilika basi Muswada huu utaweza kuwasilishwa Bungeni. Niombe aridhie kuipa nafasi Serikali kumaliza mambo ambayo ni ya muhimu kabisa kufanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Maelezo ndiyo hayo. Mheshimiwa Maige, bado unashika shilingi?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, niishukuru Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Masauni, kwamba, sasa tumeanzishiwa Jeshi la Zimamoto kule Wilayani Nyasa. Suala langu ni la kisera kwamba, hili Jeshi la Zimamoto inaonekana linatoa mkazo mkubwa sana kwenye kuzima moto kuliko uokozi na hasa katika maeneo ya majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi sana za majanga katika maji na hata hapa alivyozungumza amesisitiza zaidi kuhusu upatikanaji wa magari, lakini masuala ya maboti nimesikia tu juu juu tu kidogo, lakini sijapata msisitizo wake. Naomba nifahamu ni namna gani Wizara, imejipanga kuhakikisha kwamba, maziwa yetu pamoja na bahari inakuwa ni sehemu salama kwa wananchi wote wanaotumia maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, maelezo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango kabambe ambao nimeueleza wa mageuzi makubwa kwenye Jeshi la Zimamoto, eneo la uokoaji katika maji limepewa kipaumbele. Ndiyo maana nikawa nazungumzia ununuzi wa boti 23 za kisasa mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari tumeshaanza maandalizi ya kuandaa askari wa

Jeshi la Zimamoto kupata mafunzo mbalimbali. Hivi karibuni kuna askari ambao walipata mafunzo kule Zanzibar kwenye Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kuweza kusomesha askari zaidi. Hata katika huo mpango wa ununuzi wa vifaa ama hizo boti kutakuwa kuna utaratibu maalum wa mafunzo kwa askari wetu kwa ajili ya matumizi ya vifaa hivyo ikiwemo boti. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Manyanya, aridhie juu ya mkakati huo wa Serikali na nimuahidi boti hizi zitasambazwa katika Maziwa yote ikiwemo Ziwa Nyasa karibu na Jimbo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, umeridhika na maelezo hayo?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sina lengo la kushika shilingi kwa maana ya mshahara wa Waziri, lakini nitaomba tu anisaidie. Wakati nachangia nilizungumzia suala zima la maslahi ya askari wetu hususani kwenye stahiki zao wanazozidai. Kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri, ametueleza kwamba, wapo kwenye mchakato na mikakati. Sasa ni kawa najaribu kutafakari hii michakato na mikakati ni lini haswa itakwenda kukamilika ili askari wetu wote waweze kulipwa stahiki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la michakato wameshafanya michakato. Mfano, Jeshi la Magereza wameshafanya uhakiki kwa miaka mitatu 2019/2020, 2020/2021, 2021/2022 miaka mitatu wamefanya uhakiki hawajawalipa hawa watu stahiki zao. Hali kadhalika Jeshi la Polisi pamoja na Uhamiaji. Watu hawa wanafanya kazi kubwa ya kulitumikia Taifa lao. Wanatumia fedha zao kidogo, hiyo mishahara yao kidogo kuendelea kulihudumia Taifa hili. Sasa nataka *commitment* ya Serikali, ni lini michakato hii

inakwisha watu hawa waweze kupewa stahiki zao ili na wao waweze kuona wanalitumikia Taifa hili na wanathaminiwa katika nchi yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, *commitment* ya Serikali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Kunti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo nilizungumzia hatua mbili kubwa. Hatua ya kwanza, nilisema kuna fedha ambazo zilihakikiwa na ni madeni ya muda mrefu ya miaka mingi. Nikaeleza kwamba, kuna fedha zaidi ya shilingi zaidi ya bilioni 51.5 zimetolewa katika bajeti hii ambayo tunamaliza nayo sasa hivi, kwa ajili ya kulipa madeni ikiwemo madeni hayo ya askari. Yapo madeni mengi sana ambayo yamepunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nikaeleza kwamba, kuna mkakati wa kupatia ufumbuzi wa tatizo hili la kudumu. Nilieleza kwamba, Mheshimiwa Rais, kwa dhamira yake njema aliunda Tume ya Haki Jinai na moja katika malengo mahususi ama hadidu rejea za Tume hiyo ni kuangalia haki stahiki za askari wetu. Mapendekezo hayo yameshakuja na andiko la aina ya maboresho yawe vipi limeshatayarishwa. Kwa hiyo, lipo katika hatua ya utekelezaji. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Kunti aridhie kwamba, kazi ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameifanya katika muda mrefu kutatua tatizo hili la muda mrefu anastahili kupongezwa na anastahili kutiwa moyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa maelezo. Kwa vile alikuwa hakusudii kushika shilingi tuna-*assume* kwamba maelezo ameyaelewa. *(Makofi)*

Tunaenda kwa anayefuata, Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilisema nitashika shilingi, lakini sasa hivi sikusudii

tena kushika shilingi kwa vile nilimwona Mheshimiwa Waziri ame-*note* pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu ni la kisera ingawa nilichangia kuhusu Kituo cha Konde. Vituo vyetu vya zamani vya Jeshi la Polisi vimechakaa sana na hakuna *furniture* na vingi vyao vipo maeneo ya mijini ambavyo ndiyo vituo mama. Sasa pale ndiyo huduma stahiki (huduma mama) zinapopatikana na viongozi wetu wa Jeshi la Polisi pia wapo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikitoa mfano Kituo chetu cha Polisi *Central*, hapa Dodoma…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa, tunataka suala la kisera na siyo mahususi.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni la kisera, kwa sababu nazungumzia vituo vya nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Ulikuwa na muda wa kulisema hilo wakati wa kuchangia lakini sasa tunataka jambo mahususi.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo mahususi, vituo vya nchi nzima ni chakavu, tunataka *commitment* ya Serikali, kwamba vitahudumiwa vipi kwa sababu vile vituo vimechakaa na havina thamani, havina *furniture*, ndiyo nahitaji maelezo ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante, ni jambo la nchi nzima. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nimshukuru sana ameelimika na hasa ile hoja yake ya pasipoti atakuwa haizungumzi tena, amejua kwamba Tanzania ni nchi moja na watu wana uhuru wa kwenda wanapotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ya pili ni hoja ya msingi, kwamba kuna changamoto ya uchakavu wa vituo vya polisi,

lakini si uchakavu tu hata changamoto ya upungufu wa vituo vya polisi, ndiyo maana nikaeleza mikakati ya kujenga vituo vya polisi vya kisasa katika maeneo ambayo havipo, nimezungumzia mikakati ya ujenzi wa vituo vya polisi kata na nikaeleza mikakati ya aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza mikakati ya TAMISEMI, nimeeleza mikakati ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi na kuna mikakati ya kibajeti vile vile. Nguvu zote hizi zikichanganyika zinakwenda kutufanya tufike huko tunapotaka kwa haraka, kwa sababu matatizo ya vituo vya polisi ni mengi nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tukaja na njia ya ubunifu, tumezoea hapa kutatua tatizo hilo kwa kutegemea bajeti peke yake na bajeti peke yake haiwezi kutosha kukabiliana na changamoto hiyo kubwa ya nchi nzima, lakini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupa maelekezo ya kuwa wabunifu na kupitia 4R zake tumelifanyia *reform* Shirika letu la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi. Tunakwenda kutumia Mfuko wetu wa Tuzo na Tozo, sasa kwa utaratibu ambao utakuwa na tija zaidi kuweza kujenga vituo vingi, kukarabati vituo vingi kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata Kituo chake cha Konde, basi katika mpango huu, mwaka huu nimhakikishie kitakuwepo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(2) na kwa mamlaka ya Kiti sasa tutapitisha kwa mafungu.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................................Sh. 24,987,361,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 838,993,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...................Sh. 1,469,583,000
Kifungu 1004 – *Probation Services Division*...............Sh. 5,144,493,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*.....Sh. 609,262,000
Kifungu 1006 - *Information and Communication Technology Unit*....................................Sh. 761,098,000
Kifungu 1007 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 699,126,000
Kifungu 1008 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 808,914,000
Kifungu 1009 - *Complaints Unit*....................................Sh. 497,215,000
Kifungu 1010 - *Legal Services Unit*...............................Sh. 897,799,000
Kifungu 1011 - *The Police, Prisons, Fire & Rescue and Immigration Services Commission*......Sh. 710,000,000
Kifungu 2001 - *Registrar of Societies Unit*.....................Sh. 880,386,000
Kifungu 4001 - *Refugees Services Division*................Sh. 2,008,467,000
Kifungu 4002 - *Anti-Trafficking in Person Secretariat*.............................................Sh. 957,748,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kifungu 3001 - *Fire and Rescue Services*.................Sh. 12,757,478,643
Kifungu 3002 - *Fire and Rescue Services Training Institute*................................................Sh. 667,476,000
Kifungu 3003 - *Fire Safety*..............................................Sh. 741,703,000
Kifungu 3004 – *Operations*...........................................Sh. 959,065,000
Kifungu 3005 - *Legal Services Unit*...............................Sh. 263,703,000
Kifungu 3006 - *Arusha Regional Office*.....................Sh. 1,643,388,000
Kifungu 3007 - *Dodoma Regional Office*..................Sh. 2,669,046,500
Kifungu 3008 - *Mwanza Regional Office*..................Sh. 2,112,616,000
Kifungu 3009 - *Mbeya Regional Office*.....................Sh. 1,907,480,000
Kifungu 3010 - *Kinondoni Regional Office*................Sh. 1,552,874,000
Kifungu 3011 - *Mara Regional Office*..........................Sh. 859,127,000

Kifungu 3012 - *Kigoma Regional Office*....................Sh. 1,381,545,000
Kifungu 3013 - *Pwani Regional Office*.......................Sh. 1,935,690,000
Kifungu 3014 - *Manyara Regional Office*.................Sh. 1,332,205,000
Kifungu 3015 - *Geita Regional Office*........................Sh. 1,186,374,000
Kifungu 3016 - *Temeke Regional Office*....................Sh. 4,188,408,000
Kifungu 3017 - *Singida Regional Office*........................Sh. 908,423,000
Kifungu 3018 - *Tabora Regional Office*.....................Sh. 1,317,363,857
Kifungu 3019 - *Iringa Regional Office*........................Sh. 1,474,934,000
Kifungu 3020 - *Rukwa Regional Office*.......................Sh. 1,190,538,000
Kifungu 3021 - *Ruvuma Regional Office*...................Sh. 1,238,548,000
Kifungu 3022 - *Kagera Regional Office*....................Sh. 1,162,289,000
Kifungu 3023 - *Mtwara Regional Office*....................Sh. 1,147,715,000
Kifungu 3024 - *Lindi Regional Office*..........................Sh. 1,048,984,000
Kifungu 3025 - *Njombe Regional Office*...................Sh. 1,088,036,000
Kifungu 3026 - *Shinyanga Regional Office*...............Sh. 1,241,317,000
Kifungu 3027 - *Ilala Regional Office*..........................Sh. 1,939,592,000
Kifungu 3028 - *Kilimanjaro Regional Office*..............Sh. 1,272,064,000
Kifungu 3029 - *Morogoro Regional Office*................Sh. 1,447,421,000
Kifungu 3030 - *Katavi Regional Office*.........................Sh. 860,535,000
Kifungu 3031 *Tanga Regional Office*.........................Sh. 1,858,482,000
Kifungu 3032 - *Simiyu Regional Office*..........................Sh. 873,088,000
Kifungu 3033 - *Songwe Regional Office*...................Sh. 1,101,093,000
Kifungu 3034 - *Fire and Rescue Training College*.....Sh. 2,382,147,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 - Jeshi la Polisi**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.................................Sh. 202,646,133,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*..................Sh. 261,758,225,000
Kifungu 1003 - *Internal Monitoring and Evaluation Unit*.......................................Sh. 313,840,000
Kifungu 1004 - *Legal and Research Services Unit*.......Sh. 646,006,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 334,283,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 277,778,000
Kifungu 2001 - *Police Main Force*.............................Sh. 4,686,557,000
Kifungu 2002 - *Police Marine*.....................................Sh. 1,443,217,000
Kifungu 2003 - *Railway Police Division*......................Sh. 3,739,441,000

Kifungu 2004 - *Police Signals Branch*.........................Sh. 2,912,391,000
Kifungu 2005 - *Police Zanzibar*..................................Sh. 9,048,172,000
Kifungu 2006 - *Police Air Wing*..................................Sh. 2,319,278,000
Kifungu 2007 - *TAZARA Police*....................................Sh. 1,722,326,000
Kifungu 2008 - *Field Force Unit*..................................Sh. 2,001,415,000
Kifungu 2009 - *Traffic Police*...........................................Sh. 965,271,000
Kifungu 2010 - *Police Airport*.....................................Sh. 3,683,017,000
Kifungu 2011 - *Police Dog and Horses*.........................Sh. 989,507,000
Kifungu 2012 - *Dar es Salaam Special Zone*.............Sh. 8,784,963,000
Kifungu 2013 - *Police Ilala*.........................................Sh. 11,305,571,000
Kifungu 2014 - *Police Kinondoni*...............................Sh. 14,551,145,000
Kifungu 2015 - *Police Temeke*...................................Sh. 8,515,144,000
Kifungu 2016 - *Police Arusha*..................................Sh. 14,035,887,000
Kifungu 2017 - *Police Iringa*.......................................Sh. 9,121,830,000
Kifungu 2018 - *Police Kilimanjaro*.............................Sh. 13,331,793,000
Kifungu 2019 - *Police Kigoma*...................................Sh. 10,734,151,000
Kifungu 2020 - *Police Kagera*...................................Sh. 11,566,115,000
Kifungu 2021 - *Police Lindi*.........................................Sh. 7,708,926,000
Kifungu 2022 - *Police Mwanza*.................................Sh. 16,394,122,000
Kifungu 2023 - *Police Mara*.........................................Sh. 8,515,461,000
Kifungu 2024 - *Police Tarime-Rorya*...........................Sh. 7,492,227,000
Kifungu 2025 - *Police Mbeya*....................................Sh. 12,067,586,000
Kifungu 2026 - *Police Mtwara*....................................Sh. 9,509,698,000
Kifungu 2027 - *Police Morogoro*...............................Sh. 15,647,440,000
Kifungu 2028 - *Police Manyara*................................Sh. 10,030,425,000
Kifungu 2029 - *Police Singida*.....................................Sh. 9,573,713,000
Kifungu 2030 - *Police Pwani*......................................Sh. 10,165,735,000
Kifungu 2031 - *Police Ruvuma*...................................Sh. 8,842,879,000
Kifungu 2032 - *Police Rukwa*......................................Sh. 7,167,857,000
Kifungu 2033 - *Police Shinyanga*...............................Sh. 9,498,828,000
Kifungu 2034 - *Police Tabora*.....................................Sh. 9,472,141,000
Kifungu 2035 - *Police Tanga*....................................Sh. 13,023,835,000
Kifungu 2036 - *Police Mjini Magharibi*.......................Sh. 11,615,614,00
Kifungu 2037 - *Police Kusini Unguja*...........................Sh. 4,056,355,000
Kifungu 2038 - *Police Kaskazini Unguja*.....................Sh. 3,650,087,000
Kifungu 2039 - *Police Kusini Pemba*..........................Sh. 3,477,301,000
Kifungu 2040 - *Police Kaskazini Pemba*.....................Sh. 3,382,644,000
Kifungu 2041 - *Police Dodoma*...............................Sh. 18,373,846,000
Kifungu 2042 - *Police Geita*.......................................Sh. 9,319,565,000
Kifungu 2043 - *Police Katavi*.....................................Sh. 5,348,829,000

Kifungu 2044 - *Police Njombe*....................................Sh. 6,682,290,000
Kifungu 2045 - *Police Simiyu*......................................Sh. 6,561,127,000
Kifungu 2046 - *Police Songwe*....................................Sh. 5,247,180,000
Kifungu 2047 - *Police Rufiji*.........................................Sh. 5,288,377,000
Kifungu 2048 - *TPF Corporation Sole Unit*.....................Sh. 248,832,000
Kifungu 2049 - *Police Bandari*....................................Sh. 2,576,013,000
Kifungu 2050 - *Police Band*........................................Sh. 1,497,445,000
Kifungu 2051 - *Police Bohari*.....................................Sh. 14,324,157,000
Kifungu 3001 - *Police College Moshi*.......................Sh. 23,785,390,000
Kifungu 3002 - *Police College*...................................Sh. 2,714,637,000
Kifungu 3003 - *Operations and Training*....................Sh. 3,956,195,000
Kifungu 3004 - *Zanzibar Police College*....................Sh. 1,041,090,000
Kifungu 3005 - *Mwanza Marine Police College*.........Sh. 952,176,000
Kifungu 3006 - *Tanzania Police Staff College - Kidatu*................................Sh. 1,553,280,000
Kifungu 4001 - *Police Vehicles Maintenance Unit*...Sh. 2,583,369,000
Kifungu 5001 - *Police Medical Unit*............................Sh. 2,794,525,000
Kifungu 6001 - *Police Ujenzi*..........................................Sh. 434,190,000
Kifungu 7001 - *Criminal Investigation Division*..........Sh. 7,460,639,000
Kifungu 7002 - *Stock Theft Prevention Unit*...................Sh. 633,636,000
Kifungu 7003 - *Criminal Intelligence Bureau*.............Sh. 1,910,842,000
Kifungu 7004 - *Forensic Intelligence Bureau*.............Sh. 3,393,123,000
Kifungu 7005 - *Community Engagement*....................Sh. 952,772,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................................Sh. 33,239,555,396
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 2,241,952,600
Kifungu 1003 – *Public Relations and Communication Unit*............................Sh. 343,876,680
Kifungu 1004 – *Intelligence and Operations Unit*.....Sh. 1,264,203,980
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 232,670,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 978,402,000
Kifungu 1007 - *Information and Communication Technology Unit*....................................Sh. 664,694,000
Kifungu 2001 – *Legal and Prisons Unit*.......................Sh. 4,797,988,000

Kifungu 2002 - *Correctional and Rehabilitation*...Sh. 112,901,299,088
Kifungu 2003 - *Resettlement of Offenders*................Sh. 6,505,290,000
Kifungu 2004 - *Prisons Arusha*....................................Sh. 6,999,274,000
Kifungu 2005 - *Prisons Dar es Salaam*......................Sh. 14,250,209,000
Kifungu 2006 - *Prisons Dodoma*.................................Sh. 7,373,080,866
Kifungu 2007 - *Prisons Kigoma*......................................Sh. 708,429,100
Kifungu 2008 - *Prisons Tanga*.....................................Sh. 6,228,072,120
Kifungu 2009 - *Prisons Kagera*....................................Sh. 4,637,654,000
Kifungu 2010 - *Prisons Mwanza*..................................Sh. 4,083,536,900
Kifungu 2011 - *Prisons Tabora*....................................Sh. 1,596,050,000
Kifungu 2012 - *Prisons Mbeya*.....................................Sh. 5,308,031,000
Kifungu 2013 - *Prisons Singida*....................................Sh. 3,736,306,000
Kifungu 2014 - *Prisons Coast*......................................Sh. 9,436,064,000
Kifungu 2015 - *Prisons Lindi*.........................................Sh. 1,214,172,400
Kifungu 2016 - *Prisons Manyara*................................Sh. 3,347,314,000
Kifungu 2017 - *Prisons Mtwara*...................................Sh. 3,247,811,800
Kifungu 2018 - *Prisons Ruvuma*......................................Sh. 618,237,200
Kifungu 2019 - *Prisons Rukwa*.....................................Sh. 3,842,856,000
Kifungu 2020 - *Prisons Mara*.......................................Sh. 3,702,722,200
Kifungu 2021 - *Prisons Iringa*.......................................Sh. 2,721,996,500
Kifungu 2022 - *Prisons Kilimanjaro*..............................Sh. 5,421,644,000
Kifungu 2023 - *Prisons Morogoro*.............................Sh. 10,760,408,000
Kifungu 2024 - *Prisons Geita*.......................................Sh. 2,814,062,900
Kifungu 2025 - *Prisons Katavi*.....................................Sh. 2,315,541,000
Kifungu 2026 - *Prisons Njombe*.....................................Sh. 435,013,400
Kifungu 2027 - *Prisons Simiyu*..........................................Sh. 955,512,000
Kifungu 2028 - *Prisons Shinyanga*..................................Sh. 703,078,270
Kifungu 2029 - *Prisons Songwe*..................................Sh. 2,499,896,000
Kifungu 3001 - *Ukonga Prisons Staff College*............Sh. 8,019,084,000
Kifungu 3002 - *Kingolwila Prisons Driving School*......Sh. 2,055,525,000
Kifungu 3003 - *Ruanda Prisons Trade School*............Sh. 2,162,656,000
Kifungu 3004 - *Prisons College Kiwira*........................Sh. 2,520,771,600
Kifungu 4001 - *Prison Building Brigade*.........................Sh. 855,807,000
Kifungu 4002 - *Prison Industries*........................................................Sh. 0
Kifungu 4003 - *Prison Farms*.............................................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji

Kifungu 2001 - *Immigration Zanzibar*........................Sh. 14,488,656,000
Kifungu 2002 - *Immigration Head Quarter*............Sh. 101,178,850,000
Kifungu 2003 - *Immigration Ilala*......................................Sh. 66,705,000
Kifungu 2004 - *Tanzania Regional Immigration Training Academy*..............................................Sh. 340,290,000
Kifungu 2005 - *Immigration Kinondoni*...........................Sh. 66,705,000
Kifungu 2006 - *Immigration Temeke*...............................Sh. 66,705,000
Kifungu 2007 - *Immigration Arusha* ..............................Sh. 153,960,000
Kifungu 2008 - *Immigration Dar es Salaam*..................Sh. 133,851,000
Kifungu 2009 - *Immigration Dodoma*...........................Sh. 138,624,000
Kifungu 2010 - *Immigration Geita*................................Sh. 135,183,000
Kifungu 2011 - *Immigration Iringa*.................................Sh. 136,803,000
Kifungu 2012 - *Immigration Kilimanjaro*........................Sh. 156,246,000
Kifungu 2013 - *Immigration Kigoma*.............................Sh. 171,138,000
Kifungu 2014 - *Immigration Katavi*................................Sh. 142,518,000
Kifungu 2015 - *Immigration Kagera*..............................Sh. 169,353,000
Kifungu 2016 - *Immigration Lindi*..................................Sh. 130,716,000
Kifungu 2017 - *Immigration Mwanza*............................Sh. 145,983,000
Kifungu 2018 - *Immigration Manyara*...........................Sh. 138,720,000
Kifungu 2019 - *Immigration Mbeya*..............................Sh. 144,405,000
Kifungu 2020 - *Immigration Morogoro*.........................Sh. 147,363,000
Kifungu 2021 - *Immigration Mtwara*.............................Sh. 147,240,000
Kifungu 2022 - *Immigration Mara*..................................Sh. 143,061,000
Kifungu 2 023 - *Immigration Njombe*............................Sh. 136,140,000
Kifungu 2024 - *Immigration Pwani*................................Sh. 145,620,000
Kifungu 2025 - *Immigration Ruvuma*............................Sh. 140,850,000
Kifungu 2026 - *Immigration Rukwa*................................Sh. 141,300,000
Kifungu 2027 - *Immigration Simiyu*................................Sh. 136,860,000
Kifungu 2028 - *Immigration Singida*..............................Sh. 140,442,000
Kifungu 2029 - *Immigration Shinyanga*.........................Sh. 138,123,000
Kifungu 2030 - *Immigration Tanga*................................Sh. 148,593,000
Kifungu 2031 - *Immigration Tabora*..............................Sh. 147,840,000
Kifungu 2032 - *Immigration Songwe*.............................Sh. 142,593,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Kamati yako ijielekeze kwenye Kitabu cha Nne, fedha za maendeleo.

## KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management Division*....................Sh. 27,756,504,000
Kifungu 4002 - *Anti - Trafficking in Person Secretariat*........................................Sh. 1,445,957,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Kifungu 3001 - *Fire and Rescue Services*..................Sh. 3,626,521,000
Kifungu 3014 - *Manyara Regional Office*...................Sh. 414,290,000
Kifungu 3015 - *Geita Regional Office*..........................Sh. 414,285,000
Kifungu 3022 - *Kagera Regional Office*......................Sh. 264,285,000
Kifungu 3025 - *Njombe Regional Office*.....................Sh. 264,285,000
Kifungu 3029 - *Morogoro Regional Office*..................Sh. 300,000,000
Kifungu 3030 - *Katavi Regional Office*........................Sh. 414,285,000
Kifungu 3032 - *Simiyu Regional Office*.........................Sh. 414,285,000
Kifungu 3033 - *Songwe Regional Office*.....................Sh. 414,285,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 28 – Jeshi la Polisi

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*..........................................................Sh. 0
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*.................Sh. 162,724,952,000
Kifungu 2004 - *Police Signals Branch*......................Sh. 40,543,899,000
Kifungu 2005 - *Police Zanzibar*.......................................................Sh. 0Kifungu 2006 - *Police Air Wing*....................................................Sh. 0
Kifungu 2015 - *Police Temeke*......................................................Sh. 0

Kifungu 2016 - *Police Arusha*........................................Sh. 139,000,000
Kifungu 2020 - *Police Kagera*....................................Sh. 1,000,000,000
Kifungu 2025 - *Police Mbeya*...........................................................Sh. 0
Kifungu 2026 - *Police Mtwara*......................................Sh. 798,000,000
Kifungu 2027 - *Police Morogoro*.....................................Sh. 90,251,000
Kifungu 2028 - *Police Manyara*....................................Sh. 800,000,000
Kifungu 2029 - *Police Singida*..........................................................Sh. 0
Kifungu 2035 - *Police Tanga*.........................................Sh. 220,000,000
Kifungu 2036 - *Police Mjini Magharibi*..........................Sh. 300,000,000
Kifungu 2037 - *Police Kusini Unguja*...............................................Sh. 0
Kifungu 2038 - *Police Kaskazini Unguja*........................Sh. 359,454,000
Kifungu 2039 - *Police Kusini Pemba*.............................Sh. 250,000,000
Kifungu 2040 - *Police Kaskazini Pemba*........................Sh. 250,000,000
Kifungu 2041 - *Police Dodoma*......................................................Sh. 0
Kifungu 2045 - *Police Simiyu*.........................................Sh. 220,000,000
Kifungu 2047 - *Police Rufiji*............................................................Sh. 0
Kifungu 2051 - *Police Bohari*.....................................Sh. 16,479,380,000
Kifungu 3004 - *Zanzibar Police College*..........................................Sh. 0
Kifungu 5001 - *Police Medical Unit*................................................Sh. 0
Kifungu 7004 - *Forensic Intelligence Bureau*..................................Sh. 0
Kifungu 7005 - *Community Engagement*....................Sh. 200,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 29 – Jeshi la Magereza

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*......................................Sh. 3,849,233,000
Kifungu 2002 - *Correctional and Rehabilitation*.......Sh. 3,487,149,000
Kifungu 4001 - *Prison Building Brigade*.....................Sh. 11,342,059,000
Kifungu 4002 - *Prison Industries*.......................................................Sh. 0
Kifungu 4003 - *Prison Farms*............................................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2002 - *Immigration Head Quarter*..............Sh. 10,916,109,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nitawahoji sasa kwa mujibu wa kanuni zetu kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Wote wameafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Napenda kutoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri *Engineer* Hamad Masauni na Naibu wako Daniel Sillo, Katibu Mkuu Ally Gugu, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Maduhu na Watendaji wote kwa hatua hii tuliyofikia ambapo Bunge sasa limepitisha makadirio ya matumizi ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani kwa mwaka 2024/2025. Vilevile niwashukuru sana Wakuu wa Taasisi zote ambazo zipo chini ya Wizara hii, Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Idara ya Uhamiaji. Wote tumesikia katika michango mbalimbali, matumaini bado ni makubwa sana, kwamba changamoto zitaendelea kutatuliwa. Pia tumesikia habari njema ya mageuzi makubwa sana kwenye Jeshi letu la Polisi na Jeshi la Magereza. Kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali kwa hayo yote.

Naipongeza sana Kamati yetu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri sana waliyoifanya katika kutupitisha na kutupa mambo mengi yaliyotokana na bajeti hii na shughuli mbalimbali.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.49 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 16 Mei 2024, Saa Tatu Asubuhi)*